

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Nane – Tarehe 13 Aprili, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu Tatu, leo ni Kikao cha Nane. Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

SPIKA: Hati za kuwasilisha Mezani, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baadaye tutakapokuwa tunaisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni muhimu vilevile kupitia Hotuba za Kamati, zinasaidia kutoa picha pana zaidi kuhusiana na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kudumu ya Bajeti na wale Wenyeviti wengine wasogee karibu karibu. Mheshimiwa Shally J. Raymond, karibu sana.

MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana, hiyo ndiyo Kamati ya Bajeti. Sasa twende Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Waheshimiwa Wabunge wengine mnaiita Kamati ya UKIMWI hapana, ni Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Endelea Mheshimiwa.

MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta na Tume ya Uratibu na Kudhibiti UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, uliza swali lako.

Na. 60

**Kuruhusu Wananchi Kandokando ya Barabara Kufanya
Biashara kwa Saa Ishirini na Nne**

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuruhusu wananchi wanaoishi kwenye Miji ambayo ipo kando ya barabara kuu kama Mji wa Mafinga kufanya biashara kwa saa ishirini na nne?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Mheshimiwa David E. Silinde, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kubuni mikakati mbalimbali katika kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo ikiwa ni pamoja na kuwatengea maeneo kwa ajili ya kuendesha biashara zao na kuwatambua kwa kuwapatia vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo na watoa huduma. Kutokana na uhaba wa maeneo ya kufanya biashara kwenye baadhi ya Miji, yameanzishwa masoko ya usiku ambayo yanaendeshwa kwa kufunga baadhi ya Mitaa nyakati za jioni hadi usiku kwa ajili ya kupisha wafanyabiashara wadogo kuendesha biashara zao. Baadhi ya Halmashauri hizo ni Jiji la Dodoma, Jiji la Dar-es-Salaam na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa biashara nyakati za usiku umeonekana kuwa na changamoto nydingi za ulinzi na usalama wa wafanyabiashara, wateja pamoja na bidhaa zao. Uzoefu unaonesha kuwa maeneo zinakofanyika biashara kwa saa 24 kuna miundombinu yote muhimu ikiwemo taa, kamera, vyoo na maeneo ya kuhifadhia bidhaa za wafanyabiashara.

Aidha, ili kuwa na usalama wa uhakika katika masoko, kunahitajika ulinzi wa Polisi au Askari wa akiba kwa maana ya Mgambo, hususan nyakati za usiku. Serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama itaendelea kutafuta namna bora ya kuwezesha wafanyabiashara waishio kwenye Miji kando ya barabara Kuu ikiwemo Mafinga kufanya biashara zao kwa saa 24 ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu ya msingi.

SPIKA: Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Leo tutajadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na sehemu ya hotuba hiyo tutajadili suala la ajira hususan kwa vijana. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali iliruhusu tusafirishe mazao ya misitu kwa saa 24 na hivyo kusisimua na kuchechemua uchumi sio wa Mafinga tu na maeneo mengine. Je, Serikali iko tayari kufanya upendeleo maalum kwa Mji wa Mafinga kutokana na *nature* yake ya kibashara kuruhusu baadhi ya maeneo watu kufanya biashara saa 24 na yenyewe ikabaki na suala la ulinzi ambayo ni kazi kuu ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, swalii pili, katika jibu la msingi Serikali imesema kuna changamoto ya miundombinu muhimu kama vile taa, kamera na kadhalika. Sisi kama Halmashauri tuko tayari kujenga baadhi ya miundombinu lakini je, Serikali iko tayari kutusaidia japo taa za barabara katika maeneo muhimu katika njia panda za Itimbo, Madibila, Mufindi na Sokoni ili kuwawezesha wananchi hawa kuendelea kujiajiri na kujipatia kipato na hivyo kuwa na mchango katika Serikali na mifuko yao?

SPIKA: Maswali mazuri sana haya, majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, Mheshimiwa Mbunge alikuwa anataka upendeleo maalum kwa Mji wa Mafinga ili uweze kufunguliwa. Katika jibu langu msingi nilieleza kabisa moja ya jukumu kubwa la Serikali ambalo tunalifanya sasa ni kuhakikisha tunajenga miundombinu na usalama unakuwepo. Baada ya kutathmini ndipo tunaweza kuruhusu Mji wa Mafinga ili uweze kufanya biashara kwa saa 24.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ambalo ni la msingi kabisa Mheshimiwa Mbunge ameainisha *commitment* ya Halmashauri yake kwamba wao kama Mafinga Mji wako

tayari kujenga baadhi ya miundombinu muhimu na sisi kama Serikali tuweze kusaidia katika kuweka hizo taa za barabarani. Nafikiri wazo hilo ni jema na mimi niungane kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kusema kwamba tunaomba Halmashauri ya Mji Mafinga waanze hiyo hatua ya kutengeneza hiyo miundombinu muhimu na sisi tutatuma wataalam wetu waende kufanya tathmini, ili tuweze kuwaruhusu waweze kufanya hiyo biashara yao kwa saa 24 na sisi tutawasaidia katika hiyo sehemu itakayobakia.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata, bado tuko TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Na. 61

**Tatizo la Kuja Maji baadhi ya Maeneo ya
Mtwara Mikindani**

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya kuja maji mara tu mvua zinaponyesha katika baadhi ya maeneo ya Kata za Magomeni, Shangani, Ufukoni, Reli na Likombe katika Manispaa ya Mtwara Mikindani?

SPIKA: Bado tuko TAMISEMI, Mheshimia David Silinde, majibu ya swali hilo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya kuja maji mvua zinaponyesha katika baadhi ya maeneo ya Kata za Magomeni, Shangani, Ufukoni, Reli na Likombe katika Manispaa ya Mtwara Mikindani. Katika mwaka wa

fedha 2017/2018, Serikali kupitia Mradi wa Uendelezaji Miji (*Tanzania Strategic Cities Projects*) imejenga mifereji ya kutoa maji kwa maana ya *stand-alone drains* yenye urefu wa kilomita 10 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.82 katika Kata za Shangani, Reli, Likombe na Vigaeni Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukamilisha Mpango Kabambe wa kuyaondoa maji ya mvua katika makazi na kuyaelekeza baharini katika Manispaa ya Mtwara Mikindani. Serikali itatafuta fedha ili kutekeleza kikamilifu Mpango Kabambe wa kuondoa maji ya mvua kwenye makazi na kuyaelekeza baharini katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

SPIKA: Mheshimiwa Tunza Malapo, nimekuona.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imejenga mifereji katika baadhi ya maeneo, lakini mfereji wa kutoa maji kutoka Kata ya Shangani, maeneo ya Kiangu kwenda baharini haufanyi kazi vizuri, maji yanajaa sana kwenye majumba ya watu. Sasa swalii langu, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kwenda Mtwara kuuona mfereji ule na kufanya utaratibu wa kuhakikisha mfereji ule unatengenezwa kwa kiwango kizuri ili kusudi wananchi wale wasiweze kupata adha hiyo maji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, maeneo mengi ambayo yanajaa maji katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ni ambayo Serikali imepima viwanja ikawagawia wananchi, siyo kwamba wamevamia. Katika kujaa maji kule kunasababisha uharibifu na wakati mwiningine vifo vya wananchi.

Je, Serikali sasa iko tayari kwenda kukaa na wananchi wale waone wanatatuwa vipi changamoto hizi kwa sababu

kadri miaka inavyokwenda tatizo ni kubwa, linaharibu mali na wakati mwingine kugharimu maisha ya wananchi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani? Nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa David Silinde.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza alilokuwa ameliomba, anaomba sisi kama Ofisi ya Raís – TAMISEMI hususani Waziri kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika eneo husika kushuhudia anachokieleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, niko tayari mara baada ya kupitisha bajeti yetu, nitaongozana naye pamoja na Mbunge wa Jimbo husika kuhakikisha tunaipatia ufumbuzi kero hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ameuliza kama Serikali ipo tayari kukaa na wananchi, nimhakikishie tutakavyokwenda kule tutakaa na wananchi ili tuweze kupata suluhisho la tatizo hilo. Ahsante.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Agnesta Kaiza, kuhusu mafuriko ya maji Mjini Bukoba. (*Kicheko*)

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Changamoto ya kujaa kwa maji yanayotokana na mvua iliyoko Mkoa wa Mtwara haina tofauti kabisa na changamoto iliyopo Mkoa wa Dar es Salaam hususan eneo la Jangwani. Kujaa kwa maji katika eneo la Jangwani imekuwa ni changamoto ya muda mrefu na haijawahi kupatiwa tiba ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani au inatueleza nini kuhusiana na

changamoto hii ya kujaa maji pale Jangwani hasa ikizingatiwa kwamba Jangwani ni kiunganishi kikubwa sana cha wafanyabiashara wanaoelekea Kariakoo eneo ambao limebeba uchumi mkubwa sana wa nchi? Naomba Serikali basi itoe majibu ni lini itaweza kukomesha changamoto hii ya kujaa maji Jangwani. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Agnesta Kaiza. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Agnesta Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amejaribu kuoanisha eneo la Jangwani na maeneo yaliyoko kule Mtwara katika Manispaa ya Mikindani kwamba na lenyewe linajaa sana maji na anataka kufahamu mkakati gani ambao Serikali inao kuhakikisha tunatatua tatizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuna mradi mkubwa wa DMDP ambao unajenga miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam. Sehemu ya miundombinu hiyo ambayo tumekuwa tukijenga ni pamoja na mifereji mikubwa ambayo imekuwa ikihamisha maji kutoka katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na kupeleka baharini.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, sasa hivi tuna Mradi mkubwa wa Mabasi Yaendayo Kasi na moja ya jukumu lao kubwa ni kuhakikisha lile eneo la Jangwani linapandishwa tuta kubwa ambalo litahakikisha ile kero ambayo inawapata wananchi inaondolewa. Kwa hiyo, nimhakikishie kabisa Serikali ipo kazini na ile kazi itakamilika na wananchi wa Jiji la Dar es Salaam hawatajutia kuichagua Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu mazuri sana. Sasa tunaelekea kwa Mbunge wa Hanang', Mheshimiwa Samweli Hhayuma. Kama hayupo Mbunge mwingine aulize kwa niaba yake. Hakuna mtu wa Hanang' hata mmoja? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Yupo.

SPIKA: Haya endelea Mheshimiwa Mbunge.

Na. 62

Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Mji wa Katesh

MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. SAMWELI X. HHAYUMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa stendi ya mabasi ya Mji wa Katesh?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ni mionganoni mwa mwa Halmashauri zilizokidhi vigezo vya kupatiwa fedha za ujenzi wa stendi ya mabasi kuititia Mpango wa Mradi Mkakati katika Halmashauri. Lengo la Serikali kuanzisha Mpango huu ni kuziwezesha Halmashauri kubuni miradi itakayoziongezea mapato ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Stendi ya Mabasi ya Katesh wenye gharama ya shilingi bilioni 5.60 ni mionganoni

mwa miradi 20 ya kimkakati nchini ambayo utekelezaji wake ulisitishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kutohana na changamoto mbalimbali zilizojitekeza kwenye hatua za mwanzo za utekelezaji. Serikali ilizifanya kazi changamoto hizo kupitia timu ya wataalam iliyoundwa na kutafuta namna bora ya kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, timu ilitoa maoni kadhaa yaliyotakiwa kutekelezwa na Halmashauri ya Hanang ikiwa ni pamoja na kupitia upya vipengele vyote veya mkataba, hususan muda wa mkataba na masharti ya dhamana ya awali kwa maana ya *advanced payment guarantee*. Hadi Machi, 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Hanang imekamilisha taratibu zote kama ilivyoelekezwa na timu ya wataalam tayari kwa kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, mradi utaendelea baada ya Wizara ya Fedha kupitia nyaraka hizo na kujiridhisha.

SPIKA: Haya. Ujenzi wa Stendi ya Hanang, Mheshimiwa Pallangyo.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Halmashauri ya Meru nayo ilikuwa *victim* ya *withdraw* ya mradi mkakati ambayo ilikuwa imetengenezwa mwaka ule wa 2019. Naomba kuuliza: Je, Serikali sasa iko tayari kuja kutekeleza ule mradi?

Mheshimiwa Spika, Mradi huo uko eneo la Tengeru mahali panaitwa Sadak, ulikuwa umeshatengenezwa na Serikali ilikuwa imeshachakata lile andiko na nilipofika kule Hazina nikakuta karibia pesa zinatoka, kuja hapa Bungeni nikaambiwa mradi umekuwa *withdrawn*: Je, ni hatua gani zinazoendelea kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Meru nayo inawezeshwa, kwa sababu sasa hivi inashindwa kuhudumia wananchi kwani haina mapato ya kutosha? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kama una maelezo kuhusu hilo, karibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka 2019/2020 Serikali ilijaribu kusitisha kwa muda miradi yote ile ambayo ilikuwa inasuasua. Sasa hivi nikuhanakishie kwamba, Serikali imejipanga na tumekubalianana *tui-review*; na miradi yote ile ambayo ilisitishwa, ile miradi ya kimkakati katika Halmashauri zote ambazo zilikuwa zimepangiwa awali, inakwenda kufanya kazi. Ahsante sana.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Monni.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa, changamoto ya Hanang inafanana sana na changamoto iliyopo kwenye mji wetu wa Chemba. Ni bahati mbaya sana uwezo wa Halmashauri yetu, ni mdogo: sasa naomba kujua, ni lini Serikali itajenga stendi kwenye Mji wetu wa Chemba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna mpango wowote wa kujengwa stendi ya Chemba au wanapaswa kuanza wao? Karibu Mheshimiwa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, nieleze tu kwa kifupi kwamba, ile miradi ya kimkakati katika Halmashauri ilikuwa na vigezo kwa kila Halmashauri kupata. Tuliajisha vigezo 13 ambavyo Halmashauri ikivikamilisha inapata ile miradi. Moja ya vigezo ikiwemo ni; katika miaka mitatu mfululizo, Halmashauri hiyo iwe imepata hati safi. Kwa hiyo, kama ulikuwa unakosa baadhi ya vigezo, basi ulikuwa *hau-qualify* kupata hiyo miradi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge kuhimiza Halmashauri zenu kutimiza vigezo vyote. Vigezo ambavyo vimekamilishwa, vinaletwa Ofisi ya Rais, *TAMISEMI* nasi tukiona kwamba Halmashauri *in-a-qualify*, basi *tunawa-guarantee* kupata huo mradi kwa ajili ya kusaidia Halmashauri zetu kuongeza mapato yao ya ndani. Ahsante sana.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maji sasa Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

Na. 63

Kupima na Kuchimba Visima Virefu Arusha

MHE. ZAYTUN S. SWAI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupima na kuchimba visima virefu Mkoani Arusha hasa Wilaya ya Longido katika Vijiji vya Noondoto, Matale, Wosiwosi na Ngereani ambapo kuna uhaba wa vyanzo vya maji safi na salama?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, tafadhalli, Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na Wilaya ya Longido kuwa na uhaba wa vyanzo vya maji hasa chemicchemi, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali ikiwemo kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchimba visima virefu, ambapo katika Kijiji cha Matale B, uchimbaji wa kisima unaendelea kuititia Bajeti ya mwaka 2020/2021 na unatarajija kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Noondoto, kinapata huduma ya maji kuititia mradi wa maji wa Kijiji cha Elang'atadabash unaohudumia vijiji vitano vya Elang'atadabash, Sokoni, Olchonyorokie, Noondoto, Losirwa na Naadare. Katika Kijiji cha Wosiwosi kisima kilichochimbwa, maji yake yalibainika kutofaa kwa matumizi ya binadamu kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha madini chumvi ukilinganisha na kiwango kinachokubalika.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itatumia vyanzo vya Mto Engaresero kutekeleza mradi wa kufikisha maji Kijiji cha Matale na Wosiwosi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kijiji cha Wosiwosi, tumeweka bajeti ya kujenga bwawa litakalosaidia mifugo na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ngereani kinapata huduma ya maji kuititia Mradi wa Maji Tingatinga Ngereani. Serikali itaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Longido wanapata huduma ya maji safi na salama kwa kutumia vyanzo mbalimbali vitakavyoonekana vinafaa ikiwemo mito, visima na mabwawa.

SPIKA: Mheshimiwa Zaytun Swai, nimekuona. Swalii la nyongeza.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, leo hii ukienda Longido kwenye vijiji vya Noondoto, Matale, Wosiwosi na Ngereani, utalia kwa jinsi wananchi wanavyopata shida ya maji na hususan akina mama; wanalahazimika kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilomita 10 kutafuta maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, akina mama hawa mara nyingine wanalahazimika kwenda kulala kwenye vyanzo vya maji kusubiria maji yanayochuruzika. Swalii langu kwa Serikali: Je. Waziri yuko tayari kwenda Longido kuona hali halisi ya maeneo haya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; kwa kuwa changamoto ya Wilaya ya Longido linafanana kabisa na changamoto walizonazo akina mama wa Monduli hususan kwenye Kata za Moita, Lekruko na Naalarami: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia akina mama wa Monduli haki

yao ya msingi ya kupata maji safi na salama? Nakushukuru.
(Makofi)

SPIKA: Haya. Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, majibu tafadhali.

MHE. NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa kufika Longido ni moja ya majukumu yangu na tayari maeneo yale nilishatembelea nikiwa na Mbunge wa Jimbo na nimeshawasiliana naye kwa kirefu sana. Hata hivyo nitajitahidi kufika tena kuona namna gani tutaendelea kusaidiana na wananchi waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mipango ya Wizara ni kuhakikisha maeneo yote yanafikiwa na maji bombani. Tupo kwenye mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yamekuwa na matatizo ya vyanzo rahisi kama chemchemi, basi visima vinaendelea kuchimbwa na tayari Wizara wataalam wake wako huko wanaendelea, hata sasa hivi hapo Chemba tayari visima vinachimbwa na maeneo mbalimbali katika Majimbo yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwondoa hofu Mheshimiwa Mbunge, akina mama tuna lengo jema la kuhakikisha tunawatua ndoo kichwani; Wizara tuna lengo jema kuhakikisha tunaokoa ndoa hizi ambazo akina mama wanalala kwenye vyanzo vya maji; tunahitaji akina mama walale nyumbani na familia zao. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige, nilikuona.

MHE. CATHERINE MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 520 katika Jiji la Arusha. Mradi huu changamoto yake kubwa unapita katika maeneo ya mjini, lakini maeneo ya pembezoni kwenye Kata kama Olmoti, baadhi ya sehemu za Muriet, Moshono na Olasiti hazifiki. Je. Serikali haioni sasa kuna umuhimu mkubwa wa

mradi huu wa maji kuhakikisha unapita katika Kata za pembezoni mwa Jiji la Arusha? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mji wa Arusha una bahati kubwa sana, kwa sababu una mradi wenye fedha nyingi sana na ni mradi ambao tunautarajia umalize kero ya maji katika Jiji la Arusha. Katika maeneo haya aliyoyataja, ni jana tu nimekuwa nikiongea na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arusha, aliyeongozana na timu ili yotoka kule ikiwa pamoja na Mheshimiwa Diwani Miriam, tayari nimeshafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yako pembezoni, wenzetu wa Mamlaka ya Maji ya Arusha, pale tayari na wenyewe wanaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuona namna bora ya kuendelea kutanua mitandao ya mabomba kuwafikia wananchi. Hili nalo tutalismamia kwa karibu kabisa kuhakikisha maeneo yote ya pembezoni, Mamlaka pamoja na *RUWASA* wanawajibika ili maji yaweze kuwafikia wananchi. (*Makofi*)

SPIKA: Mbunge wa Jimbo husika la Longido, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba maji ya Ngaresero hayataweza kufika katika Wilaya ya Longido, kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kurekebisha hapo. Hata hivyo, nashukuru kwa jitihada ambazo Serikali inaenda kufanya katika kutupatia maji kwa gharama yoyote, iwe ni mabwawa au chemichemi ama chanzo chochote cha maji salama katika eneo la Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Spika, naomba tu kutumia fursa hii kuikumbusha Serikali kwamba, kuna ahadi ambayo imerudiwa tena na tena ya kutoa tawi la maji ya Mto Simba

ambayo yamekwenda mpaka Mjini Longido na sasa hivi yanaelekea Namanga. Naiomba sana Serikali Kijiji cha Eilarai eneo la Motong' wapate maji maana ni Kijiji cha kwanza kilichopitiwa na bomba hilo kubwa na wananchi wale wameendelea kunikumbusha kwamba ahadi imetolewa na Mawaziri watatu hadi sasa; Mheshimiwa Waziri Mbarawa, Mheshimiwa Waziri Kamwelwe na huyu aliyeko sasa hivi wakati ule akiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo, ni lini Serikali itakwenda kuwapelekea watu wa Imotong' maji safi na salama ya Mto Simba?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusu maji ya Mto Simba, ni mpango mkakati wa Wizara kwenda kutumla mito, maziwa na vyanzo vyote vya maji kuhakikisha maeneo yote tunayafikia. Kwa upande wa Longido, Mheshimiwa Mbunge tuna mpango wa kuendelea kuona chanzo hiki cha maji cha Mto Simba kinakwenda kutumika katika mwaka wa ujao wa fedha.

SPIKA: Sasa tunahamia Hai. Mheshimiwa Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe uliza swali lako.

Na. 64

**Mgogoro wa Ardhi Kati ya Wananchi na Mamlaka
ya Viwanja Vya Ndege – KIA**

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza:-

Je, lini ni Serikali itatekeleza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni ya kumaliza mgogoro wa ardhi uliopo kati ya wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *KIA*?

SPIKA: Nawaletea Naibu Waziri mpya kabisa katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu tafadhali. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa mbele baada ya kupewa kura za kutosha na wananchi wa Tarime Vijiji, naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano. Pia, namshukuru Mungu kwa yote yaliyotokea na namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan kuniamini na kunipa nafasi ya kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Ujenzi na Uchukuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: - (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1969 Serikali ilitenga eneo lenye ukubwa wa ekari 11,085 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (*KIA*). Eneo hilo lilipimwa mwaka 1989 kwa ramani ya upimaji Na. E255/18 iliyo sajiliwa na namba 231264 inayofahamika kama *FARM* No.1 lenye Hati namba. 22270 iliyotolewa 20 Machi, 2005.

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2001 Serikali ilibaini kuwepo kwa baadhi ya wananchi kutoka vijiji vinavyopakana na *KIA* vya *Sanya Station*, Chemka, Tindigani na Mtakua vilivyopo Wilaya ya Hai na Vijiji vya Majengo, Samaria na Malula vilivyopo Wilaya ya Arumeru kuingia kwenye eneo la *KIA* na kuweka makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilichukua hatua za kufanya tathmini shirikishi wa mali za wananchi ili kuwaondoa kwa lengo la kutimiza azma ya Serikali kuendeleza *KIA* na pia kulinda usalama wa Kiwanja. Katika utathmini huo, ilibainika kwamba ndani ya eneo hilo kuna kaya 289 zenye thamani ya fidia iliyotakiwa shilingi 426,020,500/=. Fedha za kulipa fidia hizo hazikuwepo wakati huo, kwa hiyo, fidia haikulipwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013, 2018 na 2019 kwa nyakati tofauti, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kushirikisha

TAMISEMI, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Arusha, Ofisi ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Wilaya za Hai na Arumeru imekuwa ikishughulikia suala hili kwa kushirikiana na uongozi wa vijiji husika ili kupata suluhu kwa kubaini idadi ya kaya zenye makazi ya kudumu katika eneo la KIA na kufanya tathmini upya.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2018 zoezi la uwekaji wa alama lilanza ambapo Vijiji vya Majengo na sehemu ya Kijiji cha Mtakuja viliwekwa alama za kudumu. Vijiji vya Samaria na Malula vilivyopo Wilaya ya Arumeru, Vijiji vya Tindigani na *Sanya Station* katika Wilaya ya Hai vilikataa kutoa ushirikiano kwa Timu ya Wataalam kwa kukataza wataalam katakata kuingia katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imejipanga kukamilisha zoezi hili kwa kurudishia mipaka ya kudumu ya KIA na kubaini idadi ya kaya zilizopo ndani na kufanya tathmini upya na kupata kiasi ambacho kinatakiwa kulipwa ili zoezi hili liweze kumalizika. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, uliza swali lako tafadhali.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Hai. Mgogoro huu umekuwa wa muda mrefu sana, jambo linalosababisha wananchi kukosa maeneo ya malisho na kuishi kwa wasiwasi kwenye maeneo yao ambayo wanaishi pale tangu mwaka 1975. Wananchi wote wa vijiji hivi vyote vinne vinavyotajwa, wana usajili wa vijiji vyao, nikimaanisha Kijiji cha *Sanya station*, Tindigani, Mtakuja na Chemka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ukizingatia eneo lilopo kwenye uwanja huo ni kubwa sana; kwenye *list* ya Viwanja vya Ndege tulivyonyavyo hapa Tanzania, Kiwanja cha Kilimanjaro *Airport* kinaongoza kikifuatiwa na Kiwanja cha

Dodoma na Songwe, halafu kiwanja cha nne ni Dar es Salaam.

Je, Serikali haioni kwa ukubwa ulioko pale, iko haja ya baadhi ya maeneo yarudi kwa wananchi ili waweze kuendelea na maeneo yanayobaki, yabaki kwenye Uwanja huu wa Ndege jambo ambalo tayari mimi mwenyewe nilishakutana na *Management* na wakaonyesha utayari wa kukubaliana na jambo hili?

Swali la pili: Je, Kwa kuwa mgogoro huu umekuwa wa muda mrefu, Serikali haioni iko haja sasa wa kufikia mwisho na Mheshimiwa Naibu Waziri sasa tuambatane tukakae na wananchi wale tumalize mgogoro huu ili kesi hii iishe na wananchi waendelee na maisha yao; na kwa kuzingatia kwamba wananchi hawa ni wema sana, walitupa kura nydingi za Chama cha Mapinduzi na pia Diwani aliyeko pale alipita bila kupingwa? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Kwa kweli niwaambie wananchi wa Hai, sasa Mbunge mnaye. Maana kabla ya hapo walikuwa na Mbunge anazurura zurura tu kila mahali, haulizi maswali Bungeni, haeleweki eleweki; lakini sasa Hai hongereni sana. Mbunge mnaye kabisa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofii*)

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu na hapo nyuma kulikuwa kuna changamoto kwamba vijiji vilipima maeneo yao yakaingia katikati ya uwanja ambao tayari ulikuwa una hati. Changamoto hiyo tayari tulishairekebisha na zile ramani za vijiji vile zilifutwa ili ramani ya uwanja wa ndege ibaki na ndivyo ilivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kweli kwamba uwanja ule ni mkubwa lakini uwanja ule ultolewa vile na muasisi wa Taifa

baba yetu Julius Kambarage Nyerere na kile kiwanja kina mipango mahsusini ya kuweka viwanda vya kitalii na viwanda vinavyohusiana na viwanja vya ndege. Biashara zote za viwanda vya ndege, sasa hivi pale kuna mpango wa kuanzisha *aviation school* ambapo Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kimekwishajidhatiti na vile vile tuna mpango na hawa watu wa *TAA* ili kuweka majengo ya kuhifadhi mipango ambayo imepangwa pale.

Kwa hiyo ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na wale wananchi wa Hai wajipange kuanzisha biashara zinazohusiana na viwanja vya ndege kuliko kupanga kuugawa uwanja wa ndege ule kwenda katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, ni kweli kwamba Wizara yangu iko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda pale kuongea na kumaliza suala hilo kwani tumejipanga mwaka huu tuweze kufika pale kufanya tathmini na kumaliza suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mhandisi Leonard Chamuriho. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii linalofuata, lakini bado tuko Wizara hii hii na swalii linalofuata ni la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, Mheshimiwa Shigongo tafadhali.

Na. 65

Kutoza Wananchi Fedha za Kuingia na Kutoka Bandarini -Buchosa

MHE. ERIC J. SHIGONGO aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaacha kuwatoza shilingi 600 wakati wa kuingia na kutoka Bandarini wananchi wa Visiwa vya Kasalazi, Yozu, Gembela na Soswa katika Jimbo la Buchosa kwa kisingizio cha uwekezaji?

SPIKA: Wasukuma hawa wanachekesha, wana sema eti wana bandari Buchosa huko. Majibu ya swali la Bandari za Buchosa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwango cha tozo ya abiria wanaopita katika bandari ndogo zilizopo katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa bahari na maziwa ni shilingi 600 kama ambavyo imeainishwa katika kitabu cha tozo cha Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*). Hata hivyo, *TPA* baada ya kupokea malalamiko ya wadau mbalimbali kuhusu tozo hizo, imeanza kuchukua hatua za kufanya marejeo ya tozo hizo kwa bandari zote ndogo nchini kwa kushirikisha wadau katika maeneo mbalimbali. Vikao vya wadau ikiwemo wananchi katika Visiwa vya Kasalazi, Yozu, Gembela na Soswa vitafanyika kwa lengo la kupokea maoni yao kabla ya kuidhinishwa kwa tozo mpya. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Shigongo, swali la nyongeza.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala hili limekuwa la muda mrefu sana, lina jumla ya miaka kama minne au mitano, wananchi wanaendelea kupata mateso ya kulipa 600 wakati wa kuingia na 600 wakati wa kutoka, wananchi hawa maskini. Mimi binafsi nimeshasumbuka sana suala hili nimezungumza na Mheshimiwa Kakoko, nimezungumza na Mheshimiwa Abood, nimezungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu amenijibu na barua ninayo hapa ya kwamba amewaaagiza *TPA* washughulikie suala hili mara moja. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutoa tamko hapa kwamba tozo hizo zitapunguzwa mara moja ili wananchi waweze kuondoka kwenye mateso? (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, kupunguza tozo za Bandari za Buchosa.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ilivyojibiwa katika swali la msingi tozo hizo zinatolewa kwa mujibu wa sheria na zinafuata *tariff book* ambayo ni ya *TPA*. kama ambavyo imejibiwa katika jibu la msingi, sasa hivi tunafanya majadiliano ili tuweze kupunguza tozo hizo kulingana na malalamiko ya wananchi ili tuweze kwenda kisheria. Hatuwezi kupunguza sasa hivi kwani ndiyo mambo haya haya ambayo yatazuka tena katika Ripoti ya *CAG* kwamba tumetoza kinyume na *Tariff Book*. Kwa hiyo, tunafanya marejeo hayo na tutakapoyakamilisha, tutawasiliana na vijiji vyote kama vilivyotajwa pale katika Visiwa vya Kasalazi, Yozu, Gembela watashirikishwa katika kikao cha wadau ili tuweze kupata tozo muafaka ambazo zitakubalika kwa wananchi wote. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Naishukuru sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuunganisha wilaya na wilaya, mikoa na mikoa. Hata hivyo, ipo barabara inayoanzia Njuki – Ilongero – Kidarafa hadi Hydom. Barabara hii nimekuwa nikiuilizia mara kwa mara ambayo inaunganisha Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Singida. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa Mikoa ya Manyara na Singida? Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swalı la nyongeza la Mheshimiwa Aysha Mattembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tupo kwenye Mpango wa Bajeti ya Mwaka mpya wa Fedha. Naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili Tukufu kipindi cha maswali tukae pamoja tuone utaratibu uliotumika. Kwa sababu, barabara zinaibuliwa kutoka ngazi ya Mkoa kuja ngazi ya Wizara, basi kama barabara hizo ambazo zina mahitaji muhimu sana katika maeneo uliyoyasema hazikuingizwa kwenye Mpango wa Bajeti mwaka huu tujipange kwa Mwaka wa Fedha ujao. Wananchi wa pale wavute subira, tupo tayari kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba maisha yao na bidhaa zao zinapata nafasi na gherama nafuu kusafirisha ili kuweza kubadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tuendelee na Wizara ya Madini sasa Waheshimiwa Wabunge. Swalı linaulizwa na Mheshimiwa Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Kyela.

Na. 66

Kufufua Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaufufua Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira?

(b) Je, ni lini baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Kiwira watalipwa stahiki zao baada ya mgodi huo kufungwa?

SPIKA: Majibu ya swalı hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Jimbo la Kyela, yenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mgodi wa makaa ya Mawe wa Kiwira ulikabidhiwa Serikalini kupitia Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) mwaka 2013 kwa lengo la kuuendeleza. *STAMICO* kwa kushirikiana na *TANESCO* wanaendelea na mpango wa pamoja wa muda mrefu wa kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme zaidi ya *megawatt* 200 utakaotumia makaa ya mawe yatakayozalishwa katika mgodi huo. Makubaliano ya ushirikiano baina ya *STAMICO* na *TANESCO* yako hatua za mwisho kabla ya kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kisha kusainiwa.

Mheshimiwa Spika, tayari timu ya wataalam wa *STAMICO* na *TANESCO* imetembelea eneo la mradi kwa lengo la kutambua mahitaji halisi ya uendelezaji wa mradi huo na *STAMICO* imeanza kufanya ukarabati wa miundombinu ya mgodi wa chini ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uzalishaji mkubwa kwa ajili ya mahitaji ya mitambo ya kuzalisha umeme.

Aidha, kutokana na ukubwa wa mradi, Mashirika haya yanaendelea na jithada za kutafuta fedha na uwekezaji kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo pamoja na kuihusisha Serikali yenye kuona uwezekano wa kutengewa sehemu ya bajeti kwa ajili ya uwekezaji huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kipindi ambacho mgodi unakabidhiwa kwa *STAMICO* kulikuwa na malimbikizo ya madeni yanayofikia shilingi bilioni 1.02 ikiwa ni stahiki na mapunjo ya wafanyakazi takriban 893 waliopunguzwa. Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na shirika tayari imehakiki deni hilo kwa mara nyingine mwezi Juni, 2019 na taratibu za ulipwaji wa madeni hayo zinaratibiwa na Hazina. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Jumbe, Mbunge wa Kyela nimekuona, swali la nyongeza.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Leo ningekuwa CAG kwa majibu haya ningetoa hati hafifu. Haiwezekani leo tunazungumza mambo ya 2013 wakati aliyekuwa Waziri Mheshimiwa Mizengo Pinda mwaka tarehe 8 Januari, 2015 alisema kwamba sasa wataanza utaratibu wa kupeleka mgodi huu *TANESCO* na kupeleka kwa *STAMICO*, lakini kumekuwa na ahadi hizi nyingi zikiendelea. Wananchi wa Wilaya ya Kyela, Wilaya ya Rungwe na Ileje wanachotaka ni kujua tarehe mahsus ambayo suala hili linaenda kutekelezeka, la kuanza mgodi hiyo ni. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kumekuwa na matamko mengi ya malipo haya. Tarehe 29 Novemba, 2018 walisema *STAMICO* sasa imesha-save hela ya Serikali, lakini tarehe 12 Septemba aliyekuwa Naibu Waziri Mheshimiwa Nyongo alisema *TRA* wanawatafuta hawa *TAN Power* ambaao walisema...

SPIKA: Sasa swali!

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, ndiyo naomba nipate tarehe ya kulipwa ili na mimi nikienda Jimboni nikawaambie wananchi kwamba Serikali sasa inalipa pesa. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Yaani Mheshimiwa Jumbe unampa Profesa hati hafifu? Profesa majibu ya swali hilo. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jambo hili limekuwa ni la muda mrefu kama ambavyo tarehe ya kukabidhiwa mgodi kwenda Serikalini imekuwa ya mwaka 2013, lakini pia tujue kwamba uwekezaji katika mgodi ni

uwekezaji unaohitaji fedha. Katika kipindi hiki ni kweli kwamba pia Shirika letu la *STAMICO* limekuwa likipitia maboresho makubwa ya kulipa uwezo wa kuendelea kufanya shughuli zake. Kwa hiyo, ahadi hizi ambazo zimekuwa ni za muda mrefu, tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa jinsi ambavyo shirika limeboreshwa na kwa jinsi ambavyo Serikali imejithahidi kuwa inalipa mapunjo hasa ya muda mrefu, hatimaye tumewaelekeza Shirika letu la *STAMICO* pamoja na *TANESCO* kwamba hata sisi hatuko tayari kuendelea kuchukua fedheha ya kuambiwa tuna hati chafu, badala yake wafanye jitihada zinazowezekana ili waweze kupata mtaji na hatimaye mgodi wa Kyela uweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mustakabali huo, naendelea kuwaagiza *STAMICO* pamoja na *TANESCO* kwamba, wakatafute fedha na ndivyo tulivyoongea kwamba sasa ifikie mahali watafute fedha, kama ni kutenga bajeti, kama ni kwa ushirika na *partners* wafanye hivyo ili hatimaye jambo hili liweze kufikia mwisho. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mwandabila.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali langu la nyongeza. Tunafahamu kabisa mradi wa *STAMICO* ni mradi ambao una maslahi kwa wananchi wa Kyela, Rungwe na Ileje. Ileje iko Mkoa wa Songwe. Ningependa kuona mradi huu unafanya kazi mapema sana.

Swali langu liko hapa, majengo yaliyojengwa eneo lile ni majengo mazuri ambayo ni kwa ajili ya ofisi na makazi ya watumishi. Makazi yale, siku hadi siku yameendelea kuharibika.

Sasa natamani kujua, je, ni nini dhamira ya Serikali katika kuendeleza haya majengo yasiendelee kuharibika na kufanyaika magofu huku wakati tukiendelea kusubiri huo mradi kufanya kazi? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Profesa Shukurani Manya, majibu kuhusu hayo majengo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mbunge, kuhusu ukarabati wa majengo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema *STAMICO* imeanza ukarabati wa mgodi wa chini kama sehemu ya maandalizi na ili tuweze kuanza mgodi ni pamoja na maandalizi ya nyumba za *staff*.

Kwa hiyo, nipende kumhakikishia Mbunge tu kwamba jambo hili pia la ukarabati wa nyumba kama maandalizi ya mahali ambapo *staff* watakaoingia katika mgodi pia litakwenda kutekelezwa na tutawaagiza *STAMICO* kwamba wafanye mambo haya kwa pamoja ili pia tusiendelee kupata hasara ya nyumba ambazo hatimaye tunaweza tukahitaji kujenga nyumba mpya kumbe tungeweza kuzihifadhi hizi kwa ajili ya mkakati wa baadaye.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Tunaendelea na Viwanda na Biashara, swali la Mbunge wa Bagamayo Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, uliza swali lako.

Na. 67

Kulipwa Fidia kwa Wananchi wa Zinga Waliopitiwa na Mradi wa EPZ Bagamoyo

MHE. MUHARAMI S. MKENGE aliuliza: -

Maeneo ya wananchi wa Kata ya Zinga, Kitongoji cha Mlingotini na Pande, yalichukuliwa na Serikali ili kupisha Mradi wa EPZ lakin hawajalipwa fidia:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhamari Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bagamoyo *Special Economic Zone* ni moja ya miradi wa kielelezo na kimkakati ambao umepewa kipaumbele nchini na umeainishwa katika Mpango wa Miaka Mitano wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu na katika llani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mradi huo, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za uendelezaji ikiwemo kulipa fidia kwa baadhi ya watu waliopisha mradi kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo lilifanyiwa tathmini ni hekta 5,743 ambazo fidia ilikuwa ilipwe jumla ya bilioni 58.5 na katika hekta hizo zilizolipwa fidia ni hekta 2,339.6 ambazo jumla ya fidia iliyolipwa ni takriban bilioni 26.6. Serikali inatambua uwepo wa maeneo yanayodaiwa fidia katika eneo maalum la kiuchumi la Bagamoyo yakiwemo maeneo yaliyoko katika Vitongoji vya Mlingotini na Pande katika Kata ya Zinga, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza azma ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, Serikali inaendelea kuangalia namna bora zaidi ya utwaaji wa maeneo ya namna hii na kuweka utaratibu wa fidia wenye kuleta tija ya uwekezaji kwa Taifa kwa ujumla. Taratibu hizo zitahusisha ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotathminiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali na fidia hufanya kwa mujibu wa Sheria. Pia utaratibu huo unalenga kuyamiliki na kuyaendeleza maeneo hayo ili yawe na tija kwa Taifa letu. Hivyo, fidia kwa wananchi ambao bado wanadai katika eneo hilo la Mlingotini na Pande itafanyaika

kwa kuzingatia utaratibu hu una Serikali italipa wadai hao haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, mnataka kuwatoa watu wa Mlingotini mtaweza? Mlingotini pazito pale. (*Kicheko*)

Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Mkenge, swalilako tafadhali.

MHE. MUHARAMI S. MKENGE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuzungumza kitu kimoja:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni mwaka wa 12 toka fidia ya mwanzo ilipofanyika na wengine mpaka sasa bado hawajafanyiwa fidia. Na lile eneo Serikali ilishatengeneza GN tayari kiasi kwamba, wananchi wanashindwa kufanya tena chochote katika maeneo yale. Na maeneo yamekuwa mapori, yamekuwa usumbufu, wafugaji wameingia pale inakuwa mgogoro kati ya wakulima na wafugaji. Je, Serikali inaweza ikafanya mpango wowote kuwarudishia maeneo yao hawa wahusika kama hawatakuwa tayari?

Mheshimiwa Spika, swalilaili; je, kwa haya majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari mimi na yeye tuongozane bagamoyo tukafanye mukutano wa hadhara Mlingotini, ili awaridhishe wananchi wa kule kwa hili janga ambalo lilewapata kwa miaka 12 sasa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, Ndugu Exaud Silaoneka Kigahe, majibu tafadhali. Muongozane kwenda Mlingotini, sijui kama mtatoka salama huko?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza fidia ya mwisho iliyolipwa kwa wananchi hao ilikuwa ni mwaka wa fedha 2017/2018 kwa hiyo, sio kweli kwamba, ni zaidi ya miaka 12 katika malipo ya mwisho yaliyolipwa fidia kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya maendelezo, hasa kwa sekta ya viwanda na uwekezaji mwingine ni muhimu sana. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa mkenge kwamba, si vema maeneo ambayo yameashaainishwa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda na uwekezaji mwingine kurudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali inaendelea kuona umuhimu wa kulipa fidia hizo haraka iwezekanavyo, ili uendelezwaji wa maeneo hayo uweze kufanyika. Lakini pili tunaendelea kushauri Serikali za Mikoa na halmashauri kuona namna bora ya kuyamiliki maeneo ambayo Serikali Kuu kwa maana ya kupitia EPZA tutakuwa bado tunashindwa kuyalipa, ili nia ya Serikali ya kuwa na maeneo maalum ya uwekezaji na hasa kwa ajili ya maendeleo ya viwanda yaendelee kuwepo kwa ajili ya maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mheshimiwa Mkenge niko tayari, tutaongozana na wewe na wataalamu wetu kutoka EPZA ili kuweza kuongea na wananchi wa Mlingotini kwa ajili ya kuona namna bora ya kuendeleza, hasa kulipa fidia maeneo haya ambayo yametwaliwa.

SPIKA: Ahsante sana. bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, uliza swali lako.

Na. 68

**Kuendeleza Kilimo cha Miwa na Kujenga Kiwanda
cha Sukari Kalambo na Nkasi**

MHE. IRENE A. NDYAMKAMA aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuendeleza kilimo cha zao la miwa kwa Wananchi wa Wilaya ya Kalambo na Nkasi na baadae kujenga kiwanda cha sukari ambacho

kitatoa ajira kwa Vijana na Wanawake ndani ya Mkoa wa Rukwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, ndugu Exaud Silaoneka Kigahe.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sukari ni kati ya bidhaa muhimu sana nchini na matumizi yake kwa maana ya majumbani na viwandani. Kwa sasa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 320,000 kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya majumbani na wakati mahitaji halisi tani 485,000 na mahitaji ya sukari kwa matumizi ya viwandani ni tani 145,000. Pengo la takriban tani 165,000 kwa ajili ya matumizi ya majumbani na tani 145,000 kwa matumizi ya viwandani huagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua ongezeko la mahitaji ya sukari lisiloendana na uwezo wa uzalishaji wa sukari nchini, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika miradi mipyä na upanuzi ya uzalishaji wa mashamba ya miwa uzalishaji katika viwanda vya sukari ikiwemo viwanda vikubwa na vidogo vilivyopo nchini. Mwaka 2015, Bodi ya Sukari Tanzania ilifanya utafiti na kubaini uwepo wa maeneo yanayofaa kwa ajili ya wakulima wadogo na wa kati kwa ajili ya kilimo cha miwa na hatimaye tuweze kuongeza uzalishaji wa sukari. Aidha, Mkoa wa Rukwa ulibainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo na viwanda ili tukipata wawekezaji katika sekta ya sukari waweze kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kitabu cha Mwongozo wa Uwekezaji cha Mkoa wa Rukwa, Mkoa umetenga jumla ya hekta 20 na hekta 15.65 katika Wilaya ya Kalambo na Nkasi Mtawalia kwa ajili ya uwekezaji wa

kilimo cha miwa. Hivyo, Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha zao la miwa katika maeneo yote yenye sifa za uzalishaji ikiwemo Wilaya ya Kalambo na Nkasi. Pia tunaendelea kuhamasisha kujenga viwanda kwa ajili ya kuchakata miwa ili kukidhi mahitaji ya sukari na pia kutoa ajira kwa Watanzania. Vile vile, Serikali kuitia Bodi ya Sukari inawahamasisha wawekezaji wakubwa na wadogo kuzalisha sukari ili kukidhi mahitaji yaliyopo hapa nchini.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa Irene.

MHE. IRENE A. NDYAMKAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, ni lini Serikali inawahakikishia wananchi wa Mkoa wa Rukwa itawatafutia wawekezaji na kuwekeza kiwanda hicho cha sukari mkoani hapo?

Mheshimiwa Spika, swali jingine, kwa kuwa, Mkoa wa Rukwa ni tatu bora kwa kilimo nchini Tanzania. Ni lini Serikali itaangalia tena mkoa huu kwa kuwekeza viwanda vingine?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Kigahe.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaendelea na kuhamasisha uwekezaji au viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mpango wa miaka mitano ambao umeuona moja ya maeneo muhimu sana ambayo tumeainisha ni kuhakikisha tunatafuta wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, ikiwemo miwa na mazao mengine ambayo yanalamwa katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, na ye ye ni mmoja wa wadau muhimu sana ambao tunaweza tukashirikiana ili kuhakikisha tunawekeza viwanda vidogovidogo vya kati na vikubwa kwa

ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Rukwa. Lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, muda wowote Wizara iko tayari kushirikiana na kukushauri na kushauriana na wawekezaji wengine, lakini pia kuangalia vivutio maalum ambavyo vitasababisha wawekezaji wengi kuwekeza katika mikoa yetu ikiwemo Mkoa wa Rukwa.

SPIKA: Mheshimiwa Dennis Londo, nilikuona.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalı la nyongeza kwa kuwa Serikali inakiri kwamba, uwezo wetu wa kuzalisha sukari ndani hautoshelezi mahitaji ya ndani na tunaagiza kiasi cha takribani tani tani zaidi ya laki moja za sukari kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa, miwa ya wakulima katika Jimbo la Mikumi ni zaidi ya tani laki nne zinateketea mashambani. Na kwa kuwa, kiwanda cha Ilovo wakati wanauziwa walikuwa na masharti ya kuongeza upanuzi wa kiwanda hicho na Serikali inasuasua. Je, ni lini Serikali inaenda kuhakikisha kwamba, upanuzi wa kiwanda hicho unakamilika na mazao ya wakulima ya miwa yanaenda kupata soko la uhakika?

SPIKA: Majibu ya swalı hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Exhaud Kigahe. Kila wakati mnalaumiwa mnasuasua, tatizo ni nin?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema mahitaji ya sukari hapa nchini ni makubwa ukilinganisha na uwezo wetu wa uzalishaji wa ndani. Suala la wananchi kukosa soko katika Wilaya ya Kilombero ni moja ya maeneo muhimu sana ambayo sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara tumeshayaona. Na moja ya mikakati ya Wizara ya Viwanda ni kuona namna gani sasa tunaongeza uchakataji wa miwa ambayo inakosa soko katika viwanda vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (*TEMDO*), tunaenda kuleta mitambo

midogo ambayo itaweza kusaidia kuchakata miwa kwa wakulima wadogowadogo ambao wanakosa soko katika viwanda vikubwa kwa sasa, ikiwemo maeneo ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, kuhisiana na viwanda vilivyopo tayari kuna mipango maalum, kwanza kuhamasisha kuongeza uwekezaji kwa kuongeza uzalishaji katika viwanda hivyo, lakini pia kuhakikisha na wao wanaingia sasa, kuna kitu tunaita *quail farming*, ili waweze kusaidiana na wakulima wadogowadogo kuzalisha miwa mingi, lakini pia na wao wenye viwanda kuwa na mashamba mengine ambayo yatatosheleza mahitaji ya uzalishaji katika viwanda vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza tutahakikisha miwa ambayo inakosa soko tunaleta hiyo mitambo midogo ambayo itachakata miwa hiyo, ili angalao wakulima wale waweze kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, la pili. Tunaendelea kushirikiana na viwanda vilivyopo ili kuhakikisha wanahamasisha wakulima wadogowadogo kwa maana ya kuingia *quail farming* katika viwanda vyao.

SPIKA: Mheshimiwa Kigahe hujamuelewa kabisa Mheshimiwa Londo, yaani pale miwa ni mingi *solution* yake sio viwanda vidogovidogo. Ilovo wako tayari kuwekeza kiwanda kingine kikubwa kwa muda mrefu, anachosema Mheshimiwa Londo ninyi Wizara mnavutavuta miguu, tatizo ni nini? Na siasa za pale ni ngumu sana, nilienda kupiga debe huko matatizo ni makubwa sana wananchi wanaotupigia kura wafanyeje?

Iko siku hawatatupigia kura. Itakuwa ni shida sana kushinda maeneo ya Kilombero kama hamuwasikilizi hiki wanachokisema. Wananchi wameshalima miwa, wanataka kiwanda wauze wapate maendeleo yao. Tufanikishe kupatikana kiwanda kikubwa kuliko vilivyopo hivi sasa pale, ili miwa yote iweze kununuliwa. Lakini viwanda vidogovidogo ndio kama Kongwa na kwingineko wanaolimalima vimiwa

kidogokidogo hivi, lakini hawa jamaa wana miwa mingi sana na kuna shida kweli pale ya miwa.

Kuna vyama vyaa ushirika pale, yaani matatizo ni makubwa, ili uuze miwa lazima ufanye mpango, uliwe hivi na nini, unachoma unategemea ndio uvune uende ukauze, ukishachoma hawanunui miwa yako. Na unajua iwa ukishachoma ndio umeliwa inaharibika, na kadhalika, yaani kuna matatizo makubwa. (*Makofi*)

Nawashauri Viwanda na Biashara mkatembelee kule mkutane na wale muongee muone namna gani ya kurekebisha jambo hili kwasababu ni uchumi mkubwa. Miwa tayari tunayo na sukari tunaihitaji. Waheshimiwa maswali ya leo yameisha tena kwa wakati. Nawashukuruni sana.

Sasa wageni tunao wageni tunao wageni 17 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wakiongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Tixon Tuyangine Nzuda na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji Prof. Godius Kahyarara. Pia wamo Manaibu Katibu Wakuu wawili ambao ni Prof. Jamal Katundu na Ndugu Caspary Muya. (*Makofi*)

Karibuni sana Makatibu Wakuu na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kweli ninyi ndio watu ambao tunafanya kazi kwa karibu sana na Bunge kwasababu ndio waratibu upande wa Serikali. Tunawahakikishieni kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu tutawapa kila aina ya ushirikiano, asanteni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wako wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara, ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Abdallah Mwinyi. Wako wapi hawa wafanyabiashara, wako pale, karibuni sana. (*Makofi*)

Ni wewe mwenyewe au Mwenyekiti ni mwingine? Ni mwingine? Ndugu Abdallah Mwinyi yuko wapi asimame,

anyoshe mkono? Ooh! Ahsante sana. Asante, hongera sana Mwenyekiti wa wafanyabiashara. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, ambaao ni wadau wa mitindo kutoka Jijini Dar-es-Salaam wakiongozwa na Ndugu Flaviana Matata. Wadau wa mitindo, karibuni sana. (*Makofi*)

Flaviana yuko wapi? *Okey, ahsante. Karibu sana Bungeni.* (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima ambaao ni jamaa zake kutoka Visiwa vya Triidad na Tobago na Afrika Kusini ambaao ni *Bishop Ronald Martin De Veteuil* wa Trindad na Tobago na Prof, Vusumuzi Nehemiah Sibya kutoka Afrika Kusini. *Those from Trinidad and Tobago and South Africa?* Hawapo, Askofu hawapo bwana? Hawapo wageni wako hapa?

Wageni watano wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaao ni Wanamaombi kutoka Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya. Wanamaombi karibuni sana.Na hapohapo nitangaze kwamba, Wabunge wote na Wafanyakazi wote wa Bunge na wageni ambaao mko maeneo ya Bunge mnakaribishwa katika *Chapel* ya Bunge saa saba mchana leo, baada ya kusitisha shughuli za Bunge mchana ambapo tutakuwa na *session* maalum ya maombi. Na tangazo hili linaletwa na Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa *Chapel* ya Bunge. Mtumishi wa Mungu, Mheshimiwa Askofu Gwajima, leo atahudumu katika ibada hiyo.

Wageni watano wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaao ni Watumishi wa Mungu kutoka Makanisa mbalimbali Mkoani Dodoma wakiongozwa na Ndugu Anna Maila. Karibuni sana Wachungaji na Wanamaombi, mliombee Taifa, mliombee Bunge lenu, muwaombee Watanzania na kubwa zaidi mumuombee Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Halima Mdee ambao ni Ndugu Amini Mushi na Ndugu Haruna Lota kutoka Taasisi ya *TWARIQATAL QADIRAYA JAILANIYA ARAZA QUIYA TANZANIA* yenye makao makuu Jijini Dar-es-Salaam. Karibuni sana ma-Sheikh. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, Mbunge, ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Malela, Tuangoma, Jijini Dar-es-Salaam, Ndugu Oswin Mkinga. Karibu sana. Upande wa wageni nimemaliza. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge jana tulikuwa tumeagiza kwamba, pafanyike uchaguzi wa Viongozi wa *Bunge Sports Club*. Ninayo heshima kuwatangazia matokeo ya uchaguzi huo wa *Bunge Sports Club* ambapo nafasi ya Mwenyekiti aliyeshinda ni Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. (*Makofi*)

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti aliyeshinda ni Ndugu Esther Nicholas Matiko. Meneja wa Timu aliyechaguliwa ni Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, ahsante yuko kule. Nafasi ya Wajumbe watano wa Kamati ya Utendaji ni Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Aeshi Hilaly, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Rose Tweve. (*Makofi*)

Basi kuitia uongozi huo tunatarajia kupata mipango na *programs* mbalimbali za *Bunge Sports Club*. Na kwa sababu huwa tuna kabajeti ketu pia Bunge kanakohusiana na *Bunge Sports Club* basi mkatazame mtupe ushauri namna gani ya kwenda vizuri zaidi kwasababu, kuitia *Bunge Sports Club* inatusaidia sana katika kujenga mahusiano makubwa sana na wananchi na kwa kweli ni jambo la afya sana kwa Waheshimiwa Wabunge. *Club* hii ni yetu wote na ni Wabunge na Wafanyakazi wa Bunge kwa pamoja. (*Makofi*)

Basi baada ya hapo tuendelee, Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama Katibu alivyokwishakutoa Mwongozo wake ni kwamba tunakwenda kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka unaokuja 2021/2022 kuitia mjadala utakaofuata ambapo sasa naomba nimuite Mto Hoja ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Shukrani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zillizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Mfuko wa Bunge na Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2020/2021 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa mwaka ujao 2021/2022. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na hotuba hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na mwelekeo wake kwa mwaka 2021/2022 tukiwa na siha njema.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa huu ni Mkutano wa Tatu wa Bunge la 12. Aidha, ni Mkutano wa kwanza wa Bunge la Bajeti tangu kuzinduliwa kwa Bunge hili tarehe 13 Novemba, 2020. Mkutano huu, unafanyika wakati

ambao Tanzania imepitia majuma kadhaa ya huzuni, majonzi makubwa na Maombolezo ya Kitaifa kufuatia kifo cha Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie tena nafasi hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Bunge lako Tukufu, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi wetu mpPENDWA. Aidha, naishukuru Kamati ya Kitaifa ya kuratibu Mazishi kwa kujitoa kwao usiku na mchana ili kufanikisha taratibu zote muhimu za maziko mazishi sambamba na kuhakikisha kuwa kiongozi wetu anapewa heshima zote za mwisho hadi alipolazwa kwenye nyumba yake ya milele.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kutoa wito kwa Watanzania wenzangu kuwa tuendelee kushikamana, kushirikiana, kupendana na kuchapa kazi. Aidha kwa upande wetu Waheshimiwa Wabunge, Viongozi na Watendaji wote, nasi hatuna budi kuendeleza ushirikiano, kuchapa kazi na kuwatumikia ipasavyo Watanzania kwa kulinda na kutetea maslahi mapana ya nchi yetu. Hii ndiyo njia sahihi ya kumuenzi mpPENDWA wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sote tutakumbuka kuwa msiba wa kiongozi wa nchi ulikuja wakati ambao Taifa lilikuwa bado halijasahau tukio la tarehe 17 Februari, 2021 wakati Taifa lilipopokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Chama cha ACTWazalendo. Maalim Seif atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa alioutoa kwa chama chake, watu wa Zanzibar na Taifa zima kwa ujumla, hususan kuititia Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, tuliondokewa pia na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Balozi John

William Herbert Kijazi. Lakini pia Mheshimiwa Balozi Kijazi atakumbukwa kwa utumishi wake uliotukuka wakati akitumikia Serikali kwenye nyadhifa mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jana tarehe 12 Aprili, 2021 nchi yetu imeanza kumbukizi ya miaka 37 ya kifo cha Hayati Edward Moringe Sokoine aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufariki dunia tarehe 12 Aprili, 1984, Watanzania tutaendelea kumkumbuka na kumuenzi Jemedari huyo kwa uzalendo wake, uhodari wake na uchapakazi wake wakati wote wa Uhai wake.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kuwa Taifa limepoteza watu muhimu waliota mchango mkubwa katika uongozi, maendeleo, ustawi wa Taifa letu sambamba na kuimarisha umaja, amani na mshikamano wa kitaifa. Hivyo, tuendelee kuenzi na kujifunza mambo mazuri yaliyoachwa na viongozi wetu hao, huku tukimuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Spika, mukano huu wa tatu wa Bunge la 12 ni wa Bajeti ya Serikali, nami naanzisha kusoma Bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/2022. Na kabla sijaendelea na hotuba yangu hii naomba sana uruhusu tusimame walau kwa dakika moja kwa lengo la kuwaombea marehemu wetu wote ili Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani.

*(Wabunge walismama kwa dakika moja ili kuwaombea
Marehemu wote)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wetu peponi amina, tukae.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kushika nafasi ya kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tena

mwana mama shupavu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa Rais wetu nguvu, ulinzi, afya na kila lillo heri katika kuwatumikia Watanzania. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia, Mheshimiwa Philip Isidor Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupitishwa kwa nguvu na Waheshimiwa Wabunge kwa asilimia 100 na Waheshimiwa Wabunge. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Sharif Kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa mukutano huu wa bajeti ni wa kwanza kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa msingi huo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuitumie vyema fursa hii kutoa michango itakayosaidia Serikali kutekeleza kikamilifu vipaumbele vivilvyoainishwa kwenye Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022 kwa maslahi ya taifa. Serikali kwa upande wake, itaendelea kuhestimu, kuthamini na kuifanyia kazi michango yenu Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kushughulikia kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kuonesha umahiri na uwezo mkubwa katika kusimamia shughuli za Bunge. Hivyo basi, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu hususan wale walioingia katika Bunge hili kwa mara ya kwanza ili tutumie vizuri usoefu wenu katika kujifunza namna bora ya kuisimamia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nawashukuru pia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijiji kwa kutoa mchango mkubwa wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge. Aidha, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge ambao kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wenu utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano mlionipatia wakati nikitekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kutekeleza majukumu yenu vizuri kwa weledi mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza kazi zake kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Pia Mheshimiwa Geofrey Idelphonce Mwambe, Mbunge wa Masasi Mjini na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Mheshimiwa William Tate Olenasha Mbunge wa Ngorongoro na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Mheshimiwa Paschal Patrobas Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu

Kazi, Vijana na Ajira pamoja na Mheshimiwa Ummey Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikiwa watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nataka nitumie nafasi hii sana kumshukuru bwana Tixon Tuyangine Nzunda, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo, Wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia wakati nikitekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru waliokuwa Makatibu Wakuu, Bibi Dorothy Aidan Mwaluko na bwana Andrew Wilson Massawe kwa kazi nzuri walioifanya wakati wote wakiwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia natoa pongezi kwa Profesa Godius Kahyarara kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Profesa Jamal Adam Katundu na Bwana Kaspar Kaspar Mmuya kwa kuteuliwa kuwa Naibu Makatibu Wakuu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, hongereni sana! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo wakiwemo nchi rafiki, taasisi na mashirika ya kimataifa, madhehebu ya dini na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, kwa kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali kujenga uchumi wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Mchango wao umekuwa muhimu kwa kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo kulingana na mipango tulijojiwekea.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya bajeti ninayowasilisha leo ni sehemu ya utekelezaji wa yale yaliyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Makadirio hayo, yamezingatia ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni na katika uzinduzi wa Bunge hili tarehe 13 Novemba, 2020. Lakini vilevile, makadirio hayo ya mapato na matumizi yamezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa kutekeleza Dira ya Taifa

ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo, matumizi ya fedha za umma sambamba na uwajibikaji. Serikali itatumia rasilimali chache zilizopo katika shughuli za uzalishaji mali na kuongeza tija ili kuchochaea ukuaji wa haraka wa uchumi na maendeleo ya watu. Aidha, Serikali itaimarisha usimamizi na utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha kuwa inakuwa na viwango vinavyoendana na uthamani wa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, ningependa kuwashakikisha wananchi na Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan ile ya kimkakati na inayolenga kuboresha huduma pamoja na kuboresha maisha ya wananchi. Serikali itahakikisha ahadi zote zilizotoa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan na aliyekuwa Rais wetu, hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli zinatekelezwa sambamba na llani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021. Tarehe 30 Juni 2021 tutahitimisha utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliokuwa umeanza mwaka 2016/2017 na kuishia mwaka 2020/2021. Aidha, kuanzia Julai mosi 2021, Serikali itanza kutekeleza Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano mingine itakayoanza mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 wenyewe dhima ya Kujenga Uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, Mpango huo ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Dira hiyo, ina lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati na hali bora ya maisha ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, hatunabudi kujipongeza kwa nchi yetu kufanikiwa kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati

miaka mitano kabla ya muda tuliokuwa tumejiwekea. Kuingia katika uchumi wa kati ni kiashirio cha kuongezeka kwa uwezo wa Taifa kugharamia huduma muhimu kwa wananchi sambamba na uwezo wa wananchi kugharamia mahitaji yao. Natoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kulinda na kuendeleza mafanikio tuliyoyapata. (Makof)

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021, Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi trilioni 34.88, kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 22.1 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.78 ilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021 umekuwa wa mafanikio makubwa. Hivyo basi, naomba japo kwa uchache nilieleze Bunge lako Tukufu na Watanzania wote baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mafanikio hayo ni pamoja na Serikali kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo imekuwa na mwendelezo kutokana na kuhitaji muda wa zaidi ya miezi 12. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo, moja Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa *Standard Gauge Railway* ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kilometra 300 umefikia asilimia 90.34 na kipande cha Morogoro – Makutupora chenye urefu wa kilometra 422 umefikia asilimia 58.

Mheshimiwa Spika, aidha, tayari Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa kipande cha Mwanza - Isaka kilometra 341 wenyе thamani ya Shilingi trilioni 3.07 na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora kilometra 294 na Tabora – Isaka kilometra 133 na hapo baadaye kujenga njia ya Tabora – Kaliua – Kigoma kilometra 411 na Kaliua – Mpanda kilometra 207. Na Mpango wetu ni kufika mpaka kwenye bandari ya Kalema, Katika kipindi cha

Julai 2020 hadi Machi 2021 jumla ya shilingi bilioni 596.8 zimetumika katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, mbili, Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere *Megawatt* 2,115, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 45 hadi Machi 2021 ambapo Shilingi triliuni 2.1 zimeshatumika na ajira zaidi ya 7,000 zimezalishwa miongoni mwa hao asilimia 90 ni Watanzania ambao pia wanaendelea kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu Usambazaji wa Umeme Vijiji kupitia Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijiji na makao makuu ya wilaya *REA III*. Hadi Februari, 2021 jumla ya vijiji 10,294 kati ya vijiji 12,317 sawa na asilimia 83.3 vilikuwa vimeunganishwa umeme ambapo Shilingi bilioni 323.7 zimeshatumika. Kwa sasa tumebakia na vijiji 1,974. Usambazaji wa umeme katika maeneo hayo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha hali ya biashara za wananchi matumizi makubwa ya umeme badala ya kuni na hivyo kujongezea kipato. Lengo la Serikali ni kukamilisha usambazaji umeme katika vijiji vyote hadi visiwani na kwenye vitongoji vikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nne, kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwenye maziwa makuu. Katika Ziwa Victoria tumejenga chelezo na meli mpya ya MV-Mwanza Hapa kazi Tu inajengwa. Aidha, tumekarabati meli za *New Butiama Hapa Kazi Tu*, *New Victoria Hapa Kazi Tu*, MV. *Clarias* na *ML Wimbi*. Ziwa Tanganyika Kukamilika kwa mikataba kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo pamoja na kuendeleza ukarabati wa meli ya MV-Liemba na ukarabati wa meli ya *MTSangara*.

Mheshimiwa Spika, ziwa Nyasa kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja na kukamilika na kuanza kufanya kazi kwa meli mpya ya MV-Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na mizigo tani 200.

Mheshimiwa Spika, tano Ujenzi wa Barabara na Madaraja makubwa kukamilika kwa barabara ya juu ya Kijazi

Dar es Salaam ambayo imezinduliwa, kuendelea na ujenzi wa daraja la Kigongo Busisi Mwanza, ambao umefikia asilimia 14.5 na daraja la *Tanzanite* Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 71.3. Kwa sasa tunajenga daraja eneo la makutano la chuo cha Uhasibu na eneo la makutano ya Keko Jijini Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sita, miradi ya maji. Kuwezesha wananchi zaidi ya milioni 25 kupata huduma ya maji ambapo wastani wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama imefikia asilimia 86 kwa mijini na asilimia 72.3 vijiji. Hadi Machi 2021, shilingi bilioni 241.3 zimetumika na kazi ya usambazaji maji vijiji na inaendelea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, saba, elimu. Hadi kufikia Januari 2021, shilingi bilioni 178 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu muhimu katika shule za msingi, sekondari na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Uimarishaji wa miundombinu ya elimu utasaidia kuongeza ubora wa elimu inayotolewa na hivyo kuongeza idadi ya wahitimu wanaoweza kuajiriwa na kujajiri.

Mheshimiwa Spika, nane, afya. Hadi kufikia Januari 2021, shilingi bilioni 69.4 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya inayohusisha hospitali za rufaa za kanda, mikoa na hospitali za halmashauri.

Vilevile, tumejenga vituo vya afya na zahanati kote nchini. Hatua hiyo imesaidia kuboresha huduma za afya zinazotolewa na kuwezesha wananchi wengi kupata huduma ikiwa ni pamoja na kusogea huduma hizo karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/2021 pia ulikumbwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kupungua kwa shughuli za kibashara na uzalishaji duniani kulikosababishwa na athari za *COVID-19* na uharibifu wa miundombinu ya barabara kutokana na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imechukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga, kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko na kuimarisha ukaguzi wake pamoja na kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa sera za uchumi jumla na bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 mwelekeo wa kazi za Serikali utajikita katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 ambapo ni wa kwanza katika hatua za utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/2022–2025/2026). Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2021/2022 vimejikita katika masuala makuu matano ya Mpango wa Tatu. Masuala hayo ni kuchochaea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza biashara; kuchochaea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2021/2022, pia, utajumuisha ukamilishaji wa miradi ya kipaumbele na ya kimkakati ambayo utekelezaji wake haukukamilika katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021).

Mheshimiwa Spika, katika kufikia malengo hayo, Serikali itajikita katika kujenga jamii yenyewe uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu wa uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha uvumbuzi na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa majini, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, ujenzi wa bandari na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuihakikishia sekta binafsi kuwa kutokana na umuhimu wake katika ustawi wa kiuchumi na kijamii, Serikali kupitia Mpango wa Mwaka 2021/2022 itaendelea kuhakikisha kuwa sekta binafsi inashamiri kwa kuainisha fursa zilizopo, kuweka vipaumbele vitakavyowezesha maendeleo ya sekta binafsi na kuweka

mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji. Nitoe rai kwamba sekta binafsi ilete mpango mafsusi kuhusu namna ambavyo itaunga mkono mipango na mikakati ya Serikali ikiwa ni pamoja na kutengeneza ajira milioni nane katika kipindi cha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi wa dunia ilidorora katika mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2019. Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) ya Januari 2021 inaonesha kuwa uchumi wa dunia ulikadiriwa kushuka kwa asilimia 3.5 katika mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2019. Kudorora huko, kumetokana na changamoto mbalimbali zilizoikumba dunia katika kipindi hicho zikiwemo janga la ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu (*COVID-19*), mgogoro wa kibiashara baina ya mataifa yenye uchumi mkubwa duniani na hatua zisizo rafiki zilizochukuliwa na baadhi ya nchi katika kujikinga na maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa inaonesha kuwa uchumi wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikadiriwa kushuka kwa asilimia 2.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.2 mwaka 2019. Sababu za kudorora kwa hali hiyo ya uchumi ni kama nilizobainisha awali kwenye uchumi wa hali ya dunia.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi nchini kwetu, Pamoja na changamoto ambazo baadhi nimezieleza hapo juu, uchumi wa Tanzania umeendelea kufanya vizuri katika kipindi hicho. Katika mwaka 2020, Benki ya Dunia ilikadria uchumi wa Tanzania kukua kwa asilimia 2.5 kutokana na athari za janga la *COVID-19* liliokumba dunia nzima. Hata hivyo, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2020, Pato la Taifa lilikuwa kwa asilimia 4.7. Kasi hiyo, ilitokana na uamuzi wa Serikali wa kutofunga shughuli za kiuchumi (*Lock down*) kufuatia mlipuko wa *COVID-19*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu katika kiwango cha chini, ambapo ulifikia wastani wa asilimia 3.5 Januari 2021, ikilinganishwa na wastani wa

asilimia 3.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Katika kipindi chote cha mwaka 2020, mfumuko wa bei ulikuwa ndani ya lengo la muda wa kat i la asilimia 5.0 na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), kiwango ambacho hakizidi asilimia 8.0.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho cha mfumuko wa bei pia kilibaki ndani ya wigo uliowekwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*) wa kat i ya asilimia 3.0 na 7.0. Kushuka kwa mfumuko wa bei kulitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani na sera madhubuti za fedha na bajeti. Serikali itaendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuwa na mwenendo tulivu wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo inayotarajiw a kuleta matokeo makubwa na ya haraka katika uchumi. Msukumo mkubwa utawekwa katika maeneo ambayo yanachochaea mageuzi ya viwanda, ukuaji wa ajira, maendeleo ya kiuchumi na kijamii ili kuhakikisha uchumi unaendelea kuwa imara, tulivu na shindani.

Mheshimiwa Spika, Bunge. Katika mwaka 2020/2021 Bunge Iako Tukufu limetekeleza kwa ufanisi mkubwa majukumu yake ya msingi ya kutunga sheria na kuisimamia Serikali. Katika kipindi hicho, Bunge lilisimamia na kuratibu shughuli za Mikutano Mitatu ya Bunge ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Kwanza wa Bunge la Kumi na Mbili. Katika Mkutano wake wa Pili, Bunge lilijadili hotuba ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitao tarehe 13 Novemba 2020 wakati akifungua Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, vilevile Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

(2021/2022 - 2025/2026) pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Ofisi ya Bunge itaendelea kuratibu shughuli za mikutano minne ya Bunge pamoja na Kamati za Kudumu za Bunge; kuratibu ushiriki wa Wabunge katika Mikutano ya Kimataifa kama *SADC – Parliamentary Forum*, Bunge la Afrika Mashariki, Maziwa Makuu, *Inter-Parliamentary Union (IPU)* na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha, itaendelea kukarabati ukumbi wa Bunge na kuboresha miundombinu mingine ya ofisi zake ili kuwezesha shughuli za Bunge kufanyika kwa ufanisi na tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mhimili wa Mahakama. Uendeshaji wa mashtaka na utoaji haki, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji haki na huduma zitolewazo na Mahakama kwa kukamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi mbili katika Mikoa ya Simiyu na Njombe.

Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya tatu katika Wilaya za Kasulu, Longido na Makete na Mahakama za Mwanzo sita katika maeneo ya Ngerengere, Mtae, Msanzi, Laela, Mtowisa na Kibaigwa na ujenzi wa Mahakama nyingine mpya za Wilaya 25 katika maeneo ambayo hayana huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 Mahakama imesikiliza na kukamilisha mashauri 127,344 ikiwa ni pamoja na mashauri 120,938 yaliyosajiliwa katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2020. Moja ya mifumo iliyotumika ili kuimarisha ufanisi katika utoaji haki kwa wananchi ilikuwa ni utekelezaji wa mradi wa Mahakama maalum zinazotembea. Lengo la Mahakama hizo ni kusogea huduma za Mahakama karibu na wananchi hususan walio katika sehemu zisizo na Mahakama ili kuweza kuzisikiliza kesi na kuzimaliza kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, katika hatua ya majaribio, Serikali imeanzisha huduma hiyo katika Wilaya tano nchini. Wilaya hizo ni Kinondoni maeneo ya Bunju, Ilala maeneo ya Chanika, Wilaya ya Temeke maeneo ya Buza na Wilaya ya Ubungo maeneo ya Kibamba kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Wilaya ya Ilemela (SAUT) kwa Mkoa wa Mwanza. Jumla ya mashauri 446 yameshasajiliwa kwenye Mahakama hizo na mashauri 401 kusikilizwa na kuhitimishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa Taifa wa kutenganisha mashtaka na shughuli za upelelezi kwa kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi ili kurahisisha shughuli za utoaji haki. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Serikali ilifungua jumla ya ofisi mpya sita za Taifa za Mashtaka katika mkoa wa Songwe na Wilaya za Mufindi, Serengeti, Kahama, Karagwe na Kilombero. Lengo ni kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi na hivyo kupunguza muda na gharama za uendeshaji wa mashtaka.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji. Serikali imeendelea kuimarisha shughuli za uwekezaji nchini kwa kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje. Juhudi hizo zilihuisisha kuunganisha watumishi walio katika Huduma za Mahala Pamoja kwenye Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (*TIC*) kwenye mfumo na kupewa idhini ya kuutumia kwa ajili ya kurahisisha maombi ya vibali vya uwekezaji. Lengo ni kuhakikisha kwamba vibali na leseni mbalimbali za uwekezaji na biashara kuititia Kituo cha Uwekezaji Tanzania vinatolewa ndani ya siku 14. Hatua hiyo inalenga kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya ukuaji wa sekta binafsi. Serikali itaendelea kutoa taarifa muhimu zinazohitajika kwa wakati na kushughulikia changamoto za wawekezaji kwa kuzingatia sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imekamilisha tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996. Tathmini hiyo imeonesha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi hicho ikiwemo ukuaji wa uwiano wa uwekezaji kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 14.7 mwaka 1997 hadi asilimia 39.7 mwaka

2019. Aidha, tathmini hiyo imeainisha changamoto mbalimbali za kisera, kisheria na kiutendaji. Kutokana na tathmini hiyo, Serikali inaandaa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji ili kuimarisha uratibu, usimamizi, uhamasishaji na ufuatiliaji wa masuala ya uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika kuvutia uwekezaji. Katika mwaka 2020/2021, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kilisajili miradi 100. Miradi hii inatarajiwa kuwekeza mtaji wa Dola za Marekani milioni 536.04 na kutoa ajira zaidi ya 9,085. Sekta ya Viwanda imeongoza kwa idadi ya miradi 64 sawa na asilimia 64 na mtaji wa uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 370.41.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itakamilisha na kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji ikiwemo kuendeleza miundombinu muhimu ya uwekezaji katika mikoa yote ili kuvutia uwekezaji, kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara, kuimarisha uhamasishaji wa fursa za uwekezaji na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za uwekezaji kwa kufanya tafiti na kuandaa kanzidata ya Uwekezaji ili kuwa na takwimu sahihi za uwekezaji wa ndani na nje ikiwa ni pamoja na idadi ya miradi ya uwekezaji, thamani na ajira zilizoweza kuzalishwa kutokana na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, sekta za uzalishaji, nianze na Sekta ya Kilimo. Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo kwa lengo la kuinua Pato la Taifa na la mtaa mmoja mmoja, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza ajira.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kuwawezesha wakulima kupata pembejio, zana za kisasa, teknolojia na mbegu bora ili kuongeza tija katika kilimo. Kadhalika, Serikali itaimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ili kuhakikisha wakulima wanafaidika na mauzo ya mazao.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa chakula cha kutosha katika maeneo yote nchini imeendelea kuimarika. Mipango madhubuti ya Serikali, mageuzi yanayoendelea kutekelezwa katika sekta ya kilimo pamoja na kuimarika kwa hali ya hewa ni mionganoni mwa sababu zilizochangia kuimarika huko. Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 18.1 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 14.4. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 126 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua za kuimarisha uzalishaji na usalama wa chakula, Serikali inaimarisha miundombinu ya kuhifadhi chakula. Hivi sasa, ujenzi wa vihenge vya kisasa, katika Miji ya Babati, Mpanda, Sumbawanga, Shinyanga, Dodoma na Mbozi hata Makambako na Songea umefikia asilimia 87.39. Vilevile, ujenzi wa maghala na miundombinu mingine katika Miji ya Songea, Makambako, Shinyanga, Babati, Mpanda Sumbawanga umefikia asilimia 60.65. Miundombinu hiyo itakapokamiliika itakuwa na uwezo wa kuongeza chakula utaongezeka kwa kiasi cha tani 501,000 kutoka tani 251,000 za sasa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea. Upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima kwa wakati sambamba na matumizi ya mbinu bora za kilimo ikiwemo teknolojia umeimarishwa. Lengo la Serikali ni kuongeza uzalishaji na kufanya kilimo chetu kiwe chenye tija kwa kuhimiza usambazaji wa pembejeo kwa wakati na kulingana na mahitaji ya kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea nchini umeendelea kuimarika. Aidha, matumizi ya mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja umekuwa chachu ya kuimarisha kwa upatikanaji na kupungua kwa bei. Hadi Februari 2021, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 631,660 sawa na asilimia 88 ya mahitaji ya tani 718,051. Serikali inaendelea kuhakikisha asilimia 12 iliyobaki inapatikana na

kusambazwa kwa wakulima kwa wakati ili kukidhi mahitaji kulingana na hatua mbalimbali za ukuaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa nzige wa jangwa. Itakumbukwa kuwa hivi karibuni baadhi ya maeneo hapa nchini yalivamiwa na nzige wa jangwa. Kufuatia uvamizi huo, Serikali imefanikiwa kudhibiti makundi yote ya nzige yaliyoingia mwezi Januari, 2021 katika Wilaya za Mwanga na baadaye Simanjiro. Pia imefanikiwa kudhibiti makundi mapya yaliyoingia tarehe 15 Februari, 2021 katika Wilaya za Longido na Monduli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua za haraka zilizochukuliwa na Serikali ziliwezesha udhibiti wa nzige hao kabla hawajaleta madhara yoyote kwenye mazao ya wakulima wetu. Niwahakikishie Watanzania wenzangu kwamba Serikali itaendelea kuimarisha mbinu zote za kupambana na wadudu hao waharibifu wa mazao mbalimbali na matumizi bora ya zana za kisasa na teknolojia mapya katika kupambana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Katika mwaka 2020/2021, Serikali imeendelea kuimarisha kilimo cha umwagiliaji baada ya kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa skimu 17 za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 8,536 kuitia Mpango wa Pili wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP II*) na kukamilisha skimu tano ni Kigugu – Mvomero (hekta 195), Msolwa Ujamaa (hekta 40), Njage – Kilombero (hekta 75), Mvumi (hekta 249) na Kilangali *Seed Farm* – Kilosa (hekta 400) kuitia Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mpunga (*ERPP*). Pia, imetoa mafunzo kwa wakulima na wakulima viongozi 1,000 katika uandaaji wa mipango ya mafunzo na uendeshaji wa skimu pamoja na usimamizi wa rasilimali maji katika skimu 50.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ushirika. Katika mwaka 2020/2021, Serikali iliendelea kudhibiti, kusimamia na kuhamasisha ushirika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo kilimo, mifugo na uvuvi ili kuchochaea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Aidha, Serikali imefanikiwa

kurejesha mali za vyama vya ushirika zenyet thamani zaidi shilingi bilioni 48.98 na kufanya mali zilizookolewa hadi kufikia Desemba 2020 kuwa na thamani ya shilingi bilioni 68.9. Mali hizo ni pamoja na majengo, viwanja, magari mitambo ya mashine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itasimamia na kuunganisha Wizara na Taasisi zinazoendesha ushirika kama vile *AMCOS*, *SACCO\$na* vikundi vidogo vya ushirika ili uweze kuwanufaisha wanaushirika wenyewe. Kwa msimu huu wa mavuno, mazao ya wanaushirika yataendelea kuuzwa na wanaushirika wenyewe kuititia minada chini ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mazao yanayozalishwa kwa wingi. Mfumo wa *TMX* nao utatumika lakini mpaka itakapotolewa elimu ya kutosha ili kuondoa manung'uniko na migogoro inayoendelea kwenye maeneo kwa matumizi ya mfumo huo. Tuwaachie wanaushirika wasimamie mazao yao na namna ya kuweza kuyauza mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta Ndogo ya Mafuta ya Kula; katika kipindi cha hivi karibuni nchi yetu imekabiliwa na changamoto ya uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kutosha ya kula. Hali hiyo, imetokana na uzalishaji mdogo wa mazao ya mbegu ikiwemo nazi, alizeti, pamba, chikichi na mengineyo. Kwa mfano, mahitaji ya mafuta ya kula kwa mwaka ni zaidi ya tani 570,000 wakati uzalishaji wa ndani ukikadiriwa kuwa tani 210,000. Katika kukabiliana na upungufu huo, Serikali imekuwa ikitumia takribani shilingi bilioni 470 kuagiza tani 360,000 za mafuta ya kula kila mwaka kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inatekekeza mikakati ya kufufua zao la Chikichi ambalo limeonekana kuwa na ufanisi mkubwa katika uzalishaji wa mafuta ya kula. Mikakati hiyo inakwenda sambamba na kuimarisha uzalishaji kwenye mazao mengine kama vile Alizeti, Nazi na Mafuta ya Pamba ili kupata mafuta mengi na kujitosheleza kwa mahitaji ya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (*TARI*) na sekta binafsi itaimarisha shughuli za utafiti hususan kwenye uzalishaji wa mbegu na miche bora sambamba na matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kupata mbegu nyingi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Mifugo; wakati Mheshimiwa Rais wa Tano akizungumzia eneo la mifugo kwenye hotuba yake ya Kuzindua Bunge la Kumi na Mbili, tarehe 13 Novemba, 2020, alisema kuwa "Mifugo ni Utajiri." Hata hivyo, licha ya nchi yetu kuwa na idadi kubwa ya mifugo, bado mchango wa sekta hiyo katika kuboresha maisha ya wafugaji na ukuaji wa uchumi wake siyo wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Sekta ya Mifugo illichangia pato la Taifa kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2018/2019. Ongezeko hilo, limechangiwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kwa lengo la kuimarisha mnyororo mzima wa thamani kwenye Sekta ya Mifugo. Hatua hizo, zinajumuisha kuimarisha biashara ya ndani kutokana na kuongezeka kwa viwanda vyatya kuchakata mazao ya mifugo, kuboreshwa kwa mbari au kosaafu za mifugo na hivyo, kuongeza uzalishaji wa nyama bora na maziwa mengi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2021 uzalishaji wa nyama umeongezeka kufikia tani 738,166 kutoka tani 701,679 mwaka 2019/2020. Aidha, uwekezaji kwenye viwanda vyatya kuchakata mazao ya mifugo umesaidia kuimarisha biashara ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi. Mauzo ya nyama nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 692.36 zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.30 mwaka 2019/2020 hadi tani 2,154 zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 4.65 mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kumekuwepo na ongezeko la viwanda vyatya ngozi nchini vikiwemo, Kiwanda cha Ngozi cha *ACE Leather*, Morogoro na Kiwanda cha Kimataifa cha Ngozi (*Kilimanjaro*

International Leather Industry Co. Ltd). Viwanda hivyo, vimechangia kuongeza thamani ya ngozi inayozalishwa nchini sambamba na kutengeneza ajira. Uwekezaji kwenye viwanda vya kuchakata ngozi utaongeza uzalishaji wa ngozi kutoka futi za mraba milioni tisa hadi futi za mraba milioni 25. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kuhamasisha ufgugaji wa kisasa na kuhimiza uwekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya mifugo ili kuhakikisha kwamba Taifa linanufaika na idadi kubwa ya mifugo iliyopo hapa nchini kwetu. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji, malisho na vyakula vya mifugo sambamba na kuboresha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua madhubuti katika kukuza Sekta ya Uvuvi kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sekta hiyo. Hatua hizo, zinatokana na ukweli kwamba Sekta ya Uvuvi inao uwezo wa kutoa mchango mkubwa kwenye kukuza pato la Taifa, kupambana na umaskini na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 Serikali imeanza kulifufua Shirika la Uvuvi Tanzania (*Tanzania Fisheries Corporation - TAFICO*) ikiwa ni pamoja na taratibu za ujenzi wa meli na Bandari ya Uvuvi. Aidha, tayari upembuzi yakinifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa bandari na mpango wa biashara wa kulifufua shirika hilo umekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Serikali itakamilisha ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania na kuendelea na taratibu za ujenzi wa bandari na meli za uvuvi. Lengo ni kuimarisha shughuli za uvuvi wa bahari kuu ili kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuwezesha mauzo ya bidhaa za uvuvi nje ya nchi na hivyo kuchangia katika kuongeza mapato yatokanayo na mauzo nje, ukuaji wa uchumi na kuzalisha ajira pia.

Mheshimiwa Spika, utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo zilikumbwa na changamoto za ukuaji mzuri katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kutokana na janga la Homa Kali ya Mapafu, *Covid 19* lililoikumba dunia kuanzia mwishoni mwa mwaka 2019. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Mataifa mbalimbali duniani katika kujikinga na janga hilo ikiwemo kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege na kuwafungia watu ndani zilichangia kutokukua vizuri kwa sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Serikali ilichukua hatua madhubuti za kunusuru Sekta ya Utalii ikiwemo kuandaa miongozo na taratibu maalum za kuendesha biashara ya utalii kwa kuzingatia taarifa na maelekezo ya mashirika ya kikanda na Kimataifa. Hatua hizo, ziliwezesha Tanzania kupewa utambulisho wa usalama katika safari (*Safe Travels Stamp*) mwezi Agosti, 2020 kutoka Shirika la *World Travel and Tourism Council (WTTC)*. Utambulisho huo ulikuwa ni kielelezo kwamba Tanzania ni sehemu salama kwa utalii dhidi ya janga la *Covid-19* hali ambayo inaendelea mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zilichangia kuimarika kwa Sekta ya Utalii kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 ambapo idadi ya watalii walitembelea Tanzania ni 624,096 ikilinganishwa na idadi ya watalii 437,000 ambao walitarajiwa kutembelea Tanzania katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia imeendelea kufahamika zaidi katika masoko makuu ya utalii duniani kama kituo muhimu cha utalii Barani Afrika. Kutokana na jitihada za utangazaji, mtandao wa *safaribookings.com* umeendelea kuitambua Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa kivutio cha utalii kinachofaa zaidi kutembelewa miongoni mwa hifadhi 50 Barani Afrika kufikia mwaka 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kuimarisha Sekta ya Utalii kwa kuimarisha usalama wa watalii wanaoingia hapa nchini. Aidha, Serikali itaongeza kasi zaidi ya kutangaza vivutio vyta utalii kama vile Mlima

Kilimanjaro, Hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro na maeneo mengine ya kihistoria ndani na nje kwa kutumia Balozi zetu, tovuti zeti na sekta mbalimbali na kupitia Sekta ya Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha Sekta ya Madini ili Taifa liweze kunufaika zaidi na rasilimali hiyo. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha masoko ya madini, kuzuia utoroshaji wa madini na kufanikisha uwekezaji wa kimkakati katika madini. Kutokana na hatua hizo, katika mwaka 2019 Sekta ya Madini imekua kwa asilimia 17.7 na kuongoza kwenye mauzo ya bidhaa nje ya nchi na uingizaji wa mapato ya Serikali. Hadi kufikia Februari, 2021, kiasi cha shilingi bilioni 399.33 zilikusanywa sawa na asilimia 72.91 ya lengo la shilingi bilioni 547.74 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha Sekta ya Uchimbaji Mdogo wa Madini, Serikali imeendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo hapa nchini kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwatengea maeneo, kuwajengea uwezo na kuwapatia leseni za uchimbaji wa madini. Katika mwaka 2020/2021 jumla ya leseni 4,652 za utafutaji wa madini, uchimbaji mdogo na uchimbaji wa kat, uchenjuaji na uyeyushaji wa madini na leseni za biashara ya madini zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, moja ya matokeo mazuri ya uvezeshaji wa wachimbaji wadogo ni kupatikana kwa mawe ya *Tanzanite* kutoka katika mgodi wa Bwana Sanini Kurian Laizer. Mawe hayo yenye uzito wa kilo 9.27, 5.103 na 6.33 na thamani ya shilingi bilioni 12.59 yalivunja rekodi ya uzito wa madini ya *Tanzanite* yaliyowahi kupatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie kuhusu usimamizi wa Masoko ya Madini. Serikali imeendelea kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini hapa nchini. Masoko ya Madini yameongezeka kutoka 28 hadi 39 na vituo vya ununuzi wa madini vimeongezeka kutoka 28 hadi 41 katika kipindi cha Januari, 2020 hadi Februari, 2021. Masoko

na vituo vya ununuzi wa madini vimekuwa chachu ya kuongeza ushindani na uwazi kwenye biashara ya madini, kudhibiti utoroshaji wa madini pamoja na kuwahakikishia ulinzi na usalama wa kutosha wanunuzi na wauzaji wa madini. Hatua hiyo, imewezesha kuinua uchumi wa wachimbaji wadogo na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kuwapa kipaumbele wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kwa kuwatenglea na kuwapimia maeneo maalum ya uchimbaji, kuwapatia leseni na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rahisi na rafiki ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini. Vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha na kusimamia utendaji kazi wa masoko na vituo vya ununuzi wa madini ili kuhakikisha kwamba vinafanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuliongezea Taifa letu mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Nishati; hali ya upatikanaji wa nishati ya umeme, mafuta na gesi imeendelea kuwa nzuri na hivyo, kutoathiri shughuli za kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2020/2021, Serikali imetekeleza miradi mikubwa ya umeme, mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Mwalimu Julius Nyerere, Mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo pamoja na ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta kutoka Hoima - Uganda hadi Chongoleani – Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, miradi hii mikubwa na ya kimkakati inalenga kuliwezesha Taifa kuimarisha upatikanaji wa nishati kwa gharama nafuu na uhakika kwa ajili ya kujenga uchumi shindani wa viwanda. Utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere wa Megawati 2,115 wenyewe thamani ya trilioni 6.55 umefikia asilimia 45 mwezi Machi, 2021. Vilevile, ajira zaidi ya 7,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zimetolewa katika mradi huo. Aidha, mradi wa uzalishaji wa umeme wa Rusumo wa Megawati 80 katika maporomoko ya maji ya Mto Kagera umefikia asilimia 75.3. Kukamilika kwa miradi hiyo, kutaihakikishia nchi yetu upatikanaji wa umeme wa uhakika, wenyewe kutosheleza mahitaji ya viwanda na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme unakwenda sambamba na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ikiwemo njia ya msongo wa KV 400 kutoka Rufiji mpaka Chalinze na Chalinze – Kinyerezi na Chalinze kuja hapa Dodoma; na njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa KV 220 kwa ajili ya treni ya mwendo kasi imeshatengwa. Nitumie fursa hii kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 kwa ajili ya treni ya mwendo kasi (Dar es Salaam - Morogoro) imekamilika kwa asilimia 99. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Septemba, 2020 Mheshimiwa Yoweri Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, alizuru Tanzania. Ziara hiyo ililenga kukamilisha taratibu za mwisho za utiaji saini wa Mkataba wa utekelezaji wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania. Mradi huo, utakaogharimu Dola za Marekani bilioni 3.5 unatarajiwa kutengeneza ajira zipatazo 18,000.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 mwezi huu Aprili, juzi Rais wetu pendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Amiri Jeshi Mkuu alishiriki katika utiaji saini wa Mkataba wa Utekelezaji nchini Uganda na hivyo kuashiria kuanza rasmi kwa utekelezaji wa mradi huo. Rai yangu kwa wananchi ni kuijandaa kuzitumia kikamilifu fursa zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huu wa bomba unaoanza nchini Uganda na kuja nchini Tanzania kwa kipande kirefu hadi pale Chongoleani Mkoani Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2021/2022 Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (*REA III*) ili kuhakikisha kuwa vijiji 2,050 vilivyosalia vinapata huduma ya umeme. Kadhalika, Serikali itasimamia miradi ya uzalishaji na usafirishaji wa umeme, sambamba na utekelezaji wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda kama nilivyosema awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaimarisha Sekta ya Viwanda ili kutengeneza ajira nyingi zaidi, kuongeza thamani

ya mazao, kupanua wigo wa masoko na hivyo, kuongeza pato la mtu mmoja mmoja; mapato ya Serikali na fedha za kigeni nayo pia ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2019 Sekta ya Viwanda ilichangia asilimia 8.5 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 8.1 mwaka 2018. Katika kuongeza mchango wa sekta hii, Serikali inasimamia azma ya Serikali ya Uchumi wa Viwanda nchini kwa kuimarisha ulinzi wa viwanda vya ndani, kuendeleza viwanda mama, viwanda vya kimkakati sambamba na kuhakikisha matumizi ya malighafi zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa ujenzi wa uchumi wa viwanda umewezesha kuongezeka kwa kasi ya ujenzi wa viwanda vipyta kila mwaka, upanuzi wa viwanda vilivyopo pamoja na ufufuaji wa viwanda vilivyokufa. Baadhi ya viwanda vilivyojengwa katika mwaka 2020 ni kama vile *Kilimanjaro International Leather* katika Mkoa wa Kilimanjaro, Kiwanda cha Usindikaji Maziwa cha *Kahama Fresh* kilichopo katika Mkoa wa Shinyanga, *Taifa Leather Company Ltd*, *Murzar Wilmar Rice Mills Ltd* na *Mahashree Agro-processing Tanzania Ltd* vilivyopo Morogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, ujenzi wa majengo ya viwanda (*Industrial Sheds*) kwa ajili ya wajasiriamali katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Geita, Mtwara na Ruvuma; Kiwanda cha Chai cha Kabambe (Njombe); Kiwanda cha *Yalin Cashewnut Company Ltd* kilichoko Mkoani Mtwara eneo la Mikindani na jengo la kiwanda kipyta cha kuunganisha matrekta *TAMCO* kilichoko Kibaha, umekamilika. Ujenzi wa majengo hayo pamoja na kuimarisha uwekezaji kwa wajasiriamali, utasaidia pia kuimarisha shughuli za viwanda na hivyo kuongeza ajira na masoko ya bidhaa zinazozalishwa.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kwamba ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya afya umeongeza mahitaji ya vifaa tiba, kinga na dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kukabiliana na ongezeko la mahitaji hayo, mwaka 2020/2021 katika kipindi

kifupi, Serikali ilifanikiwa kuhamasisha uwekezaji mkubwa ambapo viwanda 17 vya dawa, vifaa tiba na kinga vilianzishwa. Kuanzishwa kwa viwanda hivyo, kutawezesha kuimarika kwa huduma za afya nchini kufuatia upatikanaji wa kutosha wa bidhaa hizo, usalama wake, kuongeza ajira na kuondokana na utegemezi kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa changamoto za ukuaji wa viwanda na biashara nchini ni upatikanaji wa masoko ya uhakika. Katika mwaka 2020/2021, Serikali imefanikiwa kupata masoko ya bidhaa zetu nje kwa lengo la kukuza uchumi na pato la Taifa. Mafanikio hayo yanajumuisha kusainiwa kwa mkataba katika Tanzania na China Oktoba, 2020 ili kuruhusu maharage aina ya soya kutoka Tanzania kuingia katika soko la China. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwezi Januari, 2021 Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kuongeza mnyororo wa thamani kwenye samaki unaojulikana kama *Fish4ACP*. Mradi huo, unaohusisha nchi 10 katika 79 za Jumuiya ya Nchi za Afrika, Karibeani na Pasifikasi utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano Mkoani Kigoma. Kupitia mradi huo, wavuvi wadogo watapata ujuzi wa kuongeza uzalishaji na mnyororo wa thamani kwenye samaki aina ya migebuka na dagaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, masoko mengine yaliyopatikana ni soko la minofu ya samaki aina ya sangara nchini Saudi Arabia, soko la nyama katika nchi za Kuwait, Qatar na Oman na soko la matunda aina ya karakara (*passion*), parachichi pamoja na nanasi katika nchi ya Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*). Katika kipindi hicho, zaidi ya tani 7,000 za nyama na kontena 22 za matunda ziliuzwa katika masoko hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itapanua wigo wa masoko ya bidhaa zetu nje ili kutoa fursa nzuri zaidi za kiuchumi kwa wakulima na wafanyabiashara wetu lakini pia kuwapa uhakika wa kipato na kukuza uchumi na pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, natoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo, Viwanda na Biashara kuendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kutafuta fursa zitakazowezesha bidhaa zinazozalishwa nchini kuongezwa thamani hususan mazao ya kilimo, pamoja na kuwaunganisha wakulima na wenye viwanda ili kupata masoko ya uhakika nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika huduma za kiuchumi, nianze na Sekta ya Ardhi. Kuimariika kwa uchumi na maendeleo ya watu kumechangia kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo zimeibua migogoro ya matumizi ya ardhi. Kwa msingi huo, katika mwaka 2020/2021 Serikali imesimamia mikakati mbalimbali yenye lengo la kuondoa migogoro ya ardhi na kuhakikisha uwepo wa mipango na matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji, kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Julai, 2020 Serikali iliridhia vijiji 920 kati ya 975 vyenye migogoro kubaki katika maeneo ya mikoa na kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii. Vilevile, Serikali imeridhia vijiji 19 kati ya 55 vilivyokuwa na migogoro na vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea na shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hatua nyininge zinahusisha kufutwa kwa mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,659.94 na misitu ya hifadhi saba yenye ukubwa wa ekari 46,715 ili kuruhusu wananchi waendelee na shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, migogoro mingine ya ardhi ipatayo 23,783 imetatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba za Wilaya. Kwa kuzingatia hatua ambazo Serikali imezichukua, naelekeza Viongozi wote wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kusimamia utekelezaji wa manunuzi ya Serikali na kuhakikisha kuwa hakuna migogoro mipya ya ardhi inayojitokeza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Januari, 2021 viwanja 95,329 vimetambuliwa, kwa kupimwa na kumilikishwa kwa kutumia dhana shirikishi katika upangaji na upimaji wa ardhi. Hatua hiyo, ni utekelezaji wa programu ya kupanga, kupima

na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Vilevile, ardhi yenye ukubwa wa ekari 424,885.40 imetengwa katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya uwekezaji ikiwemo ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itatekeleza mipango na programu za upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika maeneo ya wananchi pamoja na miradi ya kimkakati ya kitaifa, uimarishaji wa muindombinu ya upimaji na ramani na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ambayo kwa pamoja itapunguza migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya usafiri na usafirishaji; pamoja na mambo mengine kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni hatua muhimu katika kukuza uchumi wa sekta za uzalishaji. Katika mwaka 2020/2021 Serikali imejenga, kukarabati na kufanya matengenezo barabara, madaraja, vivuko, bandari, viwanja vyatia na ndege na reli.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Barabara na Madaraja; hadi Februari, 2021 Serikali imejenga na kukarabati kilomita 401.60 ikilinganishwa na lengo la kilomita. 520.47 sawa na asilimia 77.16 kwa mwaka 2020/2021. Ujenzi na ukarabati huo ulihusisha barabara kuu, za mikoa na wilaya ili kuziwezesha zipitike wakati wote. Lengo la Serikali ni kuhakikisha mikoa na wilaya zote nchini zinaunganishwa kwa barabara za lami. Aidha, kazi ya kuunganisha Mikoa ya Rukwa – Katavi, Katavi – Tabora, Singida – Tabora, Tabora – Kigoma na Kigoma – Kagera inaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunapunguza msongamano wa magari Mkoani Dar es Salaam, Serikali imekamilisha ujenzi wa barabara ya juu ya John Kijazi, iliyozinduliwa tarehe 24 Februari, 2021. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa barabara kwa njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha yenye urefu wa kilomita 19 ambaao ujenzi wake umefikia asilimia 62.32. Vile vile tunajenga barabara ya juu makutano ya Keko ili kupunguza msongamano wa

magari yanayotoka *airport* kuja Jijini Dar es Salaam. Hata hivyo bado tunaendelea na pia na ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya Chuo cha Uhasibu Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano. Miradi hii yote itasimamiwa na itakamilika kwa wakati uliokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mingine ya ujenzi wa madaraja makubwa ambayo ni pamoja na Kigongo-Busisi lenye urefu wa kilomita 3.2 uliofikia asilimia 25.71, *Tanzanite* lenye urefu wa kilomita 1.03 uliofikia asilimia 70.6 na Wami lenye urefu wa mita 513.5 uliofikia asilimia 46. Aidha, ujenzi wa madaraja mengine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga; Serikali inaimarisha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuchochaea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi ikiwemo utalii, kilimo na madini. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Geita ambaao umefikia asilimia 98; Songea asilimia 95; na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara ambaao umefikia asilimia 53.2.

Aidha, maandalizi ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato utakaogharimu shilingi bilioni 759 yamekamilika. Vilevile, ujenzi na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Shinyanga, Kigoma, Tabora na Sumbawanga vitakavyogharimu Shilingi bilioni 176 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na uimarishaji wa miundombinu ya usafiri wa anga, Serikali imekamilisha malipo ya ununuzi wa ndege mpya tatu, mbili zikiwa ni *Airbus A220-300* na moja ni *Dash 8-Q400 De-Havilland*. Ndege hizo zinatarajiwa kuwasili mwaka 2021/2022 na hivyo kuwezesha Serikali kuwa na jumla ya ndege zake 12. Nitumie fursa hii kulipongeza Shirika la Ndege Tanzania kwa kuanzisha safari za kwenda nje ya nchi Guangzhou, China. Safari hizo zitakuwa chachu ya kuimarisha biashara, utalii na ajira. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja, viwanja vya ndege, nyumba na majengo ya Serikali. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya vivuko katika maeneo mbalimbali nchini inayohusisha na ujenzi wa maegesho ya vivuko, ukarabati na ujenzi wa vivuko vipyta.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Reli ya Kisasa (*SGR*) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye jumla ya urefu wa kilomita 1,219 unaendelea kwa awamu. Ujenzi wa kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (kilomita 300) umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90.34 na ujenzi wa kipande cha Morogoro hadi Makutupora (kilomita 422) umekamilika kwa asilimia 57.57. Vilevile, Serikali imesaini mkataba na mkarandasi ili kukamilisha kipande cha Mwanza hadi Isaka (kilomita 341).

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha taratibu za manunuzi ya vichwa vya treni na mabehewa ya mizigo na ya abiria. Kuboresha kwa miundombinu ya reli kutarahisisha usafirishaji wa mizigo ya ndani na nchi jirani, lakini pia kuboresha utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kuimarisha uchumi wa wananchi, hii ni hatua kubwa kwa Taifa letu kwani kwa mara ya kwanza Tanzania itakuwa na treni inayoendeshwa kwa kutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Bandari; Serikali inaboresha Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga. Uboreshaji wa gati Na.6 na Na.7 katika Bandari ya Dar es Salaam umekamilika kwa asilimia 90 na 75 mtawalia. Kwa upande wa Bandari ya Tanga kazi ya kuchimba lango la kuingia meli lenye urefu wa kilomita 1.75 imekamilika na linatumika na ujenzi wa sehemu ya kugeuzia meli lenye upana wa mita 400 unaendelea.

Aidha, ujenzi wa gati lenye urefu wa mita 300, ukarabati wa yadi ya kuhudumia shehena na ghala Na.3 katika Bandari ya Mtwara umekamilika. Miradi hiyo itawezesha Taifa kutumia kwa ufanisi fursa za kijiografia

tulizonazo pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi na kurahisisha usafirishaj.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itakamilisha miradi iliyoanzishwa na kuanza utekelezaji wa miradi mipya.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; dunia hivi sasa ipo katika mapinduzi ya nne ya viwanda ambayo yanaongozwa na sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Kama zilivyo nchi nyingine duniani, nasi ni lazima kuendana na mabadiliko haya. Hivyo basi, katika miaka mitano ijayo, Serikali itafikisha miundombinu ya Mkongo wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu hususan wilayani, kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi (*Broadband*) na kuongeza watumiaji wa *Internet*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021, Serikali imesimamia utekelezaji wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi, Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao (*National Cyber Security Strategy*), ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuendelea kufikisha huduma za mawasiliano kwa maeneo hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuweka miundombinu ya Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi inaendelea na jumla ya kata 118 katika Halmashauri za Majiji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Tanga na Manispaa ya Morogoro zimefikiwa. Vilevile, Mkakati wa kukamilisha Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi kwa maeneo yote nchini ifikapo 2025 umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022, Serikali itaongeza matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ya kasi (*Broadband*) kutoka asilimia 45 ya mwaka 2020 hadi asilimia 60 ya mwaka 2022, kuimarisha huduma za Posta ikiwemo biashara mtandao (*e-Commerce*) ili kupanua wigo wa masoko ya bidhaa na huduma ndani na nje ya nchi sambamba na kuwezesha upatikanaji wa

bidhaa na huduma kwa wananchi na kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma ya Mkongo kwa ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Jamii, Sekta ya Elimu; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetekeleza mpango wa Elimumsingi Bila Ada pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu nchini. Hadi kufikia Februari 2021, Serikali imetumia Shilingi billioni 166.17 kwa ajili yakutekeleza mpango huo kwa ajili ya shule za msingi na sekondari. Pia Serikali imeboresha miundombinu ya shule za msingi 1,372 na sekondari 554 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, imekarabati shule 18 za wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya juu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi 142,179. Shilingi billioni 464 zitatumika kwa mwaka wa masomo 2020/2021 ukilinganisha na Shilingi bilioni 450 zilizotumika kwa wanafunzi 130,883 katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kuinua kiwango cha ubora wa elimu inayotolewa kwa kuimarisha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu; ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu ili kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini; lakini pia kutoa mafunzo kazini kwa Walimu na wakufunzi pamoja na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maji; Serikali inasimamia vizuri sekta hii tena kwa ukaribu na kuhakikisha kwamba inatoa mchango unaostahili katika kukuza uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu. Katika mwaka 2020/2021, Serikali ilipanga kutekeleza miradi 1,346 katika maeneo ya mijini na vijiji. Hadi Februari, 2021, miradi ya maji iliyokamilika ni 422 ambayo imegharimu Shilingi bilioni 913.74. Kati ya miradi hiyo, 355 ipo vijiji na 67 ipo mijini. Halikadhalika, utekelezaji wa miradi 924 iliyobaki unaendelea katika maeneo mbalimbali kwa hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa iliyokamilika ni pamoja na Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga na Nzega na Mradi wa kupeleka Maji katika Miji ya Kagongwa na Isaka. Kukamilika kwa miradi hiyo, kumewanufaisha wananchi wapatao milioni 3.52 wa mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Serikali itaweka kipaumbele katika kukamilisha miradi 924 inayoendelea kutekelezwa kote nchini; Kuanza utekelezaji wa miradi mipyä ikiwemo miradi katika miji 28; Kuboresha huduma ya maji Jijini Dodoma kwa kujenga Vwawa la Fwarka na Mradi wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kipaumbele katika kipindi hicho ni Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dar es Salaam, Mradi wa Maji wa Orkesumet, Mradi wa Maji wa Mji wa Mugango – Kyabakari - Butiama, Mradi wa kutoa Maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tinde na Shelui, Mradi wa Maji wa Same – Mwanga, Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha, Mradi wa Maji katika Jiji la Mwanza na Mradi wa Maji ambao umekamilika wa Mjini Lindi. Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi yote ili ilete tija katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya; kulinda na kuimarisha afya ya Watanzania kimeendelea kuwa ni kipaumbele cha Serikali yetu. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imejenga na kuboresha miundombinu ya afya, huduma za kibingwa, upatikanaji wa vifaa tiba, kinga, dawa na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu ya huduma za afya; utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali maalum umefikia hatua mbalimbali za ukamilishwaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Njombe (asilimia 80), Simiyu (asilimia 70), Mara-Kumbukumbu

ya Mwalimu Nyerere (asilimia 74), Geita (asilimia 94), Songwe (asilimia 80), Katavi (asilimia 65), Mwanza-Sekou Toure (asilimia 73), Dar es Salaam Mwananyamala (asilimia 98), Ruvuma (asilimia 45), Tanga (asilimia 75), Kigoma - Maweni (asilimia 75), Kilimanjaro - Mawenzi (asilimia 65), na Hospitali ya Uhuru iliyopo Chamwino, Dodoma imekamilika na huduma zinaendelea kutolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali tatu za Rufaa za Kanda ambazo ni Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini ambayo iko Mtwara (asilimia 90), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya (asilimia 72) na Kanda ya Ziwa – Burigi (awamu ya kwanza asilimia 98) unaendelea. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya uchunguzi kwa ajili ya maabara katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto – Wilayani Siha, Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 102, Vituo vya Afya 487 na ujenzi wa Zahanati 1,198. Hadi Machi mwaka huu 2021, Hospitali 57 za Halmashauri, Vituo vya Afya 296, na Zahanati 654 zimekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mapambano dhidi ya magonjwa ya mlipuko ikiwemo homa kali ya mapafu katika juhudi za kupambana na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza; mwezi Februari, 2021, Serikali imeingiza nchini mitambo saba yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 ya hewa ya oksijeni kwa siku. Mitambo hiyo itasimikwa kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa za Amana, Dodoma, Geita, Manyara, Mbeya, Mtwara na Ruvuma kwa kuanzia. Sambamba na usimikaji wa mitambo hiyo, Hospitali zote saba zimepatiwa mitungi 74 kila moja.

Mheshimiwa Spika, kila mtambo mmoja kwenye hospitali hizo utakuwa na uwezo wa kusambaza gesi ya oksijeni katika vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 18. Hatua hiyo, inalenga kuimarisha mfumo wa huduma za afya ili kuwa tayari kukabiliana na changamoto za sasa na baadaye. Maeneo yanayolengwa ni vyumba vya kutoa

huduma za dharura, huduma ya mama na mtoto, upasuaji na vyumba vya uangalizi maalum. Katika mwaka 2021/2022, Serikali itaongeza mitambo mingine ya aina hiyo 12.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Afya za Kibingwa; Serikali imeimarisha huduma za afya za kibingwa na kuwawezesha wananchi wengi kupata huduma hizo ndani ya nchi na hivyo kuokoa fedha zilizokuwa zitumike kugharlamia huduma hizo nje ya nchi. Katika mwaka 2020/2021, wagonjwa 62 wamepandikizwa figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na wagonjwa 16 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma. Aidha, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (*JKCJ*) imetoa huduma za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua kwa wagonjwa 114 na zimepata mafanikio. Vilevile, watu wazima 36 walifanyiwa upasuaji uliohusisha mishipa ya damu, nao pia wamefanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba; pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya unaoendelea kote nchini, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo hivyo umeendelea kuimarika. Hadi mwaka 2021, Shilingi bilioni 74.38 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 15 ni za ununuzi wa chanjo.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi na Usalama; hali ya ulinzi na usalama katika nchi na mipaka yetu imeendelea kuwa shwari. Vilevile, Jeshi la Wananchi Tanzania limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia na mataifa mengine kupambana na matishio ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara haramu ya dawa za kulevyta na usafirishaji haramu wa binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jeshi letu limeendelea kushiriki katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kisasa (*SGR*) na mradi wa kufua umeme Rufiji (*Julius Nyerere Hydropower Project*) pamoja na kutoa huduma

wakati wa majanga na matukio yenyewe kuleta athari kwa watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, jeshi letu linashiriki katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa katika maeneo ya Darfur, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Afrika ya Kati na Lebanon. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa mistari wa mbele katika masuala ya kuimarisha amani na maslahi ya Taifa katika nyanya za Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kuliimarisha na kuliongezea uwezo JWTZ kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa wanajeshi ikiwemo mafunzo, maslahi, huduma bora za afya na makazi ili kuongeza uwezo wake wa klitendaji na utayari wa kulinda mipaka ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi na wafanyakazi; Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kazi na wafanyakazi kwa kusimamia viwango vya kazi na wafanyakazi pamoja na afya na usalama mahali pa kazi. Hadi Februari, 2021 jumla ya kaguzi 4,771 za viwango vya kazi zimefanyika, sawa na asilimia 99.4 ya kaguzi 4,800 ambazo ziliikuwa zimepangwa kufanyika. Aidha, kaguzi 110,123 zilizohusu afya na usalama mahala pa kazi zimefanyika. Kufuatia kaguzi hizo, waajiri 1,162 walichukuliwa hatua kali mbalimbali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Serikali itaimarisha utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa kufanya ukaguzi katika maeneo ya kazi na kutoa elimu na ushauri kwa wafanyakazi, waajiri na vyama vyao. Lengo hapa ni kuelekeza namna bora ya kutekeleza sheria hizo; kuimarisha majadiliano ya pamoja baina ya waajiri na wafanyakazi pamoja na Serikali na pia ushirikishwaji wa wafanyakazi katika maeneo ya kazi kuititia Mabaraza ya Wafanyakazi ili kuongeza uzalishaji na tija, sambamba na kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Aidha, itashughulikia maombi ya vibali vya

kazi na maombi ya msamaha kwa raia wa kigeni wanaoomba kufanya kazi nchini.

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya jamii; katika Mwaka 2020/2021 gharama za uendeshaji wa Mifuko ya Pensheni ziliendelea kupungua kutoka asilimia 6.8 Mwaka 2019/2020 mpaka kufikia asilimia 5.4 Disemba, 2020. Sambamba na kushuka kwa gharama za uendeshaji, Mifuko ya Pensheni imeendelea kulipa mafao kwa wastaafu. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya wanachama 203,418 walilipwa mafao ya pensheni ya jumla ya shilingi bilioni 1,361.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2021/2022, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kusimamia utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ili kuwezesha kupata kanuni za ulipaji wa mafao ambazo zitakidhi matarajio ya wafanyakazi wa Sekta ya Umma na Binafsi na kuhakikisha mifuko inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali itaendelea kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuhakikisha kwamba Sera ya Kinga ya Jamii inakamilika. Aidha, Ofisi yangu ya Waziri Mkuu itaendelea kutekeleza majukumu yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha Taasisi zote za Hifadhi ya Jamii zinafuata Kanuni na Miongozo iliyopo ili kupunguza kero kwa wananchi wanaowahudumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi; Serikali imeimarisha usimamizi wa mabenki, mifuko na programu mbalimbali za uwezeshaji katika kuhakikisha kwamba wananchi wanawezeshwa kiuchumi kwa kupatiwa mikopo isiyo na riba au yenyewe riba nafuu ikiwemo mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri zetu. Lengo ni kuhakikisha Watanzania wengi wanajihusisha na shughuli za kiuchumi ili kujiongezea kipato na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi; katika Mwaka 2020/2021 Serikali inaendelea na mapitio na tathmini ya mifuko ya uwezeshaji wananchi ili

kuwezesha kuunganisha mifuko hiyo na hivyo kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija kubwa kwa wananchi. Katika kipindi hicho, hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa ajili ya kuwapa fursa wananchi wengi kufahamu kuhusu uwepo wa mifuko na programu hizo na fursa zinazopatikana.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo hayo, mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilifanya maonesho ya wiki moja kuanzia tarehe 7 hadi 13 Februari, 2021 kwenye Viwanja vya Sheikh Amri Abeid kule Jijini Arusha. Maonesho hayo yamewapatia fursa Watanzania kufahamu kwa undani mifuko na programu zilizopo, majukumu yake na fursa za uwezeshaji zinazopatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 mifuko na programu za uwezeshaji zimetoa mitaji ya masharti rafiki yenye thamani ya shilingi billioni 898.12 kwa wajasiriamali 3,614,857. Mitaji hiyo, imewanufaisha wananchi wanaojishughulisha na shughuli za uchumi zilizo katika sekta mbalimbali kama vile viwanda, afya, elimu, biashara, madini, uvuvi, ufugaji, kilimo na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2021 shilingi billioni 22.3 zimetolewa kwa vijana (asilimia 4), wanawake (asilimia 4) na watu wenye ulemavu (asilimia 2) ikiwa ni mikopo ya asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri. Ninaendelea kusisitiza halmashauri zote nchini kuzingatia matakwa hayo ya kisheria ya kutenga fedha zinazotokana na mapato ya ndani na kuhakikisha fedha hizo zinatolewa na kutumika kama ilivyokusudiwa kwa makundi hayo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuwezesha wananchi kiuchumi, Serikali imetekeliza miradi ya kimkakati yenye kuhusisha masoko na vituo vya basi. Miradi hiyo, sambamba na kuimarisha mapato ya ndani ya halmashauri husika imelenga kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi kwa wananchi hususan wanaozunguka maeneo hayo. Miiongoni mwa miradi iliyokamilika ni kituo cha mabasi

cha Magufuli cha Mbezi Luis, kilichopo Dar es Salaam, na Soko la Chifu Kingalu lililopo Manispaa ya Morogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni soko la Kagunga (Kigoma), Muhange (Kakonko), ghalia la mazao (Ruangwa) na Soko la Kisutu (Dar es Salaam). Miradi mingine 33 ya namna hiyo inaendelea kutekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali. Lengo la Serikali ni kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na hivyo kujiongezea kipato, kuboresha huduma katika maeneo husika na kuimarisha mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Serikali kwa Mwaka 2021/2022 ni kukamilisha zoezi la tathmini na kuiunganisha mifuko na programu za uwezeshaji ili kuleta ufanisi na tija iliyokusudiwa. Kadhalika, Serikali itahakikisha asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri inawafikia walengwa na kusimamia miradi ya kimkakati inayotekelizwa ili thamani ya fedha zinazotolewa ziweze kuendana pamoja.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji wa fursa za ajira na ujuzi; katika Mwaka 2020/2021 Serikali imechukua hatua za makusudi hususan utekelezaji wa miradi ya kielelezo, ujenzi wa viwanda, sambamba na kuimarisha sekta binafsi kwa ajili ya kuongeza fursa za ajira na ujuzi kwa Watanzania. Hadi kufikia Februari, 2021 ajira 594,998 zimezalishwa katika sekta mbalimbali. Kati ya hizo, ajira 314,057 zimetokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ajira za Serikali. Vilevile, ajira 280,941 zimezalishwa kuititia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ujuzi nchini, vijana 18,956 wamepatiwa ujuzi unaowawezesha kujajiri au kuajiriwa. Kati ya hao, vijana 5,538 wamepatiwa mafunzo ya uanagenzi (*apprenticeship*) katika fani za ufundi stadi ambapo wanaonufaika 77 ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, aidha, vijana 10,178 wamepewa mafunzo ya kurasimishiwa ujuzi walioupata kupitia mfumo usio rasmi wa mafunzo ambapo kati ya wanufaika hao 28 ni watu

wenye ulemavu. Vilevile, vijana 3,240 wamewezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu kazini (*internship*) katika taasisi binafsi na za Umma ambapo kati yao wahitimu 92 ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, 2021/2022, Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala ya ukuzaji ajira na kazi za staha katika sera, mikakati na mipango mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inapata ujuzi stahiki pamoja na kuongeza fursa za ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, masuala mtambuka; uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba, hapa Dodoma. Serikali imeanza maandalizi ya awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za kudumu za Wizara mbalimbali katika Mji wa Serikali Mtumba, hapa Dodoma yatakayotosheleza watumishi wote kufanya kazi zao kwenye majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Serikali imekamilisha usanifu wa majengo husika. Aidha, mradi wa ujenzi wa barabara (km. 51.2) kwa kiwango cha lami katika Mji wa Serikali umefikia asilimia 71.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI; kutokana na juhudzi za Serikali na wadau mbalimbali hali ya maambukizi ya UKIMWI imepungua. Hadi kufikia Desemba 2019, inakadirisha kuwa Watanzania milioni 1.7 waendelea kuishi na VVU. Aidha, takwimu zinaonesha kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka watu 130,000 mwaka 2001 hadi watu 77,000 mwaka 2019. Hali kadhalika, vifo vimeitungu kutoka 52,000 mwaka 2010 hadi kufikia vifo 27,000 mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maambukizi hayo, Serikali imeimarisha huduma za tiba ikiwemo matumizi ya dawa za *ARV* na afua za kinga zinazotekelzeza na wadau mbalimbali nchini. Hadi Desemba, 2020 zaidi ya watu milioni 1.36 walikuwa wanapata huduma za dawa za *ARV*. Aidha, juhudzi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kutoa afua za

mabadiliko ya tabia, tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Spika, takwimu zetu zinaonesha kuwa vijana wengi ndio wanaoathrika na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Hivyo, napenda kusisitiza kuwa kampeni za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia kwa vijana ni lazima ziwe endelevu kupitia njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, kazi za wasanii ziendelee kuelimisha kwa vijana wetu. Pia niendelee kuitaka Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iendelee kufanya kazi na itumie majukwaa na iendelee kuwatumia wasanii wetu ili kufikisha ujumbe kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2021/2022, Serikali itaendelea kufanya jitihada za kupunguza kasi ya maambukizi mapya na vifo vinavyotokana na UKIMWI katika jamii kwa kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali muhimu kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Aidha, itapunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kuimarisha huduma za elimu ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya dawa za kulevy; Serikali imeendelea kupambana na dawa za kulevy ambapo katika kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021 watuhumiwa wa dawa za kulevy 5,374 walikamatwa. Katika kipindi hicho, kilogramu 67.2 za *heroin* na kilogramu 1.96 za *cocaine* pamoja na tani 12.8 za bangi, tani 6.1 za mirungi na tani 57.6 za kemikali bashirifu zilikamatwa. Aidha, mashamba ya bangi 39 yenye jumla ya ekari 49 yaliteketezwa kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevy na kusogeza huduma karibu na wananchi, Serikali imefungua Ofisi mbili za Kanda za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy katika Mikoa ya Mtwara na Mwanza. Kwa upande mwingine, Serikali imeongeza vituo vya kutolea huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevy kutoka vituo sita mwaka 2019/

2020 hadi kufikia vituo tisa vinavyohudumia waathirika wapatao 10,567.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, 2021/2022, Serikali itaendelea kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevyta nchini, kutoa elimu kwa Umma juu ya athari za biashara na matumizi ya dawa za kulevyta, kudumisha ushirikiano na nchi nyngine katika kupambana na dawa za kulevyta na kuendelea na upanuzi wa tiba ya *methadone* katika vituo vingine vitakavyoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, maafa; Serikali imeimarisha uwezo wa usimamizi wa maafa nchini ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga. Katika Mwaka 2020/2021, Serikali imewezesha upatikanaji wa vifaa vya huduma za kibinadamu na hivyo kuongeza utayari wa kukabiliana na maafa. Sambamba na kutoa elimu kwa Umma na Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa, Serikali imekamilisha taratibu za kumiliki eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa hapa Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mwaka ujao wa fedha, Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa, kuimarisha uwezo wa usimamizi wa maafa nchini na kuchukua hatua stahiki katika kuzuia au kupunguza, kuijiandaa na kukabiliana na maafa yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira; Serikali imeendelea kusimamia matumizi ya rasilimali na maliasili ili kuleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kuwa na mazingira endelevu. Lengo hapa ni kuhifadhi mazingira, kupambana na uharibifu wa mazingira na athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imefuatilia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 pamoja na kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Kupiga Marufuku Matumizi ya Mifuko ya Plastiki nchini za mwaka 2019. Lengo la Serikali hapa ni kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya mifuko mbadala

pamoja na vifungashio vyatupi plastiki vinayokidhi viwango viliviyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*).

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imetekeleza miradi na shughuli wezeshi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania; Mradi wa Kusaidia Kujenga Uwezo wa Taasisi na Jamii Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Kwenye Maeneo ya Kaskazini mwa Nchi; Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa; Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumo ya Ikolojia Vijijiini na Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu hifadhi ya mazingira hapa nchini. Kupitia utekelezaji wa miradi hiyo, ajira 729 zimetengenezwa wakati shughuli wezeshi zimezalisha ajira 1,528.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha, Serikali itaandaa na kutekeleza mikakati, mipangokazi na miongozo mbalimbali ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Aidha, itaratibu, kufuatilia na kupima utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Utawala Bora; katika kuimarisha masuala ya utawala bora Bunge lako Tukufu kwenye Mkutano wake wa pili mwezi Februari 2021 lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa Mwaka 2021. Sheria ile imefanya marekebisho katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya 1), Sheria ya Mahakama za Mahakimu (Sura ya 11) na Sheria ya Mahakama za Migogoro ya Ardhi (Sura ya 216).

Mheshimiwa Spika, mabadiliko haya muhimu yameweka msingi kwa Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya sheria na lugha ya mahakama, mabaraza na vyombo vingine

vyenye jukumu la kutoa haki badala ya Kiingereza kama ilivyokuwa hapo awali. Mabadiliko hayo, yanazingatia ukweli kwamba Kiswahili ndio Lugha ya Taifa, lugha ambayo inaeleweka na inatumika na kila mmoja ndani ya jamii yetu na nchi jirani ambazo sasa zinaanza kutumia lugha hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, marekebisho hayo yataboresha mfumo wa upatikanaji haki kwa wananchi ambao ndio walengwa wa sheria husika. Vilevile, Serikali inaendelea na zoezi la kutafsiri sheria kuu na sheria ndogo zote ambazo ziliandikwa kwa Kiingereza kwenda kwenye Lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali itayafanya kazi maoni na ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2021 ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha mfumo wa upatikanaji haki hapa nchini. Aidha, kuanzia sasa Serikali itatayarisha na kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu miswada yote ya Sheria kwa Lugha ya Kiswahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la utawala bora lilioimariswa ni mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali za Umma. Serikali ilichukua hatua ya kufungua jumla ya mashauri sita kwenye Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Divisheni ya Mahakama Kuu na kufikisha jumla ya mashauri 21 yaliyosajiliwa katika mahakama hiyo. Hadi Februari, 2021 mashauri matano yamehitimishwa na mengine 16 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango na Bajeti ya mwaka 2021/2022, Serikali pamoja na mambo mengine imepanga kukamilisha zoezi la kutafsiri sheria kuu na sheria ndogo zote kutoka Lugha ya Kiingereza kwenda Lugha ya Kiswahili na kutekeleza mipango ya kitaifa ya masuala mtambuka yanayohusu vita dhidi ya rushwa na ujisadi.

Mheshimiwa Spika, Muungano; katika Mwaka 2020/2021, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kushirikiana kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuulinda, kuuenzi na kuudumisha Muungano wetu kwa lengo la kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili kufurahia matunda yake.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Julai, 2020 kilifanyika kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kwa ajili ya kushughulikia masuala ya Muungano. Miiongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni tukio la kihistoria la kusainiwa kwa makubaliano ya kuondoa hoja tano zilizopatiwa ufumbuzi kwenye orodha ya hoja za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja hizo tano zinajumuisha ushirikishwaji wa SMZ kwenye masuala ya kimataifa na kikanda; ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; gharama za kushusha mizigo kwenye Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayotoka Zanzibar; utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na utaratibu wa Vikao vyta Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kushughulikia masuala ya Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, miiongoni mwa faida za kusainiwa kwa hati hizo ni kuimarisha Muungano hususan ushiriki wa nchi katika Jumuiya za Kikanda pamoja na ushirikiano katika sekta ya uchukuzi. Kwa msingi huo, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano kwa jitihada zao kubwa katika kuhakikisha Muungano wetu unaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2021/2022, Serikali itaendelea kuimarisha uratibu wa vikao vyote vyta Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ili kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizopo na zitakazojiteza kwa madhumuni ya kuuenzi, kuulinda na kuudumisha

Muungano wetu. Kuratibu masuala ya kiuchumi pia nayo itakuwa ni sehemu ya agenda na kijamii kwa kufuatilia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa pande mbili za Muungano; lakini pia kutoa elimu ya muungano kwa umma kwa makundi tofauti ya kijamii; na kuratibu masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya ushirikiano vya Wizara, Idara na Taasisi za SMT na SMZ zisizo za Muungano zenyenye majukumu yanayoshabihiana.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa. Tanzania imeendelea kuheshimu misingi ya ushirikiano na mataifa mengine duniani zikiwemo Taasisi za Kimataifa na Kikanda sambamba na kusimamia, kulinda na kutetea maslahi yake ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiusalama huko nje. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Serikali imeendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji, watalii na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje ya nchi kwa lengo la kukuza uchumi na Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kutumia ziara za viongozi wakuu wa kitaifa kutoka nje pamoja na majukwaa ya kimataifa na kikanda katika kukuza ushirikiano kwenye nyanja za biashara, uwekezaji, masoko ya bidhaa zetu, utalii na lugha ya Kiswahili ili kuchochea maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 tuliwapokea Waheshimiwa maraisi kutoka nchi mbalimbali, Mheshimiwa Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi alikuja hapa nchini, Mheshimiwa Dkt. Lazarus McCarthy Chakwera, Rais wa Jamhuri ya Malawi alikuja hapa nchini, Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda naye alikuja hapa nchi na Mheshimiwa Sahle-Work Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia, mwanamke shupavu naye pia alikuja hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ziara za viongozi hao zimekuwa na mafanikio makubwa katika nyanja za kiuchumi na kuimarisha ujirani mwema. Kwa mfano, ziara ya Rais wa Burundi ilikuwa chachu ya kufanyika kwa Mkutano wa Tume

ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Burundi tarehe 3 hadi 5 Machi, 2021 uliofanyika mijini Kigoma. Lengo la mukutano ule, lilikuwa ni kuimarisha ushirikiano katika maeneo ya uchukuzi, biashara, nishati, utalii, ulinzi pamoja na masuala ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda mwezi Septemba mwaka 2020, iliwezesha kujenga mazingira mazuri kuelekeea utiaji saini wa mkataba wa mwisho wa utekelezaji wa ujenzi wa bomba la kusafirishia mafuta ghafi kutoka Uganda kuja hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, akiwa nchini Tanzania mwezi Januari 2021, Mheshimiwa Sahle-Work Zewde, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia alieleza utayari wa nchi yake kukifanya Kiswahili kuwa moja kati ya lugha zinazozungumzwa nchini humo sambamba na kushirikisha kwenye fursa ya mafunzo katika sekta ya usafiri wa anga na uwekezaji katika sekta ya viwanda vya kuzalisha bidhaa za ngozi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jumuiya za Kikanda, Rais wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikabidhi Uenyekiti wa SADC kwa Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji katika Mkutano wa 40 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika kwa njia ya mtandao Agosti 2020. Jambo la kujivunia wakati wa uenyekiti wa hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ni lugha ya Kiswahili kuongezwa kuwa moja ya lugha rasmi za SADC. (*Makofii*).

Mheshimiwa Spika, masuala mengine ya kuanzishwa kwa Baraza la Biashara linalolenga kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza mtangamano wa kanda; kuhamasisha utendaji na uendelezaji wa viwanda kwa lengo la kukuza ajira. Pia biashara ya mapato ya nchi wanachama pamoja na kufanikisha kuandaliwa kwa Mwongozo wa Uwezeshaji Biashara na Usafirishaji katika kipindi cha *COVID-*

19 ambao nchi zote ziliendelea kuutekeleza kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa Serikali kwa mwaka wa fedha ujao 2021/2022 kwa upande wa mahusiano ya kimataifa ni kutekeleza diplomasia ya uchumi, kudumisha na kuimarisha mahusiano ya Tanzania na mataifa mengine, kushiriki katika shughuli za Umoja wa Mataifa na Mashirika yake, Umoja wa Afrika na jumuiya za kikanda, pia nao utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Tanzania itashiriki katika juhudzi za kuleta amani na usalama kwenye Jumuia za Kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama; sambamba na kulinda na kutetea misingi na maslahi ya Taifa letu ndani na nje. Wakati tunaelekea huko, tunatekeleza hayo, ni matarajio yetu kuwa mataifa mengine nayo yataendelea pia kuheshimu uhuru wa nchi yetu hususan katika kujiamulia mambo yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika Mkutano wa Pili wa Bunge lako Tukufu kuititia kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu, nilitoa maelekezo kwa Balozi zetu zote kuanzisha vituo vya kujifunza Kiswahili. Hatua hiyo inakwenda sambamba na kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili ndani na nje kwa kutoa mafunzo ya matumizi sanifu na falsafa ya Kiswahili. Hatua nyiningine ni kutoa ithibati kwa vitabu vya lugha ya kiswahili vinavyokusudiwa kutumika shulenii. Vilevile kufanya tafsiri ya nyaraka mbalimbali na kuanzisha mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuendelea kukua kwa sekta ya sanaa, michezo na burudani bado mchango wake katika uchumi ni mdogo. Kwa mfano, tangu mwaka 2013 hadi mwaka 2019 sekta ya sanaa na burudani ilichangia asilimia 0.3 kwenye pato la Taifa. Hata hivyo, sekta hii inapata hamasa kubwa, inaa jiri vijana wengi kwa sasa na imekuwa miongoni mwa sekta zinazotumika kulitangaza Taifa letu nje na wakati mwininge kuvutia utalii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa changamoto zinazoikumba sekta ya michezo, sanaa na burudani ni eneo la kiufundi na mbinu. Hili linadhihirishwa na uwepo wa walimu wengi wa kigeni hususan kutoka baadhi ya nchi jirani kwenye michezo wa soka. Kwa mantiki hiyo, natumia nafasi hii kutoa maelekezo kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na kurugenzi zake zilizo ndani ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuja na mkakati wa kuendeleza wataalam wetu wa michezo wa ndani wa sanaa walioko ndani lakini na burudani kupitia ubunifu kwa ushirikiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na nchi washirika kwenye eneo la utamaduni, michezo na sanaa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaweka mazingira bora ya kuimarisha michezo nchini kwani faida za michezo ni nyinyi, ikiwemo ajira kwa vijana, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, kinga kwa tiba na magonjwa yasiyoambukizwa.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Nimeelezea kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza. Aidha, nimetoa mwelekeo wa kazi zitakazofanyika katika mwaka 2021/2022. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa kisekta yatawasilishwa na Mawaziri watakapokuja kuwasilisha bajeti zao za kupitia wizara zao. Kwa kuhitimisha napenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo ambayo Serikali itatekeleza kwa umuhimu wake, kama ifuatavyo:- (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, moja; kuenzi na kuendeleza jitihada, maono, juhudhi za Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan katika ulinzi wa rasilimali za Taifa, nidhamu katika matumizi ya fedha za umma, utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kuenzi lugha ya Kiswahili, mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi, kuunganisha na kuwajali wananchi wanyonge na kudumisha umoja wa kitaifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mbili, kutekeleza kwa kasi miradi ya kimkakati ambayo inalenga kukuza uchumi, kuimarisha

huduma za jamii na kuongeza fursa za ajira. Kwa kasi tulioanza nayo, Serikali itaendelea kuongeza nguvu zake na hatimaye kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuimarisha huduma za jamii zikiwemo afya, elimu na maji pamoja na utekelezaji wa miradi inayoendelea na uanzishwaji wa miradi mipya;

Mheshimiwa Spika, nne, kuimarisha makusanyo ya mapato kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na mashine za *POS* na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma na kuendeleza rasilimali fedha katika miradi ya kimkakati na kielelezo. Na katika hili la matumizi ya *ki-electronic* hatua kali zitachukuliwa dhidi ya taasisi ambayo tumeiyagiza kutumia mifumo ya *ki-electronic* na bado haitumlii mifumo hilo ya *ki-electronic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tano; kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali zinazolenga kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, sita; kuchukua hatua za kukabiliana na majanga mbalimbali ikiwemo magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Watanzania wote bila kujali itikadi za kisiasa, dini au ukabila waendelee kufanya kazi kwa bidii, kwa weledi, kwa uadilifu, kwa tija na ufanisi; lakini pia uaminifu na kupiga vita rushwa ili tuweze kulinda mafanikio tuliyoyapata. Jitihada hizo ndizo zitatuvwxyzesa kuingia katika nchi ya uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2021/2022. Kwa mwaka 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake inaliomba sana lako Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 116,784,244,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 93,303,370,000.00 ni kwa ajili ya matumizi

ya kawaida na Shilingi 23,480,874,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 128,873,377,000.00 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge letu. Kati ya fedha hizo, shilingi 121,875,906,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 6,997,471,000.00 ni kwa ajili ya maendeleo. (*makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

(*Hoja Ilitolewa lamuliwe*)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba ambayo umewasilisha vizuri sana na kwa *details* za kutosha. Na Waheshimiwa Wabunge hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ipo ndani ya Kishikwambi chetu pamoja na hotuba za wenyeviti wa kamati zote zipo humu ndani chini ya dirisha lililoandikwa hotuba za bajeti. Kwahiylo zote zipo mle ndani, ahsante sana kwa kutuanzishia *marathon* hii ya Hotuba za Bajeti, ambapo kama ilivyo ada huwa tunaanza Ofisi ya Waziri Mkuu.

Sasa kabla hatujaendelea naomba niwatambue baadhi ya wageni wetu ambao pia tunao hapa ikiwepo na viongozi vyama vya siasa, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa Mheshimiwa John Shibuda, ahsante sana, karibu sana Mheshimiwa Shibuda.

Pia yupo Katibu Mkuu wa Chama cha DP ndugu Abdul Mluya, karibu sana Abdul Mluya pale ulipo.

Wengine ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Wenyeulemvu Ndugu Ernest Kimaya popote pale ulipo. Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) Dkt. Aggrey Mlimuka, karibu sana. Rais wa TUCTA Ndugu Tumaini

Nyamhokya, karibu sana, mwakilishi wa ALO Ndugu Edmund Mushi karibu pale ulipo, mwakilishi wa *UNFPA* Dkt. Majaliwa Marwa, karibu sana, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri wa Watu Wenye Ulemavu Dkt. Lucas Kija, karibu sana, Mwakilishi mkazi wa *UNDP* Ndugu Christine Musisi, Christine Musisi karibu sana sana Christine. Rais wa *Chamberya Wafanya Biashara*, Viwanda na Kilimo Ndugu Paul Koi, ahsante sana. Mwenyekiti wa Shirikisho la Umoja wa Machinga kifupi wanaitwa *SHIUMA* Ndugu Ernest Matondo, ahsante sana. Mwenyekiti *TPSF* Ndugu Angeline Ngalula, ahsante sana.

Tunao wahadhili wawili wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Neema Robert na Dkt. Amina Abdul; karibuni sana, na wageni wote wengine ambao hatukupata majina yao hapa karibuni sana, wote kwa pamoja mnakaribishwa. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge ili twende kisayansi na tumalize kwa wakati wake nawaomba wenyeviti wanne hawa wanaokuja tukianza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria *mta-present* hapa kwa dakika kumi tu badala ya nusu saa, kila mmoja *ten minutes*. Na tunachokihitaji hapa ni maoni na ushauri wa kamati tu. Zile ngonjera zingine ziachenii kwa sababu tayari kwenye Kwishikwambi cha Waheshimiwa Wabunge yote yamo watayapitia kwa wakati wao, tunachohitaji hapa *ku-capture* ni maoni na ushauri wa kamati *ten minutes*.

Mwenyekiti wa Katiba na Sheria tuanze, na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ajiandae, Katiba na Sheria na wale wengine wote Wenyeviti muwe karibu karibu hapa. Naona anakuja Mheshimiwa Najma Giga, karibu sana, karibu Makamu Mwenyekiti wa Kamati. (*makofi*)

MHE. NAJMA MURTSAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijaanza naomba Taarifa ya Kamati iingine kwenye taarifa rasmi za Bunge kama iliyowasilishwa mezani. Na sasa naomba niende moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa kamati kama ambayo

umeelekeza; Fungu 37 na Fungu 25. Kwa kuwa utaratibu wa shughuli za Serikali unaotekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu unawezesha na bajeti ya matumizi ya kawaida ya mafungu 37 na 25 ikiwemo shughuli za Waziri Mkuu mwenyewe na wasaidizi wake ambapo kupungua kwa makidiro ya bajeti ya matumizi ya kawaida kunaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vyta ofisi hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa kwanza, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Ofisi hiyo iandae na kuwasilisha bajeti ya matumizi ya kawaida yenye kuendana na uhalisia wa mahitaji ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Ofisi hiyo ili kamati iweze kushauri ipasavyo. Na pili, Serikali ihakikishe kuwa fedha zote zinazoizinishwa na Bunge kwa ajili ya kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake ya uratibu ziwe zinatolewa kwa wakati kwa lengo la kuiwezesha Ofisi hiyo muhimu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 65 Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;

(a) Wakala wa Usalama na Afya mahala pa Kazi (*OSHA*). Pamoja na kamati kubaini kuwa uwezo wa Wakala huu umeendelea kuongezeka katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria pamoja na kutekeleza ushauri wa kamati kuhusu kuchukua hatua za kufuta baadhi ya tozo zenye kero kwa wadau wake. Kamati inaendelea kushauri kuwa:-

(i) Wakala uendelee kubuni mikakati endelevu ya kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa viwanda nchini katika kulinda usalama wa wafanyakazi.

(ii) Kuimarisha kitengo chake cha Elimu kwa umma ili kuweka msisisitizo mkubwa katika utoaji wa Elimu na kuimarisha mahusiano ya karibu na Wadau wake ili kuvutia wadau wengi

kutii sheria za usalama mahala pa kazi pasipo kutumia nguvu kubwa isiyo ya lazima,

(iii) Kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana karibu na taasisi nyingine za Serikali kwa lengo la kupunguza urasimu usiyo wa lazima kwa Wawekezaji na kupunguza gharama zisizo za lazima, hatua ambayo inaweza kuwakatisha tama wawekezaji hao, na

(iv) Serikali ichukue hatua za dhati katika kuondoa changamoto ya kukaimishwa kwa Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa OSHA kwa zaidi ya Miaka Mitano (5), bila kupatikana kwa Mtendaji Mkuu, changamoto ambayo inaathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Wakala huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi yaani *WCF*. Pamoja na Kamati Kubaini mafanikio makubwa yaliyofikiwa na Mfuko huu kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015 katika kukusanya mchango, kufanya uwekezaji na kutoa mafao kwa wafanyakazi wanaoumia wakiwa kazini mafao ambayo hayatolewa katika Mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii. Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Serikali ihakikishe inaimarisha Mfuko huu na kuufanya kuwa endelevu kwa lengo la kujenga imani kwa sekta binafsi kama wawekezaji muhimu wa mfuko pasipo kuyumbisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni zake, kwa lengo la kuhakikisha kuwa Mfuko huu unaendelea kuwa kichocheo kikubwa cha uwekezaji na wafanyakazi wao kwa kuendelea kutofautisha na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii kama inavyoelekeza sheria yake.

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa waajiri na wafanyakazi hususan kwa Vyama vya Wafanyakazi, kwa lengo la kuhakikisha kuwa waajiri wote nchini wanazingatia matakwa ya sheria katika kuhakikisha wanajiardikisha kwenye Mfuko, wanalipa ada na michango kwa wakati na kutoa taarifa sahihi.

(iii) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya *TEHEMA* katika kuendesha shughuli zake hususan katika kuwafikia wadau wake nchi nzima pia kukusanya michango kwa mujibu wa sheria na kutoa huduma kwa wakati kwa wanufaika wake.

(iv) Mfuko uendelee kuimarisha mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya kupata fidia inayostahiki.

(c) Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa kuwa moja ya malengo ya Serikali ya kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mwaka 2018 na kuanzishwa mifuko miwili ambayo ni Mifuko ya Hifadhi ya NSSF na Mfuko wa Hifadhi wa Jamii kwa Watumishi wa Umma (*PSSSF*), ilikuwa ni kuhakikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inatoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na mifuko hii kuendelea kupanua wigo wa kuongeza wanachama na kufanya uwekezaji wa kimkakati wenye tija kwa Taifa na kupata faida kwa wakati. Hivyo basi, Kamati sasa inashauri kuwa:-

(i) Mfuko wa NSSF uanzе kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza wanachama wapya hususan vijana walio katika sekta isiyo rasmi, wanavyuo na makundi yenye mahitaji maalum na kuwajengea uwezo ili wawe wanachama endelevu wa Mfuko kwa maendeleo yao na kuwezesha Mfuko kuongeza makusanyo endelevu.

(ii) Mfuko wa NSSF kukamilisha mkakati wake wa kutangaza huduma na fursa mbalimbali zilizopo kwa makundi mbalimbali hususan katika sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza program maalum ya kutumia baadhi ya Wabunge vijana na baadhi wanavyuo kwa ajili ya kuwaandaa na kuwatumia katika kutangaza fursa za Mfuko huo, kwa lengo la kuhamasisha makundi mengi ya kijamii kuijunga na Mfuko kuanza, kuchangia na kunufaika na fursa mbalimbali za uwekezaji kwa ustawi wa makundi hayo.

(iii) Mfuko wa NSSF uboreshe mkakati wake kwa wateja wa miradi yake ya nyumba kwa kupunguza bei ya mauzo na bei za pango za nyumba hizo ili kuwawezesha Watanzania wenye kuhitaji huduma hiyo kununua au kupanga nyumba hizo. Hii ni pamoja na kuendelea na mkakati wake wa kufanya mazungumzo na vyuo vikuu nchini ili viweze kukodi baadhi ya nyumba kwa ajili ya mabweni badala ya kuacha nyumba hizo bila ya kupata wapangaji au wanunuvi wa muda mrefu.

(iv) Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii ianze kufanya uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya viwanda kwa kuzingatia masharti ya Sheria za Uwekezaji wa Fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hali ya uendelevu mifuko, ustawi wa wanachama wake na Taifa kwa ujumla. Hatua hiyo iambatane na kufanyika kwa tathmini ya kina kuhusu uwekezaji unaotarajiwa kabla ya kutumia fedha za wanachama kwa miradi ambayo haina tija na mfuko. (*Makofii*)

(d) Mheshimiwa Spika, masuala ya watu wenye ulemavu. Pamoja na Kamati kuendelea kuridhishwa na hatua ya Serikali kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Masuala ya Watu Wenye Ulemavu Nchini, ikiwemo kuanzisha rasmi Baraza la Taifa la Kuratibu masuala ya kundi hili kwa ujumla na kuwepo ongezeko la bajeti kwa Kitengo hicho, kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Kitengo katika kuratibu masuala masuala ya watu wenye ulemavu kwa ufanisi Zaidi, Kamati imeshauri kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inachukua hatua za dhati za utatuzi wa changamoto zifuatazo:-

(i) Kubaini na kutambua Vyama vyote vya Watu Wenye Ulemavu Nchini na kwa kuvipatia elimu ya kutosha kuhusu usimamizi wa haki za watu wenye ulemavu na jinsi ya kuzifikia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali na wadau wengine wa maendeleo kwa ajili kundi hilo maalum.

(ii) Kubaini na kutatua migogoro mbalimbali inayoendelea kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Nchini ambapo inaathiri ustawi wa vyama hivyo na hivyo

kukwamisha baadhi ya makundi hayo na kufikia fursa za kujkwamua kiuchumi.

(iii) Kuandaa na kuziandaa kanzidata ya Taifa ya watu wenye ulemavu nchini yenye kuainisha idadi watoto, vijana, watu wazima, wazee, mikoa na wilaya wanazoishi na majina ya vyama vyao vinavyoratibu masuala yao kwenye maeneo yao, kwa lengo lenye kurahisisha uratibu wa haki na fursa zao kwa kuanzia ngazi za Vijiji, Mtaa, Kata, Tarafa, Wilaya, Mikoa hadi Taifa.

(iv) Kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mfuko Maalum wa masuala ya watu wenye ulemavu kwa kuandaa mfumo mzuri wa vyanzo vya fedha mfuko kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya ustawi wa kundi hilo maalum.

(e) Mheshimiwa Spika, maendeleo ya vijana. Kamati imebaini kuwa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007 imepitwa na wakati ukilinganisha na mabadiliko makubwa yanayotokea nchini kwa sasa, ambapo tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza mchakato wa kuboresha sera hiyo ili iendane na wakati. Hivyo basi, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa:-

(i) Ikamilishe mchakato ya kubadilisha Sera ya Maendeleo vijana na iwasilishe Rasimu ya Maboresho ya Sera hiyo kwa Kamati ili Serikali ishauriwe ipasavyo. (*Makofii*)

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI wafanye maboresho ya Uratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuwepo mfumo mmoja wa vyanzo vya fedha vya maendeleo ya vijana nchini, hatua ambayo itasaidia kuondokana na changamoto ya kuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Nchini, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambaa hawapokei fedha yoyote kila mwaka pamoja na mfuko huo kuwa unatengewa bilioni moja kila mwaka wa fedha. Aidha, hatua hiyo iambatane na kuongeza usimamizi na udhibiti wa fedha zote za mikopo zinazotolewa kwa ajili

ya vijana ili zirejeshwe kwa wakati na vijana wengi wanufaike na fursa hiyo.

(f) Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini, Mradi Na. 6581. Kwa kuwa Kamati imebaini kuwa kuwepo kupungua kwa bajeti ya Program ya Kukuza Ujuzi Nchini mwaka hadi mwaka kutoka shilingi billioni 18 kwa mwaka wa fedha 2016/2020 hadi billioni 9 kwa mwaka 2021/2022, pasipo kujali wakati huu ambaeo Serikali inajenga miradi mingi nchi nzima yenye kuhitaji vijana wenyewe ujuzi unaotakiwa ili vijana wengi waweze kushiriki fursa ya ajira katika miradi hiyo, hivyo basi, Kamati inashauri kuwa:-

(i) Ofisi ya Waziri Mkuu ijipange kimkakati na kuhakikisha kuwa bajeti ya mradi huu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inakuwa halisi na kuongezea fedha hadi kufikia shillingi billioni 18 kama bajeti ya uhalisia wa mahitaji ya programu hiyo ilivyodhamiria na kuhakikisha kuwa vijana walio wengi wanaohitimu ngazi mbalimbali za masomo nchini wanaendelea kujengewa ujuzi kwa lengo la kuwawezesha kumudu ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi yetu.

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu wajipange kimkakati kutangaza huduma zinazotolewa na programu hiyo na jinsi ya kuziflikia kwa lengo la kuwawezesha vijana wanaohitimu masomo katika ngazi mbalimbali kujengewa ujuzi ili waweze kujajiri na kupata ajira katika taasisi mbalimbali ndani na nje Nchi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili la Kumi na Mbili kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Vilevile, nashukuru kwa msaada wa karibu sana unaon��leak kutoa kwa Kamati yetu katika kuwawezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa na pia kunipa nafasi hii ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge kwa weledi

na umahiri wake wa kusaidia kuongoza Bunge. Pia niipongeze Kamati ya Uongozi kwa kazi nzuri inayofanya kushauri na kusaidia kuendesha shughuli za Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika utekelezaji wa majukumu mliyopewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hakika alikuwa msaada mkubwa kwa Kamati hii na sisi tutaendelea misingi mizuri aliyoituachia. Naye tunamtakia afya njema na mafanikio mema katika majukumu yake mapya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama kwa ushirikiano wake mkubwa na wenye tija, uchapakazi wake mzuri na wenye nidhamu na unyenyekevu mkubwa kwa Kamati na hivyo kurahisisha shughuli za Kamati na shughuli za Waziri Mkuu anaye mwakilisha.

Aidha, tunawashukuru wasaidizi wake ambao ni Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wote wanaoongoza taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa ushirikiano wao mzuri katika kufanikisha shughuli za Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kipekee tunamshukuru na kumpongeza aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi, Ndugu Masha Mshomba ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Hifadhi ya Jamii *NSSF*, kwa ushirikiano mzuri wa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa kuongoza na kufanikisha vipaumbele vya mfuko huo katika kipindi chote kwa maendeleo ya Taifa, kwa ustawi wa Jamii wa Tanzania. Tunamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wao naomba majina yao yaingie kwenye *Hansard*.

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama iliyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Jijini Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya **Kanuni ya 118 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Hivyo basi, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6 (2) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, Watu na wenge Ulemavu.

Aidha, **Kifungu cha 7(1)(a)** cha Kanuni za Kudumu za Bunge, inazitaka Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti hutekelezwa sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha, kwa mujibu wa **Kanuni ya 117(1) na (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba tarehe 17 Machi, 2021, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua Miradi ya ujenzi wa Nyumba inayotekelzeza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) Jijini Dar Es Salaam pamoja na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa kukuza ujuzi nchini (**Mradi Namba 6581, Fungu 65**) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi hiyo, kwa Mafungu yote Sita (6) yaliyo chini ya Ofisi hiyo, tarehe 28 Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa **Kanuni ya 118 (4)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatoa sharti kuwa, kabla ya taarifa za utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kujadailiwa Bungeni, zichambuliwe na Kamati za Bunge za Kisekta, hivyo, naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Katiba na Sheria imechambua Mafungu Sita (6) ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira, na Watu wenye Ulemavu na kuridhia kuwa mapendekezo hayo ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ilivyowasilisha na Mtoa Hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Mafungu hayo ni:-

- i) **Fungu 37** - Ofisi ya Waziri Mkuu,
- ii) **Fungu 25** - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu,
- iii) **Fungu 65** – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,

- iv) **Fungu 15** - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA),
- v) **Fungu 61** - Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na
- vi) **Fungu 27** - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-

- i) Tathmini inayotokana na ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha;
- ii) Uchambuzi wa Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na;
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na ziara na uchambuzi wa Kamati.

2.0 TATHMINI INAYOTOKANA NA ZIARA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza **Kanuni ya 117 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kwa kibali chako, mnamo tarehe 17 Machi, 2021, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua Miradi iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Orodha ya miradi hiyo inajumuisha utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya NSSF katika maeneo ya Kijichi, Tuangoma na Mzizima Jijini Dar Es Salaam. Kabla ya ziara hiyo, tarehe 12 Machi, 2021, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi na tathmini ya Kamati, umeonesha kuwa, utekelezaji wa Miradi ya Nyumba za NSSF katika maeneo ya Kijichi, Tuangoma na Mzizima Jijini Dar Es

Salaam, ni miradi yenye tija kwa Taifa, mbali na changamoto kadhaa kama ifuatavyo:-

2.1 Mradi wa Ujenzi wa Nyumba Mtoni Kijichi

Mheshimiwa Spika, Mradi huu umegawanywa katika awamu tatu za utekelezaji, ambapo awamu ya kwanza na ya pili zimekamilika na awamu ya tatu iko katika hatua za mwisho za utekelezaji. Awamu hizi zilianza katika vipindi tofauti kuanzia awamu ya kwanza iliyoanza mwezi Novemba 2008 na kukamilika Mei 2009 na Awamu ya pili iliyoanza Mwezi Machi 2011 na kukamilika Desemba 2012.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya tatu ya ujenzi iliyokaguliwa katika ziara ya Kamati, ilianza kutekelezwa mwezi Disemba, 2013 na mpaka sasa ujenzi haujakamilika. Zipo sababu mbalimbali zillizochelewasha kukamilika kwa awamu hii, ikiwemo baadhi ya wakandarasi kuondoka eneo la ujenzi na migogoro mbalimbali ya kimkataba kati ya wakandasi na Mfuko. Katika hatua za kukabiliana na baadhi ya changamoto zilizojitokeza, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) uliiomba Mmalaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kufanya ukaguzi maalum. Katika kujiridhisha zaidi kuhusu utekelezaji Kamati ilichambua Taarifa zilizowasilishwa na kubaini kama ifuavyo:-

2.1.1 Gharama za Mradi

Mheshimiwa Spika, taarifa ya NSSF iliyowasilishwa mbele ya Kamati imebainisha kuwa, awamu ya kwanza ya mradi iliyokamilika imegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni Tano na Milioni Tatu,Laki Tano Arobaini na Sita, Mia Mbili Kumi na Saba na senti Sabini na Moja (5,003,546,217.71)** pamoja na VAT, awamu ya pili ya mradi imegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Saba Thelathini na Tisa, Laki Sita Sabini, Mia Tisa Themanini na Moja na Senti Themanini na Moja (17,739,670,981.10)** pamoja na VAT na awamu ya tatu ambayo haijakamilika, hadi sasa, imegharimu kiasi cha **Shilingi Bilioni Mia Moja na Tatu, Milioni Mia Nane Kumi na Mbili na Thelathini na moja Elfu, Mia Nne Sitini na Saba na**

senti themanini na moja (103,812,031,467.81). Uchambuzi wa Kamati kama inavyobakia katika Jedwali Na 1 na Grafu Na. 1, za Taarifa hii unaonesha mambo yafuatayo:


- i) Mradi wa Nyumba Mtoni Kijichi ambao hadi sasa umefikia awamu ya tatu, kabla ya kukamilika, umegharimu jumla ya Shilingi Bilioni Mia Moja Ishirini na sita, milioni mia tano Hamsini na tano, laki mbili Arobaini na nane, Mia sita sitini na sita na senti sitini na mblili (126,555,248,666.62) pamoja na kodi ya ongezeko la thamani (VAT);
- ii) Awamu ya kwanza na ya pili ambazo zimekamaikia zimegharimu jumla ya shilingi bilioni ishirini na mbili, milioni mia saba arobaini na tatu, laki mbili na elfu kumi na saba, mia moja tisini na nane na senti themanini na moja ikiwemo kodi ya ongezeko la thamani;
- iii) Awamu ya kwanza na ya pili, ambazo zimekamilika, zimechukua jumla ya **asilimia 18** ya gharama za mradi hadi sasa,
- iv) Awamu ya **Tatu** ambayo haijaakamilika, imefikisha **asilimia 82** ya gharama za mradi hadi sasa.

Jedwali Na 01: Mchanganuo wa gharama zilizotumika hadi sasa kwa kila awamu ya mradi

AWAMU	GHARAMA	%
Kwanza	5,003,546,217.71	4
Pili	17,739,670,981.10	14
Tatu	103,812,031,467.81	82
JUMLA	126,555,248,666.62	100

Chanzo: Limeandaliwa kutokana na uchanganuzi wa Taarifa za NSSF zilizowasilishwa kwenye Kamati

Grafu Na. 1: Ufafanuzi wa Mchanganuo katika Jedwali Na. 1



Chanzo: Kutokana na Jedwali Na 1

Mheshimiwa Spika, Taarifa za NSSF zilionesha kuwa fedha zilizokuwa zimepangwa kutumika kwa mradi huo ni **Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Milioni Mia Tano Thelathini na Nne, Laki Tano Hamsini na Nane, Mia Saba Sitini na Moja na senti thelathini na Moja** (159,534,558,761.31). Uchambuzi unaonesha kuwa kiasi kilichotumia hadi sasa ni sawa na **asilimia 79** ya gharama iliyokusudiwa.

2.1.2 Uuzaji wa Nyumba zilizokamilika

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara Kamati ilijulishwa kuwa nyumba nyumba 417 zimekamilika. Uchanganuzi wa nyumba hizo unaonesha kuwa vyuo mbalimbali vimepewa nyumba 360 kwa ajili ya hosteli za wanafunzi ambazo zina uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,248. Katika hatua hiyo, makubaliano ya bei ya mauzo baina ya NSSF na Vyuo vinavyohusika hayajakamilika. Hata hivyo, Kamati ilishuhudia kuwapo kwa Wanafunzi wa vyuo hivyo waliokwisha hamia katika baadhi ya Nyumba za mradi.

2.2 Mradi wa Ujenzi wa Nyumba Toangoma

2.21 Maelezo ya Mradi

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi huu, nianze kwa kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, mradi wa ujenzi wa nyumba Toangoma uliana mwaka 2014, kwa mpango wa kujenga jumla ya nyumba 161. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa,

mpaka sasa ni nyumba 76 tu zimekamilika na nyumba 85 ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa takwimu hizo, nyumba zilizokamilika ni asilimia 47 na ambazo hazijakamilika ni asilimia 53. Uwiano huo wa nyumba zilizokamilika ikilinganishwa na lengo unaonesha kuwa, licha ya kufikia mwaka wa saba tangu kuanza kwa mradi, nusu ya lengo la mradi haijafikiwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa kati ya nyumba 76 zilizokamilika, nyumba 15 sawa na **asilima 19.7** ya nyumba hizo zimepangishwa kwa wapangaji mbalimbali. Kiasi cha pango kwa kila nyumba iliyopangishwa ni kati ya **Shilingi Laki Tatu Hamsini Elfu (350,000.00)** hadi **Shilingi Laki Sita Elfu (600,000.00)** kwa nyumba bila gharama ya huduma (Service charge) ambayo ni Tshs 100,000.00,. Pamoja na hivyo, hakuna nyumba hata moja iliyokamilika ambayo imeuzwa. Bei iliyopangwa kuwa ya kuza nyumba illkuwa ni kati ya **Shilingi Milioni Mia Moja Tisini na Nne (194,000,000)** kwa nyumba na **Shilingi Milioni Mia Saba Sitini na Saba (767,000,000)** kwa nyumba. Tafsiri yake ni kuwa nyumba 61 sawa na **asilimia 80.3** nyumba zilizokamilika hazitumiki na uwekezaji katika nyumba hizo hazo hadi sasa haujwa na manufaa.

2.2.2 Gharama za Mradi wa Toangoma;

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa nyumba Toanguma ulipangwa kugharimu, jumla ya kiasi cha **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Nane Sitinoi na Mbili na Thelathini na Tano Elfu, na Tisa na Senti Hamsini na Tano(61,862,035,009.55)**. Hadi sasa zimetumika **Shilingi Bilioni Thelathini na Saba, Milioni Mia Nane Arobaini na Nne, Laki Sita Themanini na Nne, Mia Tatu Ishirini na Tisa(37,844,684,329.00)** pamoja na VAT. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 61.18** ya gharama iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi unabainisha kuwa hadi kufikia mwaka wa saba tangu mradi uanze kutekelezwa, jumla ya fedha iliyotumika ni **asilimia 61.18** lakini utekelezaji wa mradi umefikiwa **asilimia 47** ya lengo. Aidha, uchanganuzi wa **asilimia 47** ya lengo unaonesha kuwa **asilimia 37** kati ya **47** haijaanza kuonesha manufaa yoyote yatokanayo

nanuwekezaji wake. Tafsiri ya uchanganuzi huo ni kuwa licha ya gharama za uwekezaji kufikia **asilimia 61.18** ni **asilimia 10** tu ya matokeo ya uwekezaji ndio ilioanza kuwa na manufaa angalau kwa kuwezesha mapato yatokanayo na pango. Ni maoni ya Kamati kuwa jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwa uzito unaostahili ili kufanikisha uwekezaji huo kiuchumi na kijamii.

2.3 Mradi wa Ujenzi wa Nyumba Dungu

2.3.1 Maelezo ya Mradi

Mheshimiwa Spika, mradi wa, ujenzi wa nyumba Dungu ulianza mwaka 2014 ukilenga kuwa na nyumba 439. Hata hivyo, hadi sasa takriban mwaka wa saba, ni nyumba 99 tu zimekamilika na nyumba 344 zilizobaki ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Nyumba zote 99 zilizokamilika tayari zimepangishwa kwa watu mbalimbali kwa pango la **Shilingi Laki Mbili Hamsini Elfu (250,000.00)** hadi **Shilingi Laki Nne Elfu (400,000.00)** kwa nyumba kwa mwezi bila gharama ya huduma (service charge) ambayo ni **Shilingi laki Moja (100,000.00)** kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, nyumba hizo zilipangwa kuuzwa kwa bei kati ya **Shilingi Milioni Mia Moja Thelathini na Mbili (132,000,000.00)** kwa nyumba hadi **Milioni Mia Nne Tisini na Nne (498,000,000.00)**, kwa nyumba. Hadi sasa hakuna nyumba iliyokwishauzwa kinyume na matarajio ya mpango wa mradi. Kamati imebaini kuwa uwekezaji uliofanywa katika mradi huu umeanza kuwa na manufaa kidogo angalau kwa kuwapangisha watu mbalimbali na kuwezesha makazi ya viongozi wa wilaya ya Kigamboni.

2.3.2 Gharama za Mradi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, jumla ya kiasi cha **Shilingi Bilioni Themanini na Saba, Milioni Mia Moja Tisini na Saba, Laki Moja Ishirini na Moja, Mia Mbili Themanini na Nne, na senti sita (87,197,121,284.06) zilipangwa kutumika katika ujenzi ambapo mpaka sasa zimetumika kiasi cha Shilingi Bilioni Sitini na Nne, Milioni Mia Tano Sabini na Mbili, Laki Moja Kumi na Saba Elfu, Mia Tano Sabini na Moja (64,572,117,571.00)**

pamoja na VAT, ambayo ni sawa na asilimia 74.05 ya gharama iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza madhumuni ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati imechambua lengo la mpango wa mradi, matokeo ya hatua iliyofikiwa hadi sasa, bajeti ya mradi na kiasi cha fedha kilichotumika hadi sasa ikilinganishwa na hatua iliyobaki kukamilisha mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Muhtasari wa uchambuzi naomba kulijulisha Bunge lako mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia takribani mwaka wa saba lengo la idadi ya nyumba lilitolekelezwa ni **asilimia 22.6** tu wakati fedha iliyotumika ni **asilimia 74** ya gharama ya mradi wote. Tafsiri ya takwimu hizo ni kuwa **asilimia 77.4** ya lengo itatekelezwa kwa **asilimia 26** ya gharama ya mradi. Kwa uwiano huo wa lengo lilitotimia na gharama zilizotumika si rahisi mradi wa ujenzi wa nyumba Dungu kukamilika.

ii) Imechukua trkriban miaka saba kufika lengo kwa **asilimia 22.6**, jambo linalomaanisha kuwa mradi huu utahitaji takribani miaka mingine 23 kukamilika. Kwa msingi huo maoteo (*Projection*) ya utekelezaji wa mradi yanaweza kuonesha kuwa hadi kufikia mwaka 2040 mradi wa ujenzi wa nyumba Dungu utakuwa haujakamilika kama kasi ya utekelezaji italingana na kasi iliyotumika hadi kufikia hatua ya sasa.

iii) Kama isingalikuwa uamuvi wa Serikali kutaka nyumba 25 zitumiwe na viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, nyumba hizo zingekuwa bado hazipata wanunuzi walilokusudiwa.

2.4 Mradi wa Mzizima

2.4.1 Maelezo ya Mradi

Mheshimiwa Spika, NSSF imewekeza katika ujenzi wa jengo kubwa la biashara la Mzizima lilitopo katika kona ya mtaa wa Mkwepu na Kisutu, Jijini Dar Es Salaam. Jengo hilo linawezza kuwa kivutio kikubwa cha uwekezaji wa kipekee jijini humo.

Ikiwa hiyo Kamati ina maoni kuwa mradi huo utakuwa na manufaa Kiuchumi, Kibishara na Kijamii.

2.4.2 Gharama za mradi

Mheshimiwa Spika, Gharama za ujenzi wa mnara wa kwanza (*Lot 2*) ni **Shilingi Bilioni Sabini na Tisa, Milioni Mia Tatu Sitini, Laki Nne Tisini na Tisa Elfu, Mia Tano Arobaini na Saba na Senti Arobaini na Nne** (79,360,499,547.44). Hadi sasa kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini na Mbili, Milioni Mia Saba Themanini na Saba, Laki Tatu Tisini na Tisa Elfu, na Thelathini na Tatu na Senti Ishirini na Nne** (42,787,399,033.24) kimeshatumika. Uchambuzi unaonyesha kuwa kiasi hicho ni sawa na **asilimia 54.92** ya gharama iliyokusudiwa kwa mnara wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa mnara wa pili (*Lot 3*) ni kiasi cha **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Moja, Milioni Mia Moja Sabini na Mbili, Laki Tisa Ishirini na Saba Elfu, Mia Nane na Tano na Senti Tisini na Saba** (141,172,927,805.97). hadi sasa kiasi cha fedha zilizokwisha tumika kwa mradi huo ni **Shilingi Bilioni Themanini na Nne, Milioni Mia Tatu Tisini na Tatu, Laki Tatu Ishirini na Mbili Elfu, Mia Nane Tisini na Sita, na senti Kumi na Nne** (84,393,322,896.14). Kiasi hicho **asilimia 59.78** ya gharama iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebainisha mambo yafuatayo:-

i) Jumla ya gharama za mnara wa kwanza na ni pili ni **Shilingi Bilioni Mia Mbili Ishirini, Milioni Mia Tano Thelathini na Tatu, Laki Nne na Elfu Ishirini na Saba, Mia Tatu Hamsini na Tatu na Senti Arobaini na Moja** (220,533,427,353.41). jumla ya gharama iliyokwishatumika kwa ujenzi wa minara yote miwili ni **Shilingi Bilioni Mia Moja Ishirini na Saba, Milioni Mia Moja Themanini, Laki Saba na Elfu Ishirini na Moja, Mia Tisa Ishirini na Tisa na Senti Thelathini na Nane** (127,180,721,929.38) sawa na **asilimia 58**,

ii) Utekelezaji wa ujenzi wa minara yote umefikia zaidi ya asilimia hamsini, na

iii) Ujenzi wa mnara wa pili umefika mbali kidogo ikilinganishwa na ujenzi wa mnara wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya Nyumba za NSSF zilizotembelewa na Kamati, umekuwa ni wa kusuasua kutokana na changamoto mbalimbali hususan kutopatikana kwa wakati kwa wateja wa kununua nyumba zilizokamilika. Changamoto nyingine ni kuwapo kwa migogoro ya malipo kwa Wakandarasi kama ilivyothibitishwa na maelezo ya NSSF iipobainisha kuwa PPRA ilibaini baadhi ya Wakandarasi walilipwa zaidi ya malipo waliyostahili kwa kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa , mfuko wa hifadhi ya jamii unaweza kuboresha mikakati yake ya uwekezaji iwapo itafanya tafiti za kina kuhusu uwezekano na tija ya miradl, ubora na uwezo wa makandarasi, pamoja na uhakika wa kupatikana wateja wa mradi utakapokamilika. Jambo hili litasaidia kupata uhakika wa soko linalokusudiwa ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za wanachama wa mfuko.

2.5 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini (Mradi Na. 6581)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusu utekelezaji wa **Mradi Na. 6581** wa Programu ya Kukuza Ujuzi nchini, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Mradi huo ultengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni Tisa (9,000,000,000/=), ambapo kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Februari, 2021, Mradi ulikuwa umepokea kiasi cha Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Hamsini Elfu (5,250,000,000)**. Kiasi hicho ni asilimia **58.33** ya fedha iliyotengwa. Uchambuzi umebaini kuwa, ghamama za utekelezaji wa programu hii muhimu ni kubwa kuliko bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ni maoni ya Kamati kuwa, ni vigumu kuikabili changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana wengi wanaohitimu elimu ya juu bila kuwa na uwekezaji wa Kimkakati. Uwekezaji huo unapaswa kuhakikisha kuwa nguvu kazi kubwa iliyopo nchini inajengewa

ujuzi wa kupambana na kumudu ushindani wa soko la ajira. Aidha kupunguza bajeti ya mradi wa kukuza ujuzi nchini kuna athiri mafanikio ya kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majadiliano baina ya Kamati na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhusu hatua za kuchukua kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu wa kuzingatia ushauri unaojipambanua katika taarifa hii kwenye sehemu ya maoni ya ushauri wa Kamati. Msisitizo ni kuwa endapo ushauri hautazingatiwa ipasavyo, Kamati itatoa ushauri maalumu kwa Spika kuhusu hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuwezesha namna bora ya utekelezaji wa mradi huu. Nia ni kusimamia dhamira ya kujenga ustawi wa vijana wengi nchini wanaokosa fursa za ajira kutokana na kutokuwa na ujuzi stahiki.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA OFISI YA WAZIRI MKUU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, kwa mujibu wa **Kanuni ya 117 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

3.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia dhamira ya **Kanuni ya 117(2)** ya **Kanuni za Bunge**, inayohusu masharti ya uchambuzi wa bajeti, Kamati ilidadisi maeneo makuu matano yafuatayo:-

- i) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli,
- ii) Mwenendo wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida,
- iii) Utekelezaji wa bajeti ya Mpango wa Maendeleo,
- iv) Masuala mengine ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, na
- v) Ushauri na Maoni ya Kamati.

3.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ina jumla ya Mafungu Manne (4) yanayokusanya maduhuli ambayo ni:

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bunge liliidhinisha Makadirio ya Mapato yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Arobaini na Moja, Milioni Mia Moja Kumi na Nane, Laki Nane Hamsini na Nne Elfu, Mia Mbili (41,118,854,200/=)**. Muhtasari wa uchambuzi unaonekana

Fungu	Taasisi Katika Jedwali Na. Na.2: Mchanga Hadi Februari 2021	Maduhuli Vijana 2020/21	Makusanyo hadi Februari, 2021	%
27	Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Sera	36,000,000	0	0
37	Ofisi ya Wazri Mkuu - Kazi, (Sera, Uratibu na Bunge)	100,000,000	12,420,936,450	621
61	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	200,000,000	18,965,000	9.4
65	Ofisi ya Wazri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu	38,882,854,200	12,154,288,768	31.3
	JUMLA KUU	41,118,854,200	24,594,190,218	60

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 28 Machi, 2021

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- i) Hadi kufikia Februari 2021 Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake ilikusanya **Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Mia Tano Arobaini na Nne, Laki Moja Kumi na Tisa Elfu, Mia Saba Kumi na Nne (24,544,119,718.00)**. Kiasi hicho ni asilimia 60 ya lengo lilioidhinishwa na Bunge kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na.2.**
- ii) Fungu 37 lilikusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Nne Ishirini, Laki Tisa Thelathini na Sita Elfu, Mia Nne Hamsini (12,420,936,450.00)**. Kiasi hiki ni ongezeko kwa asilimia 621 ya lengo. Sababu za kuvuka lengo hilo la ni kazi maalim ya uchapaji wa nyaraka za Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika tarehe 28 Oktoba 2020.
Mheshimiwa Spika, Kamati inakupongeza wewe binafsi, Uongozi wa Kamati ya Katiba na Sheria na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na Bunge la kumi na moja, kwa kusimamia maboresho makubwa ya Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Kutokana na hilo, Ofisi hiyo imeweza kuwa chanzo cha uhakika kwa ukusanyaji wa Mapato ya Serikali ikilinganisha na hali ilivyokuwa hapo awali.

Maoni ya Kamati ni kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu, itaendelea kuboresha Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili izidi kuwa na ufanisi zaidi, kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya uchapaji, maboresho ya mazingira ya nguvu kazi pamoja na kuongeza udhibiti na usimamizi wa Nyaraka za Serikali.

Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwaajili ya matumizi ya ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Muhtasari wa matokezo ya uchambuzi unaoonekana katika **Jedwali Na. 3**

JEDWALI NA. 3: Uchambuzi wa Uwiano wa Bajeti iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida hadi kufikia Februari, 2021

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 28 Machi, 2021

Mheshimwa Spika, Kamati imebaini mambo mbalimbali kama ifuatavyo:-

NA	FUNGU	BAJETI 2021	FEDHA	ASILIMIA
i) Hadi kufikia mwezi Februari 2021				asilimia 66.6
kipindi ya cha utekelezaji				iliyoidhinishwa na Upatikanaji wa
1. 61 tu ya klasi cha fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi	37,0 Fisi ya Waziri	19,145,347,000	12,034,369,991	lipokea asilimia
2. ya Kawaida kwa mafunguyeote sita Tafsiri yakeeni kuwa	Waziri Mkuu	10,000,000	9,371,000	
3. upatikanaji wa fedha ikilinganishwa	Vijana na Wenye Ulemavu	13,674,800,000	11,794,619,114	kipindi cha
utekelezaji unzeptungua kwa asilimia 6.6.				
4. 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa	24,751,706,000	15,312,967,405		57
5. ii) Tume ya usuhuhishi na uamuzi – Fungu 15 ilipokea kiasi	4,193,618,000	1,846,822,980		44
kidogo zaidi cha fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya uamuzi				
6. matumizi ya kawaida. Kiwango hicho ni asilimia 44 tu ya Bajeti	6,991,165,000	4,102,211,300		67
yake kwa madhumuni hayo Maana halisi ya takwimu hiyo ni				
kuwa huenda Tume hiyo hanukaraniwa kupata bajeti yake				
kwa asilimia 12.6 kwa kipindi hicho ikilinganishwa na kipindi				
cha utekelezaji. Tafsiri ya matokeo hayo ya uchambuzi ni kuwa				61
JUMLA	76,607,103,000	46,930,096,743		

iii) Kazi Ajira, Vijana na wenye Ulemavu ilipokea fedha ambazo ni **asilimia 58** ya Bajeti yake ya matumizi ya kawaida katika kipindi muda ambao ni **asilimia 66.6** ya kipindi cha utekelezaji. Tafsiri ya matokeo hayo ya uchambuzi ni kuwa

shughuli za Umma kuhusu Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu zilipata mkwamo kwa **asilimia 8.6** ikilinganishwa na Bajeti na Mpango ulioidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake ipate bakaa ya fedha kufikia kiwango kilicho idhinishwa na bunge kabla ya tarehe 30 Juni 2021.

3.1.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi Kamati ilizingatia kuwa jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Mbili Kumi na Tisa, Milioni Mia Nne Sabini na Mbili, Laki Sita Ishirini na Tano Elfu (219,472,625,000/=)** ziliidhinishwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Uchambuzi umebainisha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari 2021 kiasi cha fedha kilichopokewa na Ofisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ni **asilimia 85** ya fedha iliyoidhinishwa. Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha za maendeelo ulikua mzuri ukilinganisha na fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa sababu za mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya maendeleo kuonekana mzuri kuliko upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ilitokana na sehemu ya bajeti ya maendeleo kutegemea vyanzo vya nje. Hata hivyo bajeti ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na bunge lako tukufu ulikua na utegemezi wa nje kwa kiwango kidogo. Kamati inaipongeza serikali kwa kupunguza utegemezi wa bajeti kutoka nje na hasa bajeti ya kugharamia shughuli za Uchaguzi Mkuu.

3.2 Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati

iliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu jumla ya mapendekezo Nane (8) yaliyoshauri namna bora ya utekelezaji wa Mafungu ya Bajeti ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yalihusu maeneo ya utekelezaji yafuatayo:-

- (i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishauriwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ,
- (ii) Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilishauriwa kuhakikisha inasimamia mwenendo wa Vyama vya Siasa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020,
- (iii) Ofisi ya Waziri Mkuu ilishauriwa kuimarisha Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali kwa kuboresha mazingira ya Miundombinu ili Ofisi hiyo itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi,
- (iv) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ulishauriwa kuendelea kutoa Elimu kwa wadau wake, kuimarisha mfumo wa TEHAMA na kuboresha utoaji wa huduma zake,
- (v) Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ulishauriwa kuweka na kuimarisha Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za wanufaika wa mafao yake na kutoa mafao hayo kwa wakati,
- (vi) Ofisi ya Waziri Mkuu ilishauriwa kuboresha na kuimarisha kitengo cha cha uratibu wa masuala ya Watu wenye ulemavu kwa kuendelea kuongeza Bajeti yake,
- (vii) Ofisi ya Waziri Mkuu kuongeza udhibiti wa marejesho ya Mikopo ya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ili uwanufaishe Vijana wengi zaidi, na
- (viii) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ulishauriwa kuendelea kubuni mikakati ya kuwafikia wadau wengi zaidi kulingana na ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda vingi nchini ili kulinda afya za Wafanyakazi

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ilipewa ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake, katika kusimamia utekelezaji wa mapendekezo hayo, ikiwa ni pamoja na kutembelea na kukagua utekelezaji wa taasisi zinazohusika, pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo hayo kabla ya kupokea taarifa ya Bajeti.

Hivyo, Kamati imeridhishwa na jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu ilivyoyapokea mapendekezo ya Kamati na kuyatekeleza kwa ufanisi mkubwa. Ni maoni ya Kamati kuwa, iwapo Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii zitaiga mfano mzuri wa Ofisi ya Waziri Mkuu wa kuheshimu na kuzingatia ushauri na maoni yanayotolewa Bunge utekelezaji wa shughuli za Bunge na Kamati zake utakuwa na manufaa zaidi katika uendeshaji wa shughuli za Umma.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 tarehe 22 hadi 23 Machi 2021. Kamati imebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/26).

4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umeainisha maeneo 17 ya vipaumbele ikilinganishwa na vipaumbele 19 vya Bajeti ya

Mwaka 2020/2021, muhtasari wa Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo;

- (i) Uratibu wa Shughuli za Serikali;
- (ii) Kuratibu Shughuli za Serikali Bungeni;
- (iii) Kuratibu Maadhimisho na Sherehe za Kitaifa;
- (iv) Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Dharura na Maafa;
- (v) Kuchapisha Nyaraka za Serikali;
- (vi) Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Sekta Binafsi, na Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi;
- (vii) Kusimamila utekelezaji wa Sera na Sheria za Kazi mahali pa kazi;
- (viii) Kusuluuhisha na kuamua Migogoro ya Kazi sehemu za kazi;
- (ix) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Hifadhi ya Jamii;
- (x) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi wanaoumia, kufariki au kupata madhara ya kiafya wakiwa kazini;
- (xi) Kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Mikakati ya Kukuza Ajira na Ujuzi nchini ili kuongeza nafasi za ajira za Watanzania nchi za nje;
- (xii) Kuratibu shughuli za Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri nchini;
- (xiii) Kuratibu na kusimamia uwezeshaji na maendeleo ya vijana;
- (xiv) Kusimamia, kuratibu na kutoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu;

- (xv) Kusimamia masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi;
- (xvi) Kutoa mafunzo na kuhamasisha ukuzaji wa tija mahali pa kazi; na
- (xvii) Kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/22, umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22-2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu (2021/22-2025/26) na maelekezo mengine ya Viongozi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha malengo yote ya kibajeti na kiutekelezaji ambayo yanatakiwa kutekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenyewe Ulemavu, kama Ofisi kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali kupitia maeneo mbalimbali ya kiutawala na kimaendeleo.

Hata hivyo, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba, utekelezaji wa vipaumbele vyake ulenge zaidi katika kuhakikisha kuwa, shughuli za Serikali zinaelekezwa kwa mwanachi wa Kawaida kwa kumrahisishia upatikanaji wa fursa mbalimbali za kujiletea maendeleo, kulingana na maeneo yake aliyomo, pamoja na kumtengenezea mazingira rafiki ya kisera, kisheria na kiutekelezaji yenye kumpunguzia Mwananchi huyo gharama zisizokuwa za lazima wakati akizitafuta fursa hizo.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa za Randama umebainisha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu kuititia Mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (**Fungu 37**), Ofisi ya Msajili Msajili wa Vyama vya Siasa (**Fungu 27**), Tume ya Taifa ya Uchaguzi (**Fungu 61**), Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu (**Fungu 65**) zinatarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi Bilioni Arobaini na Tano, na Milioni Themanini na Sita Elfu** (45,086,000,000), kiasi ambacho kimeongezeka kwa **Shilingi Bilioni Nne na Milioni Ishirini na Moja, Laki Nne Hamsini na Nane Elfu** (4,021,458,000), ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 9.8%** ya maduhuli ya mwaka 2020/2021.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu - **Fungu 37** inakadiria kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Shilingi Bilioni Tano (5,000,000,000.00)** kutohana na kazi za uchapaji wa nyaraka za Serikali zinazofanywa na Idara ya Kupiga Chapa ya Serikali. Uchambuzi umebaini kuwa, makisio ya makusanyo hayo yameongezeka kwa **Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000)** ambayo ni sawa ongezeko la asilimia 150 ya Maduhuli yaliyoidhinishwa kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali **Na.4**.

**Jedwali Na.4. Makisio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha
2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu**

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 28 Machi, 2021

**4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka
wa Fedha 2021/2022**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Sabini na Nne, Milioni Mia Nane Ishirini na Saba, na Kumi na Mbili Elfu (74,827,012,000.00)** kwa ajili ya Mafungu yake Sita (6), ambapo kati ya fedha hizo zinazoombwa, **Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Nne Kumi na Mbili, Laki Nane Ishirini na Sita Elfu (18,412,826,000.00)** ni Mishahara, **Shilingi Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Nane Thelathini na Sita, Laki Mbili Tisini na Nne Elfu (35,836,294,000.00)** ni Matumizi ya Mengineyo na **Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tano Sabini na Saba, Laki Nane Tisini na Mbili Elfu (20,577,892,000.00)** ni ruzuku ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Ofisi ya Waziri Mku-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umebaini kuwa, bajeti ya jumla ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa Shilingi Bilioni

Moja, Milioni Mia Saba Themanini, na Tisini na Moja Elfu (1,780,091,000.00) ambayo ni pungufu ya asilimia 2.32, ukilinganisha na bajeti ya Matumizi ya kawaida kwa mwaka 2020/21, ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Hata hivyo, uchambuzi umebainisha kuwa, kumekuwepo na Ongezeko la Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **Fungu 61** (Tume ya Uchaguzi), kiasi cha **Shilingi Bilioni Mbili , Milioni Mia Saba Tisini na Tatu, Laki Tano Arobaini na Sita Elfu (2,793,546,000)** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 46.60** ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Fungu hili kwa mwaka unaoisha. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Mbili Tisini na Tatu, Laki Tano Arobaini na Sita Elfu (293,546,000)** kwa upande wa Mishahara, pia imebainika kuwepo kwa ongezeko kubwa kwa upande wa Bajeti ya matumizi Mengineyo kwa fungu hilo, kiasi cha **Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano Elfu (2,500,000,000)** ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 50.30** ya Bajeti ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa ongezeko hilo ni hatua ya kupongezwa kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inayotekeleza majukumu muhimu ya Kitaifa ya kuendelea kusimamia chaguzi ndogo mbalimbali zitakazoendelea kujitokeza, kwa mujibu wa Sheria. *Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuwa, Hazina ihahakishe inatoa fedha kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa.*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, uchambuzi umebaini kuwa, Bajeti ya Mishahara kwa mafungu ya Ofisi ya Waziri Mkuu imeongezeka kwa **Shilingi Milioni Mia Tano na Tano, Laki Nne Themanini na Saba Elfu, Mia Nne Themanini na Nne (505,487,484)**, ambayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 2.82**, ikilinganishwa na Bajeti ya Mishahara kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, uchambuzi umebaini kuwa, bajeti ya jumla ya Matumizi Mengineyo (OC) imeongezeka kwa **Shilingi Bilioni**

Saba, Milioni Mia Tisa Sabini na Tano, Laki Sita Arobaini na Saba Elfu, Mia Tisa Arobaini na Saba(7,975,647,947) ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 28.63 ya Bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka unaoisha.

Hata hivyo, uchambuzi umebaini kupungua kwa bajeti ya ruzuku kwa **shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja, Laki Mbili Ishirini na Sita Elfu, Mia Nne Thelathini na Moja (10,261,226,431)**, ambayo ni sawa na pungufu ya **asilimia 33.27** ya Bajeti ya ruzuku kwa mafungu yanayohusika kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kuwa, kupungua kwa bajeti ya jumla ya Matumizi ya kawaida kwa kiasi cha Shilingi Bilioni 1.7 kwa Ofisi ambayo kazi yake kubwa ni kuratibu shughuli zote za Serikali, ni eneo linalohitaji maboresho kwa Bajeti ijayo ya Mwaka 2022/2023, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu inakuwa na Bajeti toshelevu itakayoiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa, pasipo kukwamishwa na changamoto za kibajeti, zinazoweza kujitokeza, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa mtiririko wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.5**.

JEDWALI NA. 5: Mchanganuo wa Bajeti ya Kawaida kwa Mwaka 2021/22

Fungu	Mishahara	Ruzuku	Matumizi Mengineyo	Jumla ya Matumizi ya Kawaida
Fungu 25 - Ofisi Binarti ya Waziri Mkuu	1,233,668,000	0	9,856,951,000	11,090,619,000
Fungu 15-Tume ya Usuluhishina Ujima	1,953,275,000	0	1,920,150,000	3,873,425,000
Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Slasa	838,826,000	17,563,000,000	1,597,370,000	19,999,196,000
Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu ("Vitabu na Bumbe")	5,203,104,000	0	12,729,156,000	17,932,260,000
Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi	3,818,320,000	0	4,970,031,000	8,788,351,000
Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vilaya, Ajira, na Wenye Olemaavu)	5,365,633,000	3,014,892,000	4,762,636,000	13,143,161,000
JUMLA KUU	18,412,826,000	20,577,892,000	35,836,294,000	74,827,012,000

Chanzo: Taarifa ya WN-OWM, tarehe 28 Machi, 2021

4.4 Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa Shilingi **Bilioni Ishirini na Mbili, na Milioni Tisini na Moja, Laki Nne na Nne Elfu (22,091,404,000.00)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo, ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Kumi na Sita (16,000,000,000.00)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Sita, na Milioni Tisini na Moja, Laki Nne na Nne Elfu (6,091,404,000.00)** fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Maendeleo inayoombwa *imepungua kwa Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Nnne Arobaini na Mbili, Laki Sita Themanini na Tisa Elfu, na Tisini na Saba (16,442,689,097), ambayo ni sawa na punguzo la asilimia 42.7% ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/21.*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, punguzo hilo ni kutokana na kupungua kwa maoteo ya Bajeti ya Nje ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa haitolewi kwa wakati na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mipango ya Maendeleo. Hivyo, hatua hiyo ya kupunguza utegemezi wa bajeti ya nje ni sehemu ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwamba Ofisi hiyo iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo, na badala yake Ofisi hiyo iendelee kubuni vyanzo vipyta vya makusanyo ya ndani ikiwa ni pamoa na kuongeza uwezo wakukusanya maduhuli kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo.

Aidha, Kamati iembaini kuwa, Mpango wa Ofisi ya Waziri Mkuu katika Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka huu wa Fedha umelenga katika **maeneo Saba (7)** badala ya **Nane (8)** yaliyopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebaini kuwa, eneo moja la utekelezaji linalopungua ni jukumu la kuendesha Uchaguzi Mkuu ambaao kwa mwaka huu siyo agenda ya kimaendeleo,

kwa kuwa uchaguzi Mkuu haupo hadi mwaka 2025. Hivyo, maeneo ya vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 itakuwa kama ifuatavyo:-

- (i) Kuratibu Programu ya Kuendeleza Mbegu za Mazao ya Kilimo na Uvuvi;
- (ii) Kuanza ujenzi wa kiwanda cha uchapaji wa Nyaraka za Serikali Jijini Dodoma;
- (iii) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa Dodoma;
- (iv) Kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za kazi ya nguvu kazi nchini kwa ajili ya uchumi wa viwanda katika sekta za kilimo-biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA, madini, mafuta na gesi,
- (v) Kuwajengea uwezo wa Kiuchumi Vijana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;
- (vi) Kuratibu na kukuza Kazi na Ajira za Staha Nchini; na
- (vii) Kuendeleza ujenzi wa Makazi ya Waziri Mkuu Mlimwa - Dodoma;

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa Vipuambele 17 vya Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Majukumu ya kila Taasisi iliyo chini ya Ofisi hiyo, na kubaini kuwa, mpango wa Maendeleo unaopendekezwa kwa Mwaka 2021/2022 wenye kuainisha maeneo Saba ya utekelezaji, umezingatia Muundo na Majukumu ya Ofisi hiyo, na hivyo Kamati imeridhika na Mpango huo kama ulivyo wasilishwa na Mtoa Hoja.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na

Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia tathmini ya Kamati kuhusu ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, pamoja na uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, hivyo, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

5.1 FUNGU 37 NA FUNGU 25

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, uratibu wa wa Shughuli za Serikali unaotekelizwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, unawezeshwa na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Mafungu 37 na 25, ikiwemo shughuli za Waziri Mkuu mwenyewe na wasaidizi wake, ambapo, kupungua kwa makadirio ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kunaweza kuathiri utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi hiyo muhimu, hivyo basi, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa:-

- (i) Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hiyo iandae na kuwasilisha Bajeti ya Matumizi ya Kawaida yenye kuendana na uhalisia wa mahitaji ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Ofisi hiyo ili Kamati iweze kushauri ipasavyo, na
- (ii) Serikali ihahakishe kuwa, Fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake ya uratibu, ziwe zinatolewa kwa wakati kwa lengo la kuiwezesha Ofisi hiyo muhimu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

5.2 FUNGU 65 – Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu

5.2.1 Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kubaini kuwa, uwezo wa Wakala huu umeendelea kuongezeka katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, pamoja na kutekeleza ushauri wa Kamati kuhusu kuchukua hatua za kufuta baadhi ya tozo zenye kero kwa wadau wake, Kamati inaendelea kushauri kuwa:-

- (i) Wakala uendelee kubuni mikakati endelevu na kuitekeleza kuhusu kusimamia Afya na Usalama wa Wafanyakazi Mahali Pa Kazi kwa kuzingatia ongezeko la uanzishwaji wa Viwanda nchini katika kulinda usalama wa Wafanyakazi;
- (ii) Kuimarisha kitengo chake cha Elimu kwa umma ili kuweka msisitizo mkubwa katika utoaji wa Elimu na kuimarisha mahusiano ya karibu na Wadau wake ili kuvutia wadau wengi kutii sheria za usalama mahala pa kazi pasipo kutumia nguvu kubwa isioyo lazima;
- (iii) Kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana karibu na taasisi nyngine za Serikali kwa lengo la kupunguza urasimu usiyo wa lazima kwa Wawekezaji na kupunguza gharama zisizo za lazima, hatua ambayo inaweza kuwakatisha tama wawekezaji hao; na
- (iv) Serikali ichukue hatua za dhati katika kuondoa changamoto ya kukaimishwa kwa Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa OSHA kwa zaidi ya Miaka Mitano (5), bila kupatikana kwa Mtenda Mkuu, changamoto ambayo inaathiri utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Wakala huo.

5.2.2 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kubaini mafaniko makubwa yaliyofikiwa na Mfuko huu kwa kipindi cha Miaka Mitano tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, katika kukusanya michango, kufanya uwekezaji na kutoa mafao kwa Wafanyakazi wanao umia wakiwa kazini, mafao ambayo hayatolewi katika mfuko wowote wa Hifadhi ya Jamii, Kamati inaendelea kushauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuetekeliza hatua zifuatazo:-

- i) Serikali ihakikishe inaimarisha Mfuko huu na kuufanya kuwa endelevu kwa lengo la kujenga imani kwa Sekta Binafsi kama Wawekezaji muhimu wa Mfuko pasipo kuyumbisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni zake, kwa lengo la kuhakikisha kuwa, Mfuko huu unaendelea kuwa kichocheo kikubwa cha Wawekezaji na wafanyakazi wao kwa kuendelea

kuutofautisha na Mifuko mingine ya Hifadhi ya Jamii kama inavyoelekeza Sheria yake,

ii) Kuendelea kutoa Elimu ya kutosha kwa Waajiri na Wafanyakazi hususan Vyama vya Wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waajiri wote nchini wanazingatia matakwa ya Sheria katika kuhakikisha Wanajiardikisha kwenye Mfuko, wanalipa ada na michango kwa wakati na kutoa taarifa sahihi,

iii) Kuimarissha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika kuendesha shughuli zake hususan katika kuwafikia wadau wake nchi nzima, kukusanya michango kwa mujibu wa Sheria na kutoa huduma kwa wakati kwa wanufaika wake, na

iv) Mfuko uendelee kuimarissha Mfumo mzuri wa kufanya tathmini za fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini na kuhakikisha kwamba malipo ya fidia yanafanyika kwa haraka kwa kila Mfanyakazi aliyetimiza vigezo vya kupata fidia anayostahili.

5.2.3 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, moja ya malengo ya Serikali ya kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mwaka 2018 na kuanzishwa Mifuko Miwili ambayo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ilikuwa ni kuhakikisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inatoa mchango mkubwa kwa Maendeleo ya nchi, ikiwa ni pamoja na Mifuko hii kuendelea kupanua wigo wa kuongeza Wanachama na kufanya uwekezaji wa kimkakati wenye tija kwa Taifa na kupata faida kwa wakati, hivyo basi, Kamati inashauri kuwa,

i) Mfuko wa NSSF uanzе kubuni na kutekeleza mikakati mipy ya kuongeza wanachama wapya hususan vijana walioko katika sekta isiyorasi, Wanavyuo na makundi yenye mahitaji maalum, na kuwajengea uwezo ili wawe wanachama endelevu wa Mfuko, kwa maendeleo yao na kuwezesha Mfuko kuongeza makusanyo endelevu;

- ii) Mfuko wa NSSF ukamilishe Mkakati wake wa kutangaza huduma na fursa mbalimbali zilizopo, kwa makundi mbalimbali hususan katika Sekta isiyo rasmi ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza programu maalum ya kutumia baadhi ya Wabunge Vijana na baadhi ya wanavyuo kwa ajili ya kuwaandaa na kuwatumia katika kutangaza fursa za Mfuko huo, kwa lengo la kuhamasisha Makundi mengi ya kijamii kuijunga na Mfuko, kuanza kuchangia na kunufaika na fursa mbalimbali za uwekezaji kwa ustawi wa makundi hayo,
- iii) Mfuko wa NSSF uboreshe mkakati wake wa Wateja wa Miradi yake ya Nyumba, kwa kupunguza bei za mauzo na bei za pango la nyumba hizo ili kuwawezesha watananzania wenyе kuhitaji huduma hiyo, kununua au kupanga nyumba hizo. Hii ni pamoja na kuendelea na mkakati wake wa kufanya mazungumzo na Vyuo Vikuu nchini ili viweze kukodi baadhi ya Nyumba kwa ajili ya Mabweni, badala ya kuacha nyumba hizo bila kupata wapangaji au wanunuzi kwa muda mrefu,
- iv) Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii ianze kufanya uwekezaji wa kimkakati katika Sekta ya Viwanda, kwa kuzingatia masharti ya Sheria za uwekezaji wa fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hali ya uendelevu wa Mifuko, ustawi wa Wanachama wake na Taifa kwa ujumla. Hatua hiyo iambatane na kufanyika kwa tathmini ya kina kuhusu uwekezaji unaotarajiwa kabla ya kutumia fedha za Wanachama kwa miradi ambayo haina tija kwa Mfuko.

5.2.4 Masuala ya Watu wenyе Ulemavu

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuendelea kuridhishwa na hatua ya Serikali ya kuanzisha Kitengo cha kuratibu masuala ya Watu wenyе Ulemavu nchini ikiwemo kuanzisha rasmi Baraza la Taifa la kuratibu Masuala ya Kundi hilo kwa ujumla, na kuwepo ongezeko la Bajeti ya Kitengo hicho kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Kitengo hicho katika kuratibu masuala ya watu wenyе Ulemavu kwa ufanisi zaidi, Kamati inashauri kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe inachukua hatua za dhati za utatuzi wa changamoto zifuatazo:-

- (i) Kubaini na kutambua vyama vyote nchini nya Watu wenye ulemavu na kuvipatia Elimu ya kutosha kuhusu usimamizi wa haki za Watu wenye Ulemavu na jinsi ya kuzifikia fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali na Wadau wengine wa maendeleo kwa ajili ya kundi hilo maalum,
- (ii) Kubaini na kutatua migogoro mbalimbali inayoendelea katika Vyama nya Watu wenye Ulemavu nchini ambayo inaathiri ustawi wa Vyama hivyo na hivyo kukwamisha baadhi ya makundi hayo kwa kushindwa kuzifikia fursa za kujikwamua kiuchumi,
- (iii) Kuandaa kanzidata ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu nchini yenye kuainisha idadi ya Watoto, Vijana na Watu wazima na Wazee, Mikoa na Wilaya wanazoishi, na majina ya vyama vyao vinavyoratibu masuala yao kwenye maeneo yao, kwa lengo la kurahisisha uratibu wa haki na fursa zao kuanzia ngazi ya Viji, Mitaa, Kata, Tarafa, Wilaya, Mikoa na hadi Taifa, na
- (iv) Kukamilisha mchakato wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Masuala ya Watu wenye ulemavu, kwa kuandaa mfumo mzuri wa vyanzo nya fedha nya Mfuko, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kwa ajili ya ustawi wa kundi hilo maalum nchini.

5.2.5 Maendeleo ya Vijana

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, **Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007** imepitwa na wakati ukilinganisha na mabadiliko makubwa yanayotokea nchini kwa sasa, ambapo tayari Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza mchakato wa kuboresha Sera hiyo ili iendane na wakati, hivyo basi, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa,

- (i) Ikamilishe mchakato wa kuboresha Sera ya Maendeleo ya Vijana na iwasilishe rasimu ya Maboresho ya Sera hiyo kwa Kamati ili Serikali ishauriwe ipasavyo,
- (ii) Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, wafanye maboresho ya uratibu wa Mfuko wa

Maendeleo ya Vijana ili kuwepo na mfumo mmoja wa vyanzo vya Fedha za Maendeleo ya Vijana nchini. Hatua hiyo itasaidia kuondokana na changamoto ya kuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambao haupokei fedha yoyote kila Mwaka, pamoja na Mfuko huo kuwa unatengewa Shilingi Bilioni Moja kila Mwaka wa Fedha. Aidha, hatua hiyo iambatane na kuongeza usimamizi na udhibiti wa fedha zote za Mikopo zinazotolewa kwa ajili ya Vijana ili zirejeshwe kwa wakati na vijana wengi wanufaiké na fursa hiyo.

5.2.6 Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini (Mradi Na. 6581);

Mhesimiwa Spika, kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa, kumekuwepo kupungua kwa bajeti ya Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini mwaka hadi mwaka kutoka **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000.00)** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi **Shilingi Bilioni Tisa (9,000,000.00)**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pasipo kujali kwamba, wakati huu ambapo Serikali inajenga Miradi mingi nchi nzima yenye kuhitaji vijana wenye ujuzi unaotakiwa ili vijana wengi waweze kushiriki fursa za ajira katika miradi hiyo, hivyo basi, Kamati ina shauri kuwa,

i) Ofisi ya Waziri Mkuu ijipange kimkakati kwa kuhakikisha kuwa, Bajeti ya Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inakuwa halisi kwa kuuongezea fedha hadi kufikia **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000.00)** kama Bajeti yenye uhalisia wa mahitaji ya programu hiyo,kwa lengo la kuhakikisha kuwa, vijana walio wengi wanaohitimu ngazi mablimbali za masomo nchini,wanendelea kujengewa ujuzi,kwa lengo la kuwawezesha kumudu ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi yetu, na

ii) Ofisi ya Waziri Mkuu, ijipange kimkakati katika kutangaza huduma zinazotolewa na Programu hiyo na jinsi ya kuzifikia, kwa lengo la kuwawezesha Vijana wanaohitimu masomo katika ngazi mablimbali za Elimu, kujengewa ujuzi ili waweze kujiajiri na au kupata ajira katika taasisi mbalimbali ndani na je ya nchi.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili la Kumi na Mbili kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa msaada wa karibu sana unaoendelea kuutoa kwa Kamati yetu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa, na pia kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Tulia Ackson, (Mb), kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niipongeze pia Kamati ya Uongozi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha Shughuli za Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza aliye kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, (Mb) kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hakika, alikuwa msaada mkubwa kwa Kamati hii na sisi tutaendeleza misingi mzuri aliyotuachia, na hivyo tunamtakia afya njema na mafanikio mema katika majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenyewe Ulemavu, Mhe. Jenista J. Mhagama, (Mb), kwa ushirikiano wake mkubwa na wenyetejia, uchapaji kazi mzuri wake kwa nidhamu na unyenyekevu mkubwa kwa Kamati, na hivyo kurahisisha Shughuli za Kamati na Shughuli za Waziri Mkuu, anayemuwakilisha. Aidha, tunawashukuru wasaidizi wake ambao ni Manaibu Waziri, Mhe. Patrobass Katambi,(Mb), na Mhe.Ummy Nderiananga,(Mb), Katibu Mkuu, na Watendaji Wakuu wote wanaoongoza taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Wazri Mkuu, kwa ushirikiano wao mzuri katika kurahisisha shughuli za Kamati hii.

Aidha, kwa kipekee, tunamshukuru na kumpongeza aliyekuwa Mtendaji Mkoo wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Ndgt.Masha Mshomba, ambaye kwa sasa ameteuliwa kuwa Mtendaji Mkoo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa ushirikiano mzuri na Kamati katika kutekeleza majukumu yake, kwa kuongoza na kufanikisha vipaumbele vya Mfuko huo katika kuchochoea Maendeleo ya Taifa, na kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania. Tunamtakia utekelezaji mwema wa Majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkoo kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wote wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkoo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkoo, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb. – **Makamu Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb. – Mjumbe
3. Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb. – Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.-Mjumbe
5. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.-Mjumbe
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb -Mjumbe
7. Mhe. Zainabu Athumanji Katimba, Mb,-Mjumbe
8. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb,-Mjumbe
9. Mhe. Lemburis Saputu Mollel Noah, Mb, -Mjumbe
10. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, -Mjumbe
11. Mhe. Elibariki Immanuel Kingu, Mb, -Mjumbe
12. Mhe. Omar Ali Omar, Mb, -Mjumbe
13. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb, -Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, -Mjumbe
15. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.-Mjumbe
16. Mhe. Ahmed Juma Ngwali Dedi, Mb,-Mjumbe
17. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb,-Mjumbe

18. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb,-Mjumbe
19. Mhe. Jackline Ngonyani Msongozi, Mb, -Mjumbe
20. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb, -Mjumbe
21. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb,-Mjumbe
22. Mhe.Agnes Elias Hokororo, Mb,-Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg.Gerald S.Magili na Ndg. Michael Chikokoto, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika nya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Najma Murtaza Giga, Mb.
MAKAMU MWENYEKITI,
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA
13 APRILI, 2021

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga.
(*Makofii*)

Sasa ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Karibu sana Mwenyekiti. Ajiandae Mwenyekiti wa Masuala ya UKIMWI. Moja kwa moja Mwenyekiti kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni 118(39) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye maoni ya Kamati. Ofisi za Wabunge majimboni. Kamati ya bado inaendelea kusisitiza juu ya suala la uwepo wa ofisi ya Wabunge majimboni na kuziwekea samani illi kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa suala hili walikasimiwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji wake ni vyema Bunge likapata maelezo juu ya mpango wa Serikali wa kukamilisha ujenzi wa ofisi hizi. Pia ikiwezekana fedha hizi zitengwe katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizi.

Mheshimiwa Spika, kuongeza eneo la Bunge. Ofisi ya Bunge imekuwa ikitabiliwa na changamoto ya uhaba wa ofisi kwa ajili ya Viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge, watumishi pamoja na kumbi za kuendeshea vikao vya Kamati na shughuli zingine za kiofisi. Aidha, ofisi ya Bunge inakabiliwa na changamoto ya eneo la kuegesha magari ya Waheshimiwa Wabunge, watumishi wa Bunge na Viongozi wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, ofisi ya Bunge imeshawalisha Serikalini maombi ya kuwezeshewa kutwaa na kumilikishwa maeneo yanayozunguka Bunge yanayomilikiwa na Taasisi za Serikali

pamoja na yale ya watu binafsi. Hatua hii itasaidia kukabiliana na changamoto hizo pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi ya Bunge inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwezesha Ofisi ya Bunge kupata hati miliki ya kiwanja Na. 2 eneo la *Central Business Park* ambacho kitatumika kama maegesho ya magari ya watumishi, Waheshimiwa Wabunge na wageni mbalimbali. Vilevile, tunamshukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kukubali ombi la kuiwezesha Ofisi ya Bunge kumilikishwa Kiwanja Na.12 eneo la *Central Business Park* ambacho kimepakana na *Hotel 56*. Kiwanja hicho kitatumika kusaidia kutatua changamoto zilizoainishwa. Aidha, Kamati inapenda kusisitiza Serikali iendelee kusaidia kupatikana kwa maeneo mengine yaliyobakia.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuboresha Ofisi ya Bunge na Kituo cha Afya. Kamati inaipongeza Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kufanya maboresho ya ukarabati wa ukumbi wa Bunge, jengo la Utawala na Kituo cha Afya. Hatua hii imesaidia kuboresha uratibu na uendeshaji wa mikutano ya Bunge pamoja na kuimarisha afya za Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge. Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Ofisi ya Bunge kuendelea kununua vifaa tiba kwa lengo kudumisha huduma inayotolewa na Kituo cha Afya cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Naomba niitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vyema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia, naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango ambaye sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee, nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge,

Kazi, Vijana na Ajira na Watu wenyewe Ulemavu kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Wabunge. Naomba niwatambulisse majina yao kama yalivyoorodheshwa.

SPIKA: Hapana, hapana. Majina hapana maliza tu.

MHE. DANIEL B. SILLO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalam ambao umesaidia Kamati kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge, Fungu 42, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge (Fungu 42) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Jenista Joackim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu), Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai na kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 pamoja na kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/22.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2021/22.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Mheshimiwa Spika, katika kuwezesha Ofisi ya Bunge kutekeleza majukumu yake, Kifungu cha 32 cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge kama ilivyofanyiwa rejea mwaka 2015 kilianzisha Mfuko wa Bunge. Hivyo, Mfuko wa Bunge hutengewa fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji mbalimbali, ambapo asilimia 80 ya mahitaji hayo ya fedha hutumika kugharamia Mikutano ya Bunge na Kamati za Bunge, Posho ya Jimbo na Usafiri kwa Wabunge, Matibabu kwa Wabunge na sehemu iliyobaki asilimia 20 hutumika kutekeleza shughuli za utawala na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge inatekeleza Bajeti yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za

Umma pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Bunge (Strategic Plan 2016-2021) na Mpango wa Muda wa Kati (Medium Term Expenditure Framework). Utekelezaji wa Bajeti umezingatia malengo yaliyotarajiwa kutekelezwa katika vipindi husika na makisio ya Bajeti yamezingatia kuboresha na kutoa huduma mbalimbali kulingana na mahitaji halisi.

2.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/21

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Mfuko wa Bunge - Fungu 42 uliidhinishiwa jumla ya **Sh.121,786,257,000.00**. Kati ya fedha hizo **Sh.23,253,494,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.90,314,153,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh.8,218,610,000.00** kwa ajili ya fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Miradi ya Maendeleo, **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.3,218,610,000.00** ni fedha za Nje. Vilevile, Mfuko wa Bunge uliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya kiasi cha jumla ya **Sh.76,215,000.00**.

2.2 Fedha zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 42 uliwezekana kuititia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina uliozingatia mgawo wa kila mwezi wa Matumizi Mengineyo, Fedha za Miradi ya Maendeleo na mahitaji ya Mishahara. Hivyo basi, mchanganuo wa matumizi na mtiririko wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo: -

2.2.1 Mishahara

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 Mfuko wa Bunge umepokea kiasi cha **Sh.10,688,694,961.45** ambazo ni sawa na **asilimia 46** ya fedha zote za mishahara zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

2.2.2 Matumizi Mengineyo

Mheshimiwa Spika, Fedha za Matumizi Mengine (OC) zilizopokelewa hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 zinafikia jumla ya **Sh.49,750,088,896.00** ambazo ni sawa na **asilimia 55**

ya fedha zote za matumizi mengineyo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

2.2.3 Fedha za Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 kiasi cha **Sh.3,368,057,681.02** sawa na **asilimia 41** ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizopangwa katika Mpango wa Maendeleo kwenye miradi minne; Ukarabati wa Majengo ya Bunge, Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (LSP) pamoja na Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

2.2.4 Maduhuli (Revenue)

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Mfuko wa Bunge uliidihihiwa kukusanya kiasi cha maduhuli ya **Sh.76,215,000.00**, hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 2021 kiasi cha **Sh.68,778,140.00** kimekusanywa. Makusanyo ya maduhuli haya yametokana na marekebisho ya mkataba katika makusanyo ya Kodi ya Pango, pamoja na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

3.0 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21.

3.1. Mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Bunge zilizopangwa kufanyika katika kipindi cha mwaka 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi tarehe 15 Machi, 2021 Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha kutekeleza shughuli mbalimbali ukiwemo uratibu wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Ofisi (*Strategic Plan 2016-2021*), Maelekezo ya Serikali katika Mwongozo wa Bajeti (*Budget Guidelines*) pamoja na Mpango wa Muda wa Kati (*Medium Term Expenditure Framework*). Utekelezaji wa shughuli hizo ulikuwa kama ifuatavyo: -

3.1.1 Utekelezaji wa Mfumo wa Bunge Mtandao (e- Parliament)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge ulisimamia uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa kutumia TEHAMA kuitia Mfumo wa Bunge Mtandao (*e-parliament*) na kufanya maboresho ya miundombinu ya mfumo kwa kuweshera mfumo kutuma nyaraka za Bunge kwa Wabunge na wadau wengine; mfumo kupatikana nje ya maeneo ya Bunge kwa kutumia mfumo wa VPN; madirisha (module) ya mfumo yameongezeka kutoka matatu hadi kufikia kumi; Mbunge kuomba nafasi ya kuchangia, kuuliza swali, kuomba kuhusu utaratibu, mwongozo wa Spika au taarifa; na Mbunge kutaarifiwa (notification) kwenye kishikwambi (Tablet) chake punde nyaraka inapotumwa.

3.1.2 Uratibu wa Shughuli za Mikutano ya Bunge pamoja na Kamati za Bunge

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa Mikutano Miwili ya Bunge, yaani Mkutano wa Kwanza uliohusisha Ufunguzi wa Bunge la 12 na Mkutano wa Pili wa Kawaida wa Bunge ambapo;

- (i) Mkutano wa Ufunguzi wa Bunge la 12 uliambatana na kusomwa kwa tangazo la Rais la kuitisha Bunge, uchaguzi na kiapo cha Spika, kudhibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, uchaguzi na kiapo cha Naibu Spika, kiapo cha uaminifu kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Hotuba ya Ufunguzi wa Bunge la 12 kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (ii) Jumla ya maswali 15 ya papo kwa papo yaliulizwa moja kwa moja kwa Mhe. Waziri Mkuu na kujibiwa;
- (iii) Jumla ya maswali ya kawaida 126 na ya nyongeza 208 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali;
- (iv) Mjadala wa Hotuba ya Rais ya Ufunguzi wa Bunge la 12 iliyotolewa tarehe 13 Novemba, 2020 ulifanyika;

(v) Mswada mmoja wa Sheria ya Serikali ulijadiliwa na kupitishwa na Bunge na kuwasilishwa Serikalini kwa Utekelezaji;

(vi) Matoleo ya Magazeti ya Serikali 44 na Nyongeza zake yaliwasilishwa; na

(vii) Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22 yalijadiliwa na Bunge.

(viii) Kuratibu mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi kumi (10) na muda mfupi kwa watumishi 256 kuhusu Afya na Maadili mahali pa kazi na wengine watano (5) kuhusu zimamoto.

3.1.3 Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa

Mheshimiwa Spika, katika midani za Kimataifa Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha yafuatayo;

a) Kuratibu Mkutano wa CPA wa Makatibu Kanda ya Afrika (*virtual meeting*);

b) Kuratibu ushiriki wa Spika kama Mwenyekiti kwenye Mkutano wa Bodi ya Uwekezaji ya CPA Kanda ya Afrika (*virtual meeting*);

c) Kuratibu ushiriki wa Spika kwenye Mkutano Maalum wa Kamati ya Utendaji (EXCO) ya CPA Kanda ya Afrika (*Virtual Meeting*);

d) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye Warsha ya kuhusu uzingatiaji wa masuala ya Jinsia katika Mabunge ilioandaliwa na CPA Makao Makuu;

- e) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye Warsha kuhusu utekelezaji wa Sheria zinazotetea wanawake dhidi ya unyanyasaji ilyoandaliwa na CPA Makao Makuu;
- f) Kuratibu ushiriki wa Bunge kwenye Siku ya Jumuiya ya Madola iliyoanyika tarehe 08 Machi, 2021;
- g) Vilevile Mfuko wa Bunge uliratibu uanzishwaji wa Urafiki wa Kibunge baina ya Bunge la Tanzania na Bunge la Burundi;

3.1.4 Uratibu wa Ofisi za Viongozi

Mheshimiwa Spika, Hadi kufika tarehe 15 Machi 2021, Mfuko wa Bunge umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Spika; Ofisi ya Naibu Spika na Ofisi ya Walio wachache Bungeni. Pia, umeweza kusimamia uendeshaji wa shughuli zinazohusu Ofisi ya Bunge kwa ujumla.

3.1.5 Kutolewa kwa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umewezesha kufanikisha kutolewa kwa ushauri wa kitaalam kwenye masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi na utekelezaji wa shughuli za Bunge, kutunga sheria na ustawi wa Bunge. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai 1, 2020 hadi Machi 15, 2021 Ofisi ilifanya yafuatayo: -

- a) Ilifanya uchambuzi wa Miswada mitatu (3) na ukamilishaji wa uandishi wa Muswada (*Final Legislative Process*) mmoja na kuuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais ili kupata idhini ya muswada huo kuwa sheria;
- b) Illichambua na kutoa ushauri kuhusu Mikataba ya ununuzi 14;
- c) Ilitoa utetezi kwa Mashauri Manne (4) yaliyofunguliwa Mahakamani dhidi ya Ofisi ya Bunge;
- d) Ilitoa ushauri kuhusu Mikataba Kumi na Mbili (12) ya Kimataifa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge; na

e) Illichapisha Toleo Jipywa la Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

3.1.6 Kutolewa kwa huduma za Matibabu pamoja na ununuzi wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge umewezesha utolewaji wa huduma za matibabu kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi pamoja na familia zao kupititia Kituo cha Afya cha Bunge. Aidha, Ofisi pia imeendelea kuimarisha na kuboresha Kituo cha Afya cha Bunge kwa kununua vifaa tiba pamoja na madawa mbalimbali kwa ajili ya kuwahudumia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi. Vifaa hivyo vilivyonunuliwa ni pamoja na :-

- i. Vifaa tiba vyaa meno pamoja na kitie chake;
- ii. Mashine ya Ultrasound;
- iii. Mashine ya uangalizi wa moyo;
- iv. Mashine ya vipimo vyaa sukari ya muda mrefu, damu kuganda mwilini na kuvilia kwenye mapafu;
- v. Mitungi ya Oksijeni kwa ajili ya wenye shida ya kupumua.

3.1.7 Ukarabati wa Majengo ya Ofisi pamoja na Ujenzi wa Makazi ya Viongozi

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2021, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kusimamia na kuratibu kazi zifuatazo:-

- a) Ukarabati wa majengo ya Ofisi ambapo matengenezo makubwa yamefanywa katika Ukumbi wa Bunge kama ifuatavyo;
 - (i) Kusimika matanki makubwa ya maji kwa ajili ya matumizi ya Ukumbi wa Bunge;
 - (ii) Kununua viti 286 kwa ajili ya kusimikwa katika Ukumbi wa Bunge;

- (iii) Kuimarisha mfumo wa baridi (air conditioning system) kwenye Ukumbi wa Bunge kwa kuagiza vifaa vyatukarabati mitambo ya kuleta baridi;
 - (iv) Kufanya ukarabati wa paa la Ukumbi wa Bunge;
 - (v) Kukamilisha ujenzi wa ghorofa ya tano katika Jengo la Utawala;
 - (vi) Kufanya ukarabati katika Jengo la Ukumbi wa Msekwa.
- b) Kufanya maandalizi ya ujenzi wa nyumba za Viongozi wa Bunge, Dodoma; na
- c) Kukarabati na kusimika mitambo ya usalama.

3.1.8 Kutoa Elimu kwa Umma

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kufanikisha utoaji wa Elimu kwa Umma kwa wadau na wageni mbalimbali walotembelea Bunge. Aidha, Watumishi wameweza kushiriki katika maonesho ya Kitaifa ya Saba Saba na Nane Nane ambapo wananchi walotembelea Banda letu walipata ufanuzi wa kina kuhusu masuala na shughuli za Bunge.

3.1.9 Urushaji wa Matangazo ya Vikao vya Bunge

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha uratibu na urushaji wa matangazo ya vikao vya Bunge wakati wa Mkutano wa 19 na 20 wa Bunge kuitia Studio ya Bunge pamoja na kuratibu ushiriki wa Viongozi na Maafisa wa Bunge katika Vipindi mbalimbali vya Bunge kuelezea shughuli za Bunge.

3.1.10 Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2021, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umefanikisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kiasi cha **Sh. 68,778,140.00** na kuingizwa kwenye

Mfuko Mkuu wa Serikali. Mapato haya yametokana na Kodi ya pango, marejesho ya masufuru pamoja na kuuza nyaraka za zabuni.

3.1.11 Utekelezaji wa majukumu mengine

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Machi 2021, Mfuko wa Bunge (Fungu – 42) umeweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwa pamoja na: -

- i. Uratibu wa shughuli za Ulinzi na Usalama kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi pamoja na Wageni mbalimbali wanaoingia maeneo ya Bunge au kushiriki safari za kibunge;
- ii. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 pamoja na kuandaa taarifa za ununuzi na kuwasilishwa kwenye Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA), Bodii ya Zabuni na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA);
- iii. Kuratibu shughuli za Muungano zinazohusiana na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kutoa huduma za kiofisi kwenye Ofisi ndogo ya Bunge, Zanzibar.
- iv. Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa kipindi cha Robo mwaka na Nusu mwaka 2020/2021ziliandaliwa na kuwasilishwa Hazina
- v. Usimamizi wa matumizi ya fedha zilizokasimiwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 ulifanyika kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Manunuzi ya Umma (PFA na PPRA).

- 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**
- 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2021/22**

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/22 Mfuko wa Bunge **unaomba** kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 128,873,377,000.00** Kati ya kiasi hicho, **Sh. 23,205,762,000.00**

zimepangwa kwa ajili ya Mishahara ya Wabunge na Watumishi, **Sh. 98,670,144,000.00** zimepangwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Sh. 6,997,471,000.00** zimepangwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 1,997,471,000.00** ni fedha za nje. Aidha, hadi kufikia Juni 30, 2022 Ofisi imepanga kukusanya maduhuli yenyе jumla ya **Sh. 124,002,000.00**.

Mheshimiwa Spika, maombi haya ya fedha kwa mwaka wa fedha 2021/22 yamezingatia mahitaji ya msingi yakiwemo mahitaji ya shughuli za Bunge (Mkutano ya Bunge na Kamati za Bunge) na uendeshaji wa Ofisi. Hivyo, Mfuko wa Bunge umepanga kutekeleza shughuli za vipaumbele kama ifuatavyo: -

4.2 Shughuli zinazotarajiwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2021/22

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Mfuko wa Bunge unatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

- a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti (1) na Mikutano Midogo Mitatu (3) ya Bunge;
- b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano minne (4) ya Kamati za Kudumu za Bunge ambayo ni Mkutano Mmoja wa Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti na Mikutano Midogo Mitatu (3);
- c) Kuwezesha shughuli za Wabunge katika majimbo na maeneo yao ya uwakilishi;
- d) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
- e) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) pamoja na nyaraka mbalimbali za Bunge na Serikali;
- f) Kutoa huduma za Utafiti kwa Wabunge ("Information Research") pamoja na kukamilisha mfumo wa kidijitali wa Maktaba;

- g) Kuratibu na kusimamia kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge;
- h) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye baadhi ya Mikutano ya Kimataifa kama vile Mikutano ya Bunge la Afrika (PAP), Umoja wa Mabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA) Kanda ya Afrika, CPA- International, Africa, Caribbean, Pacific and European Union (ACP/EU), Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC-PF), Bunge la Afrika Mashariki na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);
- i) Kuandaa vipindi vya televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;
- j) Kuratibu utoaji wa habari kwa wananchi kuhusu shughuli za Bunge na Kamati;
- k) Kuratibu ushiriki wa Wabunge kwenye vikao vya Kamati na Bunge kwa kuwezesha malipo ya posho na stahiki zao (Posho ya Jimbo, vikao, kujikimu na usafiri);
- l) Kuratibu shughuli mbalimbali za kiutawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);
- m) Kuwezesha matibabu ya Waheshimiwa Wabunge ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia Bima ya Afya;
- n) Kuwezesha Watumishi kushiriki mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi;
- o) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba;
- p) Kusimamia uendeshaji wa Ukumbi wa Bunge, mitambo na mashine;
- q) Kuratibu kazi ya kukarabati Jengo la ukumbi wa Bunge na majengo ya Ofisi ya Bunge.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

5.1. Ofisi za Wabunge Majimboni

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inaendelea kusisitizia juu ya suala la uwepo wa ofisi za Wabunge majimboni na kuziwekeea samani kwa utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pindi wanapokuwa majimboni. Aidha, kwa kuwa suala hili walikasimiwa OR-TAMISEMI kwa ajili ya utelekezaji wake, ni vema Bunge likapata maelezo juu ya Mpango wa Serikali wa kukamilisha ujenzi wa Ofisi hizi. Aidha, ikiwezekana fedha hizo zitengwe katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizi.

5.2. Kuongeza eneo la Bunge

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Bunge imekuwa ikakibiliwa na changamoto ya uhaba wa Ofisi kwa ajili ya viongozi wa Bunge, watumishi pamoja na kumbi za kuendeshea vikao vya Kamati na shughuli nyingine za kiofisi. Aidha, Ofisi ya Bunge inakabiliwa na changamoto ya eneo la kuegesha magari ya waheshimiwa wabunge, watumishi wa Bunge na viongozi wa Serikali. Kutokana na changamoto hiyo, Ofisi ya Bunge imeshawasilisha Serikalini maombi ya kuwezeshwa kutwaa na kumilikishwa maeneo yanayozunguka Bunge yanayomilikiwa na taasisi za Serikali pamoja na yale ya watu binafsi. Hatua hii itasaidia kukabiliana na changamoto hizo pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa maeneo ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, aidha ofisi ya Bunge inapenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kuititia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwezesha Ofisi ya Bunge kupata hati miliki ya kiwanja Namba 2 eneo la *Central Business Park* ambacho kinatumika kama maegesho ya magari ya watumishi wa Bunge na wageni mbalimbali. Vilevile, tunamshukuru Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi (Mb), Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kukubali ombi na kuiwezesha Ofisi ya Bunge kumilikishwa kiwanja Namba 12 eneo la *Central Business Park* ambacho kimepakana na *Hotel Fifty Six*. Kiwanja hicho kitatumika kusaidia kutatua changamoto zilizoainishwa.

Aidha, Kamati inapenda kusisitiza Serikali iendelee kusaidia kupatikana kwa maeneo mengine yaliyobakia.

5.3. Kuendelea kuboresha Ofisi ya Bunge na Kituo cha Afya

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kufanya maboresho ya ukarabati wa ukumbi wa Bunge, jengo la utawala na kituo cha afya. Hatua hii imesaidia kuboresha uratibu na uendeshaji wa mikutano ya bunge pamoja na kuimarisha afya za waheshimiwa wabunge na watumishi wa Bunge. Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Ofisi ya Bunge kuendelea kununua vifaa tiba kwa lengo la kudumisha huduma inayotolewa na kituo cha afya cha Bunge.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia naomba kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango ambaye sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge.

Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:

- | | |
|---------------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb | Mjumbe |
| 6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb | Mjumbe |

7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalo, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu na kutoa ushauri wa kitaalamu ambaa umesaidia Kamati katika kukamilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Sillo Daniel Baran (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI

13 Aprili, 2021

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kutuwasilishia mezani ya Kamati yake. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba katika makadirio, eeeh! Kuna watu yaani wako sokoni Kariakoo kabisa, hasa upande huu. (*Makofii*)

Katika Makadirio na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu basi na Ofisi ya Bunge iko ndani yake mle. Ni vizuri tukajua hilo kwamba na mambo yenu yako humohumo. Kwa hiyo, hii Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inatakiwa ipite haraka haraka, mambo yote yanayohusu utaratibu yako huko ndani pia. (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge mtakaochangia, mnaweza kuchangia Wizara yoyote, jambo lolote, kwa sababu Waziri Mkuu ndiyo Mratibu wa Shughuli zote za Serikali Bungeni. Unaweza jambo lako ukasubiri kwenye Wizara husika lakini inawezekana siku ya Wizara husika ukakosa nafasi ya kusema, basi hapa kwa Waziri Mkuu unaweza kutumia nafasi hiyo kuzungumzia lolote unaloliona wewe mwenye kwamba ungependa ulizungumzie.

Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, karibu sana Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofii*)

MHE. FATMA H. TOUFIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kusoma Taarifa ya Kamati yetu. Naomba taarifa ya Kamati kama ilivyowasilishwa mezani iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na

Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) na Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa la Kulevy, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Mafungu mawili 91 na 92. Naanza na Tume ya Kudhibiti UKIMWI, mionganoni mwa mapendekezo tuliyopendekeza ni pamoja na upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za dawa za UKIMWI. Haya yako katika ukurasa wa 14 wa Taarifa yangu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kamati inasilitiza Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa kwa ajili udhibiti wa UKIMWI. Aidha, iweke mipango madhubuti ya kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ni jambo jema bajeti ya UKIMWI kwa kiasi kikubwa itokane na fedha za ndani badala ya kutengemea fedha za wafadhili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna kuanzishwa vyanzo vya Mfuko wa UKIMWI wa Taifa yaani *Aids Trust Fund*, hii imebainishwa katika ukurasa wa 16. Sambamba na hilo, tumeshauri kuhusu lishe kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI inakwenda mpaka ukurasa 17.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumependekeza ni upimaji wa *VVU* na Tohara ya hiyari ya kitabibu kwa wanaume. Hili naomba nilisome. Pamoja na kampeni kubwa ya Furaha Yangu iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhamasisha wanaume kupima na kutambua afya zao inayoitwa Pima, Jitambue, Ishi ya mwaka 2019 ili kuzuia maambukizo ya *VVU* bado takwimu zinaonyesha kuwa kuna idadi kubwa sana ya wanaume wenye umri mkubwa ambao hawajajiteza kupima kama ilivyo kwa wanawake. Ili kuendeleza mapambano ya kuzuia maambukizo ya *VVU* kwa wanaume, aidha, kumekuwa na mwitikio mdogo sana wanaume kujitokeza kupata tohara. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza haya yote yafanyike, hii iko ukurasa wa 18.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunalopendekeza ni kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu za

UKIMWI na kifua kikuu na watu wenye ulemavu. Katika jambo hili, utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana ubora wa takwimu zinazopatikana katika vyanzo mbalimbali. Kuna upungufu mkubwa sana wa ukusanyaji, uhifadhi na matumizi mbalimbali ya taarifa zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU, kifua kikuu na UKIMWI hasa kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuititia Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACA/DS*), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na *TAMISEMI* kuimarisha na kujenga wa uwezo, usimamizi na ufuatiliaji wa takwimu katika maeneo yote ya Halmashauri na vituo vyote vya afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza mpango wa Kimataifa wa Kudhibiti na Kupambana na Ukimwi 95, 95, 95.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tunapendekeza, kwenye mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevyta, Bajeti ya miradi ya maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Kamati ilibaini kwamba tangu kuanzishwa kwa mamlaka hii ya kupambana na dawa za kulevyta, mamlaka imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mojawapo ya athari ya kutotengewa fedha za maendeleo ni kuwepo na changamoto ya vituo vichache vya kliniki vya kutolea dawa za *methadone* na waraibu wa dawa za kulevyta ambapo huduma ya tiba hiyo inatolewa katika Hospitali za Wilaya tu. Kwa hiyo, taarifa hii iko ukurasa wa 20 hadi 21.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tulipendekeza ni kuongeza huduma za nyumba za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevyta (*sober houses*) kwamba, huduma hizi zinatolewa zaidi na sekta binafsi kulingana na miongozo ya Kitaifa. Gharama wanazotozwa kiwango ni kuanzia shilingi 150,000/= hadi 200,000/= kwa mwezi. Kwa hiyo, Serikali inaona kwamba imefikia wakati Serikali ianzishe *sober houses* kwa gherama nafuu ili waraibu waweze kutunzwa. Sambamba na hilo, ushirikishwaji wa asasi

za kiraia, katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya iko ukurasa wa 22 wa taarifa yangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika, Wenyevit wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. Halikadhalika nawapongeza wote walioshiriki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti Ukimwi Fungu 92, jumla ya Shilingi bilioni 4.3 na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Fungu 91, jumla ya shilingi bilioni 8.5.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI
YA WAZIRI MKUU TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA NA
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA
KULEVYA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 NA MAKADIRIO
YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Jijini Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka

ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy - **Fungu 91** na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*) - **Fungu 92** kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 (e) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, kimeipa Kamati ya Masuala ya jukumu la kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy. Katika kutekeleza jukumu hilo, mnamo tarehe 29 Machi, 2021, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 92** – Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*) na **Fungu 91** – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa na Makadirio ya (**Fungu 92 & 91**), naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua mambo makubwa matano (5) yafuatayo: -

- (a) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- (b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- (c) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACA/DS*) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- (d) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevy Tanzania kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- (e) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Fungu 91 na Fungu 92.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

Mheshimiwa Smpika, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kushauri ipasavyo kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilifanya uchambuzi wa wasilisho la serikali kuhusu mambo makuu mawili ambayo ni:

i) Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na

ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yanatokana na kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo:

i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 91 – Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa na Fungu 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa mwaka wa fedha 2020/2021;

ii) Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2021; na

iii) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Uchambuzi huo ulilenga kuliwezesha Bunge lijiridhishe na utoshelevu wa utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi, ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti inayohusika.

2.1 Uchambuzi kuhusu Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Ili kujiridhisha na namna serikali inavyozingatia ushauri wa Kamati unaotolewa na Bunge lako

Tukufu, Kamati ilichambua taarifa iliyowasilishwa kuhusu utekelezaji wa Maoni na ushauri uliotolewa wakati wa kujadili Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu: Fungu 91 – Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevyta na Fungu 92 TACAIDS. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kama ifuatavyo:

2.1.1 Uzingatiaji wa Maoni kuhusu Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

Mheshimiwa Spika, Maoni yaliyokuwa yametolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalihusu maeneo makuu matatu ambayo ni: (1) Kutenga fedha za ndani za Mfuko wa UKIMWI; (2) Serikali kushirikiana na wadau wa sekte binafsi katika Miradi ya Maendeleo; na (3) Uimarishaji wa kujenga uwezo, usimamizi na ufuutiliaji katika maeneo ya ukusanyaji. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa. Hata hvyo, kuna baadhi ya maoni na ushauri haujazingatiwa kikamiliflu. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa sehemu ya ushauri ambayo hajazingatiwa inaendelea kufanyiwa kazi. Mfano wa ushauri huo ni kuhusu vyanzo vya uhakika na endelevu vya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Taifa wa UKIMWI (*AIDS Trust Fund*) ili angalau 75% ya Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania itokane na fedha za ndani. Kamati ilibaini kuwa **bado Tume imendelea kutenga kiasi kidogo cha fedha za ndani kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI** tofauti na ushauri wa Kamati. Ni maoni ya Kamati kuwa bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha kwa ajili ya mwitikio wa UKIMWI yanakuwa na bajeti ya uhakika na isitegemee sana ufadhili wa nje.

2.1.2 Uzingatiaji wa Maoni kuhusu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta Tanzania

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, maeneo manne yalitolewa ushauri. Maeneo hayo yalihusu kutenga bajeti ya miradi ya maendeleo kwa ajili ya Mamlaka, kuweka utaratibu au mfumo rasmi wa namna ya kushughulikia dawa za kulevyta na kukamilisha mwongozo wa Hadidu za Rejea za namna ya Kamati za UKIMWI katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyoweza kutekeleza majukumu ya kudhibiti na

kupambana na dawa za kulevy. Naomba kutoa taarifa kwamba katika baadhi ya maeneo ushauri umezingatiwa na maeneo mengine ushauri unaendelea kuzingatiwa katika hatua tofauti za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Mamlaka kwa kukasimisha majukumu ya udhibiti wa dawa za kulevy yaliyoainishwa chini ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri nchini kupitia gazeti la Serikali, GN (TS) Namba 142 la tarehe 6 Aprili, 2018. Aidha, Kamati inaridhika na hatua iliyofikiwa ya kuandaa rasimu ya Mwongozo wa namna Kamati hizo zinavyoweza kutekeleza majukumu ya kudhibiti na kupambana na dawa za kuleyya.

2.2 Uchambuzi kuhusu Upatikanaji wa Fedha

2.2.1 Upatikanaji wa Fedha za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) - Fungu 92

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge ni jambo la msingi katika kufanikisha utekelezaji wa mpango wa bajeti unaopitishwa na Bunge. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilichambua taarifa ya upatikanaji wa fedha ili kujiridhisha iwapo fedha imepatikana kama ilivyokusudiwa. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari 2021 Fungu 92, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilikuwa imepokea kiasi cha asilimia 71.4 ya Bajeti yake. Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa pamoja na kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni asilimia 64 ya Bajeti yote ya Tume hii, fedha zilizopatikana kwa ajili ya Maendeleo zilizidi uwiano huo kwa kufikia asilimia 71 ya fedha zote zilizopokewa. Takwimu hizo, zinaonekana katika Jedwali Namba 1.

Jedwali Na 1: Ulinganisho wa uwiano wa bajeti na Upatikanaji wa fedha hadi Mwezi Februari, 2021

BAJETI ILIYOIDHINISHWA			UPATIKANAJI WA FEDHA HADI FEBRUARI		
Mhanganuo	kiasi	%	Mhanganuo	kiasi	%
Jumla	7,689,447,000.00	100	Jumla	5,488,985,666.62	100
Kawaida	2,788,708,000.00	36	Kawaida	1,588,246,666.62	29
maendeleo	4,900,739,000.00	64	maendeleo	3,900,739,000.00	71
Ndani	1,000,000,000.00	20	Ndani	3,900,739,000.00	100
Nje	3,900,739,000.00	80	Nje	0	0

Chanzo: Taarifa ya Tume (TACAIDS) ya Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, licha ya uwiano huo wa fedha zilizopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuonekana mkubwa, fedha za nje kwa ajili hiyo, zimechukwa asilimia 100 ya fedha za maendeleo zilizopatikana. Tafsiri ya matokeo hayo ni kuwa, Tume haikupata kiasi chochote cha fedha za ndani za maendeleo. Hali hii inaoenesha utegemezi mkubwa wa kibajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayohusu mapambano dhidi ya UKIMWI. Ni maoni ya Kamati kuwa uwiano uliojitekeza kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni jambo linalohitaji kurekebishwa ili kuijimarisha katika kupambana na janga la UKIMWI kwa mustakabali wa taifa.

2.2.2 Upatikanaji wa Fedha za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta (DCEA) - Fungu 91

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta (Fungu 91), zilitarajiwa kuwezesha mapambano na udhibiti wa dawa za kulevyta. Aidha, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionesha kuwa kati ya shilingi **9,033,345,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge, Mamlaka imepokea jumla ya shilingi **5,308,281,428.00**. Kiasi kilichopokewa ni sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mamlaka hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa Bunge liliidhinisha asilimia 68 ya bajeti ya Mamlaka kwa ajili ya Uendeshaji na asilimia 32 ya bajeti kwa ajili ya mishahara. Ulinganisho umeonesha kuwa, kiasi cha fedha zilizopatikana kwa ajili ya mishahara ni asilimia 23 ya fedha iliyopokewa, na kiasi kilichopokewa kwa ajili ya uendeshaji ni asilimia 77 ya fedha yote iliyopokewa. Tafsiri ya matokeo hayo ni kuwa uzito uliotolewa na Bunge kuhusu uwiano kati ya bajeti ya mishahara na bajeti ya uendeshaji unatofautiana na uzito wa uwiano unaojitokeza katika kiasi cha fedha zilizopokewa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Kiasi Kilichopokewa

BAJETI ILYOIDHINISHWA		FEDHA ILYOPOKEWA	
Mchanganuo	Kiasi	%	Kiasi
Uendeshaji	6,167,415,000.00	68	4,111,610,000.00
Mishahara (PE)	2,865,930,000.00	32	1,196,671,428.00

Chanzo: Taarifa ya Mamlaka Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022

2.3 Uchambuzi wa yaliyobainika wakati wa ziara ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 10 (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, kinachohusu jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na Udhhibit wa Dawa za Kulevyta, Kamati ilifanya ziara kati ya tarehe 1 – 5 Machi 2021, kutembelea na kukagua utekelezaji wa afua na shughuli zinazotekelzeza na Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali katika mwitikio dhidi ya mapambano ya UKIMWI, Kifua Kikuu pamoja na biashara na matumizi ya Dawa za Kulevyta katika Mikoa ya Njombe, Mbeya na

Songwe. Ufuatiliaji huo ulifanyika kwa kukagua konga, hali ilivyo magerezani, huduma za CTC na upatikanaji wa Methodone kwa ajili ya kurekebisha uraibu (*addiction*).

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto na kudadisi kuhusu hatua zinazochukuliwa ili kuzikabili changamoto zilizoripotiwa. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kama ifuatavyo: -

2.3.1 Utoro wa kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU kutokana na umbali wa vituo vya kutolea dawa

Mheshimiwa Spika, changamoto ya watu wanaoishi na VVU kutoroka matumizi ya dawa za kufubaza makali ya VVU kwa kiasi kikubwa umechangiwa na umbali wa vituo vya kutolea dawa, gharama za usafiri kutokana na watumiaji wengi kuwa wakazi wa maeneo ya pembezoni mwa Halmashauri zao. Kwa watumiaji wachache ambaon ni wakazi walio karibu na maeneo ya upatikanaji wa dawa hizo, baadhi yao hutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu makazi yao na mawasiliano yao, kutokana na hali iliyopo ya unyanyapaa. Hali hiyo pia imechangia kwa baadhi ya watumiaji wa dawa kwenda kuchukua dawa katika vituo vilivyoko mbali na maeneo wanayoishi.

2.3.2 Kuenea kwa Ugonjwa wa Kifua Kikuu Magerezani

Mheshimiwa Spika, kama inavyoileweka, Magereza mengi nchini yanakabiliwa na tatizo la msongamano hali inayosababisha changamoto ya kukosekana kwa mzunguko wa kutosha wa hewa kwa wafungwa na mahabusu. Mazingira haya yanachochea maambukizi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa haraka. Kamati ilibaini kuwa ili kukabiliana na kuenea kwa Ugonjwa wa Kifua Kikuu hatua za awali za upimaji na kuanzishowiwa dawa kwa wanaokutwa na Kifua Kikuu ni njia ya inayotumika katika mapambano dhidi ya kifua kikuu. Kamati ina maoni kuwa hali ya msongamano magerezani inaweza kupatiwa ufumbuzi chini ya uratibu unaofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

2.3.3 Kuenea kwa ugonjwa wa homa ya ini na vvu kwa waraibu wa Dawa za Kulevy

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizotolewa kwa Kamati wakati wa ziara zinaonesha kukosekana kwa takwimu za ugonjwa wa Kifua Kikuu na Homa ya Ini B na C kwa waraibu wanaotumia dawa za kulevy waanaishi na VVU. Aidha, ilibainika kuwa wapo waathirika wa dawa za kulevy wenyewe magonjwa mengine zaidi ya uraibu ikiwemo magonjwa ya akili, Kifua Kikuu na UKIMWI. Hali hii inaonekana kuathiri kasi ya upataji nafuu na kudhoofisha tiba na ushiriki mdogo katika kuchangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati imebaini kuwa hali ya maambukizi ya ugonjwa wa homa ya ini mionganoni mwa waraibu wa dawa za kulevy inaendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa, jambo linalotishia ustawi wa jamii nzima. Taarifa zilizopatikana katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati zilionesha kuwa jumla ya waraibu 345 wanatumia dawa ya *methadone* kila siku. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kati ya idadi hiyo, wanaume ni 329 sawa na asilimia 95.4 na wanawake 16 sawa na asilimia 4.6. Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa ama wanaume wamejitokeza zaidi kupata dawa na kupambana na uraibu au wanawake hawakuathirika kwa kiwango kama cha athari kwa wanaume. Kamati ina imani kuwa, pamoja na kutoa huduma za *methadone* kwa waraibu ni muhimu kwa kliniki zote kuhakikisha zinakuwa na takwimu sahihi za kutosha na zinazonyambulisha makundi mbalimbali ya kijamii ili kuwezesha mikakati ya mapambano dhidi ya tatizo la uraibu wa dawa za kulevy.

2.3.4 Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati katika Mkoa wa Songwe, Halmashauri ya Mji wa Tunduma-Momba, ilitumika kama sampuli kwa maeneo mengine. Takwimu za taarifa zilizowasilishwa zilionesha kiwango cha maambukizi ya VVU ambapo takribani watu 43,819 waliripotiwa kuwa wanaishi na VVU. Aidha, takwimu zilionesha kuwa jumla ya WAVIU 39,267 sawa na asilimia 89.6 ya watu wanaokadiriwa

kuambukizwa VVU wanatambua hali zao za maambukizi na asilimia 99 ya wote waliobainika kuambukizwa VVU wapo katika tiba na matunzo ya ARVs.

Mheshimiwa Spika, Taarifa zaidi ilionesha kuwa Mkoa wa Songwe uliweza kuwafikia wanaume wapatao 57,202 sawa na asilimia 42.5 na wanawake wapatao 77,394 sawa na asilimia 57.5 kwa huduma ya upimaji, ambapo kati yao wanaume 1,883 sawa na asilimia 40.15 na wanawake 2,806 sawa na asilimia 9.84 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na wote waliunganishwa katika huduma ya tiba na matunzo. Kundi lenye kiwango kikubwa cha maambukizi ni umri kuanzia miaka 25 - 49 kwa asilimia 37.5 na kundi la umri kati ya 20 - 24 kwa asilimia 11.4.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hizo zinadhahirisha mwamko na mwitikio mdogo wa wanaume kujitokeza kupimla na kufahamu hali zao za maambukizi. Hali hii ya Mkoa wa Songwe ndivyo ilivyo katika mikoa yote nchini na inachangia kurudisha nyuma kasi ya mapambano ya kitaifa dhidi ya UKIMWI/VVU. Ni maoni ya Kamati kuwa ili kufikia malengo yanayotarajiwa ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI wa 95 95 95 ifikapo mwaka 2025 na kufikia 0 0 0 ifikapo mwaka 2030, Uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu unahitajika zaidi. Jambo hilo, linaweza kuwahuisha wizara za sekta, ofisi za wakuu wa mikoa na wadau wengine mbalimbali wanaojihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI. Mikakati madhubuti ya kuhakikisha wanaume wanapima inaweza kupatikana na kufanikisha Malengo ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Tarehe 29 Machi, 2021, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Fungu 91 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa) na Fungu 92 (Tume ya

Kudhibiti UKIMWI Tanzania) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 tarehe 22 hadi 23 Machi 2021. Uchambuzi ulilenga pamoja na mambo mengine kuhakiki kama Mpango na Makadirio haya vimezingatia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 na Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango. Uchambuzi unaonesha kuwa maeneo ya vipaumbele katika makadirio hayo yamezingatia miongozo inayotakiwa ikiwemo llani ya Uchaguzi.

3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

3.1.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kupitia **Fungu 92** inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **5,000,000.00**, ambayo yanatarajiwa kusatikana kutokana na uuzaji wa vifaa chakavu na tozo kutokana na matumizi ya Ukumbi wa Mikutano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makadirio ya matumizi katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** inaombewa jumla ya shilingi **4,317,818,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 1,389,470,000** sawa na **asilimia 32** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi **2,928,348,000** sawa na **asilimia 68** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa makadirio haya yameongezeka kwa shilingi **139,640,000.00** ambayo ni sawa na asilimia **8.9** ikilinganishwa na fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na uhamisho wa fedha kwa mwaka 2020/2021 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/21 na Makadirio ya matumizi kwa mwaka 2021/22

Chanzo: Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo, uchambuzi umeonesha kuwa bajeti inayoombwa imepungua kwa asilimia 72 ambacho ni kiasi kikubwa cha tofauti. Kwa kawaida fedha zinazotumika

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2020/21			MAKADIRIO 2021/22		
Mchanganuo	kiasi	%	Mchanganuo	kiasi	% Tofauti
Jumla	7,689,447,000.00	100	Jumla	4,317,818,000	-44
Kawaida	2,788,708,000.00	36	Kawaida	2,928,348,000	+5
Maendeleo	4,900,739,000.00	64	maendeleo	1,389,470,000	-72

3.1.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta-Fungu 91

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umeonesha kuwa kiasi kinachoombwa ni **Shilingi 8,529,789,000.00** ambapo **Shilingi 6,167,415,000** sawa na **asilimia 72** ya fedha yote inayoombwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi

2,362,382,000, sawa na **asilimia 28 ni** Mishahara. Makadirio haya yamepungua kwa kiasi cha shilingi **503,548,000** sawa na **asilimia 6** ikilinganishwa na bajeti ya Fungu hili iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4 la Taarifa hii.

Jedwali Na. 4 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka 2021/2022

BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2020/21			MAKADIRIO 2021/22		
Mchanganuo	kiasi	%	Mchanganuo	kiasi	% Tofauti
Jumla	9,033,345,000.00	100	Jumla	8,529,789,000.00	6
Mishahara	2,865,930,000.00	32	Mishahara	362,382,000.00	87
OC	6,167,415,000.00	68	OC	6,167,415,000.00	0
Maendeleo	0	0	Maendeleo	0	-72

Chanzo: Taarifa ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umebainisha kuwa bajeti ya mishahara imepungua kwa kiasi kikubwa kufikia punguzo la asilimia 87. Tofauti hiyo ni kubwa na ilitoa mashaka kwa Kamati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Kudumu za Bunge (3)(2), Kamati ya Bajeti ilipitia na kuchambua masuala muhimu ya kibajeti yaliyojitekeza katika Fungu 91 ambapo majibu ya Serikali ni kuwa kiasi cha shilingi **503,548,000** kimezingatiwa katika Fungu 21 – Hazina kuititia Kasma ya *Salary Adjustment* ambazo zitatumika kulipa Makamishna wa Tume wanaotarajiwa kuteuliwa wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 na Makadirio ya

matumzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kupambana na kudhibiti Dawa za kukevya, Sasa naomba kutoa maoni na ushauri kwa mafungu yote mawili: Fungu 91 na Fungu 92.

4.1 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania

4.1.1 Upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia Bajeti, Kamati imebaini kuwa mpaka sasa asilimia kubwa ya Bajeti ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania bado imekuwa ikitegemea fedha za wahisani. Katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi **Bilioni 4.9** tu sawa na **asilimia 76.6** ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Tume. Kati ya fedha hizo shilingi **3.9** ni fedha za nje na shilingi **Bilioni 1 (Bil 1)** fedha za ndani ambazo mpaka Kamati inapitia Bajeti ya Fungu 92 hakuna kiasi chochote cha fedha za ndani kilichotolewa na hazina bali ni fedha za nje za wadau mbalimbali wa masuala ya UKIMWI. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (3)(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, baada ya mashauriano baina ya Serikali na Kamati ya Bajeti kiasi cha **shilingi 500,000,000.00**, sawa na **asilimia 50** kimetolewa kwa ajili ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (*ATF*). Fedha zilizobaki kiasi cha **shilingi 500,000,000.00** zitatolewa katika kipindi kilichobaki cha utekelezaji wa Bajeti hadi Juni 2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na Tume kuendelea kutegemea fedha za wafadhili kutoka nje ambazo hazina uhakika na zenye masharti magumu kwa ajili ya mwitikio endelevu wa mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuzingatia kwamba, baadhi ya wafadhili wameanza kupunguza kiwango cha ufadhili wa fedha za UKIMWI kwa Tanzania.

Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI. Aidha, iweke mipango madhubuti ya kupata vyanzo vingine vya mapato vitakavyosaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya Miradi ya

Maendeleo. Ni jambo jema bajeti ya UKIMWI kwa kiasi kikubwa itokane na fedha zetu za ndani.

**4.1.2 Kuanzisha Vyano kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa
(AIDS Trust Fund - ATF)**

Mheshimiwa Spika, Pamoja na Serikali kuonesha nia nzuri njema na nzuri ya kutenga fedha kwa ajili ya *ATF*, bado Kamati inaona upo umuhimu wa Serikali kufanya uchambuzi na upembuzi wa kina wa vyano mbalimbali nya mapato kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI (*Aids Trust Fund - ATF*).

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mfuko wa Udhagini wa UKIMWI kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 unaonesha kuwa, shilingi **bilioni moja (1 Bil)** zimetengwa kwa ajili ya *ATF*. Kamati imebaini kuwa, pamoja na jitihada za Serikali kutenga fedha katika Mfuko huu, bado Serikali inatakiwa kufanya uchambuzi na upembuzi wa kina kuhusu mapato mbalimbali kwa ajili ya kutunisha Mfuko. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kubuni namna bora na nzuri ambayo itawezesha kupata chanzo cha mapato kwa ajili ya Mfuko wa *ATF*.

4.1.3 Lishe kwa Watu Wanaoishi na Virusi nya UKIMWI

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoa dawa za kufubaza makali ya VVU kwa watu wanaoishi na VVU, Kamati imebaini bado hakuna elimu ya kutosha kuhusiana na masuala ya lishe na ulajii bora wa kuzingatia makundi maalum ya vyakula ili kudumisha na kuboresha afya za WAVIU. Kamati inaishauri Serikali na wadau wote wanaojihusisha na masuala ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevyta, kutoa elimu ya lishe katika vituo vyote nya tiba na matunzo juu ya umuhimu wa kula vyakula mchanganyiko kwa kuzingatia makundi matano ya vyakula vilivyopo katika jamii wanayoishi. Pia upimaji wa hali ya lishe ufanyike kwa wateja katika vituo vyote nya tiba na matunzo kwa wateja wanaogundulika na changamoto ya lishe. Aidha, uwepo

ufuatiliaji wa karibu kwa kuwatumia watoa huduma ngazi ya jamii na kutumia mtandao wa WAVIU.

4.1.4 Upimaji wa VVU na Tohara ya Hiari ya Kitabibu kwa Wanaume

Mheshimiwa Spika, pamoja na kamjeni kubwa ya **FURAHA YANGU** iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhamasisha wanaume kupima na kutambua afya zao inayoitwa “**PIMA, JITAMBUE, ISHI**” ya mwaka 2019 ili kuzuia maambukizi ya VVU, bado takwimu zinaonesha kuwa kuna idadi kubwa ya wanaume wenye umri mkubwa hawajajitezea kupima kama ilivyo kwa wanawake, ili kuendeleza mapambano ya kuzuia maambukizi mapya ya VVU kwa wanaume. Aidha, kumekuwepo na mwitikio na ushiriki mdogo wa wanaume kujitezea kupata huduma ya Tohara Kinga. Kwa mfano, Mkoa wa Njombe ulijiwekea lengo la kuwafikia wanaume 14,055, ambapo hadi Disemba 2020 wanaume wapatao 8,319 sawa na asilimia 59 walikuwa wamefanyiwa Tohara Kinga.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali, Baraza la Watu Wanaoishi Virusi vya UKIMWI pamoja na wadau mbalimbali wanaojihusisha na mapambano ya VVU, kuendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kamjeni za upimaji VVU na tohara kwa wanaume zinaendelea kufanyika ili kupunguza maambukizi mapya. Kamjeni hizo ziwashirikishe Viongozi wa Ngazi za Juu (*Public Figures*) kama Mawaziri, Wabunge na Viongozi wa Dini.

4.1.5 Kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na matumizi ya takwimu za UKIMWI na Kifua Kikuu kwa Watu wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unategemea sana ubora wa takwimu zinazopatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kuna upungufu mkubwa katika ukusanyaji, uhifadhi na matumizi mbalimbali ya taarifa zinazohusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU, Kifua Kikuu na UKIMWI kwa Watu wenye ulemavu. Kamati

inaishauri Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAI/DS*), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na TAMISEMI kuimarisha ujengaji wa uwezo, usimamizi na ufuatiliaji wa takwimu katika maeneo yote ya Halmashauri na vituo vyote vya afya. Jambo hili ni muhimu ili Taifa liweze kuongeza kasi ya kutekeleza Mpango wa Kimataifa wa Kudhibiti na Kupambana na UKIMWI wa 95 – 95 – 95.

4.2 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta

4.2.1 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Mamlaka imekuwa haitengewi bajeti kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mojawapo ya athari za kutotengewa fedha za maendeleo ni kuwepo kwa changamoto ya vituo vichache vya kliniki za kutolea dawa ya *methadone* kwa waraibu wa dawa za kulevyta ambapo huduma hiyo ya tiba inatolewa katika hospitali za wilaya tu.

Mheshimiwa Spika, ajenda ya kupambana na dawa za kulevyta ni kubwa na inapaswa kuangaliwa kwa uzito wa pekee. Kamati inaona kuwa Miradi ya Maendeleo inayoweza kutekelezwa kwa fedha za maendeleo ni pamoja na kuwawezesha waraibu kiuchumi kwa kuwapa mbinu za ujasiriamali, mikopo nafuu ya biashara, kilimo, ushonaji, ufugaji na stadi za maisha. Fedha hizo zikitengwa zinaweza kusaidia uongezaji wa vituo vya upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevyta pamoja na kufanya uraghibishi kwa jamii wa namna ya kupambana na kudhibiti dawa za kulevyta pamoja na kuanzisha ujenzi wa vituo vya ofisi za kanda katika maeneo ambayo yana viashiria vya matumizi makubwa ya dawa za kulevyta. Kwa mfano, hivi sasa Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyopo Mkoani Mbeya inahudumia Mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya.

4.2.2 Kuongeza huduma ya nyumba za upataji nafuu kwa waathirika wa dawa za kulevy (Sobber Houses)

Mheshimiwa Spika, huduma za *Sobber Houses* zinazotolewa na sekta binafsi kulingana na miongozo ya kitaifa ambapo wagonjwa hulipia gharama kulingana na makubaliano ya mgonjwa na watoa huduma na pia kulingana na muda ambao mgonjwa ataishi katika nyumba hiyo. Gharama hizo zinatozwa kwa kiwango cha shilingi 150,000 hadi shilingi 200,000 kwa mwezi. Kamati inapongeza Serikali kwa kutoa miongozo ya namna ya kuziratibu. Hata hivyo, Kamati inaona wakati umefika sasa wa kuanzisha *Sobber Houses* za Serikali ambazo zitapunguza mzigo wa gharama za kuwatunza waraibu. Hatua hii ni muhimu kwa sababu tiba ya *methadone* ina mchango mkubwa kwa taifa kijamii na kiuchumi pia.

4.2.3 Ushirikishwaji wa Asasi za Kiraia katika Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevy

Mheshimiwa Spika, kufuatia kazi nzuri inayofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy kwa kushirikiana na Wadau wa Walter Reed kupitia Halmashauri wamefanikwa kuwaunganisha waraibu katika kuwatibu waraibu wa dawa za kulevy na kupunguza maambukizi ya VVU, kituo cha upataji nafuu cha Mkoa wa Mbeya kimefanikiwa kuwasaidia kuwafuatilia kwa ukaribu mienendo ya kuacha matumizi ya dawa hizo, kupunguza unyanyapaa mionganoni mwa jamii, kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi, pamoja na kupata takwimu sahihi za waraibu. Hata hivyo, bado asasi zilizopo ni chache sana ukilinganisha na mahitaji, badala yake kila asasi inafanya jithada zake peke yake. Kamati inaishauri Serikali kuzihimiza asasi nyingine kuiga mfano wa Walter Reed ili kurahisisha kuwatambua, kuwashirikisha na kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevy.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi muda wa kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kukupongeza kwa uongozi wako thabiti ulionao katika kuliendesha Bunge letu.

Nawashukuru na kuwapongeza pia Naibu Spika na Wenye viti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yenu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb) pamoja na Manaibu Waziri; Mheshimiwa Ummey Nderiananga (Mb) na Mheshimiwa Patrobas Katambi (Mb). Vilevile namshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mhe Dorothy Gwajima na Naibu Waziri Mhe. Godwin Mollel kwa ushirikiano wao mkubwa wanaondelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati. Vilevile napenda kuwashukuru Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Watu wenye Ulemavu, Ofisi ya Waziri Mkuu Nd. Txon Tuyangine Nzunda pamoja na Maafisa Waandamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Kamishna Jenerali Gerald Kusaya Musabila na Watendaji wote, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ili kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Pamoja na ufinyu wa muda, Wajumbe hawa walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:-

- | | |
|--|----------------|
| 1. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb | - M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb | - Mjumbe |

- | | | |
|---|---|--------|
| 4. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb | - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Justin Lazaro Nyamoga, Mb | - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb | - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb | - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mb | - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Oliver D. Semuguruka, Mb | - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - | Mjumbe |
| 14. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb | - | Mjumbe |
| 15. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb | - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb | - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mb | - | Mjumbe |
| 18. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb | - | Mjumbe |
| 19. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb | - | Mjumbe |
| 20. Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma, Mb | - | Mjumbe |
| 21. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb | - | Mjumbe |
| 22. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb | - | Mjumbe |
| 23. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb | - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb | - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Ndugu Stephen Kagaigai - Katibu wa Bunge, Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndg. Gerald Magili, Mkurugenzi Msaidizi, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Asia Msangi, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania - **Fungu 92** jumla ya shilingi **4,317,818,000.00** na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta - **Fungu 91** jumla ya shilingi **8,529,797,000.00**.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja

Mhe. Fatma H. Toufiq, (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

13 Aprili, 2021

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Ukimwi, Mheshimiwa Fatma Toufiq. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Humphrey Polepole, karibu sana. Karibu sana. (*Makofii*)

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 fasili ya (9) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Naomba kama ulivyoelekeza nijikite katika maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za utekelezaji wa Bajeti iliyopita na maombi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) ikamilishe haraka uandaaji wa Mwongozo wa Taifa kwa uwekezaji (*National Investments Guidelines*) ambao utatoo mwelekeo wa Taifa kuhusiana na masuala ya uwekezaji. Aidha, mwongozo huo uwekwe kwenye mtandao ili kuwawezesha wawekezaji kutambua matakwa ya kuzingatia kabla ya kuanza mchakato wa kuomba vibali vinavyohusiana na uwekezaji. Baadhi ya Mikoa imefanya kazi

nzuri ya uandaaji wa miongozo na mazingira ya uwekezaji. Hata hivyo, bado tunahitaji kuwa na mwongozo wa Taifa ambao utakuwa rejea kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali iendelee kuelimisha wananchi kuzingatia sheria na utaratibu kwa kuwa makini wanapoingia mikataba ya ubia na wawekezaji wa nje ili kupunguza au kuondoa kabisa migogoro na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba wamekuwa wakidhulumiwa na wawekezaji wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, imebainika kwamba wananchi wengi wanakosa umakini wanapoingia kwenye makubaliano ya ubia na wawekezaji wa kigeni na ndiyo maana wanapowasilisha malalamiko hayo kwenye vyombo vya kisheria hushindwa kutokana na kubanwa na vipengele vya mikataba.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iendelee kuboresha mazingira ya uanzishaji na ufanyaji wa biashara nchini kwa kupunguza urasimu, hali ambayo itaendelea kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara wengi kuja kuwekeza mitaji yao nchini. Hatua hii itasaidia nchi kuendelea kupanda juu katika nafasi za dunia katika mazingira bora ya ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya ufanyaji biashara katika mwaka 2019 Tanzania ilikuwa nchi ya 141 kati ya nchi 190 duniani zenyne mazingira mazuri ya kufanya biashara ikiwa imepanda nafasi tatu zaidi. Ni matumaini ya Kamati kwamba, kwa jitihada zilizopo Tanzania ina fursa ya kupanda zaidi na kuwa kinara wa mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji biashara katika Afrika nzima na hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ihakikishe muda wa mwekezaji kushughulikia na kupata vibali vya uwekezaji hauzidi siku saba za kazi ilimradi mwekezaji huyo, awe amezingatia matakwa ya kisheria na vigezo vilivyowekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali iweke vivutio zaidi kwa wawekezaji wa nje ambao wako tayari kuwekeza mitaji mikubwa hapa nchini na kuboresha mazingira ya kisera, kisheria, kiutaratibu ili kuwajengea imani ya kuwajengea na kukuza mitaji ya uwekezaji wao nchini.

Mheshimiwa Spika, sita, Serikali iangalie namna ya kuhamasisha na kuanzisha kada ya wataalam washauri wa masuala ya uwekezaji *investments consultants* kwa lengo la kuwasaidia kuhamasisha kutoa takwimu taarifa na ushauri wa kitaalam na wageni na wananchi wanaohitaji kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, jukumu hili kwa sasa linatekelezwa na watu waslo na ujuzi wala taarifa za kitaalam kuhusiana na masuala ya uwekezaji, yaani madalali wa uwekezaji ambao wameshindwa kutoa ushauri wa kitaalam kwa taarifa zinazojitosheleza kwa watu wenyе nia ya kuwekeza nchini. Katika Mataifa yaliyopiga hatua kubwa katika uwekezaji, wataalam washauri wa uwekezaji ni miongoni mwa wataalam muhimu wanaochangia maendeleo ya uchumi wa nchi na wanatambuliwa kisheria katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, saba, Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha tovuti maalum itakayounganisha Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) na Balozi za Tanzania ili kuziwezesha kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu kwa lengo la kuyafikia kwa urahisi majukwaa ya uwekezaji duniani (*International Investment Platforms*).

Mheshimiwa Spika, nane, Serikali iandae utaratibu wa kuwezesha wananchi wenyе fursa ya kuwekeza nchini kukutana na wageni wanaokusudia kuwekeza nchini. Kwa hali ilivyo hivi sasa, ni vigumu kwa mgeni kutoka nje kutambua namna ya kukutana na mwananchi ambaye wanaweza kuwekeza kwa ubia kwa sababu hakuna jukwaa la kukutanisha pande hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, tisa, Serikali ifanye tathmini ya kitaalam ili kubaini iwapo sera yetu ya uwekezaji bado inakidhi matakwa au inahitaji kuhuishwa, ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea kwa kasi duniani kuhusiana na masuala ya uwekezaji na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kumi, Serikali iendelee kuhakikisha Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) kinatimiza majukumu yake kwa kuzingatia, sheria, uadilifu, uwajibikaji, uwazi na tija ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo kuu la kukuza uwekezaji kutoka nje na ndani.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, Serikali itekeleze kwa haraka mchakato wa uanzishaji wa kanzidata (*database*) ya Taifa ya kuhusiana na uwekezaji ili kuwezesha nchi kuwa na takwimu sahihi za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kumi na mbili, Taasisi zinazohusiana na masuala ya uwekezaji ziwe na mifumo ikiwemo ya TEHAMA ambayo inasomana ili kupunguza muda na kupusha usumbu kwa wawekezaji pale wanapofutilia masuala ya kiuwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika hitimisho, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa Bajeti ya Fungu hili hadi kukamilika kwa taarifa hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia taarifa yote hii iingie kwa *Hansard*. Natamani kuwataja Wajumbe wote wa Kamati kwa usemi, naomba niwatambue kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee natambua na kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Steven Kigaigai na Watendaji wa Bunge (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi Fungu 11 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mto hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa wajibu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, hutanguliwa na jukumu la ukaguzi wa utekelezaji wa miradi iliyo tengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge.

Hata hivyo, taarifa hii haitagusa eneo la ukaguzi wa utekelezaji wa miradi kwani hakukuwa na fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Fungu 11 – Uwekezaji ni fungu jipya la bajeti ambalo limeanzishwa ili kuwezesha uratibu na usimamiaji wa masuala ya uhamasishaji wa uwekezaji (*investment facilitation*) na ufuatiliaji wa uwekezaji (*investment monitoring*) nchini.

Uanzishaji wa fungu hili ni sehemu ya uzingatiaji wa maelekezo ya Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dokta John Pombe Magufuli, aliyoyatoa wakati akifungua rasmi Bunge la Kumi na Mbili (12) mwezi Novemba, 2020 ambapo alisisitiza juu ya azma ya Serikali ya kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya uwekezaji nchini.

Aidha, msisitizo wa kuimarisha uratibu wa masuala ya uwekezaji ulirejewa tena na Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan tarehe 01 Aprilli, 2021 wakati akiwaapisha Mawaziri alliowateua, Ikulu ya Chamwino, Dodoma. Alielekeza kushughulikiwa kwa urasimu na kero ambazo wawekezaji wamekuwa wakikumbana nazo katika taasisi za Serikali pale wanapofuattilia vibali vya uwekezaji na vibali ya kufanya kazi nchini hasa kwa wageni.

Kabla ya kuanzishwa kwa fungu maalumu la bajeti shughuli za uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji zilitekelezwa na Idara ya Maendeleo na Uwekezaji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mintarafu maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii itatoa maelezo kuhusu maeneo matatu yafuatayo:-

- i. Mapitio ya Utekelezaji wa Shughuli za Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- ii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na
- iii. Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 idara ya maendeleo na uwekezaji ambayo inahusisha Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ilitekeleza jumla ya kazi 25 na baadhi ya kazi hizo ni zifuatazo:-

- i. Mikutano miwili ya wadau kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997;
- ii. Kuratibu utekelezaji wa Mipango na Programu za Kitaifa za kuboresha mazingira ya kibiashara na uwekezaji ikiwemo tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*The Government Roadmap*) wa mwaka 2010 kwa kipindi cha miaka kumi;
- iii. Kuratibu maandalizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya Wawekezaji (*online investors feedback platform*) kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Baraza la Biashara la Taifa (TNBC);
- iv. Kutembelea miradi ya uwekezaji kwa ajili ya kutathmini maendeleo ya uwekezaji na kutatua changamoto katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Iringa, Dodoma na Tanga;
- v. Kukutana na Mashirika ya Kimataifa na balozi za Sweeden, Marekani, Umoja wa Ulaya na Benki ya Dunia kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji kutoka katika nchi wanazoiwakilisha;
- vi. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu huduma zitolewazo na Kituo cha Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Centre – OSC);

- vii. Kufuatilia na kutatua migogoro ya wawekezaji kuhusu vibali
vya kazi, upatikanaji wa ardhi na umiliki wa kampuni;
- viii. kusajili miradi 134 yenye thamani ya Dola za Marekani
milioni 624 ambayo itaa jiri Watanzania 11,806;
- ix. Kutafiti, kuibua na kuchambua fursa za uwekezaji kutokana
na Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR);
- x. Kuandaa makongamano ya uwekezaji kwa kushirikiana na
Ofisi za Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Rukwa na Singida;
- xi. Kuwezesha Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kuongeza
uelewa wa Virusi vya UKIMWI kwa kufanya Semina kwa
Watumishi;
- xii. Kuwezesha Baraza la Taifa la Biashara kutoa elimu ya
kupambana na kuzuia rushwa kwa Watumishi;
- xiii. Kufanya Mikutano 17 ya Mabaraza ya Biashara ya Mikoa
(RBCs) na Mikutano 26 ya Mabaraza ya Biashara ya Wilaya
(DBCs);
- xiv. Kuwezesha Baraza kuratibu mikutano na TRA, EWURA,
PCCB, TIC, FCC, TPA, TARURA na Washirika wa Maendeleo;
na
- xv. Kutembelea vituo vya pamoja katika mipaka sita (6) ya
Rusumo, Kabanga, Tunduma, Sirari, Horohoro na Mtukula.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa fungu maalum kwa ajili
ya kuratibu na kusimamia masuala ya uwekezaji ni hatua
muhimu ambayo siyo tu inadhihirisha azma ya Serikali katika
kusimamia kikamilifu masuala ya uwekezaji, bali pia inatoa
fursa kwa shughuli za uwekezaji kuwa na bajeti mahsusii

itakayowezesha kugharamia uratibu wa masuala ya uwekezaji.

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Fungu 11 – Uwekezaji umeandalishiwa kwa kuzingatia:-

- i. Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025;
- ii. Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22 - 2025/26);
- iii. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2020;
- iv. Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022;
- v. Hotuba ya Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, wakati akizindua Bunge la Kumi na Mbili (12); Pamoja na
- vi. Maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ofisi hii kwa ujumla wake imepanga kutekeleza malengo matano (5) katika mwaka ujao wa fedha na malengo hayo ni haya yafuatayo:-

- i. Kuimarisha Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji (NIDS) kwa kuratibu, kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia uwekezaji. Aidha, kuwezesha uendelezaji wa miundombinu muhimu ya uwekezaji katika mikoa yote nchini na kujenga uwezo wa kufuatilia kwa ngazi ya kitaifa na mikoa;
- ii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Biashara (Roadmap);

- iii. Kufanya tafiti zenye lengo la kuibua fursa za uwekezaji na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za uwekezaji;
- iv. Kuandaa Kanzi Data (*Database*) ya Uwekezaji ili kuwa na takwimu sahihi za uwekezaji wa ndani na nje; na
- v. Kuimarisha utoaji wa Huduma Mahali Pamoja (*One Stop Center*) ili kuboresha huduma na kuwezesha upatikanaji wa vibali ndani ya siku kumi na nne (14).

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Fungu 11 - Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji linaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 7,018,213,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Aidha, katika fedha hizo **Shilingi 710,688,000** sawa na **asilimia 10.13** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 6,307,525,000/=** sawa na **asilimia 89.87** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kwa asili ya shughuli za uwekezaji fungu hili jipya la bajeti linastahili kutengewa fedha za maendeleo ili kuliwezesha kutekeleza malengo yake kikamilifu hasa kwa kuzingatia baadhi ya malengo yanayotarajiwu kutekelezwa.

3.1 Uchambuzi wa Bajeti ya Uwekezaji kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Lengo la ulinganisho huo lilikuwa kubaini ni kiasi gani cha fedha kimeelekezwa kwenye uratibu wa shughuli za uwekezaji ikilinganishwa na bajeti ya Taifa.

Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelizwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

i. Bajeti ya OWM - Uwekezaji, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Bilioni 7.02** ni sawa na **asilimia 0.02** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ni **Shilingi triliioni 36.26/=**


ii. Bajeti ya OWM - Uwekezaji (**shilingi bilioni 7.2**) ambayo inahusisha Matumizi ya Kawaida pekee ni sawa na **asilimia 0.03** ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2021/2022 ambayo ni **Shilingi Triliioni 23.**

Jedwali Na. 1: Ulinganisho wa Bajeti ya Uwekezaji dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022			BAJETI YA OFISI UWEKEZAJI 2021/2022		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh. Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti Kuu	Mgawanyo	Bajeti ya OWM - Uwekezaji	Asilimia ya Jumla - Uwekezaji
OC	3,946,164	10.98	OC	6,307,525,000	89.87
Deni la Taifa	10,663,278	29.59	-	-	-
Mishahara	8,150,509	22.57	Mishahara	710,688,000	10.13
Maendeleo	13,255,855	36.86	Maendeleo	-	-
Jumla	34,879,793	100	Jumla	7,018,213,000	100


Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Randama ya OWM - Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Uwekezaji, yameoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01 na Na. 02** kama ifuatavyo:-



Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

Chati Na. 02: Bajeti ya OWM - Uwekezaji kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022



Chanzo: Randama ya OWM – Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

- Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) ikamilishe haraka uandaaji wa Mwongozo wa Taifa wa Uwekezaji " National Investment Guidelines" ambao utatoa mwelekeo wa Taifa kuhusiana na masuala ya uwekezaji. Aidha, mwongozo huo uwewe kwenye mtandao ili kuwawezesha Wawekezaji kutambua matakwa ya kuzingatia kabla ya kuanza mchakato wa kuomba vibali vinavyohusiana na uwekezaji.

Baadhi ya mikoa imefanya kazi nzuri ya uandaaji wa miongozo na mazingira ya uwekezaji. Hata hivyo, bado tunahitaji kuwa na mwongozo wa taifa ambao utakuwa rejea kwa wawekezaji wa ndani na nje.

ii. Serikali iendelee kuelimisha wananchi kuzingatia sheria na taratibu na kuwa makini wanapoingia mikataba ya ubia na wawekezaji wa nje ili kupunguza au kuondoa kabisa migogoro na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kwamba, wamekuwa wakidhulumiwa na wawekezaji wa kigeni. Imebainika kwamba, wananchi wengi wanakosa umakini wanapoingia kwenye makubaliano ya ubia na wawekezaji wa kigeni, na ndiyo maana wanapowasilisha malalamiko hayo kwenye vyombo vyaa sheria hushindwa kutokana na kubanwa na vipengele vyaa mikataba;

iii. Serikali iendelee kuboresha mazingira ya uanzishaji na ufanyaji wa biashara nchini kwa kupunguza urasimu hali ambayo itaendelea kuwavutia wawekezaji na wafanyabiashara wengi kuja kuwekeza mitaji yao nchini.

Hatua hii itaisaidi nchi kuendelea kupanda juu katika nafasi za dunia kwenye mazingira bora ya ufanyaji biashara. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya Ufanyaji Biashara (*World Bank's Doing Business Report, 2020*) katika mwaka wa 2019 Tanzania ilikuwa nchi ya 141 kati ya nchi 190 duniani zenyne mazingira mazuri ya kufanya biashara, ikiwa imepanda kwa nafasi tatu zaidi. Ni matumaini ya Kamati kwamba, kwa jitihada zilizopo Tanzania ina fursa ya kupanda zaidi na kuwa kinara wa mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji biashara katika Afrika nzima na hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara;.

iv. Serikali ihakikishe muda wa mwekezaji kushughulikia na kupata vibali vya uwekezaji hauzidi siku saba (7) za kazi, ilimradi muwekezaji huyo awe amezingatia matakwa ya kisheria na vigezo vilivyowekwa;

v. Serikali iweke vivutio zaidi kwa Wawekezaji wa nje ambao wako tayari kuwekeza mitaji mikubwa hapa nchini kwa kuboresha mazingira ya kisera, kisheria na kiutaratibu ili

kuwajengea imani ya kuendeleza na kukuza mitaji ya uwekezaji wao nchini;

vi. Serikali iangalie namna ya kuhamasisha na kuanzisha kada ya wataalam washauri wa masuala ya uwekezaji "*investment consultants*" kwa lengo la kusaidia kuhamasisha, kutoa takwimu na taarifa na ushauri wa kitaalamu kwa wageni na wananchi wanaohitaji kuwekeza nchini. Jukumu hili kwa sasa linatekelezwa na watu wasio na ujuzi wala taarifa za kitaalam kuhusiana na masuala ya uwekezaji "*madalali wa uwekezaji*" ambao wameshindwa kutoa ushauri wa kitaalam na taarifa zinazojitosheleza kwa watu wenye nia ya kuwekeza nchini.

Katika Mataifa yaliyopiga hatua kubwa katika uwekezaji, wataalam washauri wa uwekezaji ni mionganoni mwa wataalam muhimu wanaochangia maendeleo ya uchumi wa nchi na wanatambuliwa kisheria katika kutekeleza majukumu hayo.

vii. Serikali iangalie uwekezekano wa kuanzisha tovuti "website" maalum itakayounganisha Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Balozi za Tanzania ili kuziwesha kufanya kazini kwa ushirikiano wa karibu kwa lengo la kuyafikia kwa urahisi majukwaa ya uwekezaji duniani "*international investment platforms*";

viii. Serikali iandae utaratibu wa kuwawezesha wananchi wenye fursa za uwekezaji kukutana na Wageni wanaokusudia kuwekeza nchini. Kwa hali ilivyo hivi sasa ni vigumu kwa mgeni kutoka nje kutambua namna ya kukutana na mwananchi ambaye wanaweza kuwekeza kwa ubia kwa sababu hakuna jukwaa la kukutanisha pande mbili hizi;

ix. Serikali ifanye tathmini ya kitaalam huru "*independent expert evaluation*" ili kubaini iwapo sera yetu ya uwekezaji bado inakidhi matakwa au inahitaji kuhuishwa ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea kwa kasi duniani kuhusiana na masuala ya uwekezaji na maendeleo;

- x. Serikali iendelee kuhakikisha Kituo cha Uwekezaji (TIC) kinatimiza majukumu yake kwa kuzingatia sheria, uadilifu, "intergrity" uwajibikaji "accountability", uwazi "transparency" na tija "effectiveness/efficiency" ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo kuu la kukuza uwekezaji kutoka nje na ndani;
- xi. Serikali itekeleze kwa haraka mchakato wa uanzishwaji wa kanzidata (database) ya taifa kuhusiana na uwekezaji ili kuwezesha nchi kuwa na takwimu sahihi za uwekezaji; na
- xii. Taasisi zinazohusiana na masuala ya uwekezaji ziwe na mifumo ikiwemo ya TEHAMA ambayo inasomana ili kupunguza muda na kuepusha usumbufu kwa wawekezaji pale wanapofutilia masuala ya kiuwekezaji.

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi mkubwa.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya fungu hili hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Hii ni ishara tosha ya utayari wa Wabunge kulitumikia Bunge, Taifa na Wananchi na hivyo niwasihii tuendeleze gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwawakilisha wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Humphrey Hesron Polepole, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
5. Mhe. Mwantum Mzamili Zodo, Mb
6. Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara, Mb
7. Mhe. Saasisha Elinikyo Mafuwe, Mb
8. Mhe. Festo Richard Sanga, Mb
9. Mhe. Rehema Juma Migila, Mb
10. Mhe. Mwatum Dau Hajji, Mb
11. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb
12. Mhe. Amandus Julius Chinguile, Mb
13. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
14. Mhe. Michael Constatino Mwakamo, Mb
15. Mhe. Dennis Lazaro Londo, Mb
16. Mhe. Lazaro Justin Nyamoga, Mb
17. Mhe. Condester Michael Sichwale, Mb
18. Mhe. Irene Alex Ndyamkama, Mb
19. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb
21. Mhe. Shanif Jamal Mansoor, Mb
22. Mhe. Zacharia Paul Issaay, Mb
23. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
24. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
25. Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb
26. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mb

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Dkt. Kitila Mkumbo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg. Gerlad Magili; Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima na Ndg. Rabisante Moshi wakisaidiwa na Ndg. Pauline Mavunde, kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 11 – Ofisi ya Rais Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji), kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kama yalivyowasilishwa na mtooa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA

13 Aprili, 2021

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Humphrey Polepole, nakushukuru sana.

Eeh, Kazi kubwa. Mnazo *documentS* nydingi sasa za kupitia na ninapenda tuanze angalau na mchangiaji mmoja, atuanzishie, halafu jioni tutaendelea na uchangiaji sasa wa kawaida. Kwa sababu huyu atakuwa ni mmoja tu anayetuanzishia sasa hivi, ninampa *bonus* ya dakika 15. Mheshimiwa Livingstone Lusinde, karibu sana. (*Makofii*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kupata nafasi hii ya kufungua dimba. Namshukuru sana Mungu kwa ajili ya vipawa na vipaji vingi alivyotujalia. Awali ya yote, nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli, Mama Janeth pamoja na Watoto; Joseph, Michael pamoja na Jesca. Tunawapa pole sana. Vile vile tumpe pole Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukupe pole na wewe kwa sababu ulishindwa hata kuchukua hela yako ya utani

kwa namna ambavyo ulikuwa umeguswa, maana yule ni mtani wako, ultakiwa paleuzuie shughuli zisiendelee mpaka upewe chochote; lakini kwa sababu alikuwa mtu wako wa karibu ukashindwa kufanya hata utani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ya kusimamia msiba wa Kitaifa. Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri Jenista Mhagama na timu yako akiwepo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, tumeona namna ambavyo Kamati yenu imefanya kazi kubwa sana; na kwa kweli tutakuwa wachoyo wa fadhila tusipokushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia msiba ule ambao umetupa heshima kubwa kama Taifa kwa namna ambavyo tumemzika Kiongozi wetu kwa heshima kubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tutoe pole kwa yule Bwana aliyepoteza mke na watoto pale Dar es Salaam kwa kukanyagwa kwa ajili ya wingi wa watu waliofika kushuhudia msiba ule. Tunawapa pole sana Watanzania wote kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imejaa mambo mengi. Imesheheni vitu vikubwa sana, imesheheni tulikotoka, tuliko na tunakokwenda na hatuna mashaka kwa usimamizi thabiti wa Rais aliyepo sasa Mheshimiwa Samia pamoja na timu aliyopanga kwamba mambo haya yanakwenda kufanyika. Kazi tuliyonayo, Bunge lako ni kuendelea kuwashauri, kuwatia moyo na kuwaunga mkono kuhakikisha kwamba haya yaliyokusudiwa yanafanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, rai yangu ni kwamba, tungetengeneza vijitabu vichache, siyo llani mpya, lakini vyakukumbusha zile ahadi za Waheshimiwa Viongozi walikopita. Ziwe katika kitabu kimoja cha Kitaifa, alikopita Mheshimiwa Mama Samia aliahidi, alikopita Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli aliahidi, sasa badala ya kila Mbunge kuwa anasimama anakumbusha ahadi ya Rais, ni vyema zikawekwa kwenye kitabu kimoja tukajua kwamba, ahadi za

Viongozi wa Kitaifa ni hizi. Kuna mahali waliahidi barabara kama Mvumi pale, kuna mahali waliahidi madaraja, kuna mahali waliahidi kuchimba mabwawa; tukifanya hivyo, tutarahisisha Wabunge wote kwa pamoja tutakuwa tunadai tu ahadi za viongozi zitekelezwe ambazo ziko kwenye kitabu kimoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikishukuru Chama cha Mapinduzi, kimefanya kazi kubwa sana kwenye uchaguzi uliopita. Hiki Chama hakina mashaka kwamba ndiyo chama pekee kilichobaki kwenye eneo la ukanda huu kinachotetea maslahi mapana ya wananchi wa nchi yake. Kwa kweli bila uchoyo, nataka nimshukuru sana Katibu Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Bashiru, tunakushukuru sana kwa kazi kubwa ambayo uliifanya. Jamani mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. (*Makof/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisema hapa ni kuhakikisha kwamba Serikali inaendelea kusimamia amani na utulivu wa nchi yetu. Amani na utulivu haviwezi kuwepo kama kuna baadhi ya Watanzania na baadhi ya Wabunge wanamsema vibaya Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli, haiwezi kuwepo amani na utulivu. Haiwezekani! Kwa hiyo, leo nataka kujitoa muhanga hapa. Haiwezekani tuwe na viongozi ambao wanajaribu kupinga mambo mazuri aliyoyafanya Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli, haiwezekani. Hatuwezi kuwavumilia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hawa wanaomsema vibaya leo Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli, watamsema vibaya Mheshimiwa Samia. Hii ni tabia! Jamani Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli amefanya kazi kubwa sana kwenye nchi hii. Maana lazima tukubaliane, unajua kuna wengine wanafikiri labda Mheshimiwa Samia alikuwa *bench* akaingia kucheza mpira, hapana. Mheshimiwa Samia alikuwa anacheza pamoja na Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aliyemtaja Mheshimiwa Samia ni Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli mwenywewe. Siku zote Hayati

Mheshimiwa Dkt. Magufuli amekuwa akisema, kama akijitabiria kifo chake; kila hotuba yake alikuwa akisema siku moja nitakufa. Kwa hiyo, alikuwa anajua, akiondoka yuko Mheshimiwa Samia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka watu wamheshimu. Huwezi kuondoa *legacyya* Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwenye nchi hii na kwenye Bara la Afrika, haiwezekani. Haiwezekani, haiwezekani! Hatuwezi kuwavumilia watu wa namna hiyo. Nasi kama viongozi ambao tumelelewa, hivi leo Mbunge gani hapa hakutetewa na Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli? Tuko humu ndani kwa sababu ya Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Samia. Kila sehemu walipita.

Mheshimiwa Spika, kuna watu hapa walikuwa hata hawachaguliki, Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Samia wakipita wanasema, tupeni huyu, tutafanya naye kazi, tutamrekebisha. Kwa sababu yao, watu wakachaguliwa. Leo wasemwe vibaya sisi tupo! Leo Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli asemwe vibaya hata arobaini haijaisha! Hili jambo halikubaliki. Hawa watu washike adabu na adabu ziwashike, hatutaki warudie tena mambo ya kipuuzi kama haya. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, anasimama mtu anasema eti mradi ule wa maji tuuache! Unajua mimi nina hakika kwamba, hata mle ndani inawezekana hata kaburi la Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli lilitikisika! Tuuache mradi ule wa Mwalimu Nyerere? Ule mradi una faida kibao! Pale ametuambia hapa Mheshimiwa Majaliwa kwamba tumetumbukiza shilingi trillioni mbili; tuziache ziteketee? Kwa sababu gani? Ule mradi kwa taarifa yenu, mimi sio Profesa Professor, mimi ni wa Darasa la Saba, lakini ngoja niwape faida za ziada za ule mradi. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ngojeni niwape faida za ziada za ule mradi. Lile bwawa linalochimbwa pale, upana wake peke yake ni kilometra 25, lakini urefu wa maji yatakayokuwa pale ni kilometra 100; hapa na Kibaigwa. Hilo ni bwawa au

ziwa? Pale linazaliwa ziwa! Hii nchi itabidi wachoraji wa ramani mbadilishe, msitaje maziwa yale tuliyonayo, mwongeze na Ziwa la Magufuli linalozaliwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye lile ziwa, pembedi kutajengwa hoteli za utalii, pale patawekwa samaki watu watavua, lakini ziwa lile linagusa Wilaya tano. Hivi jamani elimu ya Tanzania kweli inatusaidia? Kama wa Darasa la Saba naelewa, halafu Profesa huelewi, inakuwaje? Inakuwaje? Inakuwaje? (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, ni lazima tusome na vile vile tuwaeleze watu vitu vya kweli. Tusiwandanganye wananchi. Amesema hapa Mheshimiwa Waziri Kalemani, umeme wa maji ndiyo umeme wa bei rahisi kuliko umeme wowote. Kwa nini tunawadanganya Watanzania? Kama tuna madili yetu tuyaeleze, lakini tusingize kuanza kuharibu *image* ya Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa wananchi wakati tegemeo lao kubwa ni Mheshimiwa Samia kutekeleza mambo waliyoyapanga na ndugu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila sehemu watu wana matumaini makubwa sana na Mheshimiwa Rais Samia. Kazi yetu sisi Wabunge ni kumtia moyo, siyo kuanza kumrudisha nyuma, siyo kuanza kuzungumza kana kwamba Mheshimiwa Samia ni mtu mwingine na Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni mtu mwingine, haiwezekani. Haiwezekani! Haiwezekani! Nasi Wabunge tuko humu, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, Samia ni Magufuli na Magufuli ni Samia. Wamefanya kazi kubwa na sasa Samia anaelekea kwenda kuitendea Tanzania jambo la ajabu, kukamilisha ile miradi waliyokubaliana na Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli na siyo hivyo tu, na kuongeza mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi hii Rais anayetawala, anatekeleza llani na vile vile anakuja na maono yake. Tusianze kumtangulia Rais. Rais ana maono yake. Mnaposikia huko watu wanafanya Ibada Makanisani na Misikitini wanamwombea, pale busara zinaongezeka, anawaza

mambo mengine makubwa ya kuitendea nchi. Nani asiyejua kwamba ziwa la mama ndiyo linalolea mtoto? Sisi tuna Imani kubwa na Rais aliyepo, kwa hiyo, tusianze kumzongazonga na kuanza kumfananisha sijui Magufuli na Samia, sijui Samia bora kuliko Magufuli, inatoka wapi hiyo? Hawa wote ni kitu kimoja, wamechezea timu moja, wote wamezaliwa na Chama cha Mapinduzi. Huyu ni kada wa Chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nimesema mimi najitoa muhanga eti kwa sababu nagombea *NEC*, sijui mtaninyima kura. Mkininyima hiari yenu, lakini leo napasuka hapa. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge! (*Kicheko*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wa CCM, naomba kuwahoji, Mheshimiwa Lusinde amepita *NEC*? (*Kicheko/Makofi*)

WABUNGE FULANI: Amepita! (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa umepita bwana. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, watu wengi wanataka kuliharibu suala ambalo umelisema. Suala la ujenzi wa bandari, Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli alieleza mabaya yaliyoko kwenye mkataba. Kazi tuliyonayo sisi ambaao tumebakai hai, kama upo uwezekano, tufanye mapitio upya ya ule mkataba. Wewe hujasema ijengwe kama ilivyo; na ulikuwa msimamo wako wa siku zote hata Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli akiwepo. (*Makofi*)

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, ngoja nataka niseme hapo.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, Taarifa, Taarifa.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Kingu.

T A A R I F A

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayesema kwamba hata watu ambao wanaendelea kumshambulia na kutaka kumchafua Spika wetu kuhusiana na Mradi wa Bagamoyo ni vile hawajui kwamba alichokuwa amekisema Spika hata kwenye Bunge la mwaka 2020 alikuwa amemaanisha kwamba kama kuna upungufu kwenye mradi wa Bagamoyo, kama nchi tuyatoe na mazuri tuyapokee, tuendeleze mradi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninatoa rai kwamba sisi kama Bunge, nampa taarifa msemaji, tusikubali kuona *image* yoyote ya kutaka kumdhalilisha Spika wetu kwenye hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, nina imani kaka yangu ataipokea taarifa yangu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde, unaipokea taarifa?

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Kingu. Hauwezi ukachoma nyumba moto kwa sababu ndani ya nyumba kumeingia panya, haiwezekani. Tunachofanya pale, yale maovu tunayaondoa, kinachobaki kinaletwa hapa Bungeni, wananchi wanaelimishwa kwamba ubora wa bandari ya Bagamoyo ni huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna kitu chochote kilichokosewa. Nimesimama hapa kufungua dimba...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Taarifa Mwenyekiti

SPIKA: Taarifa ya Mheshimiwa Musukuma.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kumpa taarifa tu mzungumzaji kwamba, mawazo yanayotolewa na *Senior Lusinde*, Darasa la Saba ni mawazo... (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, msicheke, ni mawazo ambayo kama alivyosema, humu ndani kuna watu watu ni Maprofesa na ma-*Ph.D* yenu hamna hayo mawazo.

Mheshimiwa Spika, sasa kiti chako, haya mawazo tukiwa tunayaacha yanapoteapotea, hayawezi kuwa na kumbukumbu kwenye Taifa letu. Unaonaje watu kama hawa ukawatunukia hata Uduktari wa heshima ili hata... (*Makofii/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde, unapokea taarifa?

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, napokea kwa mikono miwili kwa sababu mtathmini naye ana elimu kama yangu. Kwa hiyo, napokea taarifa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka nipige mabomu ya ndani na ya masafa marefu. Kabla ya uchaguzi uliopita, tuliwaasa baadhi ya viongozi, tujenge tabia ya ustaarabu; ukiongoza chama, ukiongoza timu ya mpira, tusishindwe na makocha? Juzi tumemwona Kocha wa Timu ya Taifa Etienne Ndayiragija; timu imefungwa, kaijuzulu katoka.

Mheshimiwa Spika, tunashangaa wako wanasiwa ving'ang'anizi; kaongoza chama, kilikuwa na Wabunge 100, sasa hivi kina Mbunge mmoja; bado naye anasimma kuzungumza eti Mwenyekiti wa chama. Mwenyekiti wa chama gani? Unasema vitu vyatuo, eti akaunti yangu

ilifungwa. Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli alikuwa anafanya kazi *BoT?* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Nani asijejua kuna utaratibu wa kibenki? Kama una madeni, una vitu vingine, akaunti yako ikafungwa, ni mambo ya *BoT* na benki ambayo umefungua akaunti. Hayo yanamhusu nini Rais? Kwa hiyo, tunataka kuwaambia Watanzania, utamaduni wa kitu kikifanywa vibaya unajiuzulu, kisiishie kwenye CCM. Vyama vyote viige. Umeongoza chama kikiwa na Wabunge 100, umepigwa uchaguzi, kimepata Mbunge mmoja toka. Onyesha ustaarabu kwamba jamani nimepigwa. Baba bata yule yupo tu; watoto wametumbukia naye mwenyewe katumbukia, bado ana haki ya kusimama. Unasimama kuzungumza nini wakati hapa kijana mdogo tu kamtoa nishai? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanasiasa wa namna hii hatuna haja nao. Kuna mmoja nataka nimtumie kombora yuko Ubelgiji, aendelee kukaa huko huko, asitubabaishe. Wamwache Mheshimiwa Samia afanye kazi ya nchi. Asije mtu akamtangulia Rais ooh, Mheshimiwa Rais huyu nataka nikae naye. Ukae naye uzungumze naye kitu gani? Sisi tuko hapa kumtetea Mheshimiwa Samia na tuko hapa kumpigania Mheshimiwa Samia.

Mheshimiwa Spika, Serikali anayoiongoza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ina Wabunge wa kutosha, tutasimama imara kuhakikisha nchi yetu inakwenda. Watanzania wanataka maendeleo, hawataki maneno mengine. Ndiyo maana *sloganya* Mheshimiwa Rais sijui kama watu wameielewa vizuri!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Samia hajasema kuna mabadiliko, kasema kazi iendelee. Maana yake wale walioko kazini waendelee. Anachokisema Mheshimiwa Rais Samia, nidhamu ya wafanyakazi iendelee, nidhamu ya uadilifu kwenye mapato na matumizi iendelee, nidhamu ya uchapa kazi iendelee, reli ijengwe, viwanja vyatia ndege

vijengwe, maji yapatikane, bwawa lijengwe, umeme upatikane, kazi iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi/Vicheko/Vigelegele*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa kutuanzishia mjadala wa hoja iliyowekwa Mezani na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli, alichokisema Mheshimiwa Musukuma, wakati mwingine kina mantiki. Kuna kusoma na kupata *accolades*, nina *degree* nina *Masternina Ph.D* mimi ni Profesa, hiyo nayo ni mojawapo, lakini kuna kuelimika. Unaweza ukaitwa majina hayo, lakini hujaelimika kabisa. (*Makofi*)

Mnaweza mkaona Wabunge ambao ni Darasa la Saba na wanasema wazi, lakini upana wa mawazo yao na *arguments* zao, hata kama hukubaliani naye, lakini unaona *argumentyake* inavyokwenda. Ukitaka kujipima, nenda kwa wananchi hawa hapa; wewe *Professor* simama ongea na wananchi wale; Darasa la Saba asimame aongee na wananchi wale. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hivi vitu vingine na hasa unapokuwa umeshaingia Bungeni havina kazi sana. Kazi yake kubwa ni kwa wananchi; kazi ya Kibunge, ndio inakuwa kazi ya maana zaidi. Vinginevyo hivi, vina-fit mahali pengine huko kwenye utafiti, kwenye kufundisha na nini. Kwa hiyo, ndio maana Mheshimiwa Kishimba nikampa Uprofesa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Musukuma, bado nafikiria fikiria wengine itakuwaje? (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, leo hapa imeshakuwa kwenye *record* zetu hapa za Bunge, Mheshimiwa Lusinde mtu wa tatu amezungumzia habari ya Maprofesa, mtu wa pili alikuwa Mheshimiwa Londo, leo asubuhi alitaka kutoa hati sijui ya aina gani? Ila mtu wa kwanza alikuwa Faustine Ndungulile; mwaka fulani hivi, niliwahi kumtoa nje ya Bunge hapa enzi hizo, alimwambia Profesa mmoja kwamba ni zero, ilikuwa ni hatari

kubwa hapa ndani. Kwa hiyo, maprofesa muwe makini sana mnapozungumza. (*Makofi/Kicheko*)

Basi baada ya Mheshimiwa Lusinde kutufungulia mjadala, tutaendelea jioni. Kwa kweli tunao wazungumzaji wengi tu wazuri sana. Nawashauri tu saa 11.00 tuwahi kurudi ili tupate kusikia michango ya aina mbalimbali kadri tunavyoendelea na Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa hatua hiyo niwakumbushe Wenyeviti wa Kamati saa 8.00 kamili pale Msekwa B kwa ajili ya kile kikao ambacho tulizungumza jana. Tutakutana pale.

Sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 juu ya alama leo jioni. Mwezi Mtukufu tayari? Bado.

(Saa 7.11 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na kikao chetu cha nane. Tunaendelea na hoja ambayo imewekwa mezani na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo asubuhi na hoja yenye ni kwamba Bunge sasa mwendelee kujadili ili mwisho wa siku muweze kukubali na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Tunaanza na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu na atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Pia nishukuru wananchi wangu wa Jimbo la Arumeru Magharibi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira tuliyonayo ya kuchangia bajeti hii tunaamini kwamba bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu inakwenda kutekeleza llani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2021/2022, ndio maana hapa tumeanza mchakato huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea ningependa sana kusema maneno machache kabla sijachangia. Nitumie maneno ya Mungu, wakati ule Yesu alipokuja duniani kwa ajili ya kuokoa dunia alikuwa na wanafunzi wake 12. Katika wale wanafunzi, Yesu alitabiri kwamba kuna wawili watakaomsaliti, alikuwa ni Petro na Yuda Iskariote. Alipokuwa pia akiendelea alijaribiwa na shetani sana akampandisha juu ya mlima mkubwa sana akamwambia ukinisujudu nitakupa dunia hii yote itakuwa ya kwako na miliki zote, lakini Yesu akamwambia rudi zako nyuma shetani kwa sababu miliki yote hii ni ya kwangu.

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo, lakini pia alipokuwa akiendelea alikutana na watoza ushuru, wakamuuliza sisi tufanye nini Bwana? Akawaambia na ninyi mtosheke na mishahara yenu. Nimeona nianzie na hapo. Nasikitika sana, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alinadi llani ya Chama Cha Mapinduzi kwa nguvu zake zote na nia yake yote na moyo wake wote, leo tunapata akina Yuda. Leo kina Yuda wamejitokeza kumsaliti Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano. Inasikitisha, mzee wa watu ametangulia mbele ya haki, hawezi kujitetea, lakini ninyi mlioko ndani na nje mnataka kumdhahilisha. Hakika, asilani kabla hamjamdhahilisha Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano, nina hakika Mwenyezi Mungu atawashughulikia usiku na mchana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Magufuli alifanya kazi ya kuwaaminisha Watanzania kwamba kweli ni Rais anayejali maskini, anayejali Taifa hili kama alivyokuwa mtangulizi wake Rais wa Serikali ya Kwanza Nyerere alifuata hizo nyayo na Serikali zote zingine zilizofuata alionesha njia kubwa. Alipokuwa akitunadi, niliumia sana ninapoona

kwenye mitandano watu wanachafua hali ya hewa Magufuli hata panya akitoboa gunia kule nyumbani kwa mtu, Magufuli! Kwa sababu yeye hayupo. Kama kuna watu wamefanya ufasadi kwenye Wizara, Bandari na halmashauri watu wanasema Magufuli, kawatuma? Nasikitika sana, lakini Mwenyezi Mungu atawashughulikia kabla ya siku zao si nydingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, akina Yuda hawakosekani, lakini nawaambia ninyi ambao mnadhani mtaishi milele hakuna nafsi, kila nafsi iliyoko hapa kwenye Bunge hili na nje ya Bunge hili itaonja mauti. Hakuna anayedumu milele wala hatuna mji udumuo katika dunia hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia, mama Samia Suluhu Hassan alikuwa ni msaidizi wa Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Rais wetu wa sasa mama Samia Suluhu Hassan alikuwa mwaminifu na muadilifu na ndiyo maana Mwenyezi Mungu amemuona akawa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mtaona jinsi gani mama yule, Rais wetu mpendwa amehakikisha kwamba wale waliokuwa wanatazamia kwamba atabadilisha Serikali kwa asilimia sijui ngapi, amesema "Kazi lendelee". (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tusifikiri kwamba kwa mwelekeo huo Mheshimiwa Rais aliyeko ataweza kumsaliti Magufuli. *Legacyya Magufuli itaendelea kubaki sasa na hata milele.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa niendelee kutoa mchango wangu. Najua kabisa Chama Cha Mapinduzi katika kutekeleza llani ya Mwaka 2020/2021 imefanya kazi kubwa na hakuna mtu asiyejua, hakuna asiyaona. Kwenye *dispensary* tumefanya vizuri Chama Cha Mapinduzi, kwenye bandari, kwenye reli, kwenye masuala ya hospitali na kadhalika. Barabara nchi hii ni kubwa lakini imetekelezwa llani kwa asilimia 90 kuunganisha mikoa yote ya Tanzania. Hakuna ubishi na anayebisha hapa asimame, hii nchi ni kubwa, hata kule Roma, Mji wa Baba Mtakatifu unajengwa mpaka leo wajenzi wapo wanajenga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kwa ajili ya kutekeleza llani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2021/2022, sasa ni kazi yetu kuikumbusha Serikali kwamba kuna upungufu ule mdogo mdogo yaliyoko kwenye vijiji, kata, wilaya na kwa ujumla kwenye mikoa. Ni wajibu wa Serikali yetu kwenda kutekeleza kwa kutumia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ahadi ya Waheshimiwa Viongozi wetu Awamu ya Tano, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne. Awamu ya Tano ambayo kwa sasa ndiyo iliyoongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliahidi barabara za lami kwenye majimbo yetu, aliahidi kutengenezwa hospitali, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye tunamuamini na tunamwona ni mchapakazi, yeye ndiyo anasimamia shughuli za Serikali Bungeni, hebu sasa Serikali ije na mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba hizi ahadi ambazo Waheshimiwa Marais wetu wanatoa, Waheshimiwa Mawaziri wahakikishe kwamba wameweka kwenye *bundle* moja ili iweze kutekelezwa kikamilifu na iweze kuwepo katika *reference*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la ahadi linasumbua sana wananchi kwa sababu wanasema Rais ametuahidi kila siku anasema Mbunge wakumbushe, wakumbushe. Sisi ni wajibu wetu kama Wabunge kuikumbusha Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi na imefanya kazi kubwa, imetekeleza ahadi nyingi imepungua hizo ndogo tu, lakini ningeomba ingewekwa kwenye *bundle* moja ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye jimbo langu Awamu ya Nne iliahidiwa barabara ya Hospitali ya Oturumeti, hospitali ya wilaya kwa lami. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ameahidi barabara ya Mianzini – Kimbolo – Ngaramtoni; barabara iliahidiwa na Mheshimiwa Jaffo, barabara ya kwenda Hospitali ya Nduruma, Bwawani na katika majimbo mengine yote Tanzania. Najua hii nchi ni kubwa, lakini ni wajibu wetu kuendelea kuikumbusha Serikali

yetu tukufu na sikivu kuhakikisha kwamba imeondoa hizo ahadi za Waheshimiwa Marais wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira; kama tunavyojuua Serikali inajitahidi, sasa niombe ijitahidi sana kuboresha katika Sekta Binafsi na kwa ajili ya kupata mazingira mazuri ya kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa ili vijana wetu ambaao wanahangaika huku na huku waweze kupata ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo; kuna mashamba makubwa yametelekezwa kama mashamba haya yangeweza kuchukuliwa na Wizara ya Kilimo wakaunganisha kama wale ma-settler walivyokuwa wanalima kahawa, maharage, mahindi, ingeweza kuleta tija na ajira. Bado naamini kwa sababu Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni sikivu itaendelea kuchapa kazi na kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanafanya kazi vizuri. Kwa mfano kwenye Jimbo langu, kuna mashamba makubwa kama ya Aga Khan, imechukua mwaka 2006 ikisema itajenga Chuo Kikuu, zaidi ya heka 3,000 hadi leo shamba hilo limesimama, lilikuwa linaajiri zaidi ya watu 1,500, lakini naamini Wizara ya Ardhi itaekwenda kufuatilia shamba hilo ili kuja hatma yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia katika ardhi na ajira, kuna suala la Mfuko huu wa Akinamama, Vijana na Wenye Ulemavu. Naomba Wizara husika ije na mpango mahsusii wa kuboresha Mfuko ule ukae vizuri kwa sababu, hivi sasa kuna utata mkubwa katika mfuko huo, watu wanaopata mikopo ni 18 – 35, lakini utaona ni jinsi gani bado watu wa *age* hiyo wako shulenii. Sasa ni vizuri wakaja pia na marekebisho kama itawezekana wakanzia 18 mpaka angalau 40, hapo utapata watu wengi ambaao wataongea uchumi na wataanzisha biashara.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi. Mheshimiwa Jafari

Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Leo nitajitahidi kidogo nichangie taratibu ili angalau wote kwa ujumla hasa Wabunge ambao tumeingia ndani ya Bunge hili kwa awamu ya kwanza hasa Wabunge vijana, baada ya hapa ni imani yangu tutakwenda wote sambamba.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi kukushukuru sana wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza hili Bunge. Nachelea kusema maneno haya kabla ukiwa ndani ya Bunge hili na ukiwa ni Spika wetu sisi kama Kiongozi wa Bunge. Ukistaafu ukiwa ndani ya Bunge hili ndiyo nipate ridhaa ya kukushukuru kwa namna unavyotuunganisha sisi Wabunge ndani na nje ya Bunge. Pia namna ambavyo unajitahidi angalau kumpa Mbunge mmoja mmoja nafasi ya kusemea yale ambayo anatakiwa ayasemee kwa mustakabali mzima wa wananchi ndani ya Jimbo lake. Mwenyezi Mungu pekee ndiyo anaweza kukulipa hili, muhimu ni kukuombea uzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nichukue nafasi kumshukuru sana Waziri Mkuu kwa namna anavyotuunganisha sisi Wabunge na Serikali kama Mtendaji Mkuu wa Serikali. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wote kwa namna ambavyo pamoja na changamoto walizopititia hapa katikati wiki tatu zilizopita, lakini bado wamebaki imara wanatuongoza na sasa tunakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nichukue nafasi kumshukuru Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan. Namshukuru kwa namna ambavyo ameanza, lakini namshukuru kwa namna ambavyo ameanza na anasema kazi iendelee kutekeleza na kulinda yale yaliyokuwa yanafanywa na pacha wake Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ametuonesha sote kwamba njia bado iko pale pale. Yale waliyokuwa wanayasimamia juu ya wananchi maskini, miradi ya maendeleo, juu ya utendaji mkubwa wa

Serikali kwa ujumla wake, bado ameahidi kuyasimamia na sasa tunaona kazi inakwenda vizuri. Ndugu zangu Wabunge tuendelee kumwombea mama yetu ili aendelee kufanya yale mazuri kwa kadri ambavyo Mungu atawea kumwongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Kifedha la Kimataifa la *IMF* mwezi Januari, kutokana na ugonjwa wa *corona* *IMF* ilikadiria uchumi wa kidunia utashuka kwa asilimia 3.5 kulinganisha na 2.8 ya mwaka 2019, lakini Serikali yetu juu ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakishirikiana na pacha wake, mimi namwita pacha mama yangu, mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu hakuna namna unaweza ukazungumza mazuri yaliyokuwa yanafanywa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli bila kumgusa mama Samia Suluhu Hassan. Hakuna namna unaweza ukazungumza mazuri yaliyokuwa yanafanywa na hawa watu wawili bila kumtaja Waziri Mkuu kama Mtendaji Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo niseme, kwa namna ambavyo walitongoza pamoja na kushuka na kuyumba uchumi wa kidunia pato letu la Kitaifa la ndani ya nchi liliongezeka kwa asilimia 4.7. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana, Wabunge waliokuwa humu wanajua changamoto ilivyokuwa hasa baada ya tikiso hilo la ugonjwa wa *corona*, walibaki imara wakawasemea wananchi, sasa haya ndiyo matunda yake ambayo wanayaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye hotuba hiyo ya Waziri Mkuu. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imejipanga sasa kufanya utafiti wa kilimo wa kuangalia namna gani sasa tunaanza kubuni mbegu bora na miche bora kwa mustakabali wa wakulima wa nchi yetu. Nina mambo mawili au matatu ya kushauri.

Mheshimiwa Spika, watakapokuwa wanafanya utafiti huu, waende sasa wakatazame namna gani wanafanya

utafiti kwa ngazi ya kimkoa, wilaya na halmashauri, washuke chini ngazi ya kata mpaka vijiji ndani ya nchi nzima, ili mwisho wa siku waje kulingana na jiografia ya kila eneo ni zao gani moja linafaa kulimwa kama zao la kibashara.

Mheshimiwa Spika, pili, utafiti huo ujikite katika maeneo gani ambayo yanaweza yakalimwa na yakafanyika kilimo cha umwagiliaji na yakawanyanya wananchi kwa ujumla kwenye kipato chao kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, tatu, waende wakafanye utafiti warudi kushauri ili angalau sasa kwenye kila wilaya tuwe tuna zao moja la kibashara ambalo wilaya moja ikisimama inasema ndani ya wilaya yangu, zao fulani ndiyo zao la kibashara ambalo kimsingi kama Mbunge nikitaka kuwashika mkono kuwasaidia wale wananchi mbegu nawasaidia mbegu ambayo wanajua wakiipanda kama zao la kibashara itainua uchumi wa wananchi kwenye maeneo yao husika.

Ningetamani sana, tafiti hizi ninaporudi ndani ya Jimbo langu kwenye wilaya nione kwamba kweli hapa kwenye kata fulani ndani ya Kijiji Fulani, nikiwashauri wananchi kulima pamba inastahimiliki na isiwe kwa *ku-guess* au kwa kuchukua yale maoni ya wakulima peke yake, badala yake, niweze kuitoa hata kwenye taarifa za utafiti huu utakaokuwa umefanywa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine, hapo hapo kwenye kilimo ningetamani sana, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Kilimo kwa namna ambavyo amejipanga kipeleka pikipiki kwa Maafisa Kilimo wote ndani ya halmashauri. Wasiishie hapo tu, ningetamani waende moja kwa moja, watengeneze mustakabali mzuri wa kuwasimamia Maafisa Kilimo ili Afisa Kilimo anapoamka asubuhi, ajue ni mashamba mangapi anakagua kwa siku, ametembelea wakulima wangapi, anategemea kupata nini kwa wale wakulima. Mwisho wa siku wampime kwa *product* inayopatikana kwenye ngazi ya chini kabisa, ngazi ya Kijiji, itakayoleta tija, lakini itaamsha ari mpya ya utendaji wa Maafisa Kilimo kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, natamani sana Wizara ya Kilimo pamoja na kwamba tunawapelekea vitendea kazi, tufike tutengeneze *assessment* nzuri ya kuwasimamia ili ninaposimama hapa kama Mbunge, yakinjwa maeneo mengine, nami nikitaja kama Ranya nataja mazao fulani ambayo wananchi wangu wameyapata kwa mwaka mmoja kwa kilimo walichokifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nizungumzie kuhusu huduma za kijamii na nitaanza na maji. Nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Waziri wa Maji. Nasema ni katika Wabunge wachache ambaao baada ya ye ye kupata uteuzi alifanya ziara kwenye jimbo langu. Kulikuwa na Mradi wa pale Shirati, mradi ulikuwa na zaidi ya miaka 10 hautoi maji, lakini alipofika alitoa maneno ndani ya mwezi mmoja, ninavyozungumza chini ya Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi, leo kuna maji yanatoka pale. Unaweza ukaona ni historia gani ndani ya miaka 10, wananchi wale walikuwa wamesahau *issue* ya maji, leo wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri pale imepelea kiasi cha kama milioni 300, najua hili unaliweza, tusaidie ili tuweze sasa isiwe Shirati peke yake badala yake na majirani wote wanaozunguka kata ile waweze kupata maji kwasababu, miundombinu ipo ni kuifufua tu iweze kuwasaidia wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna miradi ya maji ambayo iko ndani ya jimbo. Nichukue nafasi hii kukuomba kuna miradi ya Nyarombo, kuna miradi kwa muge pale Kyang'wame na miradi mingine ambayo kimsingi ukiwekeza fedha pale itawsaidia sana wananchi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri tusiishie mradi mmoja, turudi tuone namna gani ya kuwasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini niliwahi kusema na nitarudia tena, ili kutatua changamoto ya maji ndani ya Jimbo ni lazima twende na ule mradi mkubwa wa maji ambao upo kwenye *plan* ya kutoa maji Ranya kwenda Tarime. Ule mradi tunazungumzia zaidi ya kata 28 zitanufaika na ule mradi na

kwasababu, jimbo langu zaidi ya asilimia 50 changamoto kubwa ni maji ni imani yangu huu mradi ukiingia kwenye *pipeline* ukaanza kutekelezwa Rarya *issue* ya maji itakuwa ni historia. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa sana na kwa sababu limesemwa na Waziri Mkuu ni imani yangu litafanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe, ni imani yangu kipindi mlikuwa mnatunadi sisi Wabunge vijana, Wabunge ambao tumeingia kwa mara ya kwanza, mlikuwa mnazunguka wewe, Spika, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mama yangu Mama Samia Suluhu Hassan. Ulipopita kwenye jimbo langu uliniahidi namna gani tunaweza tukapata *ambulance*, ili angalau iweze kusaidia wale wananchi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hili tusaidie.

Mheshimiwa Spika, la kumalizia la mwisho nimalizie kuhusiana na *issue* ya TARURA, tuna daraja pale la Mto Mori, kwa sasa hivi kwasababu nimemuona Waziri wa TAMISEMI amekuja mama na lile daraja tunazungumzia kipenyo ambacho hakizidi hapa na Mheshimiwa Waziri alipo upana wa lile daraja. Ni imani yangu kwasababu limekuwa likizungumzwa zaidi ya miaka 10 huku nyuma sasa amekuja Waziri ambaye ni mama na ninaamini ni mchapakazi mzuri sana wanaoteseka kuvuka kwenda kutafuta huduma za kijamii, huduma za hospitali, huduma za masoko ni akinamama na watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na niliwahi kusema mto ule watu wamekuwa wakifariki pale. Angalia kipenyo tunachohitaji daraja ambalo tumekuwa tukiliomba kwa miaka 10 ni hapa na pale alipo Mheshimiwa Waziri. Ni imani yangu sasa amekuja mama atawasaidia hawa wamama ili lile daraja sasa badala ya kila mwaka kufanyika upembuzi yakinifu liweze kupata suluhisho la kudumu ili hawa wananchi sasa waweze kuokoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia la mwisho kabisa nizungumzie kwenye sekta ya afya kwenye upande wa Waziri.

Ndani ya jimbo langu nina kata 26 ni kata tatu tu ambazo zina vituo vya afya na bahati mbaya sana Kata ya Kinesi ambayo ina Kituo cha Afya cha Kinesi kwa mujibu wa *projection* ya Wizara ilitakiwa ihudumie vijiji viwili peke yake. Hivi ninavyozungumza kituo kile cha afya kinahudumia zaidi ya vijiji 27 zaidi ya tarafa tatu wanapata huduma tena mpaka Kijiji Jirani cha Butiama, watu wanaokwenda pale *projection* yake imekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, na kwasababu kimeshapanuka na Serikali ilitupa fedha tukakipanua zaidi ya milioni 500 hapa kilipofikia nichukue nafasi hii kumuomba sana Waziri tuone namna gani sasa tunakihamisha kwasababu, kimeshatoka kwenye vigezo vya kutoa huduma kama kituo cha afya kiende kiwe hospitali ya wilaya ili angalao tuweze kuwa na hospitali ya wilaya kwa ukanda wa chini upande wa Suba. Na hili hospitali ya wilaya ambayo Serikali ipo kwenye mchakato wa kuifungua upande wa pili maana yake tutakuwa na hospitali mbili, angalau kwa jiografia ya jimbo langu liliivyokaa tunawenza tukawasaidia sana wale wananchi kwenye sekta ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache nichukue nafasi hii na niseme kwamba, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ni Mbunge wa Rarya. Kule Rarya wakati wa uchaguzi, wakati wa kuchukua fomu za Chama Cha Mapinduzi kugombea nafasi ya ubunge wa Rarya nafasi moja, naambiwa walichukua fomu wagombea zaidi kidogo ya 260. Katika hao 260 wote walikuwa na *degree* na maprofesa hawakupungua dazani moja katika hao wote Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ndiye aliyeshinda. (*Makofi*)

Kwa hiyo, muwe mniamtembeleatembelea mnamuuliza kuhusu alitumia mkakati gani katika msitu huo wa wagombea halifu akawa namba moja, sio rahisi. Hongera sana Mheshimiwa Jafari. (*Kicheko*)

Nilishakutaja Mheshimiwa Joseph Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani. Atuchangamshe kidogo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu kwa kuteuliwa kuwa Rais wetu wa Awamu ya Sita, lakini pili nikushukuru wewe kama mlezi wetu sisi Wabunge, najua na sisi tulipoanza humu tulitwa vijana, lakini naona sasa tunaenda tunazeeka-zeeka kwa sababu umesajili vijana wengine, Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze sana Katibu Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Bashiru, tunakushukuru sana. Kwa sisi tuliosota CCM tunatambua mchango wako Mheshimiwa Katibu Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri uliyoifanya. Umeweza kutuunganisha Wabunge wote pamoja na Serikali yako unayoiongoza, lakini pamoja na Mawaziri unaowasimamia.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kushauri upande wa kodi, nimezungumza humu zaidi ya mara mbili mara tatu nikiomba Serikali ione namna ya kuweza kukaa na wafanyabiashara, ili kuweza kuona jinsi nzuri ya watu walipe kodi bila kuichukia Serikali na bila kuwa maadui na wataalamu wetu wa *TRA*. Lakini mara nydingi mawazo mazuri tunapoyatoa sisi kwa kuwa ni darasa la saba, yaani tukitoa wazo, yaani kabla hamjalielewa ninyi wasomi mnalibeba linakuwa la kwenu wakati utafiti umefanywa na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nishauri, tunajua kwamba, Mheshimiwa Waziri amepewa maagizo na Mheshimiwa Rais kwamba, nendeni mkaarekebishe *TRA*, hawawezi kurekebisha. Na mimi nikuombe kwenye hili hata Waziri tunamvalisha kengele ambayo hawezি kuicheza. Ningombaa Mheshimiwa Rais awaite wafanyabiashara, suala hapa sio *harassment*, suala hapa ni kodi ambazo ni za miaka

25 ya nyuma. Kwa maisha ya sasa inabidi tubadilishe kulingana na hali halisi, ukisema tu wasitusumbue bado wanakuja na mavitabu yaleyale, kilichobadilika wamekuwa tu na ka-lugha, tunaomba utulipe, wameacha kufunga yale makufuli, lakini kodi ni ileile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba ni vizuri Mheshimiwa Rais akawaita wafanyabiashara akakaanao, kama tulivyofanya kwenye madini, wamwambie hiki kinatukwaza, hiki kinatukwaza, aone namna aseme nendeni mkabadijishe hili. Kama hatutabadilisha hakuna namna ambayo mtamsaidia mfanyabiashara wa Tanzania bado mteseo ni yaleyale na ninadhani ndio kama rushwa itaongezeka japokuwa haitaombwa kwa ukali, itakuwa ni ya maelewano tutoe kidogokidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri mawazo haya mkayafanya yawe endelevu muwaite wenye matatizo. Ninyi wengi huku mnaoelekezwa mnakaa ofisini, hamjui huko *field* watu wanavyoteseaka. Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu ni vizuri Rais akwasikiliza wafanyabiashara ndio *hub* yetu kwenye nchi yetu. Baada ya kuwasikiliza aone namna ya kitu gani na kitu gani tutakachokiondoa, ili wafanyabiashara wawe na amani na walipe bila kusumbua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natoa mfano; leo ukienda Kariakoo utakuta watu wamekimbia wale wafanyabiashara, nakupa mfano mdogo tu wa glasi. Glasi ina aina kama sita, kuna glasi inauzwa 200/= tunatumia kule kwetu kijijini, kuna ya 1,500/= wanatumia Wagogo, kuna 15,000/= wanatumia Dar-es-Salaam, ukienda kwenye kodi *tariff* inayotajwa ni ushuru wa glasi. Inawezekanaje ushuru *uni-charge* 2,000/= wakati glasi inauzwa 1,000/=? Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na uwanja mpana wa kuweza kuwasikiliza hawa wafanyabiashara ili muweze kukusanya kodi bila kusumbuana na bila kuwalaamu watu wa *TRA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, napenda nishauri kwenye upande wa *tanzanite*. Maisha yangu nimekulia

kwenye madini ni vizuri wakatusikiliza watu tunaotoka kwenye madini. Huwezi ukasema *tanzanite* inatoroshwa, na sisi kama kamati tumeenda kwenye *tanzanite* pale Mererani, kwa kweli Serikali imefanya kazi kubwa sana na askari wetu wako pale wanalinda vizuri na kamera. Tumeingizwa chumba cha kamera unaona mita 50 nje mita 50 ndani ni ulinzi ambao unajiuliza sisi watu wa dhahabu tungepewa huo ulinzi pengine Serikali ingekusanya mara tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nishauri mnaibiwaje Serikali. Unaweza ukalaumu wanajeshi, unaweza ukalaumu wizi uko pale, naomba nitoe mfano; tangu mpate lile jiwe la Laizer lile lililotangazwa kwenye TV la bilioni sita mkatoza kodi, halafu mkaapeleka ma-*valuer* mkaweka na askari na askari na askari, kama aina tatu za maaskari wako pale na watu kweli wanapita kwenye geti. Niwaulize swalii, ni lini toka mmeputa jiwe la Laizer ni lini mmeputa *tanzanite* ambayo imezidi milioni thelathini, arobaini? Ni kwasababu, nyie mkipewa mawazo kabla hamjayafanyia kazi mnapeleka utaalamu. Sasa watu wanawapigia chenga palepale na tochi yenu mnamulika pale.

Mheshimiwa Spika, ni watu wanazunguka na wale vijana wa tochi pale. Hatuna sababu ya kutumia akili nyingi ya *degree* tu. Mnaona *degree* zinatufelisha, naomba nikupe dawa moja ndogo tu; kesho Serikali iwe na hela pale waweke vijana wa darasa la saba tu wanaojua mawe, tunahitaji tochi wala sio *binocular* hiyo mnayotumia pale, muwaweke pembedi pale hawa ma-*valuer* wenu wenye *degree* wapimee wakifika mwisho wakisema hii ni milioni 30 muwape wale vijana wa darasa la saba wachungulie wawaambie kama ni 30 mpe mara moja muone kama hawatayakimbia mawe pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mnapigwa chenga palepale na askari wenu wako pale. Kwa hiyo, ni vizuri wataalam mtutafute tuwape madini, msione aibu kufundishwa na darasa la saba tumekulia huko, nyie *field* yenu mmesoma miezi mitatu sasa sisi tumekulia kulekule. Kwa hiyo, ni vizuri

msishikane uchawi wowote wizi mnapigwa na makamera yenu yako pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nishauri pia, nchi kama Tanzania tuna ma-*valuer* wasiozidi kumi na moja, kumi na tano, ni aibu. Kama tuko *serious* chukueni wanajeshi hata 100 ni miezi sita tu kujifunza u-*valuer* kwa nini tuwe na watu kumi na moja, kumi na mbili? Walewale wanazungumza, ukzungumza na huyu akimaliza *deal* biashara imeisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana ushauri wangu hawa wataalamu waweze kuufanya kazi, lakini nataka nizungumze kuna mtu mmoja msomi humu mtaalamu Profesa alizungumza juzi akasema dhahabu hatujafanya vizuri. Nimekulia Geita, wakati wa utawala wa Mhesimiwa Profesa Muhongo wachimbaji wadogo mwaka 2015 tulikusanya gramu 120, 2016 wakati tumeanza kuruhusu wachimbaji wadogo baada ya kupokelewa mawazo yetu tumekusanya 337,000 gramu kwa mwaka, 2017, 800,000, 2018,6 1,600,000, 2019 4,000,000, na 2020 5,000,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunahitaji kuwa na maprofesa wa *design* hii? Hata kama hatujui kusoma, hatuoni haya maandishi hapa ndani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri mtu anapofanya kazi nzuri tuisitengenezeane ajali lazima apewe sifa. Hongera sana Waziri wa Madini, umefanya kazi nzuri wala hutuhitaji kupata *degree* hapa, tunajumlisha hesabu tunajua kutoka gramu 120 leo tuko milioni tano halafu mtu anasimama hapa anaanza kubeza. Nakumbuka maneno ya mtu mmoja nikiwa sio Mbunge, alikuwa anakaa pale nikimuangalia kwenye TV anaitwa Mheshimiwa Kigwangala, alimwambia binafsi hajawahi kuona Profesa muongo kama Mheshimiwa Muhongo kwa sababu... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma namlinda Mheshimiwa Mbunge Profesa Muhongo. Sijui yupo humu ndani?

MBUNGE FULANI: Hayupo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, atapata taarifa.

SPIKA: Nadhani ametoka kidogo? (*Kicheko*)

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, univumilie kidogo ninazungumza kwa uchungu. Mwaka 2016 Mheshimiwa Profesa Muhongo akiwa Waziri nimemuita Geita kumwambia Waziri tunaibiwa; hadharani kwenye *mic*, tunaibiwa haya makinikia wakipakia humu kuna dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Profesa alishika *mic* ananiambia wewe ni darasa la saba, nyie watu wa Geita mlkosea kuchagua mtu wa darasa la saba. Tukamchenga Profesa, dakika moja Mheshimiwa nimalizie hoja yangu, tukampelekea marehemu Mheshimiwa Magufuli kamfuko tu kadogo tukamwambia Mheshimiwa hatuhitaji Profesa, naomba utusimamie tuoshe haka kamfuko tu kadogo tukaoshea na *Coca-cola*.

Mheshimiwa Spika, dakika 15 tulikuwa na dhahabu ya milioni 16, Mheshimiwa Dkt. Magufuli akawakia na kwenye gia. Sasa maprofesa wa *design* hii watatuchelewesha ni vizuri mtuiamini na sisi *LY* tunaumia, tunatumia nguvu kuwapa *material* halafu wanakuja wanapotoshya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma. Ahsante sana, kwa hakika *LY* ni jeshi kubwa. (*Makofi/Kicheko*)

Na kama anavyosema siku zote ni kweli uchumi wa nchi yetu sehemu kubwa sana ya uchumi wameushika *LY* kwa hiyo, lazima tuwa-*appreciate*, kweli kabisa. Mpaka hapo tutakapoona hizi *degree* zetu nazozina utajiri wa nchi hii ndio

tutakapoamini tofauti. Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma.
(Kicheko/Makofi)

Sasa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani. Atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Gambo.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima kuweza kusimama tena ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo machache kulingana na umuhimu wenyewe wa Wizara, Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini mambo mengine ninaweza kushauri kwenye Wizara nydingine za kisekta..

Mheshimiwa Spika, nitaanza na suala la ajira, sote tunajua kwamba, suala la ajira bado ni changamoto kubwa sana kwenye Taifa letu. Tukitazama wahitimu wa kada mbalimbali kwa mwaka na idadi ya ajira zinazotolewa ni vitu viwili tofauti, lakini pamoja na kwamba, Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali namna ya kuwasaidia vijana, imekuja na Habari ya Mfuko wa Vijana bado haijaweza kumaliza changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na mfuko uliopo ambaao uko chini ya TAMISEMI ambaao unazungumzia asilimia 4 kwa vijana, asilimia 4 kwa wanawake na asilimia 2 kwa watu wenyе ulemavu ni vizuri suala hilo likaangaliwa upya. Najua kuanza hatua moja inatufanya turudi na turekebishe makosa yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza changamoto inaanizia kwenye asilimia mbili ya watu wenyе ulemavu. Watu wenyе ulemavu wako wa aina tofauti na hapa kumekuwa na shida sana kwenye hili jambo. Kwa kuwa, Wizara hii pamoja na kwamba, tulipitisha hiyo asilimia 2 ni vizuri tukaangalia sera yetu kwasababu, lengo ni kuwasaidia watu wenyе ulemavu na lengo ni kuwasaidia vijana pamoja na wanawake.
(Makof)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na ushauri kidogo, leo tuna *VETA* na tuna vyuo vya ufundu, wale watu wakishamaliza pale wamepewa *knowledge* shida yao inakuwa ni suala la *capital*. Na kwasababu, kumekuwa na changamoto kwa vijana wengi ambao wanamaliza vyuo hawana uwezo wowote wa kwenda kufanya biashara wa kwenda kufanya jambo lolote kwa hiyo, inakuwa ni changamoto kurudisha ile fedha ambayo wamekopa. Ni kweli wanajikusanya huko wanaona namna gani ambayo wanaweza wakajisaidia ili wakakope, wanakopeshwa. Kurudisha fedha ile inakuwa ni ngumu, lakini hali tukiangalia halmashauri zetu ni mbaya sasa hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini kwenye jambo hili; wale watu wanaokuwa wamemaliza vyuo vya ufundu au waliotoka *VETA* tayari wamepewa ujuzi na ninazungumza leo nikwa mara ya tatu ndani ya Bunge. Wale watu wakipewa mkopo na tutoke kwenye asilimia 4 tufikiri zaidi ikiwezekana vijana peke yake wapewe asilimia 10. Lengo ni kwamba, kwasababu, wameshapewa ujuzi wakienda kule kwasababu wana uwezo wa kujajiri wao wenyewe wanaajiri vijana wengine kuitia kazi ambazo wamezifanya. Kutakuwa na tija na lengo ambalo tulikuwa tunafikiri kuwa-*empower* vijana wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini hata wanawake. Wanawake sasa wamejitoa wameamua kuingia kwenye ujasiriamali na shughuli mbalimbali, tukizungumzia asilimia 4 ni wanawake wangapi ambao wanapewa huo mkopo?

Mheshimiwa Spika, na kwa bahati mbaya hata hiyo asilimia 4 kuna halmashauri zinashindwa kuwapa wanawake kwa sababu ya hali iliyopo kwenye halmashauri zetu. Kwa hiyo, ni vizuri ikiwezekana itoke TAMISEMI tukaona namna bora ambavyo tunaweza *ku-control* jambo hili, ili tuweze kuwasaidia wanawake ambao tuliwalenga pamoja na vijana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitakuja kidogo kwenye kilimo kwasababu, nitakuja kluchangia kwenye Wizara ya Kilimo.

Tunapozungumzia uwekezaji, tunapozungumzia viwanda, tunapozungumzia uchumi wa kati huwezi kuacha sekta ya kilimo Tanzania kuizungumzia ili kufikia uchumi wa kati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia palepale ambapo nazungumza kila siku, ili kuboresha kilimo chetu na kiwe kilimo chenye tija lazima tuwekeze kwenye utafiti. Nategemea leo tunapozungumzia kilimo cha Tanzania cha kwanza tuangalie vyuo vyetu vya utafiti viko vingapi, lakini tunapeleka fedha kiasi gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo hata tukija na njia mbadala kwamba, tunahitaji mazao ambayo yatakuwa labda mbadala wa mahindi, kwa mfano Nyanda za Juu Kusini. Kabla ya kufanya hivyo mmeefanya utafiti kiasi gani wa udongo? Mmeefanya utafiti kiasi gani juu ya mbegu ambazo zinapelekwa kwa ajili ya kilimo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mbadala wa mahindi kwa mfano nyanda za Juu Kusini kabla ya kufanya hivyo mmeefanya utafiti kiasi gani wa udogo, mmeefanya utafiti kiasi gani juu ya mbegu ambazo zinapelekwa kwa ajili ya kilimo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba mwaka uliopita ni asilimia 20 tu ya mbegu bora ambazo zilipelekwa kwa wakulima wetu. Ukipeleka mbegu ambazo si bora kwa hali ya kawaida unategemea mazao yake yatakuwaje? Kama tutawekeza kwenye utafiti lazima pia tutatafiti ni zao gani ambazo linaweza likasaidia Taifa, ni zao gani ambalo linaweza kupandwa kulingana na aina ya udongo ambayo tumepata majibu kutoka kwa watafiti.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaendelea cha mazoea sana, ukiangalia kwenye shina moja labda nitolee mfano zao la mahindi, wanachukua kile kifuniko cha maji au kisoda wanapimia mbolea wanaweka pale, nani alifanya utafiti kwamba lile tundu linafaa kwa kile kizibo kimoja kuweka mbole? Lakini wananchi wengi wanatumia ni kwasababu ukiangalia hata Maafisa wa ugani wetu ni wangapi wanafika

kule kwa wakulima wetu kuwapa elimu na kwamba wamefanya utafiti ni kiasi gani kinafaa kutumika kwenye shina moja la mahindi.

Mheshimiwa Spika, bado ninarudi Ofisi ya Waziri Mkuu. Pamoja na kwamba Wizara zote zinaweza kuzungumzia kulingana na sekta zao ni vizuri kuangalia uchumi wa kat iwa Taifa hili tunaenda kuangalia kwenye vitu gani? Leo tunazungumzia uchumi wa kat i ukienda kwa Mtanzania mmoja mmoja wa chini kabisa kwa mfano kule Nkasi ukimwambia tupo kwenye uchumi wa kat i atakushangaa uchumi wa kat i upo wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka hii hali Mheshimiwa Waziri Mkuu hizi takwimu ambazo tunasoma kwenye vitabu zikaonekane kwa wananchi moja kwa moja kwenye uhalisia wa maisha yao ya kila siku na hapa tutakuwa tunazungumzia lugha moja. Ni kweli kwamba yawezekana wataalam wetu wanatuambia hivyo, lakini nataka uhalisia.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida hata mimi Aida ukiniambia kwamba uchumi wa kat i, bado najiuliza uchumi wa kat i ninaangalia nini? Vigezo gani ambavyo naviona kwangu kwamba kweli tumefikia kwenye uchumi wa kat i. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati nataka kwenda kuzungumzia habari ya Tume Huru nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na kwamba nimezungumza mara kadhaa...

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, taarifa

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Getere

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, Ahsante naomba nimpe taarifa Mbunge ya Nkasi, anasema

uchumi wa kati umekujaje aende akaangalie vigezo vya *IMF* na *World Bank*, kwamba uchumi wa kati unapatikana kwa *capital income per capital income* *GDP*; kwa hiyo angalia tu hivyo vigezo mama utajua kwamba vinaendaje Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

SPIKA: Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Sisi hatujazoea kukaririshwa tumezoea kuona na kuyaishi maisha yenyewe ya uchumi wa kati; kwa hiyo hatuwezi kuelewana lugha zipo tofauti kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tumekuwa na ahadi ya muda mrefu kuhusu suala la MV Liemba kwenye ziwa Tanganyika. Ni vizuri wakati unahitimisha; kumekuwa na kelele nyingi kwamba yawezekana wale watu wamejitoa, sijui mkataba umefanya nini, ni vizuri mkaja hapa mkatueleza hatua ya MV Liemba imefikia wapi na nini kinaendelea ili na sisi tupate kujua watu tunaotoka kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kwasababu ya muda naomba nizungumzie Tume Huru ya Uchaguzi, Fungu la 61. Miiongoni mwa Wabunge wa CHADEMA waliotangazwa ni mimi hapa kupitia Tume hii iliyopo sasa hivi, natambua hilo. Lakini pamoja na kutambua kwamba nilitangazwa si kwamba nilikuwa Mgombea bora kuliko wagombea wengine wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), lakini ni miiongoni mwa wale wachache, au mimi niliyepenya kwenye tundu la sindano. Naomba nizungumze mambo machache kwa ajili ya Taifa letu, kwa nia njema kabisa,. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia Tume Huru ya Uchaguzi tulianza na mchakato wa kutaka Katiba mpya ambayo ilikuwa ni maoni yetu. Natambua kwamba yalitokea yaliyotokea, lakini pamoja na hayo mlifikia hatua kubwa sana ya Katiba mpya. Ndiyo maana leo tunasema kwakuwa kelele ni nyingi na tunahitaji umoja wa Taifa letu tuangularie vipengele

ambavyo bado vinashida, hasa kwenye eneo la Tume Huru ya Uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Tume Huru ya Uchaguzi tukisema tuongeze idadi ya watu kuna ghamra ya fedha, lakini kama lengo ni kuponya taifa ni vizuri tukazungumza.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya Wakurugenzi ambao sheria imekataza kabisa kwamba Msimamizi wa Uchaguzi hatakiwi kuwa kiongozi wa Chama cha Siasa, lakini sote tunajua wapo Wakurugenzi ambao walikuwa viongozi wa vyama vyaya siasa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata ningekuwa mimi leo nimepewua ukurugenzi kila mtu alikuwa anajua Aida ni kada wa CHADEMA katika wagombea wa Chama cha Mapinduzi lazima nitalinda maslahi ya chama changu, na lengo ni jema tu. Naomba nitolee mfano mdogo tu wa kama yangu alikuwa Mkurugenzi hapa Dodoma, alikuwa mkurugenzi Dodoma amekwenda Jimbo la Mlimba Mheshimiwa Kunambi...

SPIKA: Unamchokoza. (*Makofi*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, aaah! nimesema ni mfano, na nia ni njema tu alikuwa Makao Makuu pale kila mtu anajua.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hali ya kawaida yaani ukiangalia suala hili ambalo nataka kuzungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu kuanzia mchakato wa awali habari ya watu kunyang'anywa fomu, habari ya watu fomu zao zina matatizo. Msimamizi wa Uchaguzi hakai pale kwa ajili ya kuvizia nani amekosea kwenye fomu yake anatakiwa awepo pale kumwelekeza mgombea kwamba hapa unatakiwa kufanya hivi, ufanye hivi Uchaguzi wa mwaka 2020...

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

TAARIFA

SPIKA: Taarifa, iko wapi taarifa, Nimekuona Mheshimiwa Kunambi.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, Hakuna mashaka na Tume yetu ya Uchaguzi. Na labda nimueleze tu kama Tume yetu ya Uchaguzi isingekuwa Tume ya kutenda haki yeche asingekuwepo hapa. Nimpe tu taarifa kwamba Tume yetu ya Uchaguzi inazingatia misingi ya demokrasia. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Aida muda wako umekwisha, dakika moja tu ili uweze kupokea taarifa.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Kunambi anatakiwa kujua kwamba mimi sikupita bila kупingwa hilo la kwanza ajue...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. AIDA J. KHENANI:lakini la pili...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. AIDA J. KHENANI: ... nataka nitoe ushauri kwenye jambo hili...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa nipo huku...

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma taarifa.

TAARIFA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi nazidi kumweleza mchangiaji kwamba, ni kweli hatuna mashaka na Tume ya Uchaguzi na imetenda

haki na mfano mzuri huko Kilimanjaro Mheshimiwa Anna Mghwira ni *ACT*, lakini tumewapiga, kwa hiyo naomba waondoe mashaka na Tume yetu. (*Makofi*)

SPIKA: Pokea taarifa.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Hajajibu hamuwezi kumpa taarifa juu ya taarifa

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Ayayayaaa!

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimwambie kaka yangu Musukuma kwamba Mheshimiwa Anna Mghwira sio *ACT* ni CCM lakini, tafakari ninayoiacha ninapohitimisha kila Mbunge aliyekuwa humu ndani anajua alishinda, kama alishinda alishinda kwa namna gani, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Tatizo lenu, nikusaidieni, mimi huwa ninakaa nawasikiliza habari ya tume huru lakini hata siku moja hajawahi kusimama mtu akasema hiyo tume huru mnayosema nyinyi inafanananje? Mnasema neno Tume huru tume huru kwani iliyoko hapa sio huru...

MHE. AIDA J. KHENANI: (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*)

SPIKA: Aaa! Umeshatumia dakika. Mheshimiwa Mrisho Gambo tunaendelea alafu atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby (*Kicheko/Makofi*)

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi kama Mbunge niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, mimi nitajielekeza kwenye mambo mawili. La kwanza tunafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu leo amewasilisha taarifa yake na kwenye taarifa hiyo ameomba aidhinishiwe fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 116,784,244.

Mheshimiwa Spika, tutakumbuka hivi karibuni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliweza kutoa hotuba elekezi wakati anawaapisha Makatibu Wakuu; hotuba ambayo ilikwenda kukonga nyoyo za Watanzania. Hotuba ambayo ilikwenda kutoa matumaini kwa wawekezaji, hotuba ambayo ilitoa matumaini kwa watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye hoja yangu ya msingi nataka nikumbushe yafuatayo. Tumekuwa na awamu tano na leo tuna awamu ya sita, na utamaduni wetu kama Taifa tumekuwa kila awamu tumeipa nafasi na heshima inayostahili ili iweze kuongoza nchi. Wakati wa Rais Nyerere tulizungumza masuala yanayohusiana na Rais Nyerere wakati wa Rais Mwinyi tulimpa fursa Rais Mwinyi, wakati wa Rais Mkapa, wakati wa Rais Kikwete, wakati wa Hayati Rais Magufuli na sasa tuna awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan lazima tumpe *credit* anazostahili, lazima tumuunge mkono lazima tutengeneze mambo humu ndani ya kisheria ili yakarahishe utekelezaji wa mambo kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nilikuwa nataka niweke wazi, kwamba lazima Wabunge tukubali kwamba tupo awamu ya sita, na ni vizuri sasa tukaweka mtiririko wa kujenga hoja zetu za kumsaidia Rais wetu kuongoza Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kwenye kipengele hicho; sisi mpinzani wetu si vyama vya siasa, mpinzani wetu ni changamoto za Watanzania. Leo ukizungumza watumishi wanamanung'uniko kuhusu mishahara yao na kupanda madaraja; kwa miaka mitano hawajapanda madaraja. Leo ukizungumza kuhusu bodi ya mkopo unaona sheria ilikuwa inasema asilimia nane baadaye imekwenda asilimia 15 na kibaya zaidi sheria zote zinazotungwa huwa zinaanza pale.

Sheria yetu ilirudi mpaka nyuma. Watumishi kule wanalia, watu waliosoma vyuo wanalia, lakini hayo mambo yamepitishwa ndani ya Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia pia tuna changamoto kwenye bima afya, tuna changamoto pia kwenye ajira, manung'unko ni makubwa. Kwahiylo, kazi ya Bunge hili ni kurekebisha sheria kutoa mapendekezo na ushauri ambao Serikali ikiufanya kazi matumaini yataendelea kudumu kule kwa Watanzania. (*makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo; mimi naona hotuba ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan tukiifanyia kazi itatusaidi sana kuirahisishia kazi Serikali kwenye masuala mbalimbali. Utaona kila Waziri atakayekuja hapa baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wote watasema mambo yao lakini hatimaye wataomba kuidhinishiwa fedha; hizo fedha zinatoka wapi kama hatukutengeneza mazingira mazuri ya kupata fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, mimi nitatoa mapendekezo yangu kwenye sheria nne. Tuna Sheria ya Kazi, Sheria ya Uhamiaji Sheria ya Uwekezaji na tuna Sheria ya Kodi; ziko nydingi, lakini kwasababu muda ni mchache mimi nitazungumzia hizo sheria nne.

Mheshimiwa Spika, ukienda kuangalia sheria ya kazi kwenye Kanuni Kifungu 9(d) tunaambiwa *the Employer has provided sufficient evidence from recognize job such mechanism that has been unable to fulfill the particular post due to lack of qualified personnel in the Tanzania labour market*. Lakini ukiangalia kanuni hiyo hiyo ya tisa kifungu (9)(2)(d) inasema *in the event bulk requirement work permit maybe granted at a ratio of ten local employees to one none citizen employee*.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda kwenye sheria hiyo hiyo la *labour* inakwambia kwamba mwekezaji anapokuja kuwekeza Tanzania atapewa kibali kwa miaka mitano, kama mtaji wake una umuhimu na mkubwa anaweza kwenda hata

zaidi ya kumi. Sasa unajuliza huyu mwekezaji unampa kibali cha kazi mwajiri wake ni nani? na mtu amekuja kuwekeza na yeye pia atakuja kuajiri watu?

Mheshimiwa Spika, ukienda *Zanzibartu* hapo wanayo sheria hiyo hiyo pia kama ya kwetu, lakini wao mwekezaji anapata *Residential Permit* hapati *work permit*, lakini ukija Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitu ni kingine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia sheria ya uwekezaji kifungu cha 24 (1) tunaambiwa

24_(1). Every business enterprise granted a certificate of incentives under this act shall be entitled to an initial automatic grant in may grand quarter of up to five persons during the startup period.

Ukitaka kuanzisha biashara utapewa watu watano lakini ukiangalia pia sheria ya Uhamiaji kifungu cha; 18 (2) nakuambia

18_2 Resident's permit shall be issued for any period not exceed three years and may be renewed for any period not exceeding two years by any endorsement of renew endorsed on it by the director but so that the total period of the validity of the original permit and its news shall not in any case exit five year.

Mheshimiwa Spika, ukisoma hivi sheria tatu hazzungumzi utafikiri kila sheria ina nchi yake, sheria ya uwekezaji inakwambia sisi tunakupa *incentives* ukija kuwekeza Tanzania tutakupa wageni watano, ukienda sheria ya kazi inakwambia sisi ukija kuajiri Tanzania kila ukiajiri 10 tutakupa mgeni mmoja, ukiangalia sheria hiyo hiyo pia *labour Kamishna* anaambiwa huyo mgeni atakubalika kama hakuna Mtanzania mwenye sifa. Ukiangalia hizi sheria kama vile kila sheria na nchi yake, kila sheria ina dini yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nchi kama Kenya leo ukienda pale na Dola yako 100,000 unaruhusiwa pale kufanya

uwekezaji na unapata vibali bila urasimu wa aina yoyote, ukienda nchi kama Dubai *same case* ukienda nchi kama Canada ukipeleka tu Dola 750,000 unapewa kabisa na unaruhusiwa kabisa kukaa *permanently*, ukienda Uturuki ukinunua nyumba tu kiasi cha Dola 200,000 unarahisishiwa kazi unafanya shughuli zako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini hakuna kazi ngumu kama kufanya biashara katika nchi ya Tanzania. Tumepata bahati, tumepata Rais mwenye maono, tumepata Rais ambaye amekubali kuwa *open minded*, tumepata Rais ambaye amewapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri mlioteuliwa ili muweze kuja hapa na mapendekezo ya kisheria ili tuweze kufanya *harmonization* ya sheria zetu, tuwe na sheria moja; mwekezaji asizurure.

Mheshimiwa Spika, mtu kama Dangote kwa mfano kawekeza kiwanda kikubwa sana kule kusini leo akitaka kuja mfano Tanzania eti na ye ye pia unamwambia aombe *work permit*, ili iweje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naangalia malalamiko na manung'unico mengi tunayoyapata nje ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninakupa mfano. Mimi nilivyokuwa Mkuu wa Mkoa, na ndio maana nikagombea Ubunge, kila kitu ninachokiona nikitaka kuingilia kati wananiambia hapana hiyo ni sheria. Sasa ukishakuwa Mkuu wa Mkoa kazi yako ni kusimamia sheria huna uwezo wa kutoa ushauri ndani ya Bunge ya namna ya kubadili sheria.

Mheshimiwa Spika, nikasema nimepata bahati na fursa ya upendeleo kwa Mwenyezi Mungu ya kuingia humu ndani nitoe mchango wangu na maoni yangu. Niombe Bunge lako Tukufu lichukulie *very serious jambo* hili ili tuweze kubadilisha na kurekebisha sheria zetu. (*makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwanini nimesema hayo, hapa Serikali ilikuja kuahidi hapa kwenye hotuba ya Rais kwamba tutatoa ajira milioni nane. Ukitungumzia kutoa ajira

milioni nane maana yake unazungumzia kila mwaka utatoa ajira milioni 1,600,000, Serikali yetu watumishi wake wa Umma toka uhuru mpaka leo hawajawahi kuzidi 600,000 na mishahara wanayolipwa kwa mwezi ni milioni 660 sasa unajiliza kama toka uhuru kwa miaka zaidi ya 50 tunaajiri watu 600,000 tutafikiaje *target* hii ya Milioni nane.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu ili tufikie *target* hii lazima tuweke msukumo na nguvu kubwa sana kwenye *private sector*. Lazima twende tukafanyile kazi changamoto zote ambazo zimesemwa kwenye *private sector* humu Wabunge kila siku tumekuwa tunalalamika...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Dakika zako zimekwisha ninakupa dakika mbili umalizie.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa nasisitiza kwamba tunahitaji kuweka nguvu kubwa sana kwenye *private sector*, tunahitaji kufanya *harmonization* ya sheria zetu, tunahitaji pia kujuliza hivi leo kwanini mtu anamaliza *degree* anaendesha boda boda? Leo tunatakiwa tuijulize kwanini mwekezaji anang'ang'ania kuja na wageni kutoka nje ilhali Watanzania hapa wapo? na akija pale atamlipa fedha nyngi atamlipa vibali pamoja na changamoto zote, lakini kwanini bado anamuhitaji?

Mheshimiwa Spika, hitimisho langu, naomba Watanzania watuelewe, tunaposema wawekezaji wapewe vipaumbele hatuna maana ya kunyima ajira za Watanzania. Tunasema wapewe vipaumbele kwa sababu tunafahamu kama tukisema mwekezaji *ratio* yetu ni 1:10 basi anapoajiri watu 10 maana yake 9 watakuwa ni Watanzania au anapoajiri mgeni mmoja 10 watakuwa ni Watanzania. Kwa hiyo, tutakuja na mapendekezo ya sheria ambayo yatawalinda Watanzania lakini pia yatampa amani

mwekezaji ili ajira ziongezeke na changamoto iweze kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimwia Spika, la mwisho kabisa sababu muda ni mdogo, sisi Arusha pale tuna kiwanda cha *General Tyre* kwenye jitihada hizi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Bahati mbaya muda hauko upande wako Mheshimiwa.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli. Mheshimiwa Shabiby tafadhali.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa mmoja wa wachangiaji katika hoja ya Waziri Mkuu, lakini leo mimi nitachangia kwa upole sana na kwa ushauri tu angalau kidogo.

Mheshimiwa Spika, labda watu wengi hawajazungumzia au Wabunge wengi wapya lakini hawaajaiona athari ya *TARURA* na *RUWASA* kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia muundo wa uliouunda *RUWASA* na *TARURA* mimi sina shida nao sana na wala sina matatizo na Mameneja wangu wa Mkoa, mimi natoka Mkoa wa Morogoro wala wa Wilaya ya Gairo, wapo vizuri kabisa. Lakini ukiuangalia ule muundo unapishana kabisa na Katiba, Ibara ya 145 na 146 iliyoweka mamlaka kwa umma katika kuamua mambo yao katika Sheria za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia leo wakati inaundwa *TARURA* ilikuwa kama *technical agency*, lakini sasa hivi

yenye ndio imekuwa na mamlaka ya kila kitu. Utakuta Meneja wa *TARURA* wa Wilaya hawajibiki kwa chochote katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo linapokuja sasa, kwa hiyo, Diwani amechaguliwa na wananchi kama mwakilishi kwneye Kata yake, na yeye naye ana maswali ya kuulizwa habari ya *RUWASA* kuhusu maji na ana maswali ya kuulizwa kuhusu barabara za *TARURA*, lakini anakuwa hana majibu ya aina yoyote. Na watu wa *TARURA* kwa mamlaka waliyopewa wao wanaamua barabara watengeneza ipi bila kushirikisha Baraza la Madiwani wala Mbunge na ukiona Mbunge kashirikishwa basi ujue hiyo ni hisani tu, umekaa naye vizuri Meneja wako, mnashirikiana, lakini akija Meneja kichaa na wewe ataamua kupeleka barabara kwa hawara wake na ya kwako ya kimkakati isipelekwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ipo sehemu hata kwa Mheshimiwa Kakunda pale Meneja wa *TARURA* kapeleka barabara *guest* kwake.

Mheshimiwa Spika, nilzungumza nyuma kidogo lakini sikupata nafasi ya kuichambua zaidi. Mama Samia juzi amesema kabisa sasa *TARURA* mtashirikiana na TAMISEMI, lazima sasa *TARURA* na *RUWASA* wa maji kwenye menejimenti zao sina shaka nazo, fedha zao wanavyokaa nazo na *technical* zao sina shaka nao, waendelee hivyo hivyo, lakini mipango mikakati yote ya bajeti ianzie kwenye Halmashauri za Wilaya. Barabara za kutengeneza zitoke pale kwenye Baraza la Madiwani, visima vya maji au maji yanatoka na kwenda wapi na kwenda wapi ya anzie kwenye Baraza la Madiwani, wao wawe watekelezaji, watoa fedha na mambo mengien yote. Lakini utakuta bajeti wanapanga, wanarudishiwa, hawasemi zimekuja shilingi ngapi, wanaanza wao, wewe una barabara ya kimkakati huku ina watu 10,000 wao wanaenda kutengeneza barabara ya watu 500.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilli jambo tusipoliangalia kwa kweli hawa *TARURA* na *RUWASA* wanakuwa sasa ni Mungu mtu kwenye Halmashauri, na ukiangalia na jiulize huyu

Mkurugenzi wa Maendeleo sasa anafanya kazi gani kama anashindwa kumdhhibit Meneja wa *TARURA* au Meneja wa *RUWASA* Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ni ni sasa, si mkitoe tu hicho cheo na mtupe sisi Wabunge tuwe Wabunge na Wakurugenzi wa Maendeleo.

SPIKA: Kwanza nikuongezee Mheshimiwa Shabiby, hao Mameneja wa *TARURA* na *RUWASA* wana mshahara kuliko huyo Mkurugenzi wa Maendeleo, yalivyo mambo ya ajabu.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Sawa kabisa na nalifahamu hilo.

SPIKA: Kamkurugenzi tu ka-*TARURA* yaani, tayari.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili, hawa watu warudi na wawajibike, hivi leo *TARURA* anatengeneza barabara, *RUWASA* anatengeneza maji, halafu Diwani kuititia Baraza la Madiwani haruhusiwi kwenda kukagua, yaani anatengeneza yeye, anakagua yeye na yeye ndio kaamua, sasa Diwani anafanya kazi gani, Diwani leo kabakia na madarasa na zahanati. Sasa Diwani ana kazi gani na Mkurugenzi wa Maendeleo ana kazi gani kama anashindwa kumdhhibit *TARURA* na *RUWASA*? Tunaomba lirudi hili suala, menejimenti na fedha zibaki kwao kama mnasema Madiwani wanafuja fedha, lakini lazima wawajibike pale na akifanya vibaya baada ya ukaguzi wa Madiwani; Madiwani wawe na amri ya kusema huyu hafai. Nataka niseme na sisi Wabunge tukiwa kule kwenye Wilaya zetu na sisi ni Madiwani.

Mheshimiwa Spika, cha pili tunatafuta hela kila siku za *TARURA*, lakini wewe ni shahidi na Waziri Mkuu ni shahidi, aliyekuwa zamani Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kabla hajawa Waziri Madini Mheshimiwa Doto Biteko ni shahidi. *EWURA* kila lita moja ya mafuta tunayoweka wanachukua shilingi 17 mpaka 16 kila lita moja ya Tanzania, hata jenereta ukiweka wanachukua fedha, kisingizio wanasema tunaweka vinasaba kwenye mafuta. Vinasaba

kwenye mafuta zimeleta mzozo, wewe umevunja Kamati ya Nishati na Madini, na walikuja hata kwako wakusomeshe ukawafukuza. Ndio mjue kule kuna wezi, kuna baadhi ya Wabunge hapa walikuwa wanakula rushwa nje, nje, tena mkinikera nitataja, ila basi acha leo ninyamaze, kwa sababu ya kutetea huu wizi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa leo mkataba kwa yule mwekezaji kwa mwezi anachukua zaidi ya shilingi bilioni tano, ambapo kila mwezi tungejenga hospitali moja.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Ni nani? Muwe mnajitaja majina.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Naitwa Mrisho Gambo.

SPIKA: Aah Mheshimiwa Gambo umekaa chini, unatakiwa usimame. Haya nakuruhusu kwa sababu....

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nadhani *allegation* aliyotoa kwamba Bunge limekula rushwa ni *allegation* kubwa, mimi ningeomba tu kama wapo waliokula rushwa wawataje ili wengine tubaki na heshima zetu. (*Kicheko*)

SPIKA: Hilo nalikataa. Mheshimiwa Shabiby endelea. (*Kicheko*)

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, hiyo nimetoa onyo, sasa hibi wapya hamjala. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lazima tuliangalie, tunao *TBS* ambaao ndio kazi yao, kwa nini wasipewe hii *tender* na *TBS* wanachukua fedha kutoka sehemu tofauti. Hii fedha shilingi 17 tuipeleke *TARURA* ili *TARURA* wafanye kazi vizuri zaidi. Profesa Muhongo pamoja na kuchambuliwa na Mheshimiwa Musukuma hapa lakini alishawaita, wakati ule ulitoa amri kwamba wafanyabiashara tukutane na Profesa Muhongo, *EWURA* walishindwa kujibu. Kwa sababu waliitwa watu wa

TRA, watu wa *TRA* wakasema sisi tunadhibiti mafuta yetu, tunajitosheleza kwa asilimia 100. Kwa sababu kama gari ya *transit* inaenda Rwanda au Burundi tunaweka king'amuzi, tunaiona gari kila kona mpaka inafika.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mimi wakati ule *EWURA* inaanizhwa ilikuwa watu wasichanganye mafuta ya taa na dizeli na mafuta ya taa na petroli ndio ilikuwa lengo. Mimi ndio nilikuwa Mbunge pekee niliyeongea miaka mitatu hapa mpaka mafuta ya taa yakapanda bei, niliyechakachua nikashinda wao wakahama, wakaona ulaji huku umeisha, wakahamia sasa tunadhibiti *transit* na mafuta ya kawaida, ilimradi tu ulaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na yule jamaa anachukua *five to seven billion per month*. Huyo *agent/mkandarasi* aliyepewa kuweka hiyo.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Jamani mimi naomba taarifa ziwe za maana, nimekuona Mheshimiwa Tabasam.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, huyu *GFI* anachukua shilingi 14 kwa lita, halafu kuna tozo zingine zote zilizopo pale sasa hivi zinafika shilingi 90; fedha inayotumika kwa siku kwa lita milioni 12 zinazouzwa ni shilingi bilioni moja na elfu themanini kila siku ya Mungu, kwa mwezi ni shilingi bilioni 32.4.

Mheshimiwa Shabiby endelea, tunapigwa vyatutu kutosha. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa yake ni nzuri sana.

Sasa hizo fedha zote zikichukuliwa na kupelekwa *TARURA* hatujapata mtaji? Na tukiongeza....

SPIKA: Yaani ni kutumbukiza tu hicho kinasaba tu hivi halafu ndiyo mabilioni yote hayo?

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Na taasisi ya Serikali hiyo *TBS* hawezi kuwa unanyunyiza hiyo? Endelea Mheshimiwa.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, nataka nikuambie kwanza mimi namiliki vituo vya mafuta.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri afadhali, Mheshimiwa Kalemani.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge lakini pia nimpongeze kwa hoja hii na tumeshatoa taarifa katika Kamati yetu kuwa ile kampuni inayofanya vinasaba tumeshasitisha mkataba wake na wala haifanyi kazi hiyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo yale maeneo mengine nadhani yanaweza kuendelea kujadiliwa lakini la vinasaba tumeshasitisha na nimetoa maelekezo kuwa kazi hiyo ifanywe na Taasisi ya Serikali ya *TBS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ahsante sana, tungakuwa na taarifa hiyo mapema ingetuokolea muda. Tunakushukuru sana na tunaishukuru sana Serikali.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Taarifa yake sipokei kwa sababu bado ipo na huyu niliyekaa naye hapa ana kampuni ya mafuta na leo wameweka. Sasa

umesitisha mkataba huku unaendelea? Kwa naomba ukasitishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nillalamika kipindi fulani hapa Bungeni wakaniandika kwenye gazeti, walikuwa wahonga mpaka baadhi ya magazeti, wakaandika Mbunge wa Gairo ni mwizi wa mafuta tunamdhibiti wakaja hawakuweka vinasaba kwenye mafuta yangu na mimi nikawafanya *timing* gari sikushusha nikaenda kuchongea kwa Waziri Mkuu, ndio wakakimbia, Waziri Mkuu akanambia andika na nikaandika, kwa hiyo wizi wote unafahamika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba hawa watoke kwa sababu wameshakula fedha ya nchi siku nyingi, huyu Mheshimiwa Doto aitwe hapa alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ambaye sasa ni Waziri wa Madini alikuja kutishwa na mtu mkubwa kwa sababu wakati akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Madini alishikilia kidedea, akaja kutishwa mtu wa juu kabisa, akaambiwa wewe dogo tunakupoteza sisi ukiendelea kufuatilia hii kitu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri nimecaa na wewe zaidi ya mara tatu lakini kila nikikueleza nilikuwa naona hunielewi, sasa nikaona napoteza muda wangu, kila nikimwelewesha. Hivi wewe unawekewa kitu, kwa mfano mimi nakodisha gari ya Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Shangazi anamtuma dereva wake aende *depot* anapakia mafuta ya Shabiby halafu dereva anawekewa mkojo wa punda anaambiwa hii ndio kinasaba hata haujui, halafu wewe unakuja kupima kwangu mimi, hapo uhalali upo wapi? Halafu hainekani kwenye rangi, wala haionekani kwenye chochote, wote ni upigaji tu, shilingi bilioni saba, bilioni sita na mpaka bilioni 30 alizosema Mheshimiwa Mbunge pale.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Utaratibu umeshaisha. Nimeshamaliza. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Shabiby ameshamaliza muda wake. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nilishamtaja Mheshimiwa Bonnah...

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

SPIKA: Mlisimama wawili mkawa mnanichanganya, Mheshimiwa Cecilia.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nazungumzia Kuhusu Utaratibu na kama ikikupendeza, hoja ambazo amezisema Mheshimiwa Shabiby ni nzito na kama Mheshimiwa aliyekuwa Mwenyekiti wetu wa Kamati alitishwa maana yake Kamati inapofanya kazi inafanya kazi kwa niaba ya Bunge na kama Kamati ilitishwa ina maana Bunge ilitishwa, hoja zilizosemwa siyo nyepesi ni nzito sana ambazo zina maslahi mapana kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikikupendeza na kama ambavyo uendeshaji wa shughuli za Bunge unafahamika ama Serikali ije hapa Bungeni itoe taarifa rasmi au kupitia Kiti chako na kwa ridhaa yako tuone namna bora ama ya kuunda Kamati Ndogo au Kamati yetu iliyoko sasa ya Nishati na Madini ishughulikie jambo hili si jambo dogo hata kidogo. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Sikubaliani nawe kwa sababu moja; hayo mambo yanayoelezwa ni ya wakati wa Bunge lile la Kumi na Moja siyo Bunge hili la Kumi na Mbili, ame-refer mambo yaliyotokea enzi hizo na hayo mambo yaliyotokea yanaendana na kilichokuwa kinaendana na hii mikataba ya vinasaba.

Sasa bahati nzuri kile ambacho Wabunge wamekuwa wakishauri miaka yote hii na kimeshauriwa hata sasa na Mheshimiwa Tabasam alishauri Mkutano uliopita sasa Mheshimiwa Waziri ananiambia kwamba Serikali imesikiliza na hiyo kampuni haitakuwa na *tender* hiyo tena, kwa hiyo,

sasa tunaanza ukurasa mpya. Kwa sababu tunaanza ukurasa mpya hatuna haja ya kuunda kitu chochote. Hii inaonyesha jinsi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanatoa ushauri mzuri kwa Serikali na Serikali inafikia mahali fulani inakuwa na usikivu, jambo ambalo ni jema sana. Tunawapongeza sana kwa hatua ambayo mmechukua. Ahsante sana. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami pia napenda niungane na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa kumpoteza kiongozi wetu Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Pia nichukue nafasi hii kusema pamoja na kwamba tuko kwenye majonzi makubwa lakini tutaendelea kumuenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na ametuachia. Pia najua kazi sasa inaendelezwa na Mheshimiwa Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa hiyo, nichukue nafasi hii pia kumpongeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee masuala matatu. Kwanza, nitaanza na vitambulisho vya wazee wetu ambavyo tumewapa kwamba wanapofika hospitalini waweze kuhudumiwa kwa sababu wenyewe ni wazee na wana miaka 60. Hivi vitambulisho kwa sasa havifanyi kazi, wazee wengi wamekuwa wakienda katika hospitali mbalimbali, siyo tu kwenye Mkoa wangu au Jimbo langu, sehemu mbalimbali wanaambiwa kwamba dawa hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niiombe Serikali kwa sababu hii imekuwa ni changamoto sisi Wabunge tunapoenda kufanya mikutano sehemu mbalimbali tunakutana na changamoto hizi, wazee wanalamika kwamba wana vitambulisho lakini hawahudumiwi. Kwa hiyo, naomba niiombe Serikali kwamba kama inaweza kusitisha hivi vitambulisho au inaweza kuwapa hivi vitambulisho na ikawapa waweze kupewa dawa basi ifanye hivyo kwa sababu hivi vitambulisho vimikuwa tu kama picha yaani hawawezi kuvitumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linafanana na hilo ni kuhusiana na akina mama wajawazito wanapokuwa wanaenda hospitalini kwa ajili ya kupimwa au kufanyiwa huduma mbalimbali hawapati zile huduma, wengi wao wanaambiwa watoe pesa. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuliangalia suala hili ni kwa nini jambo hili linatokea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niongelee, ni kuhusiana na *issue* ya fidia mbalimbali kwenye Majimbo yetu ambapo wananchi wametoa maeneo yao kwa sababu ya kuiachia Serikali ili iweze kupitisha miradi. Katika miaka yangu mitano kuanzia 2015 mpaka 2020, nimekuwa ninaongelea jambo moja la fidia ya wakazi wa Kipunguni, Kata ya Kipawa ambao wameiachia Serikali Uwanja wa *Airport*. Leo ni miaka 24 wakazi hao hawajalipwa pesa zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akiwa Mheshimiwa Kwandikwa aliongea hapo kwamba kuna bajeti imepangwa kwa ajili ya kuwapa wale wananchi fidia yao lakini haijawahi kutoka mpaka leo. Hawa wananchi wametoa maeneo yao kwa miaka 24 na mpaka sasa hivi maeneo yao mengine yapo tu hawawezi kuyaendeleza, hawawezi kufanya kitu chochote cha wenyewe kujipatia kipato, nyumba zao tayari *Airport* wameshakuja kuweka mawe yakisemekana kwamba hilo ni eneo la Airport, hawa wakazi kwa kipindi cha miaka 24 wako tu wamekaa hawaelewi kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiomba Serikali itoe tamko kama hawa wakatizi waendelee na shughuli zao katika hizo nyumba au katika hilo eneo, hiyo fidia haitalipwa ili wajue waendelee na mambo yao. Kwa sababu katika kipindi cha miaka 24, ukipita hilo eneo kwanza huduma za kijamii zenyewe, hazipo. Barabara ni mbovu, halafu wengine hawawezi kuziendeleza nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua, mtu akiwa na eneo lake; shamba lake au nyumba, kama hana pesa, anaweza akachukua leseni yake ya makazi au hati akaenda

kukopa, lakini wale hawawezi. Wakienda benki yoyote wanaambiwa kwamba hilo eneo ni la *Airport*, lakini pia Serikali kwa muda wa kipindi cha miaka mitano ambayo mimi nimo humu Bungeni na kila mwaka nilikuwa nauliza maswali na katika kuchangia naulizia, hawajawahi kusema watawalipa au hawawalipi; watalichukua hilo eneo au hawalichukui. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba jibu la Serikali ili wajue kwamba wenyewe wapo pale au wanaondoka? Watalipwa au hawalipwi; ili masuala mengine yaendeleee? Kwa sababu sisi Wabunge tunapokwenda huko, tunapata malalamiko mengi sana kutoka kwa hawa wananchi; na kweli kulalamika ni haki yao kwa sababu kama fidia ilifanyika 1997, mpaka leo ina maana hata hiyo kama watalipwa, watatumia sheria gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kuhusiana na mradi wa umeme ambaao unapita Kinyerezi unakwenda Chalinze. Hawa watu wa Kata ya Kinyelezi Kifuru pia wamechukuliwa eneo lao sasa ni miaka minne, mpaka leo hawajalipwa. Siku zote wamekukwa wakija hapa kumwona Waziri, wamekuja kumwona Katibu, lakini pesa hazilipwi na mpaka sasa hivi tayari nimeona *TANESCO* wameshaanza kuweka nguzo zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iwalipe wananchi kwa sababu wanapotoa maeneo yao, nasi tunasema Serikali inawasaidia wananchi kiuchumi, maeneo yao hayo ndio yanawategemea. Kwa hiyo, Serikali iweze kuwalipa hao watu wa Kipunguni kama inawalipa. Kama haiwalipi, iseme. Serikali iwalipe watu wa Kinyerezi kwa sababu Kinyerezi nimeona tayari wameshaanza mradi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililotaka kuongelea ni kuhusiana na *issue nzima* ya Mkoa wa Dar es Salaam kuhusiana na miundombinu. Sisi watu wa Dar es Salaam hatuwezi kusimama hapa tukaomba mbolea, sijui vitu gani; sisi hatulimi kitu chochote. Sisi uchumi wetu sana sana ni kuhusiana na miundombinu. Yaani wananchi wetu wakiweza kupita vizuri kwenye maeneo yao ili kwenda kwenye kazi zao

na biashara zao, kwanza inawaongezea Serikali mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukubaliane, Dar es Salaam haiwezi ikalingana na mkoa wowote hata kama siyo Makao Makuu. Kwanza ndiyo inachangia pato kubwa katika nchi yet una ndiyo ina wakazi wengi. Kwa sasa hivi Dar es Salaam ina wakazi karibu milioni sita. Sasa tuna mradi unaitwa *DMDP*; huu mradi Hayati Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliahidi kwamba utaanza kutekelezwa mwezi wa Tatu, lakini mpaka sasa hivi hakuna chochote kinachoendelea, tunavyofuatilia, mradi wa *DMDP* // bado haujatekelezwa na wala hakuna matayarisho yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka niseme, sisi wakazi wa Dar es Salaam tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ametuwekea miradi mikubwa sana ya miundombinu, lakini bado kutokana na wingi wetu na kutokana na umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam, bado tunahitaji huo mradi wa *DMDP*. Tunaiomba sana Serikali iweze kuamua, kama umekwama mahali iweze kuukwamua ili huu mradi uweze kutekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi Dar es Salaam mvua inanyesha. Kwa Wabunge wote wa Dar es Salaam; wa Majimbo pamoja na wa Viti Maalum hakuna mtu anaweza kurudi Dar es Salaam sasa hivi kutokana na mambo yanayoendelea. Barabara ni mbovu, zimejaa maji, mafuriko yanaendelea na wananchi wanadhani kwamba labda sisi tumekaa huku hatufuatili kitu chochote wala hatusemei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba na kwa sababu tuliahidi, tuliahidi katika kampeni na lilikuwa ndiyo jambo kubwa, wananchi waliomba kwa kusema kwamba, sisi tunaomba miundombinu. Tukaahidi kwamba tutakapopata tu nafasi, miundombinu itaanza kutekelezwa; na tulikuwa na mradi wa *DMDP* ambao ulianza, lakini sasa hivi haupo tena.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, haya ambayo nimeyasema kuhusiana na fidia pamoja na mradi, naomba sana sana uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.
(Makofi)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa, Bonnah Ladislaus Kamoli. Mheshimiwa Joel Luhaga Mpina. Mheshimiwa Mpina yupo?

MBUNGE FULANI: Hayupo.

SPIKA: *Okay.* Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Endelea Mheshimiwa, utafuatiwa na Mheshimiwa Ishengoma.

MHE. IDDI KASSIM IDDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipatia leo nafasi hii ya kuchangia. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala naomba niipongeze Serikali kwa mambo makubwa na mazito kabisa ambayo yamefanyika ndani ya miaka mitano iliyopita na ambayo kwa sasa yanaendelea kufanyika kwa Awamu hii ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumesomewa mpango hapa na hotuba ya Waziri Mkuu kwa ajili ya bajeti ya Waziri Mkuu. Hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu ni hotuba iliyoshiba kweli kweli; imeeleza wapi tumetoka na inatuelekeza wapi tunaenda. Niseme kwamba katika hotuba hii ya bajeti Waziri Mkuu ameelezea mambo mengi na nijikite kuelezea mambo machache.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuelezea mradi wa Julius Nyerere. Mradi huu wa Julius Nyerere ni mradi muhimu sana na niseme tu kwa niaba ya wananchi wa Msalala, tunaunga mkono Serikali ili mradi huu uende ukatekelezwe na ukamilike. Kwa hiyo, tunafahamu *the cheapest source of energy* kwenye nchi hii ni umeme unaotokana na maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia gharama ya sasa ya umeme, wananchi wetu wanalia huko; *unit* moja kwa sasa ni shilingi 100/=, lakini ukiangalia manufaa ya mradi huu utakapokamilika, uzalishaji wa *unit* moja katika mradi huu wanaenda kutumia kiasi cha shilingi 36 kuzalisha *unit* moja. Maana yake nini? Ni kwamba itaenda kushusha gharama ya uzalishaji kwenye viwanda na pia itashusha gharama ya *unit* kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme, japo mradi huu utaenda kukamilika, niipongeze Wizara ya Nishati, inafanya kazi kubwa. Katika Jimbo langu la Msalala ni ukweli usiopingika kwamba watu wa Nishati wanafanya kazi kubwa, lakini kuna baadhi ya maeneo umeme huu haujafika. Wananchi wa Msalala tunapoona mtu anasimama na kuupinga mradi huu, tunashikwa na hasira kwa sababu Jimbo la Msalala lina Kata 18 na Kata zaldi ya 12 hazina umeme. Kwa hiyo, matarajlo yetu ni kwamba mradi huu wa *REA* /ambao kimsingi utaenda kukamilika, ni kwamba baada ya mradi huu wa Mwalimu Nyerere kukamilika tutakuwa na umeme wa uhakika lakini pia nasi wananchi wa Jimbo la Msalala tutanufaika na nishati hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la kilimo. Katika Kata 10 katika Jimbo langu la Msalala ni wakulima wa mpunga. Kuwepo na ukamilishaji wa mradi huu na uwekwaji wa umeme katika Kata zetu hizi utachochaea uchumi kwa wakulima. Maana yake nini? Wakulima wataweza sasa kuchakata na kuongeza dhamani ya mazao hayo katika maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la madini. Nimeona hapa imeelezewa na ninaipongeza Wizara imefanya kazi nzuri sana kwenye Sekta ya Madini. Namwomba Mheshimiwa Waziri Dotto hapa, sisi tunaotoka katika maeneo ya migodi, Mheshimiwa Bonnah Kalua amezungumza hapa, kuna masuala ya fidia ambayo kimsingi imekuwa ni tatizo katika maeneo yetu haya.

SPIKA: Mheshimiwa, anaitwa Bonnah Kamoli.

MHE. IDDI KASSIM IDDI: Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

SPIKA: Eeeh! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. IDDI KASSIM IDDI: Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la fidia kwenye eneo langu. Tunatambua ya kwamba kuna mgodi umeanzishwa pale katika eneo letu Kata ya Bulyanhulu ambao ni mgodi wa Bulyanhulu. Baada ya hao watu kuanzisha mradi pale kuna watu mpaka leo toka mwaka 1966 hawajalipwa fidia ya ardhi yao. Naiomba Wizara na Serikali kuhakikisha ya kwamba tunamaliza tatizo hili, kwani ni la muda mrefu sana. Tatizo hili limedumu toka Mheshimiwa Rais Mwinyi akiwa bado ni Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Wizara kwamba sasa tuhakikishe tunatatua tatizo hili la mgogoro na fidia kwa wananchi hao wa Kata ya Bulyanhulu.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, maslahi ya wafanyakazi. Bado kuna wafanyakazi wanadai. Naomba sasa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wameshaanza kulifanya kazi, waharakishe kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale wanapata stahiki zao mapema ili waweze kujikita kwenye shughuli za uchumi na kutumia fedha hizo katika mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la maji. Tuna miradi ya maji katika Jimbo langu la Msalala. Ni kazi nzuri inafanywa na kaka yangu Aweso, lakini namwombwa Mheshimiwa Aweso aweze kuharakisha mradi wa maji unaotoka Mangu mpaka llogi uweze kukamilika. Baada kukamilika sasa waanze usambazaji wa maji mara moja katika Kata ya Ikinda, Kata ya Runguya na Kata ya Segese ili wananchi wale nao waweze kufaidika na huduma hii ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la barabara limekuwa ni mtihani. Wabunge wengi wanalia hapa kuhusu suala la TARURA, lakini mimi naweza nikasema ni jimbo langu la Msalala ni jimbo ambalo lina miundombinu mibovu sana

katika. Leo hii tunapozungumza hapa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa kampeni, tuliahidiwa kupata barabara mbili zenye kiwango cha lami. Kuna barabara inayotoka Geita - Bukori - Kata ya Bulyanhulu – Kahama. Barabara hii tuliahidiwa kujengwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba niikumbushe Wizara kwamba wakati Serikali inaingia makubaliano na mgodi huu wa Twiga, moja ya makubaliono ambayo walikaa wakakubaliana ni kuhakikisha kwamba wanatenga kiasi cha dola milioni 40 ili waweze kukamilisha barabara hii kwa kiwango cha lami. Fedha hizi zipo, naiomba Wizara husika iweze kuona ni namna gani sasa wanaenda kukaa na kuzungumza fedha hizi zipelekwe ujenzi ili barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, tuna barabara nyingine ambayo inatoka Solwa inakuja Bulige inaenda Ngaya na Kahama. Barabara hii pia imeahidiwa kwa kiwango cha lami. Naendelea kuomba Wizara ione namna gani basi inaweza kuanza ujenzi wa barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna barabara moja ambayo ni ndefu sana ina zaidi ya kilometra 85. Barabara hii inaunganisha Makao Makuu na Jimbo la Solwa. Naomba Wizara ya Ujenzi waone namna gani basi wanaweza kuanza mchakato wa kuihamisha barabara hii kutoka TARURA iende TANROADS ili ingie kwenye matengenezo ya kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuishia hapo, niseme kwamba naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi. Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina, sasa yupo.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nampa

pongezi Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoendelea kuifanya ya Chama chetu cha Mapinduzi akitekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuongea kuhusu afya. Nianze kwa kutoa pungezi kwa Serikali kwa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi hasa kwa kujenga vituo vingi nya afya kwenye Halmashauri zetu na kuboresha Zahanati zetu, Hospitali zetu zote za Rufaa. Ila natoa ushauri kwa sababu unakuta Vituo nya Afya vimejengwa lakini vingine havina watumishi wa afya.

Mheshimiwa Spika, mfano mmoja ni Kituo cha Afya Kisaki ambacho tulipewa hasa na Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli alipotembelea Bwawa la Nyerere; allona kuwa kuna umuhimu wa pale Kisaki kuwa na Kituo cha Polisi na Kituo cha Afya. Kituo cha afya kimemalizika, lakini mpaka sasa hivi hakina watumishi. Kwa hiyo, kuna vituo nya namna hiyo. Naomba vituo nya afya vilivyokamilika ambavyo havina watumishi wa afya viweze kupewa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana kuona kuwa bajeti ya dawa imeongezeka. Ni kweli imeongezeka lakini bado wananchi hawajapata dawa. Bado kuna tatizo la dawa. Nilishaongea na Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dorothy kuhusu dawa na nilifanya ziara kwenye Mkoa wangu wa Morogoro; na ikiwa ni mojawapo ya mikoa mingine kuwa bado tuna tatizo la madawa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, ameongelea kuhusu mambo hayo, kwa hiyo, naomba waichukulie kwa undani tuweze kupata dawa, waweze kutibiwa watu ambao tunaumwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ushauri kuhusu Bima ya Afya. Viongozi wetu walishatuambia kuhusu Bima ya Afya kwa watu wote, naomba nalo walifanyie kazi kusudi liweze kutekelezwa. Jambo lingine ni watumishi wa afya kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kuongelea ni dirisha la wazee. Ni kweli tulisema kuwe na dirisha la wazee, lakini inategemea na Halmashauri na Halmashauri. Wazee wengine wanatibiwa vizuri, wengine bado wanahangaika, wanaambiwa mkanunue dawa na unakuta wazee wengine hawana uwezo. Kwa hiyo, nashauri kuwa nalo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nashauri ni kuwa na maboma hasa kwenye Zahanati. Kwa ile miradi ambayo haijakamilika hasa maboma ya Zahanati naomba yaweze kukamilika na Vituo vya Afya kusudi tuweze kuendelea na miradi mpya kwa kukamilisha miradi ya zamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimekumbana nalo ni chanjo ya watoto wachanga. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Afya aifanyie kazi. Bado kuna matatizo; akina mama wengine wanalamika kuwa watoto wao hawapati chanjo kadiri inavyostahili ambalo ni tatizo kubwa sana. Kama mtoto hajapata chanjo kadiri inavyostahili, anaweza baadaye akapata ugonjwa ambao ungetibiwa kutokana na chanjo. Hilo ni jambo ambalo nimekutana huko vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasiyoambukizwa nayo sasa hivi imekuwa ni tatizo. Naomba ifanyiwe utafiti na jinsi ya kuyatibu tuweze kuepukana na magonjwa haya ikiwepo kisukari, kansa, magonjwa ya ini pamoja na magonjwa ya moyo. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kuwa elimu iweze kutolewa kwa wananchi pamoja na kuona jinsi ya kuepukana na hili, lakini na utafiti uweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, nikiwa bado kwenye mambo ya afya; tumeingia kwenye *Covid* tumesahau kuwa bado UKIMWI upo. Naomba suala la UKIMWI, ingawa tuna Kamati ya UKIMWI, ifanyiwe kazi, elimu izidi kutolewa kwa sababu sasa tumekwenda na *Covid*, tumesahau UKIMWI bado upo. Kwa hiyo, naomba iangaliwe sana kuwa UKIMWI bado upo.

Ndiyo sababu uliunda Kamati ya UKIMWI ukijua kuwa UKIMWI bado upo.

Mheshimiwa Spika, wananiambia ni Kamati ya Mambo ya UKIMWI, siyo Kamati ya UKIMWI. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilindie muda wangu, huyu Shangazi ananisumbua. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, elimu; naishukuru Serikali kuwa kwa kweli imefanya vizuri katika mambo ya elimu.

SPIKA: Mheshimiwa Shangazi usimsumbue Mheshimiwa Ishengoma. (*Kicheko*)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya vizuri kwenye mambo ya elimu, elimu bila malipo hasa kwa upande wa ada, lakini tatizo bado lipo kwenye chakula hasa kwa shule za msingi na sekondari zile za kutwa ambapo hawapati chakula cha mchana.

Naomba hilo lisitisizwe kwa sababu bila ya kupata chakula huwezi kuwa na lishe bora na huwezi kufikiria na huwezi kufanya vizuri darasani, kwa hiyo naomba hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, tumetembea kwenye shule za pembezoni bado kuna tatizo la Walimu, kwa hiyo naomba nalo liangaliwe ingawaje wataajiriwa wengine, lakini awatoshi bado kuna Walimu ambao wapo tu lakini hawajaajiriwa. Kwa hiyo tunaomba utumishi watoe vibali kusudi Walimu waweze kuajiriwa ambao bado hawajaajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miundombinu bado mingine ni mizuri lakini mingine bado matatizo. Kwa mfano, madawati nashukuru Mheshimiwa Ummy alisema kuwa atanunua madawati, lakini naomba waliangalie watoto wasikao chini waendelee kukaa kwenye madawati. Pia madarasa na nyumba za walimu bado ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi kwa ukarabati wa Shule Kongwe kweli shule kongwe zimekarabatiwa hasa za shule za sekondari, lakini nikija kwenye madarasa ya shule za msingi, bado ni matatizo. Kwa hiyo shule za msingi naomba na zenyewe ziangaliwe katika kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; nashukuru na natoa pongezi ndio, mikopo imeongezeka, lakini bado ni tatizo. Kuna wanafunzi ambaao wamefaulu na unakuta wengine ni wasichana ambaao hawajapa mikopo, wako vijijini, juzi juzi nimekutana na msichana mmoja analia kabisa, wako wengi vijijini, wako wengi mitaani, wamefaulu lakini wamekosa mikopo. Kwa hiyo, naomba vigezo vya mikopo ya elimu ya juu viangaliwe, hata watoto wa maskini ambaao ni hitaji waweze kupata mikopo kwa sababu kweli wengine hawajapata mikopo hiyo. (*Makof*)

Mheshimwa Spika, sekta ya utafiti hasa Vyuo Vikuu; naomba uangaliwe, uweze kutengewa fedha za kutosha na hiyo asilimia moja inayotengewa iweze kutolewa kwa wakati. Mafao ya Walimu wakiwemo Wahadhiri naomba yaangaliwe na hapa naongea kwa pia kwa ajili ya wafanyakazi wote. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake amesema *pension* inatolewa, nashukuru sana, lakini kuna wengine ambaao wanasonda hawapati *pension* kwa muda mrefu, naomba waangaliwe, waweze kupata *pension* zao. Wengine wanatuambia tuwaombee na ndiyo hivyo hapa nawaombea kuwa waweze kupewa *pensions* zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, siwezi kumaliza bila kuongelea miradi ya kimkakati. Namshukuru sana Hayati Dkt. Magufuli, Rais wetu mpendwa, alale mahali pema peponi. Mheshimiwa mama Samia ambaye ni Rais wetu waliungana kwa pamoja na Serikali yetu wakaona miradi ya kimkakati ambayo ilikuwa imekaa kwa muda kabla ya kufanya kazi, sasa imefufuliwa, reli ya mwendokasi ambayo ni *SGR*, inaendelea kujengwa vizuri. Mpaka sasa hivi tumeambiwa ni asilimia 90.3 Dar es Salaam mpaka Morogoro.

Mheshimiwa Spika, sasa nauliza ni lini itaanza kazi hasa hiki kipande cha Dar es Salaam mpaka Morogoro au tutasubiri reli nzima imalizike? Wananchi wa Morogoro wanaisubiri kwa hamu. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aniambie kwa sababu inaenda vizuri na nashukuru sana kwa sababu hiyo reli ya mwendokasi ikiisha ambayo ni mradi mkubwa, ambaye haoni aje angalie pale inavyopendeza. Watanzania tunajivunia hii reli ambavyo itapunguza mizigo ambayo inaharibu barabara zetu, pamoja na wasafiri na utalii itakuwa ni kivutio kikubwa na itaongeza ajira kwa vijana wetu na wajasiriamali wote pamoja na kipato kwa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuongelea kuhusu bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, bwawa hili ni kubwa kama tulivyoambiwa ambalo litaweza kutoa umeme wa kutosha ambao...

SPIKA: Ahsante

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunawashukuru, waendelee iweze kukamilika ili tufaidikea kwa hilo. Nashukuru kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Ahsante Dkt. Christine Gabriel Ishengoma. Nilishakutaja Mheshimiwa Luhaga Mpina, utafuatiwa na Mheshimiwa Kunambi na Mheshimiwa Dkt. Kimei ajilandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza baada ya uchaguzi wa mwaka 2020, nikushukuru sana Chama changu cha Mapinduzi na wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa, kwa kunirejesha tena Bungeni kwa mara ya nne. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe na Naibu Spika mnavyoliendesa Bunge vizuri sana. Sasa kwa sababu ya muda naomba niongelee Jimbo la Kisesa; jimbo hili lina changamoto nyingi sana; moja ni uvamizi wa tembo ambao umekuwa ni wa muda mrefu. Wananchi wanavamiwa na

tembo, mazao yao yanaliwa yakiwa shambani na hata yakiwa nyumbani. Chakula kinaliwa mashamba yote yanakanyagwa, watu wamepoteza Maisha, wengine wamepata vilema vyta kudumu. Tumelalamika sana na tumeomba sana Serikalini kulitatta hili tatizo, lakini leo miaka miwili, mitatu sasa wananchi hao bado wanaendelea kwenye dhiki kubwa sana ya uvamizi wa tembo, lakini huu uvamizi wa wanyama wakali pia upo kwenye maeneo mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni muda mrefu sana na tumekuwa tukipeleka haya malalamiko Serikalini na hajjatatalia mpaka sasa hivi ambao imepelekea umaskini mkubwa sana kwa wananchi, tunaomba sasa kwa mara hii tatizo hili lifike mwisho. Tunajua Serikali ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita imetatta mambo mengi yaliyokuwa yameshindikana, imeweza kutatta mambo makubwa, haiwezi kushindwa kuwazuia tembo. Tumeweza kumaliza mambo ya rushwa na ujisadi, tumeweza kumaliza madawa ya kulevyta, tumeweza kumaliza ujambazi na ujangili, tumeweza kumaliza uvuvi haramu, tuje tushindwe na tembo; hapa kuna mtu mmoja tu ambaye hajawajibika sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunataka safari hii wananchi waishi kwa amani katika maeneo yao na tatizo hili tembo Mheshimiwa Waziri Mkuu, aagize likomeshwe mara moja. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mpina, Waheshimiwa Wabunge wa Zanzibar wanashangaa kwamba jimbo limevamiwa na tembo, endelea kuchangia Mheshimiwa.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo pia kubwa sana la wananchi wafugaji ambao walikuwa wanafuga wakakamatwa na wahifadhi kwamba wanachungia ndani ya hifadhi na baada ya hapo wakakatiwa rufaa wakaenda kushinda kesi mahakamani, zaidi ya wafugaji 30 wenye ng'ombe wasiopungua 5,000, ng'ombe wao mpaka sasa hivi wanashikirwa na Serikali, licha

ya kushinda kesi mahakamani. Wamefuatilia Serikalini kurudishiwa mifugo yao kwa sababu wameshapewa haki hiyo na mahakama kwamba warudishiwe mifugo yao, lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza ng'ombe hao hawajarudishwa.

Mheshimiwa Spika, sababu za kutorudishwa hazijulikani, mtu ameshinda kesi mahakamani, kwa nini uendelee kuzuia mifugo yake? wafugaji ukichukulia wa sehemu zingine mbalimbali lakini wa jimboni kwangu tu peke yake ni ng'ombe zaidi ya hizo 5,000 wa Jimbo la Kisesa ni zaidi ya 1,000 ambao mpaka sasa hivi zinashikiliwa licha ya wananchi hao kushinda kesi mahakamani. Wananchi akina Malimi Sendama na wenzake Ndatulu Malolo, Kwandu Malaba, Masunga Muhamali, Subi Maduhu na wengine ng'ombe 5,000 wanashikiliwa.

Mheshimiwa Spika, tunataka tuambiwe huko Serikalini aliyekataa hawa ng'ombe wasitolewe ni nani? Kama mahamaka imesha-*granthaki* ya hawa wafugaji, aliyekataa huko Serikalini ni nani? Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alilingilie kati suala hili, tukatende haki kwa hawa wananchi wanyonge ambao mifugo yao imeshikiliwa na Serikali licha ya wao kushinda kesi mahakamani. Tukitoka kwenye hili Bunge niende na hao ng'ombe wa wananchi hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala limezungumzwa hapa, nataka nishauri, suala la ukusanyaji wa mapato. Wabunge wengi wamezungumza hapa mianya mbalimbali, fursa mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato ambayo bado hatujakusanya sawasawa, nami nakubaliana nnalo. Naomba hapa tufanye upya tathmini ya mapato yetu, zile Wizara pamoja na taasisi ambazo zinakusanya mapato na zina vyanzo vingi vya mapato ziende kwenye Kamati ya Bajeti ili tuweze kuyaona maeneo ambayo tunaweza tukakusanya mapato kwa wingi. Hatima yetu na maendeleo yetu yanategemea upatikanaji wa fedha ili tuweze kutekeleza miradi hii ya maendeleo, hatuna njia nytingine ya mkato zaidi ya kutafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita cha Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na mbabe wa vita, Rais wa wanyonge, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tulipiga hatua kubwa sana katika ukusanyaji wa mapato. Ndio maana tukaweza kutoka kwenye kuanzia ukusanyaji wa mapato wa bilioni 850 kwa mwezi mpaka leo tumefikia trilioni mbili kwa mwezi. Tukaenda kwenye maduhuli kutoka bilioni 697 mpaka trilioni 2.4.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato haya umeiwezesha nchi yetu kuweza kugharamia miradi mingi sana, tumeweza kuzuia maeneo ambayo mapato yetu yalikuwa yanapotea. Tumetunga sheria, tumefanya marekebisho ya sheria, tumezua hata ile *transfer pricing* ambayo ilikuwa inabeba mapato yetu mengi sana, tumedhibiti hata *e-risk financial flow* ambayo nayo inachukua fedha zetu nyngi sana tumeweza hata kufuta mikataba iliyokuwa inanyonya Taifa letu mikataba ya *IPTL, Aggreko* lakini *Symbion* iliyokuwa inachukua 719,000,000,000 kwa mwaka, leo tumeweza kufuta mikataba hiyo na Watanzania wanaendelea kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwenye madini ndio maana hapa imezungumzwa, madini, tulikuwa tunakusanya 194,000,000,000; tumefika 500, 000,000,000; kule Mererani baada ya kujenga ukuta, tulikuwa tunakusanya 70, 000,000kwa mwezi leo tunakusanya 3,000,000,000 kwa mwezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Mifugo na Uvuvi tulikuwa tunakusanya 21,000,000,000 tu kwa mwaka, leo tunakusanya 74, 000,000,000 kwa mwaka. Sasa katika kuyafanya haya tumeweza kupiga hatua kubwa sana kwa maendeleo. Nataka niseme na nirudie kusema tena, nawahurumia hata wale ambao wanajaribu kubeza jithada za Serikali ya Awamu ya Tano iliyoongozwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo aliweza kujipambanua na kupata haya mapato, wengine wanasema alikuwa fisadi.

Mheshimiwa Spika, hivi wewe fisadi, ukusanye fedha hizi, ununue ndege za Watanzania wote, huo ni ujisadi! Wewe fisadi, ukusanye hizi, ujenje barabara nchi nzima, ukarabati meli zilizokuwa hazitembe leo zinatembea, Watanzania wanaenda kote wanakotaka, ufufue reli iliyokuwa imelala miaka nenda rudi ya kutoka Dar es Salaam mpaka Arusha! Huyo ni fisadi! Kwa hiyo nawahurumia watu wa namna hiyo kwa sababu fikra zao ni fupi na uelewa wao wa kupambanua mambo ni mdogo sana. Tutaendelea kumuenzi Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kazi kubwa ya maendeleo aliyopigania kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unakimbia sana, nataka niongelee kidogo tu kwenye taarifa ya ukaguzi. Nizi-*alert* hizi kamati zinazoenda kufanya uchambuzi wa mambo yaliyopo kwenye taarifa yenye. Kuna mambo yaliyvoandikwa kwa jinsi yaliyvoandikwa si ya kawaida, kwa mfano ukienda kule maliasili, walipokuwa wanajaribu kuandika fedha zilizoibowi na adhabu za watu wanapaswa kuchukuliwa hatua. Ukienda kule wanasema kuna matumizi ya fedha zinazotoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Utalii, bilioni 34, mwanzo wakasema sehemu ya fedha hizo bilioni 5.7 kama sikosei na bilioni 2.8 na milioni 100, zilihamishwa kupelekwa kwenye taasisi nyingine bila Afisa Masuhuli kujua. Halafu adhabu inayopendekezwa inasema Mkurugenzi wa Utalii pamoja na Mhasibu wake wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, Afisa Masuhuli ambaye hakujua fedha zinahamishwa amekingiwa kifua cha nini? Kwa nini taarifa ya CAGiwe na kinga kwa wahalifu wengine, ukienda huku kwengine, upande mwengine utakutana na fedha 171,000,000 zimetumika kwa ajili ya *bonanza*, halafu milioni zingine kama 148,000,000 zilihamishwa na zenyewe zikatumika bila Afisa Masuhuli kujua, lakini adhabu inayopendekezwa, Waziri wa Maliasili wa kipindi kile, tena akatajwa kwa jina Mheshimiwa Dkt. Kigwangala na Katibu wake wachukuliwe hatua. Katibu Mkuu ambaye ndiye Afisa Masuhuli ambaye huyu Waziri aliandika dokezo, lakini waliyoidhinisha fedha na kutoka ni Katibu Mkuu na Ma-CEO hawa, kwa nini taarifa hii inawakingia kifua?

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Mpina pokea taarifa ya Mheshimiwa Kingu

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyeketu mkubwa, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa anayezungumza, kwanza hatujaanza bado kujadili ripoti ya *CAG*. Bunge hili ni Bunge la utaratibu, ni Bunge linaloongozwa kwa misingi ya utaratibu, lakini hata sivyo, tusubiri hoja za Serikali zitakapokuwa zimejibowi, tutakuja kuanza kuteteana humu, lakini si sasa hivi. (*Makof*)

SPIKA: Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Mpina.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, sipoeki taarifa yake na najua ninachokizungumza. Sasa hivi Kamati zetu za *PAC* na *LAAC* zimeipokea hii taarifa, zinaenda kufanya uchambuzi juu ya hizi taarifa. Zinapoenda kufanya uchambuzi sisi Wabunge hatujazuiwa kuzi-*alert* mambo yaliyomo humu, ziende zikayaangalie. Wewe jana ulikuwa unazungumza *ATLC* na unazungumza taarifa ya *CAG*, ulikuwa unazungumzia taarifa gani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niongeze muda kidogo niongeze nimalizie.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Tunaendelea, Mheshimiwa Mpina inatosha, muda hauko upande wetu.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Amemaliza dakika yangu huyu.

SPIKA: Mheshimiwa Kunambi.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe binafsi, lakini katika mambo ambayo

Watanzania hawatamsahau Hayati Magufuli ni pamoja na mapinduzi makubwa ya fikra. Yapo mambo tunayosema yanaonekana kwa kuona, lakini jambo kubwa ni mapinduzi ya fikra za Watanzania. Ndio maana *come rain come fire*, kamwe hatuwezi kuwabadilisha Watanzania vile wanavyomwamini Hayati Dkt. Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kwa habari ya mapato. Tunapozungumzia utelekelezaji wa miradi ya maedeleo ni lazima tuangalie pia suala zima la mapato, suala la mapato ni jambo mtambuka na sio kazi peke yake ya Wizara ya Fedha na *TRA*. Naomba nieleze hapa ili tuone namna gani tunaweza kupata fedha kwa ajili ya miradi yetu ya maendeleo. Wengi tunasema barabara, maji, umeme, kama tutasimamia vizuri na kama tutakusanya vizuri mapato, kamwe hatufanikiwa; nazungumzia suala mtambuka maana yake ni.

Mheshimiwa Spika, Wizara za kisekta zina jukumu kubwa sana kufikiri tofauti kuongeza *tax base* ya Taifa. Ninavyozungumzia *tax base nazungumzia* wigo wa mapato ili tuondokane na mazoea ya vyanzo vilevile tulivyovizoea. Mathalani unavyoongeza tija kwenye sekta ya kilimo maana yake utaongeza *tax base*, unavyoongeza tija kwenye viwanda na biashara unaongeza *tax base*, unavyoongeza tija kwenye utalii utaongeza *tax base* na kwa kuwa nina nafasi ya kuchangia wakati tunachambua hizi Wizara moja baada ya nyngine nitaeleza kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, eneo linguine, jambo kubwa lingine kubwa ambalo Hayati Dkt. Magufuli ambalo amelifanya ndani ya Taifa letu ni kuhamisha kwa vitengo Makao Makuu ya Nchi kuhamia Dodoma. Labda tu Waheshimiwa Wabunge nieleze kwa ufupi ya harakati za kuhamishia Serikali Dodoma. Mnamo mwaka 1966 aliyekuwa mdogo wake Hayati baba wa Taifa, Joseph Nyerere alipeleka Muswada Bungeni wakati huo wa kuitangaza Dodoma kuwa Makao ya Nchi, lakini baadaye Mkutano Mkuu...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, baadaye

SPIKA: Kila wakati mie nawaomba ukisikia kelele wewe peke yako tu anza kupunguza na mwingine na mwingine.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, baadaye Mkutano Mkuu wa *TANU* mwaka 1973 uliamua rasmi sasa Makao Makuu ya Serikali yawe Dodoma. Lakini zipo jitihada zilizofanyika na hayati Baba wa Taifa, pamoja na kuanzisha Wizara ya Ustawishaji wa Makao Makuu mwaka 1973 ambayo Waziri wake wa kwanza alikuwa Adam Sappi Mkwawa, *Retired Speaker* wakati huo akisaidiwa na *Sir George Kahama* kama *Director General* wa *CDA*.

Mheshimiwa Spika, na walifanya kazi kubwa sana; unavyoliona *Area C* ya leo, unavyoliona *Area D* ya leo, unavyoioana Uzunguni ya leo, ni kazi ya Adam Sappi Mkwawa na Sir George Kahama wakiongoza Wizara ya Ustawishaji wa Makao Makuu ya Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili limechukua muda, baadaye akaja mzee Samuel Sitta, hatimaye mama Anna Abdallah alihudumu kama Waziri na baadaye mchakato uliendelea kwa sabbau ya changamoto ya vita mwaka 1978/1979 ya Nduli Idd Amin, kidogo *political will* ya kuhamisha Serikali ilipungua kwasabbau uchumi wa nchi yetu ulipita katika kipindi kigumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, amekuja kutimiza ndoto za Hayati Baba wa Taifa. Leo hii sisi wote Wabunge tuliomo humu ndani ni wadau wa Makao Makuu ya Nchi. Na yapo mambo makubwa yamefanywa na Serikali ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Hayati sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii unavyoitazama Dodoma, angalia sekta ya barabara, sekta ya afya, miundombinu mbalimbali, unaiona Dodoma kwa kweli ni makao makuu kwelikweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nishauri jambo kwasababu Mheshimiwa Rais wetu mpendwa wa sasa wa Serikali ya Awamu ya Sita, mama yetu Samia Suluhu Hassan – na ndio maana kauli mbiu yake inasema kazi iendelee. Maana yake pale alipoishia Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yeye sasa anaendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyohiyo, leo hii kama siyo mashahidi hapa Waheshimiwa Wabunge, tumeanza kupata changamoto sasa hapa Dodoma za huduma mbalimbali, hasa huduma ya maji, ukienda umeme kidogo na maeneo mengine. Naomba nishauri Serikali; changamoto hii inaletwa na changamoto kubwa ya uratibu wa namna ya kujenga Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, leo hii utaona watu wa *RUWASA* wana bajeti yao, watu wa *TARURA* wana bajetyi yao, Jiji la Dodoma lina bajeti yake. Kwa hiyo, taasisi zote hizi za Serikali kila mmoja anapanga kivyake. *TANROADS* naye ana mipango yake, hatuwezi kutoka, hatuwezi kusogea. Na ndio maana leo hii utaona huna wa kumuuliza.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wnagu, changamoto hii ya uratibu wa makao makuu ya nchi, nishauri jambo ikiipendeza Serikali, kwa kuwa Mheshimiwa Rais wetu aliyeo sasa anaendeleza kazi iliyochwa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ushauri wangu; ni lazima tuwe na chombo cha uratibu kinachoweza kuzifanya taasisi hizi zote za Serikali zizungumze pamoja. Kazi ni ndogo sana, zizingumze pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unapozungumzia suala la umeme, pamoja na uwepo wa Jiji la Dodoma, chombo hiki kitakutanisha taasisi zote hizi za Serikali hapa Dodoma, na kazi yake ni kuratibu. Sasa inategemea vile Serikai itakavyoona inafaaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano wenzetu Uganda. Ukienda Uganda wana chombo ambacho wanakiita *Ministry*

for Kampala Capital City na Waziri wake wa sasa anaitwa Bi. Betty Amongi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Nairobi wenzetyu wana Nairobi *Metropolitan Ministry* ambayo Waziri wake wa sasa anaitwa Bw. Kamau, lengo kubwa hapa ni kufanya – na hakuna gharama, naomba nishauri Serikali – hakuna gharama ya uendeshaji wa chombo hiki, ni uratibu. Kinachoongezeka ni hawa watu kwenye chombo lakini bado taasisi zinaratibiwa kwa bajeti zao isipokuwa sasa chombo hiki kinafanya hizi taasisi zote zzungumze lugha moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kinyume cha hapo, wakati wangunikiwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma tuliweza kufanya yale tuliyoyafanya. Unajua, niseme tu mtakuja kuyaona haya baadaye. Tuliona mambo yanakwenda vizuri, siyo bure, utashi wa mtu katika utendaji wa Serikali hauwezi kuwa *sustainable*. Na ndiyo maana nashauri hili, tuwe na mfumo mzuri kwa ajili ya kuhakikisha kweli tunakwenda kujenga Makao Makuu ya Nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimpe elimu kidogo dada yangu, Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, maana mtoto akichezea wembe muache umkate. Alivyokuwa anasema Serikali anasahau kwamba kuna sheria ya asilimia 4.4.2 iliyopitishwa hapa Bungeni. Unavyosema vijana wapewe asilimia kumi zote *determinant...*

Mheshimiwa Spika, kumradhi, *determinant...*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ya pili tayari Mheshimiwa, nakushukuru sana.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Lakini kwa Habari...

SPIKA: Ahsante sana; dakika kumi ni chache.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, siyo mbaya naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Hata hivyo nakupongeza kwa kukumbushia na kupigia mstari suala la Dodoma Makamo Makuu ya Nchi kwasababu ni katika *achievable* kubwa sana za Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Naona watu wanachangia tu bwawa na nini lakini Makao makuu Dodoma hawasemi, hiyo nayo ni moja ya mambo ambayo ni *fundamental* kwelikweli. Maana kabla yake haikuwezekana lakini sasa Dodoma Makao Makuu, nafikiri mnanielewa. (*Makofii*)

Nilishakutaja Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, utafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona na kunipa fursa hii nichangie kwenye mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameanza kazi yake vizuri, amerejesha amani na matumaini mapya kwa watu wengi. Lakini pia kwa kuzingatia kwamba ametuambia tunaendeleza yale yallyioanzishwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, na tunaamini pia kwamba kwa jinsi ambavyo tunmfahamu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ataongeza hata ile kasi ambayo tunaipokea.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba kielelezoo kikubwa cha kuonesha kwamba kweli Mheshimiwa Rais wetu anatekeleza kama anavyoahidi ni timu ya Mawaziri aliyweka kumsaidia yeye, akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amekuwa ni kichocheo kikubwa na naamini kwamba ataendelea na kasi ileile, ataendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa namna hiyo lakini pia na Mheshimiwa Makamu wa Rais aliyechaguliwa, naamini wote ni watu poa kabisa, siyo poa, ni bomba kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naamini tukiangalia timu iliyopo mtu anapokwenda kwenye kiwanja cha mpira unaangalia kwamba amebeba timu gani na yeye ameingia kwenye uwanja huu akiwa amebeba timu ya Yanga au ya Simba? Ya Yanga tuseme, lakini itabadiilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hivi; nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wake mzuri, wa kina na unaoeleweka, ripoti ambayo imeandaliiwa kweli kitaalam na ina-cover kila kitu ambacho mtu unataka kuona. Lakini nimpongeze zaidi kwa jinsi ambavyo amesimamia shughuli za Serikali kwa miaka hii yote ya Awamu ya Tano na mwaka huu ambao tumeanza na jinsi ambavyo amejitoa kutembea kwenye maeneo mbalimbali, na nina matumaini kwamba kule kuona kwake kumesaidia sana kusukuma utekelezaji wa miradi na mikakati ambayo ilikuwa imewekwa mbele yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimpongeze na niseme kwamba tunaamini na mimi naamini kwamba hatasahau kutembelea Vunjo. Na ninaamini pia kwamba Mheshimiwa Rais kule Vunjo hatujaona viongozi wa kitaifa wa kubwa kwa miaka mingi, takribani miaka saba – naamini tutaanza kuwaona pia kule wajue kwamba kule pia sisi CCM tumejipanga vizuri na tumejipanga kwa safu ambayo italeta maendeleo kwa jimbo letu sana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe na Naibu Spika kwa jinsi ambavyo mnatuweka pamoja na kutupa fursa na kujua ni yupi aseme saa ngapi na kadhalika. Nawapongeza sana, naamini naona ufahari sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba huu utani wa darasa la saba na maprofesa siyo mzuri sana. Kule nilikotoka mtu anajulikana kwa kazi na umuhimu wake na wote tuna kazi moja ya Ubunge, hatujuani kwa elimu tulizonazo na elimu tulizonazo hazina maana yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapofika hapa tupeane heshima kwamba wewe uko darasa la saba au gumbaru umetoka huko we don't care unajua kusoma na unaweza

kuchangia vitu vizuri. Naamini kwamba sisi kila mtu ana nafasi yake lakini tusianze kuingiza utani, utani huo ni mzuri lakini, hasa Mheshimiwa Musukuma akiwepo...

SPIKA: Haya, sasa endelea na hoja Mheshimiwa Dkt. Kimei.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Endelea na hoja iliyopo Mezani.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, niache Mheshimiwa.

SPIKA: Ukiwachokoza nawajua hawa, endelea tu Mheshimiwa Dkt. Kimei. Ukiwachokoza darasa la saba utatafuta mlango wa kupitia.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nawafahamu, nawafahamu sana. Nawafahamu na ninawapenda sana lakini...

SPIKA: Maana yuko Rafiki yangu mmoja, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, alikosa kuona mlango wa kupitia baada ya kuwagusa darasa la saba. Ndiyo maana nasita, usije ukawagusa huko Vnjo watakuvunja mguu, endelea tu na hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, darasa la saba waache.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Niseme hivi; kuna jambo moja ambalo linatakiwa liangaliwe kwa ujumla, hasa kwenye hii nyanja ambayo inahusiana na mambo ya uajiri wa wafanyakazi serikalini na kadhalika. Ni suala zima la kutathmini skimu ya mishahara ili kuiweka bayana ili mtu kama ni profesa atake kukaa kwenye uprofesa wake. Lakini ukweli ni kwamba mtu anaafuata pale penye maslahi, lakini kuna wengine tunakuja hapa kwa sababu tunataka kutekeleza mambo fulani fulani kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, na ninataka kusema kwamba ninashauri kwamba skimu ya mishahara iangaliwe ili stadi zile ambazo ni *rare professions* na kadhalika na ambao tunataka wabaki kule kwenye *specialties* zao waweze kufanya utafiti, walete *innovation*, wasaidie nchi hii kwenda *forward professionally*, tuweze kuwabakiza kule zaidi kuliko kuwatoa na kuwaleta kwenye siasa na kuwavutia kwa sababu huku kuna maslahi mazuri mengine, lakini naamini kwamba tutaaingalia hili ili mambo yaye vizuri zaidi na watu wakae kwenye *professions*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ninataka kuchangia kwenye maeneo matatu; eneo la kwanza kabisa ni eneo la utawala bora, utawala bora unaendana na *span of control*. Sasa imekuwa kwamba kuna halmashauri nyingine ambazo ni kubwa sana, zinaweza zisiwe kubwa sana kwa maeneo lakini kwa wingi wa watu.

Mheshimiwa Spika, sasa kama halmashauri ni kubwa sana, zaidi ya watu laki tatu, inakuwa ni ngumu sana kusema kweli halmashauri ile kutenda kwa kuwafikia watu ambao tunataka tuwafikie kwa karibu, tuwapelekee elimu ya uvezeshaji na tuwasaidie kwa kuwaonesha kwa vitendo. Lazima halmashauri hizi zinagaliwe ili kama zinaweza zikapangwa kivingine zipangwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais Hayati wetu, mpPENDWA wetu, JPM, alipokuja kwetu alisema kwa mfano tuwe na Halmashauri ya Himo, alikubaliana na hilo. Na ninaamini kwasababu naunga mkono mambo mengi nasema Mungu atujalie na Mheshimiwa Rais wetu mpya, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aweze kukubali pia twende na Halmashauri yetu ya Vunjo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, nataka nizungumzie suala la Kamati ya UKIMWI kudhibiti UKIMWI. Naomba hii ijiongeze kidogo na kuhusu la gongwa la *COVID*, ninaomba hii Kamati iingize masuala hayo kwenye mchakato wake ili tuweze kujua tunapoendelea huko mbele na tuweze kudhibiti, siyo tu UKIMWI, kwasababu UKIMWI naamini tumeshaanza kuu-

contain na mtu ambaye kweli amejipeleka hovyohovskyo natumaini ni... lakini ukweli UKIMWI kwenye *rate ya three to five percents*yo mbaya, *at least* tunaweza tukadhibiti. Lakini naamini kwenye magojwa haya mapya yanayojitokeza, hasa *COVID*, pia tuangalie.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, niseme kwamba kwenye suala zima la *COVID Private Sector Foundation* ilitoa mchango wake, ilifanya utafiti wkae kuhusiana na athari na ninaamini kwambs Serikali itaendelea kusoma na kuona mapendekezo gani yalifanyika hususan kwenye sekta ya utalii, kwamba sekta ya utalii iliathirika sana na ukiwaambia kwamba walipe tozo zile walizokuwa walipe *NGOs fees* ambazo ni *fixed*, waendelee kulipa wakati hawajawa na watalii, zitakufa. Hawataweza kuendelea. Kwa hiyo, tukasema kwamba wale waangaliwe kwa namba yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na siyo sekta ya utalii tu, na sekta nyininge pia zimeathirika lakini ile ripoti najua ilikuja Serikalini na tunaomba kwamba Serikali iisome tena ione kama inaweza ikaitumia ili kuweza kupunguza makali ya gonjwa hili. Kama kwetu halipo limekuwa nje kwa hiyo, limeathiri wale wateja wet, na kadhalika. Lakini nataka kusema kwamba ni lazima tuangalie namna ya kusaidia watu.

Mheshimiwa Spika, suala la uvezeshaji. Uwezeshaji naamini kila Mbunge hapa amejipanga kwa namna moja kwasababu hii miundombinu tunayoijenga haitakuwa na maana kama haitatumwiwa kuzalisha, na ndiyo sababu moja nasema lazima tuangalie kwamba tumejenga barabara, ni kitu gani kimetokea hapo kwenye barabara.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na *Central Corridor Programme* ambayo ilikuwa isaidie ku-*develop* vitu fulani fulani *along the central corridor* ya *railway* na ile *railway* baadaye iweze kuwa na tija zaidi na watu wengi wanavutiwa na jambo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji ni jambo la msingi lakini kuna masuala ambayo lazima tuyaa galie. Kwanza ishu ya *finance* kama alivyosema mwenznagu, kwamba mtaji ni kitu kikubwa. Sasa mitaji tunayotegemea, kwa mfano ukiwa kwenye halmashauri, haijawa *revolving fund*, mtu anachukua mkopo lakini ukiuliza ni mingapi imerejeshwa kwenye halmashauri wale waliokopa utakuta kwamba urejeshaji ni *very low*.

Mheshimiwa Spika, ndio sababu inakuwa kila mwaka lazima uingize hela mpya na ukiuliza leo hela ya kukopesha ni ngapi watakwambia ni ile waliyopokea mwaka huu, hawakwambii ukichanganya na ile ambayo tumekopesha mwaka jana ikarudi na hii ambayo leo imetolewa tunaweza tukakopesha mara tano, haijatokea namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kwasababu kuna *weakness* kwenye *level* ya halmashauri kutoa ile mikopo, ile mikopo inatolewa na watu ambao kwanza ni wale maafisa maendeleo wako wachache, hawana *staffwa ku-follow up*, hawashirikishi sana watu wa kwenye vijiji.

Kwa hiyo, ikiwa kama mtu amechukua mkopo ijulikane anatumia kwa njia ya uzalishaji na kadhalika, kwa hiyo inatokea kwamba yule mtu anayechukua hela hawezi hata kuitumia vizuri na anakuwa hajaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba ni vizuri hizi hela halmashauri...

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kimei, tunakushukuru sana.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Dakika kumi zimekwisha kweli?

SPIKA: Eeh, tayari kabisa. Tayari, sasa Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kwamba hata kama umezungumza bado unaweza kuchangia kwa maandishi. Kama hujaongea bado unaweza ukachangia kwa maandishi, huenda usipate nafasi, lakini pia kama pointi yako ina msisitizo maalum, hata kama umechangia humu ndani bado unaweza ukachangia kwa maandishi ili tuhakikishe kwamba ujumbe wako unafika sawasawa Serikalini.

Na *tablets* zetu zina hiyo *facility* ya kuweza kuchangia kwa maandihi. Kwa hiyo, *as we sit here* bado unaweza ukawa unaendelea kuweka sawa, naamini kabisa tunaweza tukafanya hivyo kwasababu inaelekea kama hatutumii sana hiyo *facility*; kifupi tu unaweka mawazo yako.

Mheshimiwa Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi, Dkt. Pindi Chana.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kuweza kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninapenda kuikumbusha Wizara hii mwaka 2017, 2018, 2020 kuja 2021 tulizingumzia suala la bima ya afya kwa wote. Taifa lisilokuwa na watu wenye afya haliwezi kuingia kwenye uchumi wa kat. Taifa ambalo lina wazee wengi walitolitumikia lakini hawana bima ya afya kuwasaidia hatuwezi kuwatendea haki wazee hao walitolumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini taifa lenye watoto wenye siku moja na miaka mpaka mitano wasiokuwa na bima tunawaweza katika matatizo makubwa sana ya kiafya na hatima yake hatuwezi kupata Watanzania ambao watatumia akili zao kwa sababu afya zao zina mgogoro na hawana bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara, kwa sababu Wizara ya Afya ilizungumza kwenye bajeti ya 2017/2018, kwamba wataleta bima ya afya, na wewe ulisisitiza sana;

tunaomba tafadhali sana tulete kwa hati ya dharula tuweze kupata bima ya afya kwa wote, maana bila afya kuna mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kuna magonjwa ambayo hayaambukizi. Leo hii tuna watu wengi wenye magonjwa ya kisukari, tuna watu wenye magonjwa ya figo, gharama zake ni kubwa sana. Tunaomba Watanzania hawa wawekewe bima ya afya maana ni haki yao ya kimsingi kuhakikisha afya zao ziko salama.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kilimo. Asilimia themanini ya watu na wananchi wa Tanzania ni wakulima, na kilimo ni uti wa mgongo. Ninafahamu na ninamkumbuka Baba wa Taifa kwa kauli mbiu hii kwa Watanzania wote. Leo hii tunapozungumzia kilimo tunategemea kilimo kinachotegemea mvua pekee. Ninaomba, sasa tuna miaka 60 ya uhuru, tunahitaji kuhakikisha kilimo chetu kinakuwa sio kilimo cha chakula pekee kwa maana kwenda mdomoni, tunakataka kilimo cha Biashara.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu tuna ekari nyingi sana hapa Tanzania na Watanzania wengi ni wakulima wanaotumia zana za kizamani. Na wale wawekezaji wanaokuja asilimia kubwa wao wanapewa ardhi ili yobora na wao wana mitaji mikubwa kwa sababu walikotoka wanakopeshwa. Watanzania hawakopesheki kwa sababu hawana vitu vya kuweka kama rehani kule benki na hivyo wanabaki kuwa wakulima wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wangu wa Mbeya tunafahamu Mikoa mitano ya Mbeya, Ruvuma tukienda na Iringa zile *big five* ambazo zilikuwa zinasaidia Taifa hili na kulisha nchi nzima leo hii Benki ya Kilimo inayokopesha wakulima ipo Dar es Salaam na wala haipo Mbeya, wala haipo Ruvuma, wala haipo Iringa. Tunaomba tuifanye benki, hii ni benki ya wakulima...

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:... wakulima wetu wanalima, leo hii tunalima parachichi, Wakenya wanakuja kununua parachichi.... (*Makofi*)

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Pokea taarifa Mheshimiwa Kagenda

TAARIFA

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa mse maji kwamba Benki ya Kilimo ipo Mkoani Mbeya pale mjini karibu na Bojan na imetenga mwaka huu bilioni 17.8 kwa ajili ya Mkoa wa Mbeya. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika

SPIKA: Mheshimiwa Mwakagenda, pokea taarifa, kumbe huna habari

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ninayo habari, hujo ndiye kaka yangu, Amenye, naomba niendeleee.

Mheshimiwa Spika, leo hii mkulima anayelima mchele pale Kyela ambako ni kakangu sasa hivi ametoka kusema, anashindwa kupata mbolea kwa wakati, anashindwa kupata mbolea kipindi cha upandaji wa Mpunga. Anasema habari ya benki kule kwao Mwaya ndugu zake walioko Mwaya hawana hata fedha ya kukopa kwenda kulima mpunga maana kumbuka mpunga wa Kyela ni mpunga bora Afrika hata Nyerere alikuwa anatoa gunia moja la mpunga kwa Wajapan wanatupa gunia kumi leo hii wanakyela hawana hela ya kukopa kwa ajili ya mashamba ya mpunga.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kilimo tunazungumzia pia masoko. Tunalima leo maparachichi ni kweli tunauza sasa hivi Shilingi 1,400 kwa kilo, lakini soko la dunia parachichi moja wanasegeza bei inauzwa kwa bei *at*

least dola moja. Kwa nini Wizara hii ya Kilimo, ndugu yangu Bashe ninaomba utusaidie, kwamba mkulima kutoka shambani asiwepo dalali wa katikati apeleke moja kwa moja Australia akauze na mchumi wa Mtanzania ukapanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia masoko, nazungumzia soko la chai, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Wilayani Rungwe; namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu aliona chai ya Rungwe inauzwa kwa bei ya kuonewa, kwa maana ya kilo Shilingi mia mbili wakati wenzetu wa Njombe wanauza kilo Shilingi mia tano. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifanya kituo chema, unafahamu, ukaweka tume ya kuchunguza kwa nini chai hii inauzwa kwa bei hiyo. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ukija utupe majibu sisi wana Rungwe na Wanambeya ile tume iliishia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia mifugo, mifugo pamoja na mazao yake, nazungumizia suala la maziwa. Leo hii kule kwetu Mbeya lita moja ya maziwa ni Shilingi mia sita, lakini utashangaa sana maji lita moja ni Shilingi elfu moja, mwekezaji wa maji anapata chanzo cha maji anaweka chupa ya plastiki anauza maji kwa Shilingi elfu moja kwa lita moja. Mkulima wa Mkoa wa Mbeya anauza maziwa kwa Shilingi mia sita yeye mkulima ni mtumwa wa ng'ombe, amkatie majani, ahakikishe anamtunza na madawa yake lita moja Shilingi mia sita. Tunaomba Serikali mtusaidie maziwa angalau yapande bei hata lita moja iwe Shilingi elfu moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ngozi. Leo hii watanzania tuna ng'ombe nyingi lakini ngozi imewekwa zile alama sijui zinaitwaje, zinaondoa ubora wa Ngozi. Ninaomba ng'ombe wetu watafutiwe namna nyingine ya kuwatambua ile hali ya kuwachoma ng'ombe maalama tuipunguze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee habari ya miundombinu. Mimi nipo kamati ya miundombinu kwa mara ya kwanza nimeona *SGR* ikiwa imejengwa vizuri, tatizo letu sisi tulikuwa tunalalamika juu ya madeni ya taifa linapokuwa

kubwa hatuoni kazi ikifanyika. Safari hii *SGR* tumekopa na fedha za ndani lakini kazi tumeiona.

Mheshimiwa Spika, pamoja na makofi haya ya furaha tunahitaji kuwajengea uwezo Watanzania kuweza kuitumia reli hii itakapokuwa tayari ili kukuza uchumi wa Watanzania. Ninaomba maeneo yale ambayo reli inapita tuhakikishe tumewawezesha Watanzania wale kujua umuhimu. Si tu hivyo ninaamini reli hii itasaidia yale malori yanayopita kwa wingi hasa njia yetu ya Dar es Salaam, Mbeya, Tunduma ambayo baada ya muda mfupi inaharibika ninaamini sasa watumie reli hiyo iliyo tengenezwa ikiwepo *SGR* lakini na reli ya TAZARA bila kuisahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini sana kwamba kila kitu kikifanywa kwa makusudi au kwa bahati mbaya tunaomba sana sana utunzaji wa mlundombinu hii, tuisimamie kama Taifa kwa umoja wetu. Ninampongeza sana Rais, Rais juzi ameenda kusaini mkataba ule wa Hoima. Tulipitisha sheria kwenye Bunge hili kwamba mkataba wowote ukipitishwa basi uje hapa Bungeni. Mimi ninampongeza sana kwamba *at least* tumemuona ameenda kusaini na sasa tunasubiri atuletee hapa Bungeni na sisi tujue ni kitu gani kizuri hiki Rais wetu amesaini, tunamsubiri na tunampongeza. Lakini Bungeni lazima mkataba huo pia uje sawa sawa na sheria tulioipitisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ninakushukuru sana, ahsante kwa kuniskiliza. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, na hasa kwa kukubali kwamba *SGR* imejengwa kwa viwango, hongera sana Serikali. Tunawashukuru sana, naona hata Salome anashangaa tu, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu Ofisi yake imefanya kazi kubwa nzuri kwenye utekelezaji wa hii llani

kipindi kilichopita tumeona na sisi Watanzania tunamatarajio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nikimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu bila kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu mpPENDWA Mama Samia nitakuwa sijakamilisha itifaki. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpPENDWA Mama Shupavu, Mchapakazi, Hodari na Watanzania tupo nyuma yako Mheshimiwa. Vilevile nitambue maendeleo makubwa ambayo yalifanyika na Baba yetu MpPENDWA Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ilikuwa imefanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naomba niende katika suala zima la asilimia kumi za halmashauri. Katika halmashauri zetu tumekubaliana kwamba tutatenga asilimia kumi kwa ajili ya vijana, wanawake na walemavu. Kwa haraka haraka zipo halmashauri ambazo mapato yake kwa mwaka yanafika bilioni tano; kwa lugha nyepesi ina maana kwa mwaka wanatakiwa watenge milioni 500. Na wakitenga ndani ya miaka mitano unapata *all most* 2.5 bilioni za kukopesha vijana, wanawake na wenyе ulemavu. Kuna Halmashauri mapato yake tuchukulie ni bilioni mbili. Maana yake kwa haraka haraka ni kiwango kisichopungua milioni 200 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinarejeshwa bila riba, lakini hatujasema zile pesa zinazorejeshwa kila mwaka utaratibu wake unakuwaje. Je, zinachanganywa na zile ambazo zinabajetiwa mwaka husika? Na kama kila halmashauri inaweza ikatenga milioni 500 kila mwaka ukachanganya na zile zinazorejeshwa kutoka mwaka uliopita maana yake mfuko huu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uchumi wa kati, uchumi shindani hili ndilo eneo ambalo hata changamoto ya ajira kwa vijana kwa wanawake na walemavu tunaweza tukapata majibu ya kutosha. Kwa hiyo mfuko huu tuungalie vizuri sana; yale marejesho yanapoingia kwenye akaunti *what next?* Kila Halmashauri baada ya kutoa kwa vikundi

wamerudisha, sasa sheria lazima itafsiri, pale ambapo pesa zimerudishwa zinachanganywa na za mwaka huu au utaratibu wake unakuwaje...

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Ndiyo taarifa.

TAARIFA

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba...

SPIKA: Aah sawa, Mheshimiwa ni Viti Maalum Tanga *Engineer*

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Haya.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba kwa mujibu wa ile sheria iliyoruhusu kutumika asilimia kumi imeweka wazi kwamba ile pesa ni *Revolving Fund and The Rollover Fund*. Kwamba hata mwaka *ukipituka* (ukiisha) ile hela itaendelea kuwepo pale na hata marejesho ni sehemu ya mkopo unaokuja. Imeweka wazi kwamba lazima kila Halmashauri ifungue akaunti ambayo pesa zile zitawekwa zote za kwa pamoja na kila zinavyo-*ji-accumulate* inakuwa *next amount* ya kuweza kuwakopesha wengine. Kwa hiyo wasiokuwa wanafanya hivyo hawana akaunti na wala marejesho si sehemu ya mkopo unaokuja wanafanya makusudi kwa sababu zao, lakini ile sheria ipo wazi imeelezwa vizuri sana. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana unapokea taarifa hiyo.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hiyo naendelea kuchangia kama ifuatavyo; na imani dakika zangu zitalindwa.

Mheshimiwa Spika, kwamba fedha hizi zitakuwa ni mkombozi sana kwa makundi haya na ni muhimu sana tukaziwekea utaratibu mzuri. Kwa tafsiri hiyo basi, maana yake halmashauri zetu zinapaswa kuwa na pesa ya kutosha sana. Hatuhitaji vijana waende benki kutafuta mikopo ya asilimia 16 au 20 kumbe kuna fedha hizi ambazo zinatengwa kila mwaka na zinatumika kukopesha pasipo riba. Hatutakiwi kuwa kilio cha kusema kwamba vijana hawana ajira, ni suala zima la Madiwani kuzisimamia hizi fedha vizuri na kuona ni namna gani tunaweza tukasaidia vijana na makundi mengine. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala zima la bima ya afya iliyoboreshwa. Bima ya afya iliyoboreshwa kila kaya ni elfu thelathi na wanatibiwa watu sita hii ni mkombozi mkubwa sana. Maana yake ni kwamba kila mtu ni Shilingi elfu tano kwa mwaka, hii haijapata kutokea. Hizi ni pongezi kubwa sana kwa Serikali yetu ambayo inawalinda wananchi. Changamoto iliyopo hapa mara kwa mara tunapokwenda katika hospitali kufuatia bima iliyoboreshwa kuna shida ya dawa. Eneo hili la dawa lazima tuliangalie tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mara nyingi wananchi tunapozidi kuhamasisha na nimekuwa nikihamasisha mara kwa mara bima ya afya iliyoboreshwa wanapoenda katika vituo vya afya changamoto imekuwa ni dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati umefika sasa wa kulifafanua jambo hili vizuri kwamba bima ya afya iliyoboreshwa ndani yake kuna *component* gani na zipi hazipo ili mwananchi anapokata bima ajue kwamba matibabu yangu yatakuwa ni haya na haya hayahusiki na bima ya afya; vinginevyo tafsiri yake inakuwa ni tofauti, wakiamini kwamba watapa huduma zote nzuri kwa wakati. Na wanapoenda wananchi wetu, na sasa hivi idadi ya watu

ni milioni 60 wakakosa hii huduma hususan dawa katika vijiji vyetu, katika wilaya zetu kwa kweli eneo hili lazima tuwe na majibu. Na tunatakiwa tuwe *transparent* ni namna gani tunaweza kuboresha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala la mahindi, na wananchi wamenituma wa Mkoa wa Njombe na mikoa minge ya kusini na Iringa. Mahindi wanasesma wanalima vizuri sana, wanaweka mbolea, mbegu changamoto ni masoko. Sasa hivi tuna mahindi mengi na tutashukuru sana tukipata *delegation* ya NFRA hata kesho waende wakanunue mahindi kwa wakulima. Wananchi wetu asilimia sitini wamejikita kwenye kilimo, sasa wanapopata mazao lakini wakakosa masoko kwa kweli inakuwa changamoto kubwa ilhali wamegharamia mbolea. Mahindi hivi sasa mahindi haya yasiponunuliwa maana yake mavuno ya mwaka uliopita yanakutana na mavuno ya sasa kuanzia mwezi ujao mikoa hii ya kusini hadi kufikia mwezi wa sita tunaanza kuvuna mahindi. Kwa hiyo taasisi husika, Wizara husika mahindi yakanunuliwe mapema sana kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na maeneo ya kuuza mahindi yapo mengi wahusika wanajua tunakambi za wakimbizi, mashirika ya kimataifa na tuna nchi jirani wanahitaji sana chakula. Kwa hiyo suala la masoko ya mahindi isiwe changamoto. Wananchi hawa haya mahindi yanasaidia kucomesha Watoto, matibabu na kuendelea kulima.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni lumbesa, suala hili bado limekuwa ni changamoto. Kwa hiyo tuone namna kama tutaweza kuuza bidhaa zetu kwa vifungashio maalum au kwa kutumia vipimo maalum. Endapo mtu anajaza gunia basi tuseme labda viazi au maharage debe moja ni kiasi kadhaa, kilo mia ni kiasi kadhaa. Lumbesa imekuwa ni changamoto na wakati mwingine katika magunia wakiweka zipu bila lumbesa baadhi ya maeneo wanavyoenda kushusha sasa kama soko la Kariakoo wanasesma pasipo lumbesa basi bei inashuka chini. Kwa hiyo eneo hili pia tutafute namna gani.

Mheshimiwa Spika, ukitokea mkoa wa Njombe bila kutaja Mchuchuma na Liganga unakuwa bado hujamaliza hotuba yako vizuri. Mradi wa Mchuchuma na Liganga bado kuna maombi kwa wananchi; tupate majibu mazuri kwamba ni lini mradi huu utaanza ku-*take off* tumekuwa tunapata majibu mara kwa mara kwamba linashughulikiwa, tunashukuru sana ipo kwenye llani lakini sasa tunataka mradi huu uanze kazi, aje Mheshimiwa Mama yetu azindue, Rais wetu, aje Waziri Mkuu na tunashukuru alifika pale Njombe, ahsante sana. Tuje tuzindue rasmi mradi huu wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Madiwani, bado Madiwani Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo za Kata wanaomba waendelee kukumbukwa. Madiwani wanafanya kazi nzuri sana kusimamia utekelezaji wa llani. Wanasi mamia ukamilishaji wa maboma, ukamilishaji wa shule, zahanati. Kwa kweli maboresho tunaomba yaangaliwe. Madiwani wanafanya kazi nzuri hivyo haki zao ziendelee kuangaliwa; ni namna gani tunaboresha haki za Madiwani. Eneo hili ni muhimu sana tuone namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Spika, na tunaposema Madiwani timu yao inakwenda pia na Wenyeviti wa Vijiji lakini *focus* kubwa tuanze kwanza na kwa Madiwani. Hawa ni watu wanaokaa katika kata siku zote, wanashughulika na changomoto aina mbalimbali katika Serikali za Mitaa. Kwa hiyo Madiwani wamekuwa wanachapa kazi sana, wanawajibika sana usiku na mchana, masaa ishirini na nne wako pale na wananchi kwa hiyo Madiwani tuone ni namna gani tunaendelea kuwasaidia... (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. DKT. PINDI H. CHANA: ...Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana kwa mchango wako. Dakika zilizobaki hazitutoshi kwa ajili ya kuweka mchango wa Mheshimiwa mwingine lakini leo imekuwa ni mwanzo mwema, tuishie hapo tutaendelea kesho.

Sasa nina matangazo mawili moja tunaomba niwatangazieni kwamba Waheshimiwa Wabunge ambaao ni waumini ya dini ya kiislamu wote kesho saa saba mchana mnaombwa mkutane pale Msekwa. Waheshimiwa Wabunge ambaao ni Waislamu mnaombwa mkutane pale Msekwa saa saba, kamili kuna jambo la kufanya.

Katibu wa Bunge anasema niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kipindii kirefu sasa magari ya Waheshimiwa Mawaziri husimama mbele ya Ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo Bunge linapositisha shughuli zake saa saba mchana au linapoahirishwa usiku kama saa hizi ili kuwachukua Waheshimiwa Mawaziri kwa hiyo gari zinakuwa zinakuwa zipo hapo nje ya ukumbi wa Bunge. Hali hiyo si tu husababisha msongamano mkubwa wa magari kwenye eneo hilo la hapo nje bali hilifanya eneo hilo kutokuwa rafiki wakati wa dharula unaohitaji uokoaji wa maisha ya watu au chochote kile kikitokea.

Hivyo, Waheshimiwa Mawaziri tunaombwa kuanzia leo kupandia magari hayo kwenye eneo la maegesho ya magari yenu lililopo nyuma ya ukumbi wa Bunge badala magari hayo kuwafuata mbele ya ukumbi wa Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri tunawaomba tena narudia kupandia magari yenu kwenye eneo la maegesho ya magari yenu lililopo nyuma ya ukumbi wa Bunge badala ya magari hayo kuwafuata hapo ili kuondoa ule msongamano mkubwa hata nyie wenyewe mnauona hali inavyokuwa. Kama hilo nalo ni usumbufu mnawenza mkatoa ushauri wa namna gari bora zaidi ya kufanya jambo hili. Hili tangazo la Katibu wa Bunge. (*Makofii*)

SPIKA: Basi baada ya hayo tutaendelea na uchangiaji kesho wa hoja hii hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo tutashughulika nayo kwa siku nne mfululizo na leo ni *day one*.

Basi kwa hatua hii tuliyofika shughuli za leo zote zimekamilika kwa hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 1.44 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 14 Aprili, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*